3. Soma P.G.O. Na. 359Utunzaji wa kumbukumbu za upelelezi wa jinai ngazi ya Mkoa 4. Ni jukumu la kila mkuu wa upulelezi wa wilaya kwa taarifa au kesi zote uchunguzi na taarifa za awali za uhalifu zilizopokelewa au ambazo amezikuta kwenye ofisi ile zitapaswa kuandikwa katika daftari la upelelezi (FP. 169). Thamani ya jumla ya mali iliyoibiwa au iliyopatikana itaandikwa katika safu ya nne chini ya maneno “Kosa au uchunguzi” Jina la Afisa mpelelezi litaandikwa kwenye safu ya 6.5. Daftari litakuwa likipitiwa mara kwa mara na hatua zilizochukuliwa na mkuu wa upelelezi wa wilaya kuhakikisha kwamba makosa yote makubwa yaliyoripotiwa katika taarifa ya awali (FP.4) inapelelezwa kwa kina na uplelezi una kukamilika kwa haraka iwezekanavyo .6. (a) Wakuu wa upelelezi wa wilaya watatunza orodha ya majina katika FP. 131 katika Mooer’s modern methods Binders. Orodha hii itakuwa na kumbukumbu za wahalifu wafuatao:-

(i) Waangaliwa wa polisi.

(ii) Wahalifu sugu amabo kumbukumbu zao zinatunzwa.

(iii) Watu wanaotafutwa katika wilaya na mikoa na wale wote waliotangazwa katika gazeti la polisi.

(iv) Watu waliorejeshwa makwao kutoka wilaya na mikoa.

(b) FP. 131 itapangwa kwa herufi kama ifuatavyo:-

(i) *Wazungu na Waasia*. – Jina la mwisho au jina la familia mfano muasia mwenye jina la Gulamali Husein Kanji yeye ataoredheshwa chini ya kundi K kwa kufuata herufi.

(ii) *Afrika waarabu n.k*-katika jina la kwanza mfano mwafrika mwenye jina la Mohamed s/o Salum ataorodheshwa katika kundi M kwa kufuata herufi.

7. Fomu ya polisi namba. 131 nyingine itawekwa kwenye jalada la

kila jina lisilo rasmi lakini maelezo ya mtu husika yataonyeshwa tu katika kadi .

8. Wakuu wa upelelezi wa wilaya watahakikisha orodha ya majina inakaguliwa kila siku “sambamba na taarifa ya ukamataji” (FP. 13) haraka atashauri kituo cha polisi husika kuhusiana na kumbukumbu za uhalifu kuhusiana na watu hao waliokatamatwa,.

Orodha yavitu vilivyoibiwa (FP. 135)

9. Wakuu wa upelelezi wa mikoa na wilaya watatunza orodha ya mali zilizoibiwa katika fomu ya polisi namba 131 ambayo itahifadhiwa katika Moor’s modern method Binders .

10. Orodha hiyo itakuwa katika mfumo wa mzunguko wa miaka mitatu ikitumia fomu ya polisi 135 ya rangi tofautitofauti kwa mwaka, kiasi kwamba katika kumaliza mwaka wa tatu, fomu ya polisi namba 135 ya mwaka wa kwanza zainaharibiwa. Fomu ya polisi namba 135 zitatolewa katika mwezi wa kumi na mbili kila mwaka na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai .

11. Orodha hii itajumlisha tu vitu ambavyo vitakavyokuwa vimechaguliwa na afisa upelelezi toka vyanzo vya ndani na kutoka katika gazeti la polisi ikiwa kama maslahi ya himaya na pia ikiwa ni rahisi kufuatiliwa mfano magari, mashine zenye namba za mtengenezaji, hati ya kusafiria na vitu vya mapambo vilivyotengenezwa kwa dhahabu..

12. Orodha ya mali ya kuokota yenye amri ya hakimu iliyochapishwa katika gazeti la serikali itakaguliwa kwa kuzingatia orodha ya mali.

Orodha ya baiskeli za wizi (Fomu ya polisi. 134)

13. Afisa wa upelelezi wa jinai wa Mkoa na Afisa wa upelelezi wa jinai wa Wilaya watatunza orodha ya baiskeli za wizi katika Fomu ya polisi namba. 134, na itahifadhiwa kwenye Field Mooer’s Modern Mehods Binders kwa kufuata utaratibu wa namba bila kujali kutengenezwa kwake.

14. Orodha itafuata mfumo wa mzunguko wa miaka mitatu kwa kutumia fomu ya polisi namba 134 yenye rangi kiasi kwamba katika kipindi cha kumaliza miaka mitatu kadi za mwaka wa kwanza zitaondolewa na kuharibiwa.

15. Mkuu wa kitengo cha forensiki atatunza orodha ya kudumu ya himaya ambayo ndiyo itakuwa ndio adidu rejea ya wakuu wa vituo na wakuu wa upelelezi.

16. Wakuu wa upelelezi wa mkoa na wilaya watatunza michoro yao kama jinsi zilivyo katika viambatanisho ‘A’ikionyesha hali ya uhalifu katika mkoa na wilaya.

Michoro ya uhalifu

17. Michoro ya uhalifu ya I itaonyesha hali ya mafanikio toka mwezi

hadi mwezi katika makosa yaliyo katika kanuni za adhabu: Sehemu ya chini ambayo ina (kivuli chekundu) itaonyesha idadi ya kesi ambazo watuhumiwa wamepatikana na hatia.

18. Sehemu ya juu (kivuli cha bluu) ambayo itaonyesha idadi ya kesi ambazo watuhumiwa hawajapatikana na hatia itajumuisha idadi ya kesi ambazo upelelezi haujafanikiwa.

19. Michoro ya uhalifu ya II itaonyesha mwelekeo wa kanuni ya adhabu katika kesi zilizochunguzwa (kwa bluu) na kiwango cha kesi ambazo watuhumiwa wamepatikana na hatia (kwa nyekundu).

20. Michoro ya uhalifu ya III itaonyesha hali ya mwezi kwa mwezi ya uhalifu mkubwa (kiambatanisho 'A' cha PGO 311), ikiwa na marejeo huru kwa mwelekeo katika makosa ya uvunjaji kama inavyoonyeshwa katika rangi ya kijani.

21 Thamani za kitarakimu za michoro zitaaachwa kwa uamuzi wa wakuu wa upelelezi wa mikoa na wilaya.

KIAMBATANISHO "A"

(KWA P.G.O. Na. 40)

20……..

..... Wilaya

KANUNI YA ADHABU

Alama ya grafu : -	Januari	Februari	Machi	Aprili	Mei	Juni	Julai	Agosti	Septemba	Octoba	Novemba	Disemba
Nyekundu –Hatia												
Bluu - Kutokuwa na hatia & Kushindwa												
Tupu – Inayongoja												

KIAMBATANISHO “B”

(KWA P.G.O. Na. 40)

KANUNI YA ADHABU

20 ..... HADI 20 .....

..... Wilaya

TARAKIMU ZA MWAKA

KITU	2003	2004	2005	2006	2007	2009	2010	2011	2012	2015
Alama ya Grafu										
Nyekundu – Hatia										
Bluu - Bila hatia & Kushindwa										
Tupu - Inayongoja										

KIAMBATANISHO “C”

(KWA P.G.O. Na. 40)

MAKOSA MAKUBWA

200 .... Wilaya

AINA		Jan	Feb	Machi	Apr	Mei	Juni	Julai	Agosti	Septemba	Octoba	Novemba	Disemba
Alama ya Grafu													
Nyekundu – Hatia													
Bluu -	Kesi za uhakika												
	Kesi zilizosajiliwa												
Kijani –	Uvunjaji wa uhakika												
	Kesi zilizosajiliwa												

PGO - 43

KIKOSI CHA MBWA NA FARASI

SEHEMU YA KWANZA:

Mtu wa idara ya mbwa na farasi :-

1. Uteuzi wa mtu wa kufundishwa kuwa askari kuongoza mbwa na farasi utafanywa na Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi cha jeshi la polisi.

2. Mkuu wa Kkosi cha Mbwa na Farasi, Dar es Salaam, atapewa taarifa mwezi mmoja kabla ya askari muongoza Mbwa au Farasi hajaanza likizo. Mbwa ambaye mwongozaji wake ameondoka kwenda likizo, anaweza kupelekwa Chuo cha Taalum ya Polisi Moshi kwa ajili ya matunzo na mapumziko.

3. Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi, Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi atatoa usindikizaji kwa mbwa wanaopelekwa chuoni kwa ajili ya matunzo. Baada ya kumaliza likizo askari mwongozaji wa mbwa atapiga timamu Chuo cha Taalum ya Polisi Moshi kwa ajili ya kumchukua Mbwa wake na kufanya mazoezi ya kujikumbusha kwa muda wa juma moja.

Ununuzi na uzalishaji wa mbwa na farasi

4. Hakuna Mbwa yeyote atakayenunuliwa ama kupatikana bila ya kuthibitishwa na Mkuu wa kikosi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi la Polisio na ama kuthibitishwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania.l

5. Hakuna Farasi yeyote atakayenunuliwa ama kupatikana bila ya kuthibitishwa na Mkuu wa Kikisi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi la Polisi , ana amba kuthibitishwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania.

Usafirishaji:-

6. (a) Endapo Nbwa wa Polisi atachuliwa toka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ndani ya gari ambalo halikutengenezwa mahsusi kwa usafirishaji wa Mbwa, askari mwongoza Mbwa ataketi nyuma ya gari na atamshikilia mbwa wake kwa ajili ya usalama huku akiwa ameshikilia ukanda wa shingo ya mbwa kwa muda wote wa safari.

(b) Kwa safari ambayo ni ndefu, na katika hali ambayo mbwa anasafirishwa kwa kazi ya muda mfupi, yafuatayo lazima yazingatiwe:-

i. Kwa usafiri wa barabara: mbwa atawekwa ndani chombo maalum cha kusafirishia na kuwekwa nyuma ya gari. Askari mwongozaji mbwa ataketi nyuma ya gari akiwa na mbwa wake muda wote wa safari.

ii. Kwa usafiri wa Reli: atawekwa katika chombo maalum cha kusafirishia na mwongoza mbwa atasafiri dani ya mkokoteni au ndani ya gari moshi akiwa na mbwa wake muda wote wa safari.

iii. Kwa usafrri wa anga: Itategemana na masharti ya usafishaji wa anga kuhusiana na ubebaji wa mifugo.

(c) Pia kanuni kwamba

i. Katika safari ndefu zote, askari mwongoza mbwa atawajibika kumpa mbwa wake maji na chakula na kumfanyisha mazoezi kwa vipindi

ii. Afisa anayeruhusu usafirshaji wa mbwa atatoa maelezo ya safari kwa askari mwongoza mbwa ikijumuisha aya (i) hapo juu, na taarifa zote zinazohusu safari.

(d) Afisa anayeruhusu safari atatoa hati ya kusafiria na atajulisha sehemu mbwa anakopelekwa muda mbwa anapoondoka na muda unaotarajiwa kufika huko. Afisa mpokeaji atafanya mipango muhimu ya usafiri na malazi mbwa na askari mwongozaji watakapofika.

Uhamisho wa mbwa na askari mwongozaji:

7. Hakuna uhamisho wa mbwa na mwongoza mbwa kutoka Kikosi cha Mbwa na Farasi unaweza kufanywa bila mamlaka ya Mkuu wa kikosi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi la Polisi Tanzania

8. Majeraha yote yaliyoathiri askari wa Mbwa na Farasi pamoja na wanyama yatolewa taarifa Makao Makuu ya Polisi kwa kutangaza katika sehemu ya pili ya Amri za Jeshi.

9. Wakuu wa Komandi watawajibika kusimamia mambo ya utawala na uendeshaji wa shughuli za kila siku za Kikosi cha Mbwa na Farasi, isipokuwa mafunzo yatakayofanyika Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi.

10. Mahali popote polipoanzishwa Kikosi cha Mbwa na Farasi, Kamanda wa Polisi Mkoa atahakikisha utawala na usimamizi wa Kikosi unakuwa chini ya Afisa wa polisi aliyetangazwa kwenye Gazeti Serikali.

Utunzaji wa mafunzo ya mbwa nawanaomilikiwa binafsi:

11. Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi wa jeshi hatafundisha wala kutunza mbwa wanaomilikiwa binafsi bila ya kibali cha maandishi cha Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania.

12. Askari mwongoza mbwa au mwendesha farasi haruhusiwi kuhifadhi au kufundisha au kwa namna yoyote ile kutunza mbwa wa farasi wanaomilikiwa binafsi.

Kumbukumbu binafsi:

13. Mbwa/Farasi dume waliothibitishwa na Mkuu wa kitengo cha mbwa na farasi ndiyo wataotumika kwa ajili ya uzalishaji wa vizazi vijavyo.

14. Mbwa majike watakuwa Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi.

15 Mbwa yeyote hatachukuliwa kwa kufanya kazi hadi awe na umri wa miezi sita

16. Kila Mbwa na Farasi atapewa namba na Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi atakapochukuliwa kwa ajili ya kuanza kazi na kumbukumbu zake zitaingizwa katika sehemu ya pili ya Amri za Jeshi na katika kumbukumbu zingine zinazohusu wanyama. Mbwa watapewa namba kwa mpangilio wa kufuatana. Kila namba itatanguliwa na herufi “P.D” na kwa farasi “P.H”.

17. Watoto wa mbwa wanapozaliwa kwa mahitaji ya Jeshi, kumbukumbu zao zitaingizwa katika karatasi ya kumbukumbu ya historia. Kumbukumbu zitahusu pia mgawanyo wa watoto wote wa mbwa. Na pia itauimika kwa Farasi.

18. Mbwa/Farasi atakapochukuwa kwa mahitaji ya jeshi au watoto wa mbwa watakapotumika kwa matazamio, jalada litafungulwa pamoja na fomu ya kumbukumbu za utumishi (PF.154) zitajazwa, nakala tatu pamoja na kadi ya kumbukumbu za matibabu zitatunzwa na Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi nakala ya pili itatumwa Makao Makuu ya Jeshi na nakala halisi itawekwa ndani ya jalada la Mbwa/Farasi husika, pamoja na kadi ya kumbukumbu za matibabu, ambalo litatunzwa katika kikosi atakachopangwa Mbwa/Farasi huyo na jalada hilo litaambatana na Mbwa /Farasi anapohamishwa. Picha ya kila Mbwa /Farasi itawekwa ndani ya fomu ya Polisi namba 154 wakati wanapanza kupangwa eneo la kufanya kazi.

19. (a) Hakuna Mbwa/Farasi atakayeuzwa au kutumiwa au kutupa na isipokuwa kwa maelekezo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi au mganga wa mifugo, isipokuwa kwa amri ya kuharibiwa au kuuzwa kutokana na majerahi, ugonjwa au kuzeeka. Au mnayama akiwa katika hali ambayo inalazimu kuharibiwa haraka. Katika mizingira hayo Afisa wa Polisi aliyotangazwa katika Gazeti la Serikali atatoa amri ya kuharibiwa na kutuma taarifa ya mazingira hayo kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi pamoja na Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi.

(b) Mambo mengine yote yatanyika kwa kuomba kibali Makao Makuu ya Jeshi, kama Mbwa wanaweza kuwa katika hali ambayo:

(i) Mbwa waliofundishwa wameshindwa kuoneysha ufanisi

(ii) Mbwa waliofundishwa muda kidogo hawaonyeshi kuja kuwa na ufanisi

(iii) Watoto wa mbwa wa ziada ya mahitaji ya jeshi kila aina itakuwa na bei tofauti, maombi ya ruhusa kuuza aina ya mbwa, itaonyesha kila aina ya bei ya kuuzia.

(c) Bei ya kuuzia kama angalizo, itazingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kwa mbwa, kama uzao wake unafahamika, thamani ya wazazi wake, na kama bei ya kuuzia mbwa katika masomo ni sawa na uzao wa wazazi wake.

(ii) Kwa watoto wa mbwa wenye umri hadi majuma 12, bei ya chini itakuwa Tsh. 100,000/= kabla ya kuzingatia vigezo vilivyoko hapo juu.

Ishara ya moto:

20. Wakati ishara ya moto ikilia, waongoza Mbwa na Farasi wote wataelekea haraka iwezekanavyo kwenda kwenye mabanda ya mbwa. Watabakia hapo hadi wakapo tawanywa tayari kwa kuwaondosha mbwa hadi eneo salama.

Sehemu ya II: ajira na mafunzo

Ajira ya mbwa na farasi:

21. Maafisa Waandamizi wa Polisi wa Kamandi ambazo mbwa na farasi wamewekwa, wataelekeza ajira ya mbwa wote waliopo katika kamandi zao. Katika hili, sera zitafafanuliwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania. Kufuatia matumizi na ukomo wa mbwa wa polisi, maofisa wa kamandi wataomba ushauri wa Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi Tanzania kadri inayowezekana. Wakati mbwa wanapotumika katika msako wa kufuatilia jambo, Mkuu wa Polisi Wilaya husika ataandaa taarifa na kuituma kwa Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi haraka iwezekanavyo. Mfano wa taarifa inapatikana kaika kiambatanisho “C” katika amri hii.

22. Nyongeza katika mahitaji aya ya 2 PGO 47, Kikosi cha Mbwa na Farasi inaweza kukaguliwa kwa maelekezo ya Mkuu wa Jeshi au kwa maombi ya Wakuu wa Komandi, Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi anaweza akaombwa ushauri kuhusiana na masuala ya mafunzo na uanglizi wa mbwa.

23. Matumizi ya Mbwa/Farasi waliofunzwa waliopo chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi yatakuwa chini ya Mkuu wa chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi, na maombi ya msaada yataombwa moja kwa moja kwa Mkuu wa Chuo kupitia kwa Kamanda wa Polisi Mkoa husika.

24. Mbwa/Farasi na au waongoza mbwa.waendesha farasi waliofundishwa kwa muda wanaweza kutumika katika kazi chini ya usimamizi wa Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi.

25. Mbwa pamoja na waongoza mbwa wote watafundishwa kwa kufuata maelekezo yaliyoonyeshwa katika kiambatanisho “A” na kufikia kiwango kilioonyeshwa katika kiambatanisho hiki.

26. Mkuu wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi atawajibika kuhakikisha kwamba hakuna Mnyama au mwongoza Mbwa/mwendesha Farasi atakayehesabika kuwa amefunzwa hadi awe amekamilisha vigezo vilivyowekwa kutokana na maelekezo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi.

27. Mkuu wa mbwa na Farasi, Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi atawajibika kwa Mkuu wa chuo kuandaa mpango wa mafunzo ya awali ya Mbwa/Farasi na waongoza mbwa katika viwango vilivyowekwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi wa kuhakikisha viwango hivyo vinazingatiwa.

Ratiba ya kila siku ya mwongoza Mbwa na waendesha Farasi

28 (a) Waongoza mbwa na waendesha Farasi watafika kazini eneo la mabanda ya kuhifadhia mbwa saa moja kabla ya muda wanaotakiwa kufoleni na Mbwa/Farasi wao. Kabla ya kufoleni watafanya yafuatayo:-

(i) Watawafanyisha mazoezi Mbwa/Farasi wao, kama aya ya 47 – 50;

(ii) Watasafisha mabanda ya Mbwa na maeneo yanayozunguka.

(iii) Watawasafisha Mbwa na Farasi: na

(iv) Wataelekea eneo la kazi

(b) Wakitoka kazini, waongoza mbwa lazima:

(i) Wawape chakula na maji Mbwa/Farasi wao
(ii) Watafanyisha mazoezi Mbwa/FArasi wao
(iii) Watasafisha vyombo vya kulia Mbwa chakula na kuhakikisha maji yanakuwepo katika mabanda ya mbwa; na
(iv) Watafungia Mbwa/Farasi ndani ya mabanda yao na kuondoka.

29. Wakati Mbwa/Farasi hawahitajiki katika kazi za mchana, mpango kazi wa waongoza mbwa/waendesha farasi utakuwa kama ifuatavyo.

(a) saa 12:30 asubuhi wataingia kazini, kusafisha mabanda ya Mbwa/Farasi na kufanya mazoezi yoyote yale yatakayokuwa yamelekezwa na Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi cha Jeshi au Afisa Mkuu yeyote aliyetangazwa katika Gazeti la Seriali, Mbwa/Farasi watarudishwa katika mabanda mara baada ya kumalizika mazoezi na kuoshwa.

(b) Saa 10.000 jioni, Wataingia kazini, kuwalisha na kuwapa maji na kuwafanyisha mazoeziMbwa/farasi (kama hawahitajiki kwa kazi za usiku angalia aya 44), Watawasafisha mbwa, kusafisa mabanda na maeneo yote na kuwafungia mbwa mabandani.

Sehemu ya III:

Usimamisi wa fedha

Usimamizi wa mafunzo kwa ajili ya manunuzi na matunzo ya Mbwa na Farasi

30. (a) Mafungu ya fedha kwa ajili hii, kwa kawaida yatotolewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa makamanda wa Polisi wa Mikoa ambao wataelekeza mafungu hayo kwa wakuu wa vikosi vya mbwa na farasi kufuatana na makadirio ya ukumbwa wa wanyama alionao na manunuzi yaliyopangwa naye kupitia kwa Mkuu wa Ghala la Polisi.

(b) Mgawanyo wa mafungu wa fedha yaliyotolewa na makamanda wa polisi wa Mikoa yatafanya kila mwezi. Mgawanyo kwa mwezi unaofuata yatazingatia matumizi ya mwezi kati ya makadirio na uhalisia wakati wa kipindi hicho.

Uhamisho wa Muda:

31. Ambapo mbwa, farasi na mwongoza Mbwa/mwendesha Farasi watahamishiwa

Mkoa mwingine kwa kazi za muda, yafuatayo yatafuatwa:-

(a) MWONGOZA MBWA/ MWENDESHA FARASI; Kipindi kisichozidi miezi miwili ataheabika kama amehamishwa kwa muda na atapata posho zake stahiki. Zaidi ya miezi miwili itahesabika kuwa ni uhamisho kamili.

(b) MBWA/FARASI: itahesabika kuwa ni hamisho wa muda (wakiwa kazini) kwa muda wowote ule watakapokuwa nje ya kituo chao mama. Mafungu ya fedha yatatolewa na kupelekwa kwa Mkuu wa Kituo ambapo wamewekwa kwa muda toka kwa Mkuu wa Kitengo mama alikotoka.

Sehemu ya VI:

Uangalizi wa mabanda ya Mbwa na Afya na usafishwaji wa mazizi ya Farasi

Usafishaji

32. Waongoza mbwa /waendesha Farasi wanawajibika kwa usafi wa mabanda ya mbwa/ mazizi ya farasi yote ya mbwa/farasi yaliyopo sehemu zao.

33. Mabanda ya mbwa/mazizi ya farasi yatasafishwa mara mbili kila siku, kwamba mapema asubuhi kabla ya mazoezi, na wakati wa kulala usiku.Mabanda ya Mbwa/Mazizi ya farasi yanaposafishwa

kinyesi kitachomwa moto. Baada ya kundoa uchafu wakati wa asubuhi mabanda ya mbwa/mazizi ya farasi yatasuzwa, isipokuwa wakati wa baridi ambapo sakari ya mabanda ya mbwa/mazizi ya farasi yatakaposafishwa kwa vumbi la mbao, mchanga na mabanda ya mbwa/maziziya farasi kupuliziwa dawa mara mbili na kila juma. Wakati wa hali ya hewa ya kawaida dawa itapuliziwa mara mbili kwa juma kwa kiasi kidogo.

34. Maji ya pamoja na vifaa vya chakula vitasafishwa na kuwa safi kila siku. Vifaa vya kulia chakula vitaoshwa baada ya kula na vitawekwa juu chini katika mahali maalum hadi hapo vitakapohitajika.Endapo mabanda ya mbwa yanayochukulika yatatumika basi vyomba vya kulia chakula vitawekwa juu ya mabanda hayo. Mara ya baada ya usafi, vyombo vya kuhifadhia maji vitajazwa maji safi na kuweka ndani ya mabanda.

Ukaguzi wa daktari wa mifugo

35. Mbwa na Farasi wote wafanyiwe uchunguzi mara moja kila mwezi na daktari wa serikali wa kutibu wanyama, au kwa vipindi tofauti kama itakavyowezekana na matokeo ya uchunguzi huo yataingizwa katika kadi ya matibabu ya wanyama “B” ya Mbwa /Farasi husika. Hii haitatumika katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi ambapo Mkuu wa Chuo, Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi wanawajibika kupata huduma za daktari wa kutibu mifugo inapolazimika. Kadi ya kutunza kumbukumbu za matibabu ya Mbwa/Farasi “B” lazima iwepo kwa kipindi ambacho Mbwa/Farasi wanakaguliwa na daktari wa kutibu wanyama.

Taarifa za ugonjwa au majerahi:

36. Waongoza mbwa/waendesha farasi wanawajibika kutoa taarifa kwa Mkuu wa Komandi au daktari wa mifugo haraka iwezekanavyo Mbwa/Farasi wanapogundulika kuugua au kuumia, kadi “A” itatakiwa kupwapo. Hali mbaya ya ugonjwa au majerahi itatolewa taarifa kwa Mkuu wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi na Makao

makuu ya Polisi kwa njia ya simu ya upepo. Kwa kuzuia na kutibu magonjwa ya kawaida angalia " maandiko juu ya Ajira na utunzaji wa Mbwa wa Polisi" ambazo zitatolewa kwa vitengo vya mbwa na farasi na itajumuisha amri za utendaji za kila kitengo.

Vifaa vya huduma ya kwanza

37. Mabanda ya mbwa/mizizi ya farasi yote yatakuwa na sanduku la huduma ya kwanza ilivyoainishwa katika kiambatanisho "B". Vifaa vitatumika kulingana na maelezo yaliyomo ndani ya sanduku la huduma ya kwanza.

kuogesha

38. Mbwa na Farasi wataogeshwa dawa mara kwa mara.Mbwa /Farasi wote wa Polisi kwa kawaida wataogeshwa dawa kila juma. Wakati wa hali ya hewa ya baridi, mbwa/farasi watazamishwa kwa kuogeshwa dawa bali watapakwa dawa ya unga aina "Gamates plus" mbwa wagonjwa hawatamishwa wakatia wa kuogeshwa dawa bali watapakwa unga wa "Gammatex Plus".

Chanjo.

39. Mbwa wote wa polisi watachanjwa chanjo:-

a) Kichaa cha mbwa: Katika hali ya kawaida watachanjwa kila mwaka isipokuwa kama kutakuwa na mlipuko wa ugonjwa wa kichaa cha mbwa ambapo mbwa wote watachanjwa haraka iwezekanavyo.
b) Ugonjwa wa kukohoa na kukosa nguvu, Homa ya manjano , Leptospirostis na parvo (DHLP) wakati wa kuyapata au watoto wa mbwa wakiwa na umri wa majuma 3 hadi 4, na watarudiwa kuchanjwa baada ya mwezi mmoja.
c) Farasi wote wa Polisi watachanjwa dhidi ya magonjwa ya Farasi wa Afrika" wakiwa na umri wa mwaka mmoja na kuendelea kila mwaka.

40. Mbwa/Farasi waliokatika matumizi ya kazi na wenye hati ya uthibitisho wa chanjo katika hali yoyote hawatapewa chango tena hadi muda mwingine wa chanjo unapofika. Kumbukumbu za chanjo

zitaingizwa katika kadi ya kumbukumbu ya matibabu ya mifugo “A” kumbukumbu za sindano za mwanzo alizochomwa zitajumuishwa katika kadi hiyo.

Sehemu ya V:

Chakula na vifaa vya Mbwa na Farasi

Ulishaji:

41. (a) Mbwa watalishwa mara moja kwa siku isipokuwa wakati wa ugonjwa au katika mazingira mengine yatakayolazimisha kubadilika kwa taratibu. Chakula cha siku cha mbwa wanaofanya kazi kitajuisha -

2 na nusu lb za nyama ilyopikwa ikijumisha na mifupa

1 lb ta biskuti , mpunga or unga wa mahindi

2 oz za mboga za majani

1 o2 ya sehemu ya chumvi kwa juma

(b) (i) Farasi watalishwa chakula mara mbili kutwa, asubuhi na jioni/ Kila mlo utakuwa na uzito wa kilo 2 na nusu, isipokuwa katika hali ya ugonjwa au mazingira mengine yatakayolazimishwa kubadilika kwa utaratibu, mfano mamba/ugonjwa

(ii) Ambapo hakuna malisho akiwa amefungiwa basi atalishwa nyasi mara tatu kutwa.

(iii) Farasi pia atalishwa mboga za majani, kabichi kilo 1 na koroti kilo 1 kwa ajili ya vitamini. Watapewa pia chumvi supremamaclik, au mchanganyiko wa madini ya bayslick.Mchanganyiko huu unaweza kubadilishwa kutokana na mazingira yatakayo lazimu ubadilishwaji mfano ushauri wa mganga wa wanyama, ugonjwa au kibali cha Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi.

42 (a) Kiwango cha chakula kitabadilishwa kwa maelekezo ya Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na farasi au mganga wa wanyama

(b) Hakuna farasi atakayelishwa “horsemalt” ndani ya masaa matatu wakati wa kwenda kazini.

43. (a) Ambapo chakula hakitapishwa kwa madhumuni ya waongoza mbwa wataandaa chakula kingi kwa madhumuni ya ratiba ya zamu za kila siku zinavyoonyeshwa

(b) Ambapo hakuna mhudumu, waendesha farasi wanawajibika kuwalisha farasi na kukata majani kwa mujibu wa zamu zilivyopangwa.

(c) Aidha wanawajibika kufanya usafi wa mazizi ya farasi mara mbili kwa siku ambayo ni asubuhi na jioni.

Usafi:

44. (a) Kila mbwa atafanyiwa usafi angalau kwa muda wa dakika 15 kila siku. Usafi utafanywa kwa kufuata njia zilizofundishwa. Msisitizo utakuwa zaidi kwenye macho ya mbwa, msikio, pua, meno na vidole na banda la mbwa na kuondoa kupe ambao wameharibiwa.

(b) Kila farasi atafanyishwa mazoezi mara moja au zaidi kwa siku kulingana na maelekezo ya Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi. Muda wa mazoezi hawatakiwi kuzidi dakika 30. Mazoezi haya yatakuwa ni nyongeza ya muda wowote uliopangwa kwa ajili ya mafunzo.

45. Mazoezi yatafanywa katika njia na maeneo ambayo Mkuu wa Kikosi wa Kikosi cha Mbwa na Farasi au afisa aliyetangazwa katika Gazeti la Serikali ambaye ndiyo Mkuu wa Kitengo husika.

46. Kwa kawaida mbwa atafanyishwa mazoezi akiwa amefungwa mkanda shingoni, lakini Mkuu wa Kikosi cha mbwa na farasi au Afisa aliyetangazwa katika Gazeti la Serikali ambaye ni Mkuu wa

kitengo hicho anaweza kuelekeza mbwa kufanyishwa mazoezi wakiwa hawajafungwa kamba katika maeneo ambayo binadamu au wengine hawapo.

49. Wakati wa kuingia au kutoka ndani ya mabanda ya Mbwa watashikwa ukanda wa shingoni. Wakati wakiwekwa ndani ya mabanda yanayobebeka mnyororo utafungwa kwenye mabanda hayo. Wakifungiwa katika mabanda ya kudumu yaliyotengenezwa kwa vifaa maalum, mnyororo wa mabanda hayo isipokuwa kama muundo wa mabanda hayo kuna eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya kufanya mazoezi kwa kila mnyama.

Vifaa:

51. (a) Orodha ya vifaa vitakavyotolewa kwa ajili ya kil ambwa ni kama ifuatavyo:-

Kifaa	Muda wa kubadilisha
Ukanda wa shingo ya mbwa mmoja	Mwaka mmoja
Kamba ya kuongoza mbwa mmoja	Mwaka mmoja
Mswaki mmoja	Mwaka mmoja
Kitana kimoja	Miaka miwili
Bakuli moja la chakula	Hadi itakapohitajika
Bakuli moja la Maji	Hadi itakapohitajika

Hatama kwa ajili ya mafunzo/kufuatilia ……. Mitano

(kwa mbwa wa kufuatilia nyao tu.)

- Kifungo cha mdomo wa mbwa, ngozi, - Miaka mitano

mbili kwa kiwa mbwa

- Banda la mbwa linalobebeka 1 kwa - Matakwa ya mkuu wa kitendo

Kila mbwa (au zaidi)

51 (b) Vifaa vifuatavyo vitatolewa kwa kila farasi

Kifaa	Muda wa kawaida wa kubadilidha
Hatamu moja	Mwaka mmoja
Blanketi moja	Mwaka mmoja
Tandiko moja	Miaka mitano
Kikuku cha kutandikia farasi kimoja	Mwaka mmoja
Viatu vya farasi pea moja	Miaka mitatu
Mafuta ya ngozi kopo moja	Miezi sita
Kitana kimoja	Miaka mitatu
Kifaa cha kukatia kwato kimoja	Miaka mitatu
Kisu chakukatia kwato kimoja	Miaka miaka mitatu
Ukanda mmoja wa matandiko	Mwezi mmoja
Chombo cha kunywea maji kimoja	Miaka mitano

PGO - 44

IDARA YA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI

UTAWALA

Uteuzi wa askari-idara ya upelelezi wa makosa ya jinai.

1. (a) Kwa mujibu wa kanuni askari mwenye cheo cha mkaguzi wa polisi na askari wa cheo na majalada (R/F) hawataruhusiwa kufanya kazi za upelelezi mpaka wawe wametimiza miaka miwili kazini (2). Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa atatakiwa kutunza orodha ya askari wote wa upelelezi ambao watatakiwa kuwa na rekodi nzuri ya utendaji na uwezo wa kufanya kazi ya upelelezi wa makosa ya jinai.

(b) Uhamisho wowote wa askari kutoka au kuingia idara ya Upelelezi na makosa ya jinai utahitaji uthibitisho wa Mkuu wa Jeshi la Polisi, na Mkurugenzi wa upelezi na makosa ya jinai anaweza kufanya uhamisho wa askari wa upelelezi wenye vyeo vya mkaguzi wa polisi na askari wa cheo na majalada ndani ya idara ya upelelezi na makosa ya jinai pasipo uthibitisho kutoka Mkuu wa jeshi la Polisi. Uhamisho wa askari mwenye cheo kuanzia mrakibu msaidizi wa polisi utahitaji uthibitisho wa Mkuu wa Jeshi la Polisi. Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya jinai anawajibu wa kuhakikisha kwamba uhamisho wowote katika idara ya upelelezi unatangazwa katika amri za jeshi (force order).

(c) Askari mbalimbali wanaohamia katika Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai watafanya kazi kwa majaribio kwa kipindi cha miezi sita chini ya uangalizi wa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa. Kila inapowezekana watafanya kazi chini ya mwongozo wa wapelelezi wazoefu. Mkuu wa upelelezi wa mkoa atahusika moja kwa moja katika kuhakikisha kuwa askari walio kwenye majaribio wanapewa fursa ya kutoona ili kuongeza uzoefu. Baada ya miezi sita ya mafunzo, Mkuu wa Upelelezi wa makosa ya jinai wa mkoa atatuma taarifa kwa Mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai kuhusu askari waliokuwa kwenye majaribio namna wanavyomudu kufanya kazi ya upelelezi. Askari watakaochaguliwa watatakiwa kuhudhuria mafunzo ya upelelezi wa makosa ya jina katika Chuo cha mafunzo ya Polisi Moshi au

Zanzibar ambapo mwisho watatahiniwa kwa mitihani ya kuandiaka na mahojiano ya mdomo.

Posho ya mavazi/nguo na upelelezi kwa askari wa Idara ya upelelezi.

2. (a) Askari yeyote wa idara ya upelelezi anastahili kupata posho ya upelelezi na nguo kuanzia tarehe aliyoidhinishwa na Mkurugenzi na Idara hiyo. Posho hizo lazima ithibitishwe Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kwa mujibu wa kanuni za kudumu za polisi (PGO 1 na 50) na Mkurugenzi huyo atahakikisha malipo hayo yanatangazwa katika amri za jeshi (force order)

i. Posho ya mavazi/nguo – Tsh. 50,000 kwa mwaka

ii .Posho ya upelelezi (P.C's na N.C.O's) Tsh.3,000 kwa mwezi

iii. Posho ya upelelezi(mkaguzi na Afisa) – Tsh. 4,000/= kwa mwezi.

(b) Posho hizi zinaweza kubadilishwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi kulingana na wakati kupitia amri za jeshi (force order)

Utunzaji/uandishi wa majalada

3. Idara zote za upelelezi zitafuata kanuni na tarativu za utunzaji/uandishi wa majalada kama inavyoainishwa na Polisi Makao Makuu kulingana na wakati. Majalada yatawekewa kumbukumbu kwa ufupisho wa kituo au kitengo (Kanuni za Kudumu za Jeshi Na.5) ikifuatiwa na herufi "CID" na namba.

PGO - 45

MITIHANI INAYO ONGEZA UJUZI MAHALI PAKAZI. SEHEMU YA KWANZA –MITIHANI YA MAAFISA WALIOTANGAZWA KATIKA GAZETI LA SERIKALI

1. Maafisa Waliotangazwa katika Gazeti la Serikali wanatakiwa kufaulu mitihani ifuatayo isipokuwa wale tu ambao hawatatakiwa kufanya kwa mwongozo katika aya ya 2:-

(a) Mitihani ya kujipima na kuongeza ujuzi kwa Maafisa Waliotangazwa katika Gazeti la Serikali.

(i) Mrakibu msaidizi baada ya kupandishwa cheo kutoka ukaguzi au kuhamishiwa toka majeshi mengine atatakiwa kufanya mitihani hiyo kwa miaka miwili isipokuwa endapo hawatatakiwa kufanya kutokana na mwongozo wa Mkuu wa Jeshi la Polisi.

(b) Mtihani wa Kiswahili kigumu :

(i) kwa Maafisa Waliotangazwa katika Gazeti la Serikali.

wote walioteuliwa kutoka majeshi mengine ndani ya miaka miwili ya uteuzi wao watatakiwa kufanya mitihani ya daraja la juu na kufaulu.Na endapo maafisa hao watakuwa na umri zaidi ya miaka 35 watatakiwa kusoma miaka mitatu na kufaulu.

(ii) Mitihani hii pia itafanywa na maafisa wote wa polisi ambao hawajafaulu mitihani ya Kingereza na Kiswahili katika mitihani ya kidato cha nne au inayofanana na hiyo.

Kuondolewa kufanya Mtihani wa Kiswahili Kigumu.

2. Msamaha wa kufanya mtihani wa Kiswahili kigumu tu na ofisi ya Raisi – Utumishi wa Umma.

3 Mitihani hii ya kuongeza ujuzi inasaidia kuongeza na kuleta ufanisi unaohitajika.Mrakibu Msaidizi aliyechini ya matazamio na akashindwa kufauru mitihani ipasavyo kama ilivyoainishwa katika aya 1(a) na (b) kwa kawaida, hatathibitishwa kwenye uteuzi wake.

4. Maafisa watakao shindwa kufaulu mtihani kama ilivyoainishwa katika aya 1(a) na (b) wataondolewa au kusitishiwa nyongeza zao.

Mitaala ya Mitihani na viwango vya kufaulu.

5. Maelezo ya kina ya mitihani kama yalivyoainishwa katika aya 1 ni kama ifuatavyo: -

(A) Mitihani ya kupima ujuzi kwa kwa Maafisa Waliotangazwa katika Gazeti la Serikali.

:

Mitihani itakuwa na masomo manne , kama ilivyoainishwa hapa chini : -

(i) Vyanzo vya sheria ya jinai:

Maswali katika Kanuni ya Adhabu na sheria zingine zinazotoa –angalia kiambatanisho “A”.

(ii) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar ya 1984;Mwenendo wa Jinai , Kazi za Polisi na kanuni za Maadili;

Maswali juu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, Sura ya . 2 iliyofanyiwa mapitio 2002 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984,Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ,sura ya . 20 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002, Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi , sura ya 322 iliyofanyiwa mapitio mwaka . 2002,Kanuni za Jeshi la Polisi, Kanuni za kudumu za Jeshi la Polisi, maelekezo ya upelelezi .

(iii) Ushahidi:

Maswali yahusuyo sheria ya ushahidi sura ya 6 kama ilivyo fanyiwa mapitio mwaka. 2002.

(iv) Muundo wa jeshi ,Utawala na Sera ya Fedha.

Maswali kuhusu kanuni za Fedha,Kanuni za kudumu za Jeshi la Polisi na Amri za Jeshi.

(v) Viwango vya kimataifa na mikataba inayohusiana na utendeji wa

kazi za polisi.

Hojaza Umoja wa wa Mataifa kuhusu maadili kwa maafisa wasimamizi wa sheria na kanuni za msingi za Umoja wa Mataifa kuhusu matumizi ya nguvu na silaha za moto.

ANGALIZO: (a) Viwango vya ufaulu wa mitihani ni: -

(i) UFAULU: Asilimia 55 ya alama zote, na si chini ya asilimia 50 kwa kila mtihani

(ii) UFAULU WA JUU: Asilimia 75 ya alama zote, na si chini ya asilimia 70 kwa kila mtihani

(b) Mtahiniwa atakayeshindwa katika somo moja anaweza kuruhusiwa, na Inspekta Jenerali , kufanya, kufanya mtihani unaofuata,

(c) Mtihani kwa kawaida utafanyika kila mwazi Novemba ya kila mwaka chini ya maandalizi yatakayofanywa na Mkuu wa chuo cha Polisi Dar-es-salaam.

(d) Hakuna kitabu cha kiada kitakachoruhusiwa kutumika wakati wa mitihani.

(B) Mtihani wa Kiswahili kigumu daraja la chini

(a) Mtihani utakuwa na sehemu mbili– wa kuongea na kuandika. Maafisa wa Polisi watapaswa kufaulu kwa asilimia 70 (daraja la juu) katika kila sehemu.

(b) Mtihani utafanyika mara mbili kila mwaka, katika mwezi Machi na Septemba, kumbukumbu zitatangazwa katika Gazeti la Serikali.

Sehemu II – Mitihani ya Wakaguzi

6. Wakaguzi wanatakiwa kufauru mitihani ifuatayo:-

(a) Mitihani ya kuongeza tija kwa Polisi, Daraja la I:

Kuwepo na ufaulu kwa maafisa wote ndani ya miaka miwili baada ya uteuzi wao kuwa wakaguzi,iwapo hakufaulu mitihani hiyo kipindi cha nyuma .

(b) Mitihani ya kuongeza tija kwa Polisi, Daraja la II

Kuwepo na ufaulu kwa Wakaguzi wote ili kupanda daraja kwa

Wakaguzi Wasaidizi.

ANGALIZO: Mitihani ya kuongeza tija kwa Polisi, Daraja la I, ni nyongeza katika mitihani iliyofanywa wakati wa mafunzo ya Mkaguzi Msaidizi yaliyofanyika Chuo cha Polisi Dar-es salaam.

(c) Mtihani wa Kiswahili Kigumu Daraja la chini:

(i) Wakaguzi wote Wasaidizi lazima wafaulu Mtihani wa Kiswahili Kigumu Daraja la chini isipokuwa endapo watakuwa wamefaulu mtihani wa Kiswahili katikt kidato cha Nne au inayofanana na hiyo na awe na Cheti husika

Mtaala wa Mtihani na Madaraja ya Ufaulu

(A) Mtihani wa kuongeza tija kwa Polisi ,Daraja la I:

7 (a) Kutakuwa na mitihani minne,kama ilivyo hapo chini : -

(i) Makosa ya JinaiCriminal : Watahiniwa wajiandae kujibu maswali yanayohusu uwezo wa Polisi katika kuingia,Kukagua,kupekua na kukamata kwa mujibu wa Sheria kama ilivyoelekezwa na Katiba,Sheria ya Jeshi la Polisi na Sheria ya Mwenendo wa Jinai Sura ya 20 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002,na maswali ya jumla katika sheria zifuatazo :

Sheria ya Usalama Barabarani ,sura ya 168 kama ilivyofanyiwa mapitio.2002

Sheria ya Vileo, Sura. 77 kama ilivyofanyiwa mapitio 2002

Sheria ya Uchunguzi wa Vifo, Sura. 24 kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Biashara za Mkononi

Sheria ya Madawa na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa, Sura. 95 kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Kuwaondosha Watu Waiotakiwa , Sura ya. 39 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka. 2002.

Sheria ya Uchawi, Sura.18 kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002.

Sheria ya Kuzuia Rushwa, Sura 329 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

(ii) Mwenendo wa Jinai, kazi za Polisi na kanuni za maadili: Mtihani huu utahusisha maswali yanayohusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 na Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984,Sheria ya Mwenendo w amakosa ya Jinai,Sura ya 20,Sheria ya Watoto na Vijana,Sura 13,Sheria ya Polisi na Wasaidizi wa Polisi,Sura ya 322 na Kanuni za Utendaji kazi za Polisi.

(iii) Ushahidi: Mtihani huu utahusu sheria ya Ushahidi,Sura ya 6,kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

(iv) Utawala: Mtihani huu utahusu Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi.

(v)Viwango vya Kimataifa na Mikataba kuhusu utendaji wa kazi za Polisi.Mtihani huu utahusisha maswali ya maadili ya Umoja wa Mataifa kwa Maafisa wasimamizi wa sheria na Kanuni za Msingi za Umoja wa Mataifa katika matumizi yanguvu na silaha kwa Maafisa wasimamizi wa sheria.

(b) Hakuna kitabu cha kiada kitakacho ruhusiwa kuingia nacho wakati wa mitihani.Mtihani wa kuongeza tija kazini utafanyika kwa mwaka katika mwezi Julai.Mtihani ya ndani itafanyika kwa maandalizi yatakayofanywa na Mkuu wa Chuo cha Polisi Dar-es-salaam .

(c) Viwango vya ufaulu wa Mitihani ni: -

(i) UFAULU: Daraja la I - Asilimia 50 ya alama zote za Mtihani, na si chini ya asilimia 40kwa kila Mtihani .

(ii) UFAULU WA JUU: Daraja la 1 – Asilimia 75 ya alama zote za Mtihani,, na si chini ya asilimia 60 kwa kila Mtihani.

(d) Mtahiniwa atakayeshindwa katika somo moja anaweza kuruhusiwa, na Inspekta Jenerali , kufanya, kufanya mtihani unaofuata,katika somo ambalo hakufaulu.

(B) Mtihani wa kuongeza tija kwa Polisi ,Daraja la II:

(a) Kama ilivyo katika daraja la I, maswali yanaweza kuandaliwa kwa kuzingatia sheria yeyote kama zilivyo orodheshwa kwenye kiambatanisho “A”.

(b) Viwango vya ufaulu wa Mitihani ni:

(i) UFAULU: Daraja la II – Asilimia 60 ya alama zote za Mtihani, na si chini ya asilimia 50kwa kila Mtihani .

(ii) UFAULU WA JUU: Daraja la II – Asilimia 80 ya alama zote za Mtihani,, na si chini ya asilimia 65 kwa kila Mtihani.

(c) Mtihani wa Kiswahili kigumu daraja la chini:

Kama ilivyo kwa Kwa Maafisa.

Sehemu ya III – Mitihani ya askari wa vyeo mbalimbali

8. Mitihani, iliyopo kwa askari wa vyeo mbalimbali nje ya sifa za mafunzo ni:-

(A) Mtihani wa kuongeza tija kwa Polisi ,Daraja la I:

Mtihani wa kuongeza tija kwa Polisi ,Daraja la,1,itafanywa na askari

wote wa vyeo mbalimbali isipokuwa mtahiniwa atatakiwa kuthibitishwa na Kamanda wa Mkoa anakofanyia kazi ambaye inamlazimu athibitishe kwamba mtahiniwa amefikia kiwango cha elimu cha kuridhisha na anauelewa wa sheria kumwezesha kufanya Mtihani huo.

(B) Viwango vya Mitihani kwa askari wa Uongozi mdogo:

(a) Mtihani huu ,utafanywa na askari wote wa cheo cha chini na Makopolo,unatoa nafasi zaidi kwa askari wa vyeo vya chini wa vyeo mbalimbali kufikiriwa kuchaguluwa kuhudhuria mafunzo ya kupandishwa cheo. Kufaulu mtihani sio sifa pekee ya kumfanya askari ateuliwe kwenda kuhudhuria mafunzo ya kupandishwa cheo katika Chuo cha mafunzo ya Polisi Moshi,ila yatasaidia kuboresh nafasi yake ya kuteuliwa kupandishwa Cheo.

(b) Mtihani utaandaliwa kwa askari wa vyeo mbalimbali wenye sifa sawa na kidato cha nne kwenye lugha ya Kiingereza.

(c) Kutakuwa na mitihani miwili:

(i) Kanuni ya adhabu, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria ya watoto na Vijana,Sura ya . 13 na Ushahidi wa awali.

(ii) Kazi za polisi na kanuni za maadili kuhusiana na Kanuni za kudumu za Jeshi la Polisi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, sura ya. 2 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

(d) Viwango vya ufaulu vitakuwa alama 50 lakini alama za ufaulu zitakazopatikana katika mitihani hiyo miwili zitaandikwa katika faili binafsi za mhusika na kuchapishwa katika amri za Jeshi .

Sehemu ya IV – Kanuni za jumla kwa Maafisa wasimamizi

9. Maafisa wasimamizi wa mitihani ya Polisi wataongozwa na Kanuni zifuatazo: -

(a) Afisa msimamizi atateuliwa katika kila kituo ambako mtihani utfanyika.Anaweza kuwa Afisa wa Polisi aliyetangazwa katika Gazeti la Serikali,Afisa Tawala ,au Afisa mwenye sifa zinzofanana na hizo katika moja ya ofisi za Umma.

(b) Mtihani utafanyika katika vituo mbalimbali katika tarehe iliyopangwa. Mitihani itafanywa katika utaratibu unaofaa katika siku

kama ilivyopangwa na mtahini.Muda uliopangwa kumaliza kila mtihani hautaongezwa.

(c) Wakiwa kwenye mtihani watahiniwa watapangwa kwa kutofautiana umbali wa futi sita.

(d) Vifuatavyo vitatolewa: Saa,Karatasi, karatasi ya kufutiakalamu ya risasi, kalamu ya wino ,wino na pini .

(e) Bahasha za Mitihani zilizofungwa na lakiri hazitofunguliwa na msimamizi hadi muda uliowekwa kwaajili ya mtihani wa somo husika utakapofika na utafunguliwa tu mbele ya watahiniwa.

(f) Karatasi za mitihani zitagawanywa na zilizokamilika zitakusanywa na Afisa Mtahini katika muda uliopangwa;hata hivyo maaaaatahiniwa yeyite atakayemaliza mtihani kabla muda uliopangwa ataukabidhi kwa Afisa Mtahini.

(g) Afisa Msimamizi anaweza kuamua kutoa muda kabla ya kuanza kwa Mtihani kwa watahiniwa kusoma maswali na kuuliza jambo lolote linalohusu usahihi wa mtihani.Maswali mengine hayatajibiwa.

(h) Vitabu vya Kiada havitaruhusiwa isipokuwa tu pale ambapo vimeainishwa katika masharti ya Mitihani,kwa mfano Mitihani ya sheria .Mtahiniwa yeyote atakayekutwa katika chumba cha Mitihani akiwa na kitabu chochote kile cha Kiada,au kunakili Mitihani kutoka kwa Mtahiniwa mwingine,au kuruhusu Mitihani yake kunakiliwa au kujaribu kutoa au kupokea msaada wa aina yeyote,atakuwapoteza sifa.

(i) Watahiniwa hawaruhusiwi kufanya mawasiliano na na chumba cha mtihani kinatakiwa kuwa kimya.

(j) Isipokuwa katika mitihani ya juu ya umaili wa Kingereza,Watahiniwa watatakiwa waandike majina yao kwa ufasaha juu ya kila karatasi ya majibu .Makaratasi yote yatakayotumika katika chumba cha mtihani yataunganishwa pamoja wakati makaratasi ya mtihani yanakabidhiwa kwa Msimamizi .

(k)Mjibu ya maswali yote yataandikwa kwa karamu ya wino (isipokuwa michoro naexcept na maumbo yanaweza kuandikwa kwa karamu ya risasi)

(l) Mtahiniwa hatatakiwa kutoka kwenye chumba cha mtihani isipokuwa pale atakapo kabidhi mitihani yake kwa Afisa Msimamizi.Pindi mtahiniwa atakapokabidhi mtihani na kutoka,hatoruhusiwa tena kuingia ndani ya chumba cha mtihani hadi muda utakapokwisha.Mtahiniwa hatoruhusiwa kutoka katika chumba cha mtihani ndani ya nusu saa tangu muda wa kuanza mtihani .

(m) Afisa msimamizi wa mtihani atakuwepo kwenye chumba cha mtihani muda wote.

(n) Kwa kila mwisho wa somo kwenye mtihani Afisa msimamizi atahakikisha kwamba majina ya watahiniwa yameandikwa kwa usahihi katika mitihani yote na kuifunga ndani ya bahasha. Bahasha itatunzwa ikiwa imefungwa kwa lakiri na kuandikwa kama ifuatavyo : -

(i) Somo

(ii) Kituo

(iii) Saini ya Afisa Msimamizi

(o) Kila bahasha itakuwa na orodha ya majina ya watahiniwa ambao mitihani yao imo humo . Orodha hiyo itasainiwa na Afisa Msimamizi. Karatasi zingine hazitawekwa ndani ya bahasha.

(p) Afisa Msimamizi atahakikisha kwamba bahasha zote zipo salama kwa nje na kufungwa kwa lakiri na atazituma kwa njia ya kifurushi kupitia Posta kwa Afisa mtahini kwa haraka iwezekanavyo baada ya kumaliza mitihani hiyo.

(q) Wakati wa kumaliza mtihani, Afisa msimamizi atatuma kwa Afisa Mtahini uthibitisho unaoonesha kanuni za mtihani zilizingatiwa, na kwamba alikuwepo muda wote wakati wa mtihani na hakuna mtahiniwa aliyepata msaada wakati wa mtihani.

(r) Kanuni (f) mpaka (k) zitasomwa kwa watahiniwa wotekabla ya kuanza kwa mtihani.

(s) Kwa mtihani wa umaili wa Kingereza utaratibu wa kufuatwa umetolewa katika maelekezo,ambayo hutolewa pamoja na karatasi za mitihani.

KIAMBATANISHO A

(Kwa P.G.O. 45)

Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka ya WilayaDist) , Sura ya. 287

Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Wanyama , Sura ya. 154 Kama ilivyofanyiwa mapitio.

2002

Sheria ya Silaha na Risasi, Sura ya. 223 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Watoto na Vijana, Sura ya. 13, Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Filamu na Maonesho, Sura. 230 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Madawa na Uzuiaji wa Usafirishaji Harmu wa Madwa, Cap. 95 R.E. 2002

Sheria ya Forodha (Utawala na Kodi) , Sura. 403 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Madini, Sura.123 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Milipuko, Sura.45 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Kuwaondosha watu wasiotakiwa, Sura. 39 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama Pori, Sura 283 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Wakimbizi wakosaji , Sura. 57, Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya kubadilishana watuhumiwa, Sura 368 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Shera ya Ushirikiano Katika Maswala ya Makosa ya Jinai, Sura.254 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Uwindaji, 2003

Sheria ya Wafuadhahabu na Wafuafedha, Sura 228 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya (Kudhibiti)Moto Mbugani , Sura. 135 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya barabara Kuu, Sura. 167 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Uhamiaji, Sura. 54 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Utafiti wa KIfo, Sura. 24 Kama ilivyofanyiwa mapitio.

2002

Sheria ya Vileo, Sura 77 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Minada, Sura. Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheri ya Utabibu na Kinywa , Sura. 152 Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Sheria ya Afya ya Akili, Sura. 98 kama ilivyofanyiwa mapito mwaka 2002.

Sheria ya Bima ya vyombo vya Moto, Sura. 169 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002

Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura. 47 Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Sheria ya (Uzuiaji) uwekaji rehani , Sura. 175 Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Shera ya Mafuta ya Petroli (Utafiti na Uzalishaji) Sura. 328. Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Shera ya Mafuta ya Petroli (Uhifadhi) , Sura. 392 Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Sheria ya Madawa na Sumu, Sura 219 Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Sheria ya Polisi na Polisi Wasidizi, Sura. 322 Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Sheria ya Wakosaji Waangaliwa, Sura 247 Kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Sheria ya Kanuni za Utumishi, Sura. 385 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Miongozo ya Utumishi wa Umma jinsi inavyoathiri Jeshi la Polisi.

Sheria ya Mitumba na Vyuma Chakavu , Sura. 354, Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Jamii, Sura ya. 337 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya kuzuia Wizi wa Mifugo, Sura ya .265 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria za Mahakama, Sura ya .11 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Miji, Sura ya . 101

Sheria ya Miji (Kuwaondosha watu wasiohitajika) [Sura. 104]

Sheria ya Mahusiano sehemu ya Kazi na Ajira , 2004

Sheria ya ya Leseni za Biashara, Sura. 208 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Usalama Barabarani, Sura. 168 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Uchawi, Sura ya. 18 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Watu Fukala, Sura. 389

Sheria ya Vivuko, Sura ya . 173 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Kuzuia Rushwa, Sura. 329 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

Sheria ya Mizani na Vipimo, Sura. 340 Kama ilivyofanyiwa mapitio. 2002

PGO 46

HATI ZA UTAMBULISHO.

1. Hati ya Utambulisho (F.P. 178 kwa “Maafisa waliotangazwa katika Gazeti la Serikali na Wakaguzi” na F.P. 23 kwa Askari wa vyeo mbalimbali”) Ikiwa na picha ya mmiliki na saini ,na upande wa kushoto itawekwa alama ya kidole gumba kama mmiliki ni askari wa vyeo mbalimbali, vitatolewa kwa Maafisa wote waliotangazwa katika gazeti la serikali na Wakaguzi na askali wa vyeo mbalimbali wanaofanya kazi idara ya Upelelezi.

2. Afisa yeyote wa Polisi aliyepewa hati ya utambulisho atatembea nayo muda wowote,awapo kazini na anapokuwa mapumziko ,na ni lazima achukuliwe hatua za kinidhamu endapo atapoteza au kukutwa hana hati hiyo .

3. Makamanda watahakikisha kwamba askari wote wanaofanya kazi katika himaya zao wamepewa Hati za Utambulisho kama ilivyoainishwa katika aya ya 1.

4. Afisa Mnadhimu,Makao Makuu ya Polisi, anawajibika na utoaji wa Hati hizo kwa Maafisa waliotangazwa katika Gazeti la Serikali na Wakaguzi ,na atatunza kumbukumbu za Hati zilizotolewa .Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai atatoa Hati za Utambulisho kwa Wapelelezi waliopo chini ya himaya yake.Kumbukumbu zitatunzwa kama ilivyo hapo juu.

5. Picha zitapatikana toka Idara ya Utambulisho na kubandikwa katika kila hati katika mahali husika .Ganda pamoja na picha vitapigwa mhuri na mamlaka husika.

6. Maombi ya Hati ya Utambulisho kwa Maafisa waliotangazwa katika Gazeti la Serikali na Wakaguzi yatatumwa kwa Afisa Mnadhimu na Makamanda, na kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kwa wanaofanya kazi Idara ya Upelelezi.

7. Utolewaji wa Hati za Utambulisho na mtililiko wa namba lazima viandikwe katika karatasi ya vifaa ya mmiliki ,kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Jehi la Polisi namba 167.

8. Hati za Utambulisho zitakaguliwa na Maafisa waliotangazwa katika Gazeti la Serikali wakati wa ukaguzi rasmi.Hati za Utambulisho zinazohitaji kubadilishwa au picha mpya ni budi zirejeshwe kwa mamlaka iliyotoa.

9. Askari yeyote aliyepewa Hati ya Utambulisho ni budi aitoe pale atakapotakiwa kuthibitisha kwamba yeye ni polisi.

10. Hati ya Utambulisho itachukuliwa na kurejeshwa kwa afisa aliyeitoa,yaani i,Afisa Mnadhimu ,Makao Makuu ya Polisi, au Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai the ,pala ambapo mmiliki atakuwa :-

(a) amafukuzwa ; au

(b) amehamishwa toka Idara ya Upelelzezi wa Jinai kwenda kufanya kazi za kuvaa sare za Jeshi(kazi za kawaida).

PGO - 47

UKAGUZI RASMI WA MAOFISA.

1. (a) Mikoa yote na Vikosi vyote vitakaguliwa mara kwa mara kama ilivyoainishwa katika amri hii.

(b) Mikoa na vikosi vyake vitakaguliwa anaglau mara moja kwa mwaka na mkaguzi mkuu au wawakilishi wake.

(c) Kila kituo na kikosi ikiwa ni pamoja na majengo ,viwanja, magari,vifaa vingine poja na askari waliopo au waliopangiwa hapo watakaguliwa rasmi na maafisa kwa mujibu utaratibu huu. -

Afisa anayekagua	Kikosi kinachokaguliwa	Muda wa ukaguzi
(a) Makamanda wa polisi wa mikoa	Vituo vyote, kikosi cha kutuliza ghasia, na askari wote walioko katika himaya zao.	Kila robo mwaka.
(b) Wakuu wa polisi wa wilaya.	Vituo vyote ndani ya wilaya zao.	. Kila mwezi
(c).Wakuu wa vikosi vya kutuliza ghasia.	Vikosi vyote vya kutuliza ghasia Tanzania.	Kila baada ya miezi sita.
(d)Wakuu wa vikosi vya kutuliza ghasia wa mikoa.	Vikosi vyote vya kutuliza ghasia vya mikoa.	Kila mwezi
(f) Kamanda wa kikosi cha reli	Kikosi chote	Kila robo mwaka

(g)Mkuu wa chuo cha mafunzo .	(i) .Chuo cha mafunzo (ii) .Kikosi cha mbwa na Farasi.	.kila mwezi.
(h)Mkurugenzi wa musiki	Bandi zote	Kila robo ya mwaka
(i) Wana maji	Kikosi cha wana maji	Kila robo ya mwaka.
(j)Usalama barabarani	Kikosi chote	Kila robo ya mwaka
(k) Kikosi cha afya.	Kikosi chote	Kila robo ya mwaka
(l) Viwanja vya ndege	Kikosi chote	Kila robo ya mwaka
(m) Kikosi cha anga	Kikosi chote	Kila robo ya mwaka
(n)Kikosi ca mawasiliano	Kikosi chote	Kila robo ya mwaka
(o)Polisi TAZARA	Kokosi chote	Kila robo ya mwaka

(Angali pia para ya 19 kwa hatua za D.C.I., C.S.O., O/C., D.M. and D.O.M.)

2. Taarifa za awal za ukaguzi nilazima zitumwe katika jedwari la ukaguzi la vituo .Ukaguzi mdogo wa dharura utakaofanyika kwa vipindi na maofisi wlioko safarini hautahesabika kama ukaguzi rasmi.Maofisa watakao fanya ukaguzi huo watakagua Silaha zilizoko kituoni narisasi,vitabu na watuhumiwa walioko mahabusu.

3. Ukaguzi rasmi ni lazima ufanywe kwa kiwango cha umakini mkubwa.Lengo kuu ni kubaini mapungufu na kuya \rekebisha.Maafisa wakaguzi wawaelimishe askari kwa mapungufu yote waliyoyabai.ni na namna ya kurekebisha mapungufu hayo.

22. (a) Tabia ya kuigwa/Mfano inastahili kutolewa kwa mtumishi aliyefanya kazi sio chini ya miaka 12, ambaye hajawahi kufanya makosa makubwa kwa idadi iliyoorodheshwa hapa chini katika muda wa utumishi wake na ambaye hana makosa katika vipindi vilivyoainishwa hapa chini-

Muda wa utumishi (miaka)	*idadi ya makosa yaliyoingizwa*	*miaka aliyofanya bila makosa*
12 na chini ya 15	1	7
15 na chini ya 18	2	8
18 na kuendelea	2	8

Kosa la ulevi lisiwe zaidi ya moja. Kwa afisa mwenye utumishi wa miaka 18 na kuendelea, idadi ya ukomo wa makosa yatakayoangaliwa ni yale yaliyoingizwa katika miaka 16 ya mwisho ya utumishi wake.

(b) Tabia Nzuru sana itatolewa kwa-(b) Tabia Nzuru sana itatolewa kwa -

(i) Afisa ambaye tabia yake ni ya mfano, lakini hana utumishi wa kutosha kumfanya astahili kutunukiwa cheti cha tabia ya kuigwa.

(ii) Afisa mwenye utumishi wa miaka 12 au zaidi ambaye utumishi umekuwa mzuri lakini hajakidhi cheti chenye sifa ya tabia ya mfano/kuigwa.

(c) Cheti cha tabia “Nzuri” kinaweza kutolewa kwa afisa ambaye amekuwa na mtumishi mzuri lakini hajakidhi vigezo vya kutunukiwa cheti cha Tabia Nzuri Sana.

(d) Cheti cha tabia ya “Wastani”kinaweza kutolewa kwa mtumishi ambaye utumishi wake haujakidhi tathmini ya sifa ya tabia zilizotajwa hapo awali.

FOMU YA POLISI NAMBA 31 A – ALAMA ZA VIDOLE

23. (a) Wino maalum wa kuchukulia alama za Vidole utatumika wakati wa kuchukua alama za vidole katika cheti cha kuachishwa kazi, Dafari la Tabia na kadhalika. Wino unaotumika kwa mihuri haupaswi kutumika.

(b) Endapo mtumishi hajapendekezwa kuongeza mkataba wa ajira Jeshini, Taarifa fupi itajazwa katika Fomu ya Polisi namba 31A, ikieleza sababu ya pendekezo hilo, Mfano, Tabia mbaya, utendaji usioridhisha, na kadhalika.

24. Tarehe rasmi ya kuachishwa kazi ni siku inayofuata baada ya kwisha muda wake wa likizo ya kumaliza mkataba.Kwa mfano, kama Konstebo ana siku 90 za likizo ambazo zinaisha tarehe 29 Agosti, tarehe rasmi ya kuachishwa kazi ni tarehe 30 Agosti.

25. Hakuna muda wa nyongeza utakaotolewa kwa mtumishi yeyote aliyeko likizo ya kuachishwa kazi kuhusiana na usafiri kati ya mahali pa kuachishwa kazi na nyumbani kwake.

Kuachishwa kazi kada ya Ukaguzi

26. Inspekta Jeneraki wa Polisi anaweza kufuta utumishi wa Mkaguzi wa Polisi kwa maslahi umma kulingana na taratibu zilizoainishwa katika kanuni ya 67(2) ya Kanuni za Utumishi wa Jeshi la Polisi.

27. Makamanda wana wajibu wa kuhakikisha kuwa kuachishwa kazi katika kada ya Ukaguzi kunafanywa kwa kufuata taratibu zifuatazo:-

(a) Silaha zote, Risasi, zana na vifaa vyote alivyokabidhiwa vinakusanywa, na kuhifadhiwa katika ghala la karibu lililoidhinishwa

(b) Kitambulisho cha Mkaguzi kitakusanywa na kurudishwa Makao Makuu ya Polisi kwa hatua zaidi.

(c) Nyaraka zote za kuachishwa kazi zikamilishwe.

(d) Mshahara na marupurupu yote italipwa hadi tarehe ya kuachishwa kazi au hadi tarehe ambayo Mkaguzi atakuwa likizo kabla ya kuachishwa kazi. Kwa mujibu wa P.G.O.NO.55*(inaendelea.)*

Kanuni za Kudumu za Serikali Mkaguzi na Familia yake watapewa usafiri wa bure kuwafikisha sehemu yao ya Makazi.

(e) Jalada binafsi la Mkaguzi litapelekwa Makao Makuu ya Polisi kwa hatua zaidi

P.G.O - 56
TAARIFA ZA SIRI

Taarifa ya siri ya mwaka kwa kila mtumishi wa kada ya Ukaguzi na Askari wa vyeo vya chini inahitajika kutoka kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya/Kikosi. Taarifa zitapitishwa na Kamanda anayehusika ikiwa na mapendekezo yake.

2 Fomu zifuatazo ndizo zitakazotumika: -

(a) Fomu C.R.1 kwa Wakaguzi walio katika kipindi cha matazamio.

(b) Fomu C.R.2.kwa Kada ya Ukaguzi waliothibitishwa kazini.

(c) Fomu ya Polisi namba 182 kwa Askari wa Vyeo vya Chini.

3. Taarifa zote zitajumuisha mapendekezo kama anastahili au hastahili nyongeza ya Mshahara, kusitishwa au kuahirisha.

4. Idara ya Utumishi Makao Makuu ya Polisi itatuma kwa Kamanda fomu husika Miezi miwili kabla ya tarehe ya kila nyongeza ya mshahara kufanyika,ikiwa katika nakala Tatu (Nakala nne kwa fomu C.R.1). Kisha Kamanda, atapeleka bila ya kuchelewa, nakala zote kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya/Kikosi ambapo mtumishi anafanya kazi.

5. Baada ya kupokea Fomu za Taarifa ya Siri,Mkuu wa Polisi wa Wilaya/Kikosi ataweka taarifa pamoja na mapendekezo yake kuhusiana na kupewa, kusitishwa au kuahirisha nyongeza ya mshahara katika sehemu husika ya fomu na kuziwasilisha nakala zote kwa Kamanda husika. Zikiwa zimewekwa ndani ya bahasha ya siri. Kumbukumbu iingizwe katika jalada binafsi la mtumishi lililopo kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya/Kikosi ikionyesha tarehe ambayo taarifa imepelekwa kwa Kamanda.

6. Kamanda ataihakiki taarifa na kukamilisha sehemu husika ya fomu. Iwapo taarifa ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya/Kikosi inapendekeza kusitisha au kuahirisha nyongeza ya mshahara kwa mtumishi, Kamanda, kama anakubaliana na mapendekezo atamfahamisha mtumishi husika kwa maandishi, yaliyomo ndani ya taarifa, akimweleza sababu za mapendekezo ya kusitishwa au kuahirishwa huko.

7. Kisha Kamanda atawasilisha nakala zote za taarifa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa njia ya Siri pamoja na nakala ya barua aliyomwandikia mtumishi husika kama ilivyoelezwa katika aya ya 6 hapo juu. Kumbukumbu ziingizwe katika jalada binafsi la mtumishi au afisa husika lililopo katika makao Makuu ya mkoa ikionyesha tarehe ambayo taarifa imepelekwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi.

8. Idara ya Utumishi ya Makao Makuu ya Polisi itachukua hatua zifuatazo:-

(a) Kwa Wakaguzi:- Itaingiza katika fomu maamuzi kuhusiana na kulipa au itapeleka mapendekezo kwa Katibu Mkuu kuhusiana na kusitisha au kuahirisha nyongeza ya mshahara na, iwapo kusitisha au kuahirisha kwa nyongeza kumethibitishwa na Katibu Mkuu, Mkaguzi husika afahamishwe sababu za kufikia maamuzi hayo na muda wa sitisho/ahirisho hilo. Nakala moja ya fomu ya taarifa itarejeshwa kwa Kamanda husika ikiwa na maamuzi yaliyofikiwa kwa ajili ya kuhifadhiwa na Kamanda.

(b) Kwa Askari wa Vyeo vya Chini:- Itahakikisha kuwa hatua muafaka za kiutumishi zinachukuliwa kutekeleza mapendekezo ya Kamanda katika kutoa nyongeza ya mshahara na sababu na muda wa kusitisha au kuahirishwa kwa nyongeza zielezwe kwa askari wa Cheo cha Chini. Nakala moja ya fomu ya taarifa irejeshwe kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya/Kikosi kupitia kwa Kamanda kwa ajili ya kuhifadhiwa katika jalada binafsi la mtumishi husika lililopo Wilayani.

TAARIFA ZA SIRI

9. Maneno yenye utata, tungo zisizoleta maana na shutuma zisizothibitika ziepukwe katika taarifa.

10. Taarifa mbaya zinazoelezea kushindwa ambazo zinaweza kurekebishwa zielezwe kwa maafisa wahusika ili kwamba waweze kuwa na fursa ya kutosha kujirekebisha. Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa Polisi(Makao Makuu)atashughulikia taarifa zinazowahusu Wakaguzi kwa kuwaandikia barua. Kwa mujibu wa aya ya 8(b) hapo juu Kamanda atahakikisha kuwa Wakuu wa Polisi wa Wilaya/Vikosi
wanawajulishwa kwa maneno askari wa vyeo vya chini.

Nyongeza za Mishahara.

11. Nyongeza za Mishahara si jambo la moja kwa moja kwa kila mtumishi zitatolewa tu kama utendaji kazi na tabia ya mtumishi ni ya kuridhisha. Taratibu za kusitisha au kuzuia nyongeza ya mshahara kwa kipindi Fulani litafanywa kwa maafisa walioshindwa kuonyesha kiwango cha kuridhisha

katika utendaji, lakini mapendekezo hayo yasitolewe kwa mtu aliyeshindwa kuboresha utendaji kwa sababu ya kiwango chake kidogo cha elimu au uwezo mdogo wa kiakili. Taratibu za kama nyongeza isitishwe au izuiwe imeainishwa katika kanuni namba 71 ya Kanuni ya Utumishi ya Jeshi la Polisi na zinapaswa kueleweka kwa maafisa wote kuanzia Mrakibu msaidizi wa Polisi.

Kusitisha Nyongeza ya Mshahara

12. Mapendekezo ya kusitisha nyongeza ya mshahara kwa kipindi cha miezi 12 yatatolewa kwa mtumishi ambaye tabia na utendaji wake umekuwa mbaya kwa kipindi kirefu na kwa wote walioshindwa kujirekebisha pamoja na hatua iliyochukuliwa ya kuzuia nyongeza kwa kipindi Fulani.

Zuio la Nyongeza ya Mshahara

13. (a) Zuio la miezi 6 au 12 la nyongeza ya mshahara litapendekezwa kwa mtumishi ambaye tabia yake imeshuka, lakini anaonyesha mwelekeo wa kubadilika.

(b) Zuio la Nyongeza ya mshahara litapendekezwa kwa afisa aliyeshindwa kufikia viwango au vigezo Fulani vilivyowekwa na ataendelea kubakia katika utumishi hadi viwango hivyo vitakapofikiwa.

Kurejeshewa Nyongeza Iliyositishwa au Kuzuiwa

14. kila itakapofika mwisho wa zuio au sitisho la nyongeza ya mshahara, Afisa Mnadhimu (Rasilimali watu) atamtaka Kamanda kupendekeza(endapo mhusika ni mkaguzi) au atatoa maelekezo (Kwa askari wa cheo cha cgini) kama nyongeza irejeshwe, iendelee kusitishwa au kuzuiwa kwa kipindi kingine zaidi. Kisha hatua nyingine zitaendelea kwa kuzingatia aya ya 8 na 9 hapo juu.

Angalizo: (a) Kwa Wakaguzi, kushindwa kufaulu mtihani wa kufuzu wa polisi au Mtihani wa Lugha katika kipindi kilichowekwa kwa kawaida kutasababisha kusitishwa au kuzuia nyongeza ya mshahara(P.G.O. namba 45 yahusika)

(b) Uamuzi wa kupendekeza kuzuia au kusitisha ongezeko la mshahara utaachukuliwa endapo kiwango cha ufanisi cha afisa husika kimeshuka chini ya kiwango kinachotakiwa,lakini kwa maoni ya Kamanda wake anaweza

kujirekebisha. Kushindwa kujirekebisha mwenendo wake utasababisha kufukuzwa kazi kwa afisa husika chini ya Kanuni 67(2) ya Kanuni ya Utumishi ya Tume Polisi.

(c) Askari wa Vyeo Vya Chini wanaopata Posho za Ujuzi (inamaanisha madereva na askari wa Bendi) kwa kawaida posho zao zitaondolewa iwapo nyongeza zao za mshahara zimesitishwa au zimezuiwa kwa za utendaji usio na tija au nidhamu mbaya. Madhara ya adhabu ya kukatwa fedha ni makubwa. Maafisa ambao wanataka kupendekeza kuzuia au kusitisha nyongeza ya mshahara kwa hiyo ni sharti azingatie matokeo kamili ya kifedha kuhusiana na hatua alichochukua. Mapendekezo yote ya kusitisha

au kuzuia nyongeza ya mshahara kwa upekee lazima yahusishe mapendekezo ya kufidia hasara au kushusha daraja la posho maalum.
Nyangeza ya Taarifa za Siri

15. Makamanda pia wanatakiwa kuandaa taarifa za kina za siri katika mfumo wa taarifa fupi(Siyo katika fomu ya Polisi namba 182) kwa kila afisa na mkaguzi waliochini ya himaya zao ambao wamehamishiwa himaya zingine. Nakala moja ya taarifa kwa Kamanda ambako afisa amehamishiwa kwa taarifa na nakala nyingine itatumwa kwa Inspekta Jenerali. Taarifa hizi ni nyongeza ya taarifa za siri za kila mwaka kama ilivyoelezwa katika aya ya 1 hapo juu.

16. Endapo Kamanda anamwandikia Afisa au Mkaguzi aliye chini ya himaya yake, iwe kwa ni kumtunuku kwa kazi nzuri au kumpa onyo kwa tabia mbaya au utendaji usio na tija, atatuma nakala ya Taarifa kwa Inspekta Jenerali.

P.G.O - 57
TAARIFA ZA MAENDELEO

Taarifa za Maendeleo, katika utaratibu ulielezwa katika aya ya tatu hapo chini, itaandaliwa kila mwezi na Makamanda na Boharia Mkuu na Mkurugenzi wa Muziki, nakala moja itatumwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi na imfikie kabla ya tarehe 15 ya kila mwezi.

Kwa nyongeza, Wakuu wa Vikosi vya Kutuliza Ghasia wa Mikoa , na Vikosi vya Simu ya Upepo watawasilisha kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa taarifa ya maendeleo kabla ya tarehe 5 ya kila mwezi. Makamanda wa Mikoa watambatanisha nakala mbili katika taaria zao za maendeleo kabla ya kuiwasilisha kwa Inspekta Jenerali.
Taarifa za Maendeleo zitaandaliwa kwa kufuata vichwa vya habari vifuatavyo, na itaelezea kwa kina na ukamilifu mambo yote ya msingi yanayohusu taarifa inayoelezwa. Taarifa za kina kuhusu hatua zilizochukuliwa au

zilizojaribu kuchukuliwa katika kushughulikia malalamiko na mashaka yaliyojitokeza katika taarifa hizi ni sharti yafafanuliwe.
Vichwa vya Habari vya Taarifa ya Maendeleo
Taarifa ya jumla kuhusu hali ya Mkoa au Kikosi.
Taarifa ya jumla ya Watumishi.
Majengo
Matumizi ya Vifaa na Vifaa vipya vilivyopokelewa katika kipindi cha mwezi.
Hali ya Usafiri.
Hali ya Nidhamu na idadi ya Mashitaka ya Kijeshi.
Maradhi/Magonjwa.
Mahitaji alisi na Ikama iliyopo(Ikijumuisha waliofutwa kwa sababu mbalimbali)

(i) Idadi ya waliofukuzwa
(ii) Idadi ya walioachishwa kwa kukosa manufaa.
(iii) Walioachishwa kazi kwa matatizo ya kiafya.
(iv) Waliojiuzulu.
(v) Waliostaafu.
(i) Ustawi wa Jamii.
(j) Taarifa ya jumla ya makosa makubwa ya jinai, kuongezeka kwa makosa ya jinai kwa kiwango kikubwa na mmambo mengine yenye mwelekeo wa jinai- Takwimu za kina hazihitajiki.

(k) Idadi ya mikutano na mandamano yaliyozuiliwa katika mwezi uliopita na sababu za kuzuiliwa.

(l) Matatizo ya wizi wa Mifugo, pamoja na taarifa ya kina matukio makubwa, hatua za upelelezi zilizochukuliwa katika kupeleleza na kuzuia.

(m) Vituo na Vikosi vilivyokaguliwa rasmi na Kamanda wa Polisi wa Mkoa na Maafisa wengine kutoka mkoani na Makao makuu ikionyesha tarehe ya ukaguzi.

(n) Idadi ya matukio yaliyohusisha matumizi ya silaha na sababu za matumizi hayo.

PGO - 58

MUDA WA MAPUMZIKO NA MUDA WA LIKIZO

1. Askari wa jeshi la Polisi wa vyeo vya chini , ukiondoa Staff Sajenti na Sajini meja, Mkuu wa kituo na askari wengine wanaofanya kazi idara za: -
(a) Upelelezi (C.I.D)
(b) intellijensia,
(c) Kikosi cha kutuliza ghasi;

(d) Vitengo vyote vya Mafunzo ;
(e) Kitengo cha kuzuia wizi wa mifugo; na
(f) Kikosi cha polisi Bendi.

ambao wanatakiwa kufanya kazi ya ziada ya kila siku inayozidi masaa nane ya kisheria kwa mujibu wa PGO No 288, wanaweza kufidiwa kipindi cha mapumziko kilicho sawa na muda waliofanya kazi za ziada kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Agizo hili.

2. Wakati muda wa mapumziko ni makubaliano, si hakii. Muda wa mapumziko hautatolewa -
(a) katika wakati wa dharura;
(b) wakati kuna upungufu wa askari wa kutosha kwa ajili ya utendaji wa kazi;
(c) Inapohusisha doria za umbali mrefu,Oparasheni na majukumu mengine maalum ambayo kwa kawaida inazidi masaa nane.

3. (a) Muda wa mapumziko unaweza kusitishwa na mkuu wa kituo kwa muda usiozidi siku saba endapo ataona kwamba uzito wa kazi husika unalazimu kuchukua hatua hiyo. Makamanda wa Mikoa wanaweza vile vile kusitisha muda wa mapumziko katika kituo chochote kwa kipindi atakachoona kinafaa.
(b) Muda wa mapumziko haupaswi kusimamishwa bila sababu maalumu na jitihada zifznyike ili kuepuka kuchelewa lazima katika kutoa muda wa mapumziko askari polisi..Wakuu wa vikosi na wakuu wa . vituo wanapaswa kuchukua hatua chini ya kifungu cha 3 (a) kama wataridhika na muendelezo wa muda wa mapumziko kuingilia kati ufanisi wa kazi za Vituo yao.

4. Muda wa mapumziko na muda wa likizo unaweza kutolewa na wakuu wa Vituo, warakibu wasaidzi wa polisi na kuendelea (Gazeted officers) na Wakaguzi wanao kaimukwa niaba yao, kama fidia kwa ajili ya muda ziada wamekuwa kazini kwa amri ya moja kwa moja toka kwaa kiongozi wao.

5. Kwa madhumuni ya Mpango huu, mahudhurio katika Mahakama itahesabika kama wajibu, ikizingatiwa a kwamba ni lazima na ya muda mfupi iwezekanavyo. Maafisa wandamizi, na maafisa waendesha mashitaka, waatahakikisha kwamba wafanyakazi hawataruhusiwa kubaki katika mahakama wakati uwepo wao hauhitajiki tena. Kama ilivyo kawaida, wafanyakazi ambao wanaotakiwa kuhudhuria mashauri yanayoendelea mahakamani na yanayochukuwa muda mrefu hawapaswi kupewa kazi za

6. (a) Muda wa mapumziko utakuwa katika viwango vifuatazo: -

Kipindi cha kazi ya ziada	muda wa mapumziko atakao pewa:
Chini ya saa 1	Hakuna malipo.
Zaidi ya saa 1, lakini chini ya saa 1.30	Anapewa saa 1
Zaidi ya saa 1.30, lakini chini ya masaa 2	Anapewa saa1.30 .
Zaidi ya masaa 2, lakini chini ya masaa 2.30	Anapewa masaa 2

(b) Viwango hivi vitatumika sawa na vipindi vyote vya kazi ya ziada kulingana na muda uliotolewa. Katika mzingira yasiyoeleweka muda wa mapumziko utakaotolewa kwa vipindi vya ziada muda usiozidi saa moja

7. Madai ya muda wa mapumziko utashughulikiwa kama ifuatavyo: -
(a) Kila askari wa cheo cha chini ambaye kifungu namba 1kitatumika atapewa kadi ya muda wa mapumziko fomu ya polisi no 217.

(b) Wafanyakazi ambao wanaofanya kazi ya ziada wajitokeza kwa wakuu wao wa vituo kwa muda huo waloamriwa na wataomba wa wakku wao maingizo ya muda wa mapumziko katika kadi zao ppolisi fomu no 217.
(c) Wakuu wa Vituo watajiridhisha wenyewe kwaamba hiyo kazi yamuda wa ziada inayodaiwan ni ya lazima na muhimu na imefanyika kwa mujibu wa maelekezo na kama ameridhika ameridhika ataingiza na kuiandika kwa wino wa blue/wino mweusi katika kadi ya muda wa mapumziko kwa mujibu wa kifungu namba 6 hapo juu.

8. (a) Askari wa vyeo vya chini ambao wana kusanyiko la masaa nane ya muda wa mapumziko katika kadi zao wanaweza kuombasiku za likizo kutoka kwa mkuu wao wa kituo. Wakuu wa vituo: -
(i) Wataangalia maingizo kwa kila Kadi ya mapumzikona kuridhika wenyewe kwamba yameingizwa kwa utaratibu;
(ii) kuchora mstari mwekundu chini ya ingizo la kila kadi kama atakuwa ameridhika na kusanyiko lamuda wa mapumziko wa masaa .

(iii) kuamua na ni wakati gani kila mwombaji anaweza kupewa nafasi ya Muda wa likizo na kumfahamisha ipasavyo na wakati huo huo kufanya marekebisho kama kuna ulazima wa kufanya hivyo katika Kitabu cha kituo cha mahudhurio na kitabu chakuandika mwenendo wa kazi za askari wa kila siku;
(iv) Ingiza wino mwekundu kwenye kadi chini ya tarehe ya mstari mwekundu ambayo askari huyo atachukua likizo ya mapumziko.

(b) Katika hali yoyote isiyoeleweka muda wa likizo unaweza kutolewa hadi kipindi cha masaa nane.

9 (a) Si zaidi ya masaa nane muda wa mapumziko unaweza kuongezwa.
(b) Askarii ambaye tayari muda wake wa mapumzikoulishaongezwa kwa muda wa masaa nanehawezi kuongezwa tena muda wa mapumziko mpaka muda wake malimbikizo kuondolewa na mtoa ruhusa ya muda wa likizo.

10. Katika hali yoyote muda wa likizo unaweza kutolewa kwa mujibu wa ingizo la muda wa mapumziko katika kadi za muda wa likizo.Wakati huohuo inatumika katika ingizo ambalo halihitaji sahihi ya Mkuu wa Kituo.

11Mwenendo wa mashitaka ya utovu wa nidhamu yatatolewa dhidi ya askari yeyote mwenye cheo kuanzia Konstabo hadi Sajini Mejaa mbaye;

(a) Kutoa taarifa ya uongo au kutia chumvi kwa madai ya muda wa mapumziko.
(b) Kuingiza au kufuta ingizo lolotekatika kadiyake ya muda wa mapumziko, au
(c) Atakuwa amepoteza haki yake ya muda wa mapumziko katika kadi yake.
12. P.G.O. Namba 288 itasomwa sambamba na Agizo hili.

PGO - 59

UHAMISHO

WAKAGUZI NA ASKARI WA VYEO VYA CHINI

1. (A) Polisi Makao Makuu itakuwa inatoa maelekezo yote muhimu kwa wote: -

(I) Uhamisho kwa wakaguzi;

(Ii) Uhamisho wa Wakaguzi ambao walikwisha tuliwa na mkuu wa jeshi la polisi kuwa maofisa wasimamizi polisi chini ya kifungu cha 8(3) cha s Sheria ya polisi na wasaidizi Cap 322 marekebisho ya mwaka 2002

(B)Uhamisho mwingine wote wa Wakaguzi ndani himaya unaweza kupangwa na Wakuu wa Vikosi au mikoa pasipokuwepo na kumbukumbu,lakini wote lazima wajulishe Makao Makuu.

2. Kama kawaida, kundi la askari wakaguzi hawataruhusiwa kufanya kazi kwenye kituo kimoja zaidi ya miaka sita isipokuwa watakuwa ni watakuwa wamejiingiza katika kazi za kitaalamu.Wakuu wa Vikosi wata,kwa hiyo watarejea Makao Makuu ya Polisi hata kama Wakaguzin watakuwa wametimiza miaka sita ya utumishi chini ya himaya zao na watapendekeza aidha au watatakiwa kuhamishiwa mahali pengine.

3. Kundi la askari wakaguzi ambao wanafanya kazi za kawaida au kutuliza fujo kawaida watatakiwa kufanya kazi kwa miaka mitatu ndani ya wilaya hiyo au kikosi cha kutuliza fujo.Uhamisho usiokuwa wa lazima, lakini wakuu wa vikosi hawabanwi/kuzuhiliwa na uhamisho huo kwa kipindi hicho cha miaka mitatu. .

4.Kundi la askari wa vyeo vya chini wanaofanya kazi za kawaida watapaswa pia kufanya kazi kwa vipindi vifuatavyo : -

(a) Katika mkoa wowote ndani ya miaka sita mfululuzo .

(b) Katika Wilaya moja Kituo cha Daraja "B" - miaka mitatu mfululizo.

(c) Katika Wilaya moja Kituo Daraja "C" - miezi kumi na nane.

(d) Wakati wowote baada ya muda mfupi kwa miezi sita, isipokuwa kwamba katika kesi ya askari wa kuanzia cheo Koplo hadi Sajini Meja, kipindi hiki kinaweza kuongezwa kwa mwaka mmoja.

(e) Katika Vyuo vya Mafunzo ya Polisi - miaka mitatu, isipokuwa askari waliochaguliwa wanaweza kufanya kazi kwa kipindi kirefu kwa maelekezo ya mkuu wa Jeshi la Polisi.

5. (a) Kipindi cha kawaida cha utumishi kwa askari wa vyeo vya kawaida ambao wanafanyakazi za Kutuliza fFjo kitakuwa miaka mitatu,isipokuwa askari waliochaguliwa wanaweza kuhitajika kufanya kazi kwa kjipindi kirefu chiniya maelekezo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi

(b) Askari wa vyeo vya chini hawatapangwa kazi za Kutuliza Fujo mpaka wawe wametimiza angalau kipindi kimoja cha utumishi wa kazi za kawaida.

(c)Kazi za Kutuliza Fujo kwa kawaida lazima zifanywe na askari kati ya umri wa miaka 22 na 40.

(d) Askari atakayepangwa katika kikosi cha Kutuliza Fujo (FFU) kwanza atatakiwa kuhudhuria kozimafunzo katika chuo cha Polisi Moshi.
(e) Uhamisho ndani ya kitengo cha kutuliza Fujo(FFU) utapangwa na Mkuu wa Kikosi husika,lakini atatakiwa kujulisha makao makuu ya Poloisi kwa uthibitisho.

(f)Uhamisho wa kuingia na kutoka kwenye kikosi utapangwa na mkuu wa kikosi cha kutliza fujo na mkuu wa kitengo hicho kutoka makao makuu ya Polisi.

(g) Katika hali yoyote Wakuu wa Polisi wa Mikoa wanaweza kupanga uhamisho wa askari wa kutuliza Fujo pasipo kuwepo kumbukumbu ya Makao makuu ya Polisi kupitia mkuu wa kikosi cha kutuliza Fujo.

6.Askari wa vyeo vya chini watakao pangiwa katika idara za matawi ya vikosi vya simu za upepo (Signals)watatakiwa kufanyakazi hizo kwa kipindi cha miaka mitatu toka tarehe ya kuhitimu mafunzo hayo maalumu.

7. (a) Uhamisho kwa kawaida unapaswa kutekelezwa mara askari anapotoka likizo.

(b) Majina ya askari kufuatia uhamisho kutka mkoa yatatumwa na Wakuu wa Vikosi kwenda makao makuu ya Polisi miezi miwili kabla ya askari kwenda likizo .Maelekezo ya uhamisho huo kisha yatatolewa .Askari naayesafiri kwenda likizo kupitia mkoa ambao atapangiwa , kama inawezekana,atachukua tahadhari kutoka makao makuu ya polisi mkoa ambapo atakuwa anafanya kazi baada ya kutoka likizo.Hii haitahadhiri malipo ya posho kwa mujibu wa aya ya 13.

(c) Uhamisho wa ndani wa wilaya utapangwa na wakuu wa vikosi ambao watafanya wa mipangilio maalumu wakati askari anapotoka likizo.Mipangilio

ya uhamisho kwa askari kutoka na kwenda vituoni mwao utachukuliwa kwa kufuatia mazingira husika.

8. Mkuu wa chuo cha polisi atashauri makao makuu ya Polisi idadi ya askari wanafunzi wanaopaswa kujiunga na mafunzo ya uaskari katika chuo husika,akitaja na tarehe ,na siku ya kuhitimu mafunzo hayo.Maelekezo ya kupangiwa vituo vya kazi yatatolewa ndani ya kipindi hicho.

9. Hakuna askari yeyote atakaye lalamikia uhamisho kama dai la haki na uhamisho utatolewa kwa kiwango na kuzingatia umuhimu wa ufanisi na bajeti iliyopo.Kwa mamlaka ya mkuu wa Mkuu wa Jeshi la Polisi,uhamisho unaweza kutolewa kwa mazingira maalumu na manufaa ya jeshi la Polisi.

10. Uhamisho lazima utolewe na kukamilika ndani ya wiki ya kwanza ya mwezi,pale inapowezekana ndani ya Mkoa au Wilaya, lazima utolewe kwa gharama ya usafirishaji wa Jeshi la Polisi pale unapohusisha safari za kazi za kawaida za kazi za polisi .Kitabu cha huduma na jalada la askari vitapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambako askari anahamishiwa .Maelekezo ya uhamisho yatajulishwa Polisi Makao Makuu kwa kutangazwa katka gazeti la polisi pasipo kuchelewa.Afisa mhusika na kutoa uhamisho lazima aweke kumbukumbu katika kitabu cha uhamisho kwa kumbukumbu za baadaye ndani ya himaya zao.

11. (a) Askari wa vyeo vya chini waliohamishwa na wanao pitia Dar es salaam wata ripoti kufika kwao na kuondoka kwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es salaam .Hakuna malipo ya posho yatakayolipwa kwa askari hao kwa kipindi chote watakapo kuwa Dar es salaam isipokuwa kwa kumbukumbu rejea ya kufika kwao na kuondoka kwao katika kituo hicho ikionyesha kuidhinishwa kwao kutokana na maelekezo ya kupitia njia hiyo.
(b)Askari wa kundi la vyeo vya chini wanaopitia njia ya Dar es salaam wataruhusiwa kubakia Dar es salaam tu kwa kitambo kirefu kama ni lazima kupata usafiri wa kuunganisha kwenda kwenye vituo vyao vya kazi.Kutokutii amri hii, ongezeko la kutokulipwa posho zao,tatizo hilo litashughulikiwa na kitengo kinachopokea malalamiko ya utovu wa nidhamu na kutokuwepo kazini pasipo likizo.

(c)Wakuu wa vikosi wanao toa uhamisho kwa askari kupitia Dar es salaam watahakikisha kwamba amri zote hapo juu zinahalalishwa katika maelekezo

ya njia watakazopitia.

12.Wakuu wa vituo watakagua sare na vifaa vya askari kabla ya kuhamishwa kwao na kuweka kumbukumbu na mapungufu yoyoyte yakayobainishwa na kupanga jisni ya kujazilizia katika mapungufu hayo.Katika mazingira yatakiayo bainisha uzembe au matumizi mabaya , utaratibu utafanywa kwa ajili kufidia hizo gharama.Madeni ya Kanteeni ya Polisi yatatatuliwa kwa ujumla kabla kabla ya uhamisho.

13. (a) Posho ya usumbufu italipwa kwa mujibu wa agizo L.18 ya kanuni za utaratibu wa miongozo ya serikali kuhusiana na uhamisho wa askari kutoka kituo kimoja kwenda kingine,lakini siyo katika mzingira ambayo uhamisho umeamuliwa kuhusina na swala la kinidhamu au katika mazingira mengine.

(b) Posho ya kujikimu ilipwa kwa mujibu wa agizo L.3 ya miongozo ya kanuni za serikali kwa mujibu wa viiwango stahili.
(c) Posho ya usumbufu na asilimia 50 ya posho ya kujikimu zitalipwa na kituo atakachohamishiwa kufanyia kazi na asilimia nyingine 50 italipwa na himya amboko uhamisho umefanyika.

(d) Gharama zote za kusafiri zitalipwa na himaya ambapo uhamisho umefanyika.

14. Askari wa jeshi la polisi watawajibika kuhamiswa kokote ndani jamhuri ya muungano wa tanzania na watapaswa kufanyakazi katika kituo chochote kwa amri ya mkuu wa jeshi la polisi Tanzania .Wakuu wa vikosi katika vikosi maalum vya jeshi la polisi wanaweza kutoa uhamisho kwa askari wa vyeo vya chini wanaofanyakazi katka vikosi vyao,isipokuwa uhamisho wa ndani wa kazi za kawaida kwa askari na kutoka vikosi maalum utakuwa ukizingatia maelekezo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi.

MAOMBI YA UHAMISHO KWENDA VIKOSI VINGINE

15.Maombi yote ya uhamisho kwenda vikosi vingine na majibu yote matangazoyanayotoa utuzi popote pale lazima yawasilishwe kupitia mkuu wa jeshipolisi katika hatua ya awali.Mawasioliano ya moja kwa moja na vikosi vingine hayaruhusiwi.

PGO NAMBA 60

VITABU VYA REJEA

1. Suala la vitabu vya kumbukumbu itakuwa kwa mujibu wa Nyongeza "A" kwa utaratibu huu.

2. Wakuu wa Vituo / vikosi na afisa mnadhimu katika Makao Makuu ya Mikoa kuhakikisha kwamba aina na idadi ya vitabu vilivyopokelewa vitasajiliwa katika Daftari la Mali za kituo (PF 168). Hii haitahusu kwa matoleo ya mara kwa mara ya gazeti la serikali, amri za utendaji na nyaraka

3. Marekebisho ya machapisho yaliyotolewa yatafanywa na maafisa wahusika waliotajwa hapo mwanzo.

4. Kiwango cha kutoshakitakuwepo katika Vituo / vikosi na Makao Makuu ya Mikoa kwa ajili ya kuhifadhiwa na kutunza vitabu vya rejea. Vitu hivi vitakuwa vinakaguliwa na Maafisa wa Polisi wakati wa ukaguzi rasmi na kutolewa maoni inapobidi.

KIAMBATANISHO “A”

(KWA P.G.O 60)

MGAWANYO WA VITABU VYA REJEA

NYENZO ZA REJEA	Makao Makuu ya Polisi	Mkurugenzi wa	Chuo cha Polisi	Chuo cha Polisi	Kamanda Kikosi cha	Makao Makuu ya	Vituo vya Polisi			Kikosi cha Kutuliza	Masuala Binafsi
							A	B	C		
Sheria za Tanzania	1	2	2	2		3	2	1	1	1	
Mwongozo wa Sheria za polisi	1	3	20	20	1	3	2	1	1	1	1
Archibald		2	1	1		1	1				
Maelezo ya alama za vidole		2	5	5		1	2	1			
Kesi za Uchunguzi wa Kisayansi (T.T)		2	1	1		1	2	1			
Simpson Forensic Medicine	1	2	1	1		1	2			1	
Taarifa za kesi zilizoripotiwa E.A	1	1	1	1		1	1	1		1	1
Kamusi za Kiingereza/Kiswahili	1	1	2	2	1	1	1	1	1	1	
Kamusi za Kiswahili/Kiingereza	1	1	2	2	1	1	1	1	1	1	
Miongozo ya Mahakama Kuu	1	2	2	2		2	1	1		1	
Kanuni za Jeshi la Poilisi	3	3	20	20	1	2	2	1	1	1	
S.J. Amb. Kitabu cha Huduma ya kwanza	1	1	2	2	1	1	1	1	1	1	1
Mwongozo wa Kwata(drill)	1	1	4	4	2	2	1	1	1	1	
Musketry Manual	1	1	2	2	2	1	1	1	1	1	
Michoro ya alama za Barabarani	1		4	4		1	1	1	1		
Akaunt,stoo na mwongozo wa manunuzi	4	2	2	2	1	2	1	1	1	1	
Mashitaka ya Mfano			2	2		2	1	1	1	1	
Orodha ya Watumishi	4	1	1	1	1	1	1	1	1	1	
Mwongozo wa Kutuliza Ghasia	1	1	1	1	2	1	1	1	1	1	

			0	0							
Gazeti	1	1	2	2	1	2	1	1	1	1	
Vifaa vya Kisayansi vya Upelelezi wa Makosa ya Jinai			2	2		1					
Sheria za Polisi – Moriarty			13	13		1		1			
Picha Katika Kugundua Uhalifu					6	1	1	1		1	
Utaratibu wa Polisi na Utawala Moriarty		3		1	1		1	2			
Mwongozo wa Sheria ya Ushahidi kwa Askari wasio na cheo		1	2	2	1	1	1		1		
Maelezo ya alama za vidole na kiganja cha mkono		1				1	1	1	1	1	
Maswali na Majibu- Wajibu wa Polisi		1	3	3	1	1	1				
Maelekezo juu ya Kuchukuwa Alama za Vidole		1	3	3		1	1				
Kamusi ya Vyumba	3	1	4	4	1	2	1	1	1		
Taarifa ya Kesi za Tanzania	1	2	2	2		2	1	1		1	
Taarifa ya Kesi za Tanzania	2	2	2	2	2	2	2	2	2	2	
Mwangozo wa Mafunzo ya Haki za Binadamu kwa askari Polisi	3	3	50	50	3	10	10	10	10	10	
Mwongozo wa Utekelezaji wa Sheria na Haki za Binadamu za Umoja wa Mataifa No. 5 1997	2	2	5	5	2	2	2	2	2	2	
Kanuni na Maadili ya umoja wa Mataifa kwa Viongozi za Utekelezaji wa Sheria	2	2	5	5	5	5	5	3	2	5	
Kanuni za Umoja wa Mataifa kwa Viongozi kwa ajili ya matumizi ya Nguvu na Silaha za Moto katika utekelezaji wa Sheria	2	2	5	5	5	5	5	3	2	5	

* Nakala mbili ambapo kamanda wa polisi wa mkoa na mkuu wa upelelezi

wa mkoa wapo katika majengo tofauti .

PGO - 61

MARADHI, VIFO NA MAZIKO KWA ASKARI

Maradhi makubwa kwa askari.

1. Wakati askari polisi anasadikika kuwa yupo katika hatari ya ugonjwa,mkuu wa kikosi ambaye ndiye kiongozi wake,anapaswa haraka sana kumjulisha mkuu nwa jeshi la polisi na pia napaswa kuratibu mawasiliana na ndugu wa askari mgonjwa kama hawapo karibu na askari huyo.Ufahamisho huo lazima uwe unatumwa rasmi,na kila siku kama inaulazima,mpaka pale mgonjwa atakapoonekana hayupo katika hatari ya maradhi hayo.Taarifa lazima zipelekwe kwa mkuu wa kikosi kumjulisha endapo askari mgonjwa yupo chini ya uangalizi wa mke/mme wake

Taarifa ya tangazo la kifo kwa serikali au mkuu wa jeshi la polisi:
2. Kama desturi vifo vyote katika idara yoyote ya Serikali mara moja lazima mara moja itolewe taarifa kwa mamlaka husika.
3. (a) Kifo cha askari polisi kama mwajiriwa wa serikali lazima kuripotiwa kwa Inspekta Jenerali katika hatua ya awali.Taarifa hiyo ya awali lazima iambatane na ripoti ya kina kutoa maelezo yafuatayo: -

(i) Saa,tarehe, mahali na ndugu/jamaa wa karibu;

(ii) anwani kama inajulikana,ndugu/ jamaa wa karibu;

(iii) Ripoti toka kwa Mganga, kupitia mkuu wa kikosi, yanafaa kwa ajili ya mawasiliano kwa ndugu na jamaa wa marehemu, ukiondoa maelezo maumivu aliyokuwa akiwapata wakati wa maradhi;
(iv) Katika tukio la kwanza,taarifa kutoka kwa mkuu wa kikosi ambaye anawajibika kufahamisha kifa cha askari huyo.Kumbukumbu ya wasifu wa marehemu inaweza kutolewa kutokana na ufanisi wake wa kazi na hadhi

yake amboyo alikuwa nayo wakati wa uhai wake .Kama kuna jambo lolote au usia wa marehemu aliutoa kabla umauti wake kumfika unaweza kutolewa katika taarifa hiyo na utaratibu wa mazishi utakavyofanyika katika taarifa hiyo.Taarifa lazima itumwe kwa Inspekta Jenerali ambaye anaweza au kujumuisha taarifa aliyopewa kwa barua kwa ndugu zake wa karibu, au kuwaslisha taarifa kama ilivyo isipokuwa kama taarifa haitajifafanua .Uangalifu lazima uzingatiwe katika kuielezea taarifa binafsi ya barua hiyo na kumfanya mpokeaji kuwa sehemu ya watu waliopatwa na msiba huo. (v) kufahamisha juu ya mipango ya kufanywa kuhusu usimamizi wa mali za marehemu.

(b) Ripoti ya hapo juu, ambayo inapaswa kuwasilishwa bila kuchelewa, itumwe pamoja na nakala ya hati ya kuingia katika Daftari la Vifo.

(c) Ripoti kama ilivyoelezwa katika aya iliyotangulia hapo juu itakuwa samani na kusimamiwa na afisa wa askari aliyefari isipokuwa kama kifo kitakuwa kimetokea ndani ya himaya yake.
GHARAMA YA JENEZA NA MSALABA:
4. (a) Gharama zifuatazo za mazishi za kila askari wa polisi na mtumishi raia anayefanyakazi katika jeshi la Polisi zitagharamiwa na mfuko wa serikali :

(I) Jeneza;
(Ii) kaburi;
(Iii) Sanda;
(Iv) mashada ya maua;
(v) Gharama za usafiri wa mfanyakazi marehemu kutoka mahali alikofia hadi nyumbani kwa marehemu alikozaliwa au sehemu nyingine iliyoamriwa na marehemu mwenyewe kabla ya kufikwa na umauti au ndugu zake au muwakilishi wake rasmi aliyekuwa karibu naye/mwandani wake.
(b) Makao Makuu ya Polisi yatasimamaia akaunti za Benki na gharama za mazishi kwa wafanyakazi wote katika Jeshi.

HAKI ZA MAZISHI KWA JESHI**:**

5. (a) Kama mrithi atakuwa amekusudia,mazishi ya kijeshi;-lazima ,wakati wa vitendo,itafutiwa na;
(i) Askari marehemu wa Jeshi la Polisi aliyekufa akiwa kazini au wakati akiendelea na utumishi au na jeshi la Polisi au kwa mkataba kwa idara za serikali; na
(ii) Askari mstaafu aumwenye cheo zaidi ya Kamishina msaidizi wa Polisi zaidi ya ofisa ambaye alifukuzwa kazi kutoka katika utumishi wa serikali.

(b) Anaweza, kwa idhini ya Inspekta Jenerali wa Polisi kwa mujibu wa askari wa zamani wa Polisi aliyefukuzwa kazi kwa utovu wa nidhamu katika utumishi na hayatahusiana na aya ya (a) ya ibara hii.

USHIRIKI KATIKA MAZISHI YA KIJESHI.

6. Kama kibali cha dharura kitatolewa,Mkuu wa kikosi anaweza,kwa hidhini ya Inspekta Jenerali wa Polisi,kibali cha kushiriki katika mazishiya kijeshi kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 4 (a) hapo juu.

PGO NA. 81

SILAHA USAFISHAJI NA UTUNZAJI KWA UJUMLA

1 (a) Silaha zote zinazomilikiwa na kituo cha polisi na makao makuu ya mkoa zitasafishwa na kilainishi mara moja kwa wiki na kikundi cha askari wasio na cheo 1 hadi 3 (kulingana na idadi ya silaha zinazotakiwa kusafishwa) silaha zitatolewa kwa ajili ya kusafishwa na kwa kawaida na zitasafishwa ndani ya ghala la kutunzia silaha, silaha zitasafishwa pia kabla ya kufanyika magwaride, ambapo mara zote yatakaguliwa.

(b) Mwenendo uliowekwa hapo juu katika (a) pia utatumika FFU isipokuwa rifles zitasafishwa na askari mmoja mmoja waliopewa silaha hizo.

(c) Silaha zote zilizotolewa kwa ajili ya doria, ulengaji shabaha n.k zitasafishwa na kutiwa kilainishi kabla ya kuzirudisha gharani,

(d) Kila afisa atakayefyatua silaha anajukumu la kusafisha kwa namna ilivyoandikwa katika kanuni hii haraka iwezekanavyo baada ya ufyatuajikutokea.

(e) Wakaguzi na maafisa wa cheo cha warakibu wasaidizi kwenda juu wana jukumu juu ya utunzaji na usafishaji wa silaha ndogo walizopewa.

(f) Silaha zote pamoja na sterling guns, revolvers, greener guns na siginal pistols zitakaguliwa kila wiki

(g) Maada ngumu kama msasa, matambara magumu, mawe ya kuogea au

matambara yenye kuchubua hayatatumika kwa kusafishia ndani au nje ya silaha.

MATENGENEZO YA SILAHA

2 (a) Mtunza silaha mkuu atafanya kazi chini ya maelekezo ya mtunza ghala kuu na atahusika na ukaguzi na utunzaji wa silaha zote za jeshi. Atatunza na kuelekeza kazi za watunza silaha wasaidizi watakaopelekwa kwenye maghala madogo yaliyoanzishwa katika kila makao makuu ya mkoa. Watunza silaha wasaidizi watafanya kazi zao chini ya uangalizi wa karibu wa maafisa watunza ghala wa mkoa. Mtunza silaha mkuu ataendeleakukagua kama alivyoelekezwa na atatoa taarifa za utunzaji wa silaha katika mikoa yao kama ilivyoelekezwa. Watunza silaha wasaidizi watahusika na utengenezaji na marekebisho yaliyopangwa katika kiambatanisho A na watakagua na kutoa taarifa juu ya utunzaji wa silaha zote katika mikoa yao kama ilivyo elekezwa. Wtatoa taarifa ya matukio yote ya kizembe au matumizi mabaya ya silaha kwa mtunzaji silaha mkuu kupitia kwa afisa wao munzaji ghala wa mkoa wote, rekodi kazi zote katika vitabu vyao vya kazi vya kila siku. Hawatofanya kazi yoyote ya ghala la silaha au matengenezo ya silaha za watu binafsi.

(b) Kama silaha yoyote imeharibiwa au haiwezi kutengenezeka mtnza silaha msaidizi atachunguza na kama marekebisho yapo nje ya upeo wa kazi zao kama ilivyopangwa katika kiambatanisho A. Silaha mbovu zitatumwa kwa mtunza silaha mkuu ghala kuu la polisi DAR-ES-SALAAM ikiwa na statio repair card PF 164 ikionyesha ipo matengenezo au inaondolewa mikononi mwa kikosi. Kama mtunza silaha mkuu anaona kwambasilaha haiwezi kutengenezeka kwa ukamilifu atatoa taarifa kwa mkuu wa ghala ambaye atatoa silaha mbadala toka silaha silaha za akiba. Mtunza silaha mkuu kupitia kwa mkuu wa ghala ataomba taarifa maalumkuhusu uharibifu wowote ambao unaonekana umesababishwa kwa uzembe.

Rifles utunzaji na usafishaji wa kila wiki.

3. Rifle zisafishwe kila wiki kwa utaratibu ufuatao;

(a) Kagua nambari ya bolt na nambari juu ya mwili kama ziko sawa

(b) Inua kilengeo cha nyuma sukuma mbele usalama wa silaha, kandamiza chini bolt catch, vuta bolt nyuma mpaka itakapofikia, geuza kichwa cha bolt juu, chomoa bolt shusha kilengeo cha nyuma.

(c) Katamiza juu magazine catch na toa magazine

(d) Gandamiza chini upande mpana wa platform magazine mpaka upande mfinyu haupo tena mbele midomoni halafu inua platform upande mfinyu kwanza.

(e) Fungua kamba ya kuvutia ,weka kipande cha “4*2” katika kitanzi cha kati na kifunike kuzunguka kamba.

(f) Dondosha uzito wa kambaya kuvutia katika breech nyuma ya bridge chamber guide. Tua upande wa dole gumba na vuta kamba kwa mara moja. Jribu kamba isipanguse muzzle. Endeleza kuvuta hadi hadi mtutu umesafika huku ukikunja sehemu ya kitambaa iliyochafuka kaadili inavyojitokeza, halafu kwa kutumia kitambaa pakaa kilainishi tunduni kiasi, tikisa chupa ya kilainishi kiasi kabla ya kutumia.

(g) Kwa kutumia “4*2” na stiki safish safisha na kupakaa kikamilifu kidogo chamber

(h) Safisha na ondosha uchafu wote toka kwenye bolt, halafu pakaa kilainishi kidogo

(i) Safisha magazine nje na ndani, platform na spring, halafu zipakae kilainishi kidogo.

(j) Safisha nje ya rifle na breech ukitumia brush ndogo kwa ajili ya nyufa futa sehem za metal kwa kipande cha 4*2 chenye kilainishi.

(k) Ijenge upya rifle

(l) Mara moja kwa mwezi paka kilainishi cha linseed sehem yenye mbao(sio metal) ya rifle katika kivuli kwa masaa matatu halafu futa linseed iliyozidi.

4. (a) Safisha rifle kama usafishaji wa wiki isipokuwa vifuatavyo view vikavu na mbali na kilainishi mtutu, chamber, uso wa bolt, magazine platform, ndani ya magazine na kipande cha kukoki.

(b) Kaagua kwa uangalifu kuuwa kilengeo cha mbele na kilengeo cha nyuma havina uchafu kabisa na uwazi unaonekana.

(c) Kagua kama sehemu ya kutolea gesi ni safi.

Hakuna maada ngumu kama msasa, jiwe la kuogea au matambala magumu yenye kuchubua yatatumiwa kusafishia nje au ndani ya silaha.

Usafishaji baada ya kufyatua

5. (a) Fungua rifle kama usafishaji wa wiki isipokuwa vifuatavyo view vikavu na haviwezi kudondokewa kilainishi.

(b) Safisha mtutu baada ya kupoa kwa kilainishi cha oung, kulingana na maelekezo katika ibara 8-11.

(c) Safisha na pakaa kilainishi magazine na bolt na metali yote ya rifle.

(d) Ijenge upya rifle

MUHIMU

(a) Bore iwe safi, ikaguliwe na kupakwa kilainishi kila siku kwa siku kadhaa baada ya kufyatua.

(b) Kama mtutu ulio choka umeharibiwa unaweza kusafishwa kwa wire gauze mtunza silaha aliyesomea pekee atumie njia hii. Gauze iunganishwe katika funda la kwanza(First loop) kwenye kitambaa na kamba ya kusafishia, loop karibu na weight.

(c) Utunzaji wa bastora na usafishaji

6 (a) Bastora zitasafishwa kila wiki

(b) Tenganisha viwambo na safisha mtutu na 4*2 iliyofungwa kamba na kitambaa kisafi cha 4*3 halafu paka chemba kilainishi kwa kujtumia stiki na kitambaa juu yake, safisha sehem iliyobakia ya silaha na kitambaa chenye kilainishi, utoaji kilainishi uso wa bolt upewe uangalizi wa pekee, ndani ya mtiririko wa bolt hadi ejector. Safisha na magazine na kitambaa chenye kilainishi na hakikisha kuwa platform ni rahisi kujongea ndani ya sanduku la magazine.

(c) Kama silaha ni revolver ya SQW (Smith and Wesson) kunjua cylinder lakini usijaribu kuiondosha. Kwa kutumia mdeki ulipewa weka kipande cha 4*2 ndani ya jicho isukume kupitia mtutu mpaka ionekane safi kabisa.

(d) Safisha cylinder kwa njia hiyo hiyo ukitumia kipande kidogo cha kitambaa chenye kilainishi, sukuma kupitia mtutu na ubaki na kilainishi kidogo futa sehemu za nje na kitambaa chenye kilainishi kidogo.

Matumizi ya kilainishi cha young

7 (a) Changanya sehemu tatu za maji kwa sehemu moja ya kilainishi cha young na tikisa sana kabla ya kutumia.

(b) totesha kitambaa “4*2) kabisa na mchanganyikona dabala mtutu kwa kutumia mdeki au kitambaa chenye kamba ambayo itatiwa kupitiliza breech.

(c) Kausha mtutu na 482 safi

(d) Paka mafuta mtutu kwa kipande cha 4*2 kilicholoweshwa kilainishi cha young epuka kutumia kilainishi bila kupima

(e) Siku 2/3 zinazofuata kausha mtutu 4*2 na paka mafuta tena kilainishi cha young bbila mchanganyiko (kavu).

(f) Rudia usafishaji wa kawaidakwa kwa kulainisha rifle baada ya siku ya 3 ambapo itakuwa kikomo

8. Kilainishi cha young sio halisia na isitumike kama hivyo. Itumike kwa kusafishia mitutu na vinywa vya bolt tu. (Baada ya kuchemsha) na kama ikitumika vizuri na itatoa jasho karibu lote. Kilainishi cha kawaida cha rifle lazima kitumike sehemu zote zinazofanya kazi.

9. Kilainishi cha young kinachopakwa juu ya uso wowote wa metali utazuwia kutu kwa muda mrefu kwa kuwa hukauka kuwa greese ya mnato ambayo haichuruziki nje. Ni lazima kuilinda mitutu kwa kujtumia yong oil, kwa hivyo itote kabisa kabla ya kujtumia.

10. Mfuta haya ya kulainishia mitambo ni aghali na haitoharibika, haitopungua nguvu, itakapochanganywa na maji au mchanganyiko wowote ulio uliotengenezwa zaidi ya ilivyohitajika kwa hivyo itaweekwa kwa matumizi ya baadae

MAJUKUMU NA RATIBA ZA MATENGENEZO YATAYOFANYWA NA WATUNZA SILAHA WASIDIZI

1. Kukagua kwa ajili ya usafi na uhudumiaji silaha zote katika mkpoa wake.
2. Kuhesabu silaha zote katika mkoa wake
3. Kuondosha vizuizi kutoka matundu yote ya silaha katika eneo lake

4. Kulinganisha rifles,mtoko wa sriker, mgandamizo wa traiga (ugumu na ulaini) , kufungua usalama, kulainisha extractor na ejector.

5. Kufungua inavyopaswa silaha zote zilizopo kwa sriker na nati, kipande cha kifuniko, traiga na pini main sping, extractor na screw extractor, spring, mwanandani na bolt na viosheo, sahani ya kitako na screw, mkono wa juu,mkono wa chini, band screw, shivel za mkanda, gadi za mikono za mbele na nyuma, ulinzi wa kieneo cha mbele na screw, usalama na kufunga kwa na screw, spring na platform, magazine spring ya pembeni, kilengeo cha nyuma , ejector screw.

PGO 82

SILAHA - TAHADHALI ZA KIUSALAMA

Tahadhali za makabidhiano.

1.Tahadhali za usalama zifuatazo itakuwa lazima kuzingatiwa na askari wa vyeo vyote wakati wowote wa kuchukua silaha na kurejesha silaha ghalani au inapokabidhiwa kutoka kwa askari mmoja kwenda kwa mwingine(hata

kama nikwa muda tu).

(a)Bunduki

(i)Fungua boliti kabla ya makabidhiano.

(ii)Jiridhishe kwamba hakuna risasi kwenye chemba na magazine.

(b)Bastola

(i)Fungua bastola kabla ya makabidhiano

(ii)Chunguza chemba kabla ya kupokea

(c)Bunduki aina ya nusu mashini

(i)Ondoa magazine

(ii)Chunguza chemba na magazine zote kabla ya kupokea

(d)Bastola aina ya T.792

(i)Fungua bleech kabla ya makabidhiano

(ii)Chunguza chemba kabla ya kupokea,pakia na kupakua risasi.

2.Isipokuwa kwa dharura silaha zote zote za jeshi la polisi zitajazwa na kupakuliwa risasi kwenye gwaride chini ya mwongozo na usimamizi wa ofisa mwandamizi kama ilivyoelekezwa na afisa katika maelekezo haya hapa chini.

Silaha ni lazima kupakiwa na kupakuliwa risasi nje ya majengo labda tu kama itaelekezwa vinginevyo na afisa au mkaguzi wa polisi.

(a)Bunduki

(i)Kujaza achia usalama,tembeza mitambo,kamua triga na funga usalama kasha toa na jaza magazine-kwa kawaida risasi tano na pachika magazine.

(ii)Kupakua risasi,toa magazine,pakua risasi zote na pachika magazine,kasha tembeza mitambo,kamua triga…….

(b)Bastola

(i)Kupakia risasi,fungua na pakia risasi tano kwenye matundu ya chemba ukianzia na tundu la upande wa kushoto mabala na striker kasha funga bastola

(ii)Kupakua risasi, fungua bastola taratibu shika risasi na kiganja cha mkono wa kulia,kasha funga bastola.

(c)Bunduki aina ya nusu mashini

(i) Kupakia risasi,weka usalama kwenye alama ``R``fungua na toa magazine na badilisha usalama kwenda kwenye alama ``S`` kwa kutumia mkono pakia risasi 30 kwenye magazine na weka magazii kwenye hifadhi au kwenye bunduki ka itaamuliwa hivyo.

(ii) Kupakua risasi,toa magazine kwenye bunduki,weka usalama kwenye alama ``A``na tembeza

mitambo nyuma na mbele mara tatuukiwa umekamua triga.kisha toa risasi zote toka kwenye

magazine kwa kutumia dole gumba na shahada.

(d)Bastola aina ya T.792

(i) Kupakia risasi,fungua na pakia risasi kwenye chemba.Funga silaha na funga usalama (kama upo).

(ii) Kupakua risasi,fungua na toa risasi zote,kasha funga silaha na funga usalama (kama up

UTARATIBU WA KUJIUNGA NA MAFUNZO

Sehemu ya I

Shule ya Mafunzo ya Polisi Moshi
1. anwani ya Shule ya Mafunzo ya Polisi ni S.L.P 3024 MOSHI.
2. Mafunzo yataanza siku ya Jumatatu, wanafunzi wanatakiwa kuripoti chumba cha Walinzi katika Shule ya Mafunzo siku ya Jumamosi saa 3:00 asubuhi.
3 (a) Hakuna huduma ya malazi itakayotolewa na chuo kwa ajili ya wake na familia za wanafunzi.
(B) Wake na familia ya Wakaguzi na Askari wa cheo cha chini. zinaweza kuja kusalimia wakati wakiwa katika Shule ya Mafunzo, ruhusa itatolewa na Mkuu wa Kikosi. Shule ya Mafunzo haitahusika na wageni wa wanafunzi kwa hali yoyote
(C) Wakuu wa Vikosi wa Jeshi watahakikisha kuwa wanatoa fedha za kutosha kwa ajili ya familia za Wakaguzi na Askari wa cheo cha chini. wakati waume zao wakiwa mbali mafunzoni.
4 Askari wa cheo cha chini wanahudhuria Mafunzo ya katika Shule ya Polisi Shule juu ya aina yoyote ya shaka ataleta pamoja nao: -
(A) Kukamilisha Kit na mapungufu yoyote ya yaliyomo katika kadi ya marekebisho katika Maduka (Fomu ya Polisi 164).
(B) Karatasi ya Kit (Fomu ya Polisi 31D).
(C) Regista ya utumishi na nakala ya mafaili yao binafsi.
5 Silaha na risasi haziruhusiwi kuletwa na wanafunzi wanaohudhuria mafunzo katika Shule ya Mafunzo.
6 Sheria zifuatazo zitatumika kwa wanafunzi wote wanaohudhuria mafunzo katika Shule ya Mafunzo: -
(A) Wataruhusiwa kuvaa nguo za kiraia muda wa jioni baada ya mafunzo ya darasani, mwisho wa wiki na wakati hawajapangwa kazini.
(B) Hawaruhusiwi kufanya fujo na hawaruhusiwi kutoa chakula nje ya bwalo la chakula wakati wa saa za kawaida za kazi.
(C) Mwanafunzi atatakiwa kulipa huduma za bwalo, kufua na kunyoosha na duka la polisi kwa mujibu wa amri za Shule ya Mafunzo.
(D) Watatakiwa kurudisha vifaa vyote vilivyotolewa kwao wakati wanahudhuria mafunzo katika Shule ya Mafunzo ya Polisi Moshi mara watakapohitimisha mafunzo.
7 (a) Posho za kawaida zitalipwa kwa wale wote wanaostahili kupata wakati wa mafunzo.
(b) Wanafunzi wana haki ya kulipwa posho ya usafiri kwa ajili ya safari ya kwenda na kutoka Shule ya Mafunzo.
8 Magari na baiskeli hayataruhusiwa kuletwa na Shule ya Mafunzo na wanafunzi, lakini endapo afisa anataka kuleta gari lazima kupata kibali

kutoka Mkuu wa Chuo kabla ya kuwasili katika Shule ya Mafunzo.
9. Askari watakaoteuliwa kuhudhuria kozi ya udereva 'lazima kuthibitishwa kuwa timamu na Afisa Afya wa Serikali kabla ya kuhudhuria mafunzo. Askari atatakiwa kuwa na taarifa ya tabibu pamoja nae.

Sehemu ya II:

Chuo cha Polisi Dar es Salaam
10. Anuani ya Chuo cha Polisi ni S.L.P 2503, Dar es Salaam. Namba ya simu ya ofisi ya Mkuu wa Chuo cha polisi Dar es Salaam ni 022283225.
11 Kozi zote zitaanza siku ya Jumatatu. Wanafunzi wanatakiwa kuripoti kwenye ofisi ya chuo si zaidi ya masaa 12:00 jioni siku ya Jumamosi iliyotangulia.
12. Usafiri utasubiri wanafunzi wanaowasili kwa usafiri wa treni ya abiria siku watakayowasili. Maombi kwa ajili ya mahitaji mengine ya usafiri yatatakiwa kuwasilishwa kwa Mkuu wa chuo kabla ya siku ya kuwasili.
13. Hakuna huduma ya Malazi itakayotolewa kwa wake, watumishi, na familia za wanafunzi.
14. Wanafunzi wanaotakiwa kutoa ushahidi mahakamani watatakiwa kukamilisha jukumu hilo kabla ya kujiunga na kozi zao.
15 Wanafunzi kuhudhuria kozi zote katika chuo watatakiwa kuleta pamoja nao: -
(a) Sare za kutosha na vifaa;
(b) matandiko, isipokuwa mablanketi ambayo hutolewa kwa wanafunzi wa kozi ya Maafisa wanaotangazwa katika gazeti la serikali Maafisa;
(c) Regista ya Utumishi na nakala ya mafaili yao binafsi;
(d) Fomu ya Polisi namba 175 - Mapendekezo maalum kwa ajili ya kupandishwa cheo kwa wanafunzi wa Kozi ya Wakaguzi wasaidizi.
16. Silaha na risasi haziruhusiwi kuletwa na Chuo cha Polisi.
17. Sheria zifuatazo zitatumika kwa wanafunzi wote wanaohudhuria Kozi katika Chuo cha Polisi: -
(A) Wanatakiwa kufuata Amri na Maagizo ya Kudumu ya chuo.
(B) Wanafunzi wanaohudhuria Kozi ya Mkaguzi Msaidizi wanatakiwa kupata milo yao yote katika bwalo la chakula la chuo.
(C) Wanafunzi watapata malipo yao chuoni kila mwisho wa mwezi.
(D) Wanafunzi watakuwa na haki ya kupata posho ya usafiri / kujikimu kwa viwango vilivyopangwa na Serikali na utatangazwa mara kwa mara na Serikali. Posho hizi kwa kawaida zitalipwa mwishoni mwa kila mwezi.
(E) Wanafunzi wote wanatakiwa kufanya mipango yao wenyewe ya utaratibu wa kufua na kuleta kwa vifaa vya kupiga pasi pamoja nao (Pasi ya umeme inaweza kuletwa).

(F) Wanafunzi wanaweza kuleta pamoja nao vitabu vyovyote vya kiada kwa ajili ya kufanya kumbukumbu binafsi kwa ajili ya matumizi wakati wa mafunzo, lakini vifaa ya kutosha ya vitabu vya kumbukumbu vinapatikana chuoni.
18 Huduma zifuatazo zinapatikana: -
(a) Chakula kinatolewa kwa ajili ya wanafunzi juu wa Kozi Maafisa wanaotangazwa katika gazeti la serikali Maafisa ispokuwa vinywaji, sigara, nk, vinaweza kununuliwa kwa misingi ya fedha taslimu.
(b) Duka la Polisi la Chuo litatoa huduma kwa ajili ya wanafunzi wa kozi ya Mkaguzi Msaidizi, huduma hiyo itaendeshwa kwa misingi ya fedha taslimu.
(c) Wanafunzi wote wanaweza kutumia kantini ya Polisi katika kambi ya Barabara ya Kilwa ambapo mikopo yaweza kupangwa kwa masharti ya kila mwezi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Maagizo ya Kudumu ya Amri za Chuo, mahitaji yote ya kuridhisha ya vyakula yanapatikana katika duka hili la Polisi.
(d) Burudani zinapatikana kwa wanafunzi wote katika chuo ikiwa ni pamoja na mpira wa meza, boga, mpira wa wavu, mpira wa magongo, mpira wa mikono, mpira wa kikapu na mpira wa miguu, vifaa muhimu vitatolewa. Wanafunzi wanatakiwa kuja na jezi za michezo wao wenyewe.

SEHEMU YA III:

POLISI SHULE YA MAFUNZO YA ZANZIBAR

19. Anuani ya Shule ya Mafunzo ya Polisi ni S.L.P 237, Zanzibar, Tanzania. namba ya simu ni 02230256.
(D) Mkaguzi anayeshitakiwa atapewa nakala ya kuridhisha au upatikanaji wa kumbukumbu vile polisi na nyaraka nyingine kama yeye inahitaji ambayo ni muhimu katika kumwezesha kuandaa utetezi wake, zaidi ya rekodi yoyote au hati katika heshima ambayo Mkaguzi Mkuu ni ya maoni kwamba fursa inaweza kuwa alidai mbele ya mahakama.

7. Namna ambavyo kesi itasikilizwa itakuwa lazima kama ilivyo kwa mujibu wa aya ya. 23-30 ya PGO No 106.

8. Tahadhari kubwa inatakiwa kutekelezwa katika uendeshaji wa vikao vya kesi. Ni lazima ifahamike kuwa katika tukio la kukata rufaa, rekodi ya mahakama itakuwa inapitia upya mamlaka.... ya rufaa na kesi itakuwa inamapungufu kama makosa au kuachwa katika utawala wa haki na Mahakama ni wa wazi. Utaratibu uliowekwa katika Kanuni masharti ya utumishi ndani ya jeshi la polisi kufuatwa bila kupotoka.

9. (A) Wakati Mahakama ina alihitimisha usikilizaji wa itatuma kumbukumbu za uchunguzi pamoja na maamuziyake kwa kila shitaka na sababu zake na

mapendekezo ya adhabu zake kwa kamanda wa mkoa. Kamanda wa mkoa pia ataongeza maoni yake kwenye maamuzi na mapendekezo na kutuma karatasi za kesi kwa mkuu wa jeshi.

(B) Inspekta Jenerali anaweza: -
(i) kuthibitisha yote au mbadala wa matokeo kwa mahakama yoyote ya kutafuta nyingine ambayo mahakama inaweza wamewasilisha juu ya ushahidi, na yeye mwenyewe kufanya tuzo katika lazimishwa uhusiano au, kama yeye anaona kuwa hali ya kesi ni kama vile kwa hati ya kutimuliwa, anatakiwa kuripoti kesi hiyo kwa Katibu Mkuu pamoja na rekodi ya kesi zote na mwenendo mzima, na matokeo yake na mapendekezo kwa ajili ya kufukuzwa, na Katibu Mkuu anaweza kumfukuza mkaguzi au kuondoa kesi kwa Inspekta Jenerali , katika kesi ambayo Inspekta Jenerali inaweza tuzo adhabu yoyote ilivyoelezwa katika aya ya 10 na utaratibu huu; au
(ii) Aweza kutupilia mbali maamuzi yaliyofikiwa na kumuachia huru mkaguzi au kuamuru usikilizwaji kurudiwa upya.

Adhabu

10. Moja au zaidi ya adhabu zifuatazo inaweza kutolewa na Inspekta Jenerali kwa mkaguzi ambaye atakuwa amekiri au kupatikana na hatia ya kosa dhidi ya nidhamu: -
(A) faini isiyozidi kulipa mwezi mmoja;
(B) Kusimamisha au kuondoa nyongeza ya mshahara ya kila mwaka
(C) kupunguza daraja;
(D) kukaripia.

11. (A) Inspekta Jenerali atamjulisha defaulter/mkaguzi kwa maandishi ya adhabu au hatua zilizochukuliwa na barua ya kuwasilisha habari kwa kawaida kuwa aliwahi juu yake na Afisa wake wa jeshi au kwa Afisa Gazetted yeyote kwa maelekezo ya kamanda wa mkoa.
(B) Katika tukio la mapendekezo ya kuwa alifanya kwa kutimuliwa kwake, Mkaguzi kubaki chini ya uangalizi - aya. 35-40 wa P.G.O. No 106, rejea.Haki ya kukata Rufaa

12, (a) Kila mkaguzi anayo haki ya kukata rufaa dhidi ya adhabu yoyote aliyopewa ndani ya siku saba kutokana na taarifa ya adhabu yake na anaweza kukata rufaa kwa Katibu Mkuu na malalamiko, katika kuandika zenye uwakilishi wowote muhimu kwa zoezi la madaraka ya Katibu Mkuu kuhusu adhabu aliyopewa.
(b) defaulter/mkaguzi atawasilisha rufaa yake kupitia njia ya kawaida kwa

kamanda wake wa jeshi ambaye ataituma mbele yake na maoni yake kwa Inspekta Jenerali kwa ajili ya kuwasilisha kwa Katibu Mkuu.

NYARAKA
13. O / C. Wilaya na kikosi ni wajibu kwamba hatua zilizochukuliwa baada ya kesi hiyo zimekamilika ili kutekeleza adhabu. Maingizo hayawezi kufanywa katika Daftari Defaulter lakini adhabu zilizotolewa zitatangazwa katika Force orders. Adhabu yote iliyochapishwa katika force orders kumbukumbu bila kuchelewa katika nafasi sahihi juu ya Rekodi ya Huduma kadi PF 104A na katika Huduma ya Daftari PF. 104. Mwenendo wa Kesi itakuwa kubakia kwenye faili la afisa wa siri katika Makao Makuu ya Polisi.

PGO - 106

NIDHAMU –UTARATIBU WA MASHTAKA WA KIJESHI KWA ASKARAI WASIOKUWA NA KAMISHENI

Mkuu

1. (A) Amri hii hutoa utaratibu wa kufuatwa kwa wanaokiuka kutoka Maafisa wasiokuwa na Kamisheni na hukunjua sheria zilizopo, zilizowekwa katika Kanuni za Utumishi wa Jeshi la Polisi mwaka 1995.

(B) Katika Agizo hili neno " Afisa" ina maana Kamanda wa Mkoa, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai, Kamkishna wa Polisi Zanzibar, Mkurugenzi wa Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Mkuu wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia, Mkuu wa Kikosi cha TAZARA, Mkuu wa Kikosi cha Polisi Reli, Mkuu wa Kikosi cha TEHAMA, Mkuu wa Kikosi Viwanja vya Ndege, Mkuu wa Kikosi Polisi Wanamaji, Mkuu wa Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo, Mkuu wa Kikosi cha Afya, Mkuu wa Ghala Kuu la Polisi, Mkuu wa Kikosi cha Bendi Dar ea salaam, Mkuu wa Kikosi cha Mbwa na Farasi.

Washtakiwa

2. Maafisa waliotangazwa kwenye Gazeti la Serikali, Wakaguzi na Maafisa wasiokuwa na Kamisheni ni wajibu wao kusimamia nidhamu ya askari walio chini yao. Na kuhakikisha kwamba kila ripoti ya madai, na malalamiko dhidi ya mfanyakazi yeyote ni vizuri kuchunguzwa na kwamba hakuna kosa, litakaloachwa au kupuuzwa.

Mashtaka rasmi katika kesi za makosa madogo madogo si lazima yakafuata utaratibu wa Mashtaka ya Kijeshi , Maafisa Waandamizi wanaweza kukabiliana nayo. Makosa mengine yote yatafuata utaratibu wa kinidhamu na Maafisa Waandamizi watakuwa na jukumu la kushughulikia makosa hayo kwa haraka kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni C.7 ya Utumishi wa Jeshi la Polisi mwaka 1995.

3. Kila Afisa asiyekuwa na Kamisheni atakayetenda kosa au kutuhumiwa kutenda kosa kinyume na Kanuni za Utumshi wa Jeshi la Polisi(makosa yameorodheshwa katika Kiambatanisho “A”), yanaweza kushughulikiwa kama mashtaka. Utaaratibu wa mshtaka unaweza kuanzishwa ikiwa ni matokeo ya taarifa iliyotolewa na Afisa wa Polisi au mtu mwingine yeyote .

4. Kumbukumbu za mawenendo wa mashtaka ya Kijeshi ni lazima ziwe katika sehemu kuu mbili . Sehemu ya kwanza ni uchunguzi wa awali katika kosa linalodaiwa kutendeka. Sehemu ya pili ni rekodi ya ushahidi wakati kesi ikisikilizwa na Afisa aliyepewa mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

5. Uchunguzi wa awali, hata kama ni mfupi ni lazima utayarishwe ili ukweli dhahiri au uwongo wa malalamiko au madai uweze kufanyiwa tathmini na maamuzi yaweze kufikiwa kama au hapana mashtaka ya kijeshi yanaweza kuandaliwa dhidi ya mkosaji.

UANZISHWAJI WA MASHTAKA YA KIJESHI.

Malalamiko kutoka kwa raia.

6. Kila malalamiko na madai dhidi ya Afisa wa Polisi kutoka kwa raia yatachunguzwa kwa uangalifu mkubwa kwa mujibu wa PGO 103, kila kesi itajulishwa kwa Afisa anayehusika na eneo hilo na kesi kubwa atajulishwa Inspekta Jenerali wa Polisi pamoja na mapendekezo ya Afisa huyo. Na kama imeonekana kuwa kuna utovu wa nidhamu maelekezo yatatolewa ya kwamba mtuhumiwa ashtakiwe na hatua ya mwisho dhidi ya mshtakiwa itaoneshwa katika fomu ya Polisi namba 32, na nakala ya hati ya mashtaka fomu ya Polisi namba 32A. Ni muhimu kwa maslahi ya Jeshi, ukweli au uwongo wa kila madai yaliyoanzishwa yasicheleweshwe.PONDEROUS na karatasi zisizokuwa za lazima ziepukwe.

7. Kesi za kinidhamu zitachukuliwa juu ya malalamiko bila majina tu kama kuna sababu nzuri ya kuamini kwamba malalamiko ni haki.

8. Afisa yeyote wa Polisi ambaye atatuhumiwa kumshambulia raia, ni lazima taarifa ya madai hayo ifikishwe kwa Mkuu wa Polisi Wilaya, Kikosi au Kituo muda mfupi baada ya tukio kutokea. Itakapogundulika kwamba mtuhumiwa ana kesi ya kujibu juu ya shambulio dhidi ya raia, Askari huyo atashtakiwa kwa mujibu wa Kanuni ya Adhabu mbele ya Hakimu.

9. Kila lalamiko la raia dhidi ya Jeshi au mtumishi yeyote wa Jeshi ni lazima litolewe taarifa kwa Mkuu wa Polisi wa eneo husika.

Taarifa kutoka kwa Askari

10. Polisi yeyote ambaye atabaini kwamba askari Polisi mwingine ni muhusika katika kosa lililotendeka ni lazima arekodi ukweli wa msingi wa kosa(tarehe, wakati, mahali, jina lamuhalifu, na namba ya kijeshi n.k) katika kitabu cha kumbukumbu na kumpa taarifa mkosaji kwamba atajulisha kosa alilotenda. Majina na anuani za mashahidi kama inawezekana yapatikane na yaandikwe.

Askari atakayekutwa amelala kazini ikiwezekana aamshwe mbele ya mashahidi. Ushahidi wote utakaopatikana juu ya kosa hilo ni lazima urekodiwe katika fomu ya maelezo na upitishwe kwa Mkuu wa Kituo.

11. Polisi yeyote ambaye ana sababu nzuri ya kuamini ama kwa uchunguzi binafsi au kutoka chanzo chochote cha kuaminika kuwa Afisa asiyekuwa na Kamisheni ametenda kosa atatoa taarifa hiyo kwa maandishi kwa Mkuu wa Kituo husika. Ikiwezekana atatoa fomu za maelezo za mashahidi kusaidia ushahidi wake .

Hatua za Mkuu wa Kituo.

12. Mara tu Mkuu wa Kituo atakapopokea taarifa dhidi ya afisa wa Polisi bila kujali kama afisa huyo yupo chini ya himaya yake atajiridhisha

mwenyewe kwa kadri ya uwezo wake kwamba ushahidi wote umekusanywa na ndani y a masaa arobaini na nane baada ya kupokea nakala halisi za ushahidi huo atapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa uchunguzi wa awali.

Hatua za Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

13. Mkuu wa Polisi wa Wilaya lazima afanye uchunguzi wa awali bilakuchelewa na lazima ajiridhishe yeye mwenyewe kwamba vigezo vyote vya tuhuma vimepatikana na ushahidi wote uliopatikana unawekwa katika taarifa kama kumbukumbu. Iwapo kama ni lazima, yeye mwenyewe atakwenda kituo husika kufanya uchunguzi binafsi.

14. Kama anaona kuna ushahidi wa kutosha kuhalalisha hatua za kinidhamu dhidi ya mshtakiwa, ataandaa mashtaka chini ya Kanuni ya Kinidhamu ya Jeshi la Polisi. (angalia Kiambatanisho 'A') kwenye hati ya mashtaka ya Polisi namba 32 nakala ya hati ya mashitaka fomu ya Polisi nam ba 32A.

Kila shitaka lazima lianze na maelezo ya kosa yaliyowekwa katika kanuni na kufuatiwa na maelezo mafupi ya kosa halisi ambayo lazima yawe maalum katika tabia, kwa mfano;

Wewe .....ukiwa askari mwenye cheo cha chini katika Jeshi la Polisi unashitakiwa chini ya kifungu namba 5(iii) cha kanuni ya utumishi wa Jeshi la Polisi kwa kutumia lugha ya kutweza kwa Sajini Meja .....ambapo ulitamka maneno yafuatayo;.....lugha ambayo ulikusudia kumtweza Sajini Meja .....

15. (a) Kama hawezi kuandaa Hati ya Mashtaka sahihi, hivyo mashtaka yanaweza kuandaliwa au atapeleka maelezo ya uchunguzi wa awali kwa Kamanda wa Mkoa au Kikosi kwa maelekezo na baadaye anaweza kufungua mashtaka au vyenginevyo kupata maelezo mengine.

    (b) Vilevile atapeleka uchunguzi wa awali kwa Kamanda wa Mkoa au Kikosi kwa ajili ya maelekezo ambapo kamati/jopo maalum litapitia maoni na hati ya mashtaka kutoka kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

16. Iwapo ataona hakuna ushahidi wa kutosha kuchukua hatua wa kinidhamu, atamjulisha Afisa wa

    Polisi ambaye alikuwa akituhumiwa kuwa hataweza kushtakiwa. Karatasi za kesi zitaharibiwa.

17. Kama yeye atapata taarifa dhidi ya Afisa wa Polisi chini ya himaya yake , bila kuchelewa atapeleka maelezo ya kesi kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa/Kikosi ambapo Afisa huyo anafanyia kazi.

Wajibu wa Mkuu wa Kituo.

18. Kama mashtaka yameandaliwa nakala moja ya mashitaka fomu ya Polisi namba 32 na nakala mbili za fomu ya Polisi namba 32A lazima ziambatanishwe na maelezo ya kesi, fomu ya Polisi namba 32 itatumika wakati kesi inapoanza kusikilizwa na itatumika kama jalada. Mkuu wa Kituo atatekeleza yafuatayo;

    (a) Ataeleza maana halisi ya kosa kwa mshitakiwa na atahakikisha kwamba mshtakiwa ameelewa kosa lake analotuhumiwa nalo.

    (b) Atamuonya kwamba anatakiwa kukubali kosa ama kukataa kosa wakati kesi yake inasikilizwa.

    (c) Atamweleza kuwa anayo haki ya kuwaita mashahidi wowote katika utetezi wake na lazima ahakikishe wanafika ili kutoa ushahidi, iwapo kama kuna ulazima Mkuu wa Kituo atamsaidia kuhakikisha mashahidi wanafika kwa tarehe, muda na mahali ambapo kesi itasikilizwa’

    (d) Atamjulisha haraka iwezekanavyo tarehe, muda na mahali ambapo atatakiwa kuhudhuria mashitaka yake na jina la Afisa atakayesikiliza mashtaka hayo.

    (e) Atamjulisha Askari huyo kuwa anayo haki ya kuomba Afisa mwengine ambaye hatakuwa chini ya cheo chake kwa ajili ya kumsindikiza na atamsikiliza katika utetezi wakati kesi inasikilizwa.

    (f) Ataweka tarehe na hatua zilizochukuliwa hapo juu kwenye fomu ya Polisi namba 32.

Tarehe ya kusikiliza mashtaka.

19. Kila mshtakiwa ataruhusiwa angalau siku mbili toka aliposomewa

mashitaka yake ili kuandaa utetezi na kesi itasikilizwa mara moja bila kuchelewa. Kila kesi yake itaendeshwa haraka bila kuchelewa na Afisa ataendesha mashtaka hayo kwa mpangilio maalum.

Mamlaka ya kuendesha mashtaka ya kijeshi.

20. Kama kanuni ya mashtaka inavyosema, mashitaka ya kijeshi yataendeshwa na Afisa aliyetangazwa na Gazeti la Serikali chini ya maelekezo ya Kamanda wa eneo husika au atatafutwa Afisa mwengine kutoka sehemu nyingine iwapo hakuna Afisa mwingine wa kusikiliza

21. Iwapo Afisa wa Polisi aliyetangazwa katika Gazeti la Serikali atashindwa kusikiliza mashtaka ya kijeshi ndani ya muda uliopangwa , atateuliwa Mkaguzi wa Polisi ambaye atakuwa na mamlaka ya kusikiliza na kuchukua ushahidi. Baada ya kumaliza atawasilisha kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kupitia ushahidi na kutoa adhabu. Kisha atapeleka jalada hilo la mashtaka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa kwa kuthibitisha adhabu hiyo kutokana na maoni hayo.

Taratibu za usikilizaji wa mashtaka ya kijeshi.

22. Maandalizi yote ya awali kwa ajili ya kusikiliza Mashtaka ya Kijeshi ikiwa ni pamoja na mahudhurio ya wakalimani, mashahidi, washtakiwa, utafanywa na Mkuu wa Kituo cha Polisi ambapo mashtaka yamefunguliwa.

23. Kila mshtakiwa anatakiwa awe amevaa sare ya kazi na atapelekwa mbele ya Afisa anayesikiliza mashtaka yake ya kijeshi. Atasimama sawa na hatorusiwa kupiga saluti kama mwanzo au mwisho wa usikilizaji wa kesi hiyo.

24. Iwapo mshitakiwa , kabla ya usikilizwaji wa shitaka lake atamkataa Afisa anayesikiliza hiyo kwa kuamini kuwa afisa huyo ataendesha kesi hiyo kwa misingi ya ubaguzi au upendeleo, atalazimika kutoa sababu kwa maandishi kwa Afisa msikilizaji, ambaye ataahirisha kesi hiyo na kupeleka maelezo ya kesi na hoja za mshtakiwa kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa/Kikosi. Kamanda anaweza kuteua Afisa mwingine kusikiliza mashitaka hayo.

25. Afisa anayesikiliza kesi ataanza kusoma hati ya mashtaka ya kijeshi kwa mshtakiwa ,kama kuna ulazima atatumia mkalimani na atajiridhisha yeye mwenyewe kwamba mshtakiwa anaelewa mashtaka yake. Atamwambia mshtakiwa kukubaili au kukataa dhidi ya mashtaka yake na iwapo kama atakubali au kukataa Afisa huyo ataandika kama mshtakiwa amekubali au amekataa kosa katika karatasi tofauti na hati ya mashtaka ya kijeshi katika fomu ya Polisi namba 32.

26. Hati ya mashtaka inaweza kufanyiwa marekebisho au mashtaka mbadala kabla ya kesi haijamalizika katika usikilizwaji, hata kama shtaka halisi likiwa na mapungufu au nje ya utaratibu. Mabadiliko hayo yakifanyika mashtaka hayo yanaweza kusomwa upya kwa mshtakiwa. Mshtakiwa anatakiwa asomewe shtaka ambalo limefanyiwa marekebisho ili aweze kupata muda wa kuweza kuandaa utetezi wake na kuita mashahidi.

27. Kila Afisa Msikilizaji anaweza kuwaita na kuwahoji mashahidi na pia anaweza kuhitaji nyaraka zote muhimu kwa uchunguzi huo, na anaweza pia kuahiarisha kusikiliza kesi hiyo mara kwa mara.

28. Afisa anayesikiliza kesi anapaswa kuipa kipaumbele zaidi taarifa ya uchunguzi wa awali ambayo lazima iwe imepatikana na inaweza kutumika kama muongozo wa kesi na ili kupata uhakika wa mashahidi ambao huenda wakabadilika au kukataa kutoa ushahidi walioutoa wa awali wakati kesi ikiendelea kusikilizwa. Taarifa ya awali ya uchunguzi haitawasilishwa ngazi za juu wakati jalada la kesi linapokuwa limetumwa katika ngazi za juu, isipokuwa kama taarifa hiyo maelezo muhumu ili kusaidia mamlaka husika kutoa maelekezo au kufanya maamuzi ya kesi hiyo.

Kukubali kosa.

29. (a) Kama mshtakiwa atakiri kosa, Afisa msikilizaji ataandika muhtasari wa kesi na pia ataandika ushahidi wa muhusika ikiwa ni pamoja na maelezo yoyote ya awali ya utovu wa nidhamu. Pia ataendelea kuandika mambo ambayo yanamuhusu mshtakiwa aliyotoa mbele yake ili yamsaidie katika utoaji wa adhabu. Ikiwa kosa ni kubwa Afisa

msikilizaji hawezi kutoa adhabu kutokana na uzito wa kosa lilotendwa na mkosaji hivyo itampasa Afisa huyo kutuma jalada la kesi pamoja na taarifa yake kwa Kamanda wa Mkoa/Kikosi kwa ajili ya kutoa stahili na mshtakiwa lazima afahamishwe kuwa kesi yake imepelekwa ngazi za juu kwa maamuzi.

(b) Wakati wowote adhabu itakapotolewa, Afisa Msikilizaji wa kesi atamweleza mshtakiwa kama ifuatavyo;

“Unaweza kusema lolote kuhusiana na kutiwa hatiani pamoja na adhabu kabla sijatuma kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa/Kikosi kwa ajili ya uthibitisho. Chochote utakachosema kitachukuliwa kwa maandishi na kutumwa kwa Kamanda wa Polisi Mkoa/Kikosi na kuwa sehemu ya mwenendo wa mashtaka.

(c) Katika hatua hii mshtakiwa hana haki ya kukata rufaa .

Kukana kosa.

30. Iwapo mshtakiwa atakana kosa, Afisa Msikilizaji anatakiwa kufanya yafuatayo;

(a) Andika ushahidi wote uliopatikana ambao ni muhimu unaomuunganisha mshtakiwa na kosa, akianzia na ushahidi wa kwanza wa mashtaka na lazima awe makini wakati wa kuandika maelezo na asipoteze muda mwingi na nafasi kwa kuandika mambo mengi ambayo hayamuunganishi mshtakiwa na kosa. Karaatasi ya maelezo lazima ziandikwe namba kuanzia namba moja hadi nyingine katika pande zote za karatasi hizo, na asiache nafasi kati ya mstari na mstari. Ni marufuku kutumia karatasi tofauti katika kuchukua maelezo.

(b) Mruhusu mshtakiwa kufanya mahojiano kinzani na kila shahidi wa upande wa mashtaka . Kama kuna unalazima atafanya mahojiano msawazo na utaratibu huu utatumika tena kwa mashahidi wa upande wa utetezi wanapotoa ushahidi wao. Ataandika mahojiano kinzani na mahojiano msawazo au kama hakuna kitakachofuata mara tu kila karatasi ya maelezo itasainiwa na Afisa Msikilizaji.

(c) Soma maelezo ya kila shahidi na uhakikishe mshtakiwa ameelewa.

(d) Jaza majina ya mashahidi wote na maelezo yao kwa namba na mtiririko wa vielelezo vilivyopokelewa kama ushahidi katika nafasi sahihi ya fomu ya Polisi namba 32.

(e) Toa matokeo ya uchunguzi;

(i) Kama uchunguzi utabainisha kuwa kuna kosa, atamweleza mshtakiwa kama ana chochote cha kumueleza ili apunguziwe adhabu na yataandikwa kwa maandishi . Atapokea ushahidi wa tabia ya mshtakiwa yakiwemo makosa ya nyuma na adhabu alizopewa.

(ii) Iwapo matokeo ya uchunguzi yataonesha kuwa mshtakiwa "hana kosa" mshtakiwa ataachiwa na kumbukumbu zitatunzwa katika jalada la mshtakiwa.

(f) Aidha,

(i) Atatoa adha stahili iwapo ana uwezo wa kufanya hivyo. Wakati wa kutoa adhabu atamweleza mambo yafuatayo;

Je una lolote la kusema kuhusiana na matokeo na adhabu kabla sijawasilisha jalada la kesi kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa kwa uthibitisho, chochote utakachokisema kitaandikwa na kutumwa kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa pamoja na mwenendo wa kesi.

Au

(2) Peleka jalada la kesi kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa kama ilivyo kwenye aya ya 29 (a) bila kutoa dhabu kama unafikiri kuwa kesi hiyo ni kubwa au ina utata ambayo unadhani kuwa huwezi kuitolea maamuzi au adhabu.

Kamanda kuthibitisha adhabu.

31. (a) Mashtaka yote ya kijeshi lazima yapelekwe kwa Kamanda wa Poliisi wa Mkoa;

(i) Kuthibitisha adhabu, au

(ii) Kutoa adhabu iwapo Afisa Msikilizaji alishindwa kutoa adhabu kutokana na uzito wa kosa.

Kuhusiana na (i) Maofisa hapo juu wamepewa mamlaka ya kuthibitisha kuondoa, kupunguza adhabu, kufuta matokeo

yoyote ya uchunguzi au wanaweza wakaamuru mashtaka hayo yasikilizwe upya. Hawana uwezo wa kuongeza adhabu isipokuwa mshtakiwa anapewa nafasi ya kwanza kusikilizwa na Kamanda wa Polisi. (i) Anaweza kutoa adhabu yoyote iliyotajwa katika Kanuni za Utumishi wa Jeshi la Polisi C.8(2) au wanaweza kupeleka jalada la kesi kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa ajili ya kutoa adhabu. Hali hii hutokea iwapo Kamanda wa Polisi wa Mkoa amependekeza mshtakiwa apunguzwe cheo.

(b) Manaibu Kamanda wa mikoa wanaweza kutumia madaraka ya kuthibitisha adhabu kwa niaba ya Maamandaa wa Mikoa kutokana na kukosekan na kwa muda mrefu katika makao makuu yao

(c) Uamuzi wa kamanda utapelekwa haraka, bila kuchelewa kwa mshtakiwa kupitia kwa Afisa aliyesikiliza mashtaka hayo.

(d) Makamanda watachunguza kwa makini mashtaka yote ya kijeshi na kuwasilisha kwa wasaidizi wao na wataweka kumbukumbu zao a uthibitisho wa adhabu au mabadiliko ya adhabu katika nafasi sahihi ya fomu ya Polisi namba 32 na nakala zote mbili za fomu ya Polisi namba 32A. Baada ya kumaliza kupitia mashtaka hayo ya kijeshi, yatarudishwa kwa Afisa aliyesikiliza kesi hiyo na ataendelea taratibu kwa mujibu wa aya 33.

(e) Iwapo kamanda ataamuru kupitia upya kesi hiyo, atarudisha jalada la kesi kwa Afisa aliyesikiliza kesi hiyo pamoja na maelekezo yanayomtaka kusikiliza kesi yote au sehemu ya kesi hiyo na kuchukua ushahidi zaidi kama ushahidi huo ni muhimu, kwa mujibu wa utaratibu uliyowekwa katika aya 18 – 30, na kasha kuwasilisha tena mashtaka kwa kamanda wake kwa ajili ya uthibitisho, kwa mujibu wa aya 31(a).

Adhabu itathibitihwa na Inspekta Jenerali wa Polisi .

32. (a) Mashtaka yote ya kijeshi ambayo mapendekezo yake ya adhabu ni kufukuzwa kazi kwa Inspekta Jeneraki wa Polisi .

(b) Inspekta Jenerali wa Polisi ataidhinisha uamuzi wake katika fomu ya polisi namba 32 na katika nakala zote za fommu ya polisi namba 32A. Nakala moja ya fomu ya polisi, fomu ya Polisi namba 32A na nakala iliyobaki ya fomu ya Polisi namba 32A itapelekwa kwa pamoja na nyaraka zote zinazosaidia kujenga kesi hiyo kwa Kamanda. Kamanda ataweka fomu ya Polisi namba 32A katika jalada na atatuma fomu ya Polisi namba 32 pamoja na fomu ya Polisi namba 32 pamoja a nyaraka kwa Afisa ambaye awali alisikiliza mashtaka hayo pamoja na maelekezo ya kumfahamisha mshtakiwa mara moja

uamuzi wa Inspekta Jenerali wa Polisi.

Haki ya kukata rufaa.

(a) Mara Afisa anayesikiliza kesi kupokea jalada la kesi husika kutoka kwa Kamanda wake pamoja na barua ya uthibitisho au mabadiliko ya adhabu iliyoidhinishwa, atafanya yafuatayo;

(i) Atamwita mshtakiwa haraka iwezekanavyo na kumjulisha matokeo ya kesi yake na haki zake za kukata rufaa ndani ya hukumu.

(ii) Atathibitisha katika fomu ya Polisi namba 32 kwamba mshtakiwa amefahamishwa uamuzi.

(iii) .....

(iv) Iwapo mshtakiwa hataki kukata rufaa, maandalizi yatafanyika mapema katika fomu ya Polisi namba 32A itekelezwe. Kisha ataweka fomu ya Polisi namba 32 katika jalada pamoja na nyaraka za kesi katika jalada la mshtakiwa na kupeleka nakala ya mbili za fomu ya Polisi namba 32A katika Makao Makuu ya Mkoa na Makao Makuu Polisi kwa ajili ya kufungwa na kupitishwa adhabu.

(v) Iwapo mshtakiwa anataka kukata rufaa, atawasilisha maombi yake kwa maandishi ndani ya siku saba, akionesha sababu zilizopelekea kukata rufaa kwa Afisa aliyosikiliza mashtaka yake. Barua yake itakuwa na maoni yake kati ka ya fomu ya Polisi namba 32 na kupelekwa jalada kamili la mashtaka kwa kamanda wake kwa ajili ya kutoa maoni yake na kuongezwa katika fomu ya Polisi namba 32 na kupelekwa kwa Inspekta Jenerali. Adhabu yoyote iliyotolewa juu yake, itasimashwa mpaka matokeo ya rufaa yake kujulikana.

(b) (i) Inspekta Jenerali wa Polisi ataidhinisha uamuzi wake katika fomu ya Polisi namba 32 pamoja na nakala zote za fomu ya Polisi namba 32A itawekwa katika jalada ya Polisi Makao Makuu na zilizobaki zitarudishwa kwa Kamanda wa Mkoa husika.

(ii)Kamanda ataunganisha na kuweka katika faili nakala iliyobaki ya fomu ya Polisi 32Ana kutuma jalada hilo pamoja na fomu ya Polisi namba 32 kwa Afisa ambaye alisikiliza mashtaka hayo, na

(iii) Afisa ambaye anasikiliza kesi atamjulisha mshtakiwa matokeo ya rufaa yake katika fomu ya Polisi namba 32 na kuthibitisha kuwa amefanya hivyo. Halafu atandaa utaratibu wa utekelezaji wa adhabu iliyotolewa kwa mshtakiwa na ataweka katika jalada karatasi za kesi pamoja na fomu ya Polisi namba 32 katika jalada la binafsi la mshtakiwa.

(c) Rufaa zote lazima ziwasilishwe kupitia kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi na taratibu za kawaida za Polisi. Rufaa zote zitakazopokelewa na Inspekta Jenerali wa Polisi ambazo hazikuwasilishwa kwa mujibu wa taratibu husika zitarudishwa bila kufanyiwa kazi.

Interdiction form duty.

34 (a) Iwapo askari atashtakiwa kwa makosa ya jinai au kosa kubwa dhidi ya nidhamu na Mkuu wa Polisi wa Wilaya atatoa maoni yake kwamba maslahi ya umma hayamruhusu askari huyo kuendelea kufanya kazi za Polisi, atamsimamisha mara moja litele;eza wakoni wale ma atamwomba Kamanda wake apate kibali mapema kuthibitisha Interdiction. Hatua hiyo itachukuliwa katika kesi zote ambapo inaonekana kwamba kazi zitafanywa.

(b) Iwapo askari atapatikana na hatia kwa kosa la kinidhamu na imependekezwa adhabu ya kufukuzwa kazi,, atatoa taarifa kwa Inspekta Jernali wa Polisi ili amsimamishe kazi na kulipwa mshahara wake kuanzia tarehe ya mapendekezo. Atasimamishwa kazi mpaka adhabu ya kufukuzwa itakapolewa. Kama ikithibika, itapelekwa kwake, tarehe hiyo itakuwa ndiyo tarehe rasmi ya kufukuzwa kazi.

35. Maombi kwa ajili ya uthibitisho wa kutisimamishwa kazi yatafanywa kwa njia ya simu ya upepo ikiwemo tarehe rasmi ya kusimamishwa kazi pamoja na maelezo mafupi ya kosa au mashtaka. Iwapo askari wasio na Kamisheni ameshtakiwa kwa kosa la jinai, tarehe ya kusimamishwa kazi itaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe ambayo kesi ilianza kusikilizwa dhidi yake. Kutokana na kusimamishwa kazi, askari atalipwa nusu mshahara bila posho, iwapo kutajitokeza ugumu wa hali ya juu, maombi kwa ajili ya uthibitisho wa kusimamishwa kazi, ikiwemo mapendekezo ya kiwango cha mshahara kilichoidhinishwa kwa kipindi hicho.

36. Iwapo mashtaka dhidi yu askari wasiokuwa Maafisa hayasababisha kufukuzwa kazi askari atakuwa na haki, isipokuwa itakavyoelekezwa na Inspekta Jenerali wa Polisi katika mashtaka, angelipwa mshahara kamili

kama angekuwa hajasimamishwa kazi.

37. Afisa ambaye amesimamishwa kazi atandelea kusimamishwa kazi mpaka pale uamuzi wa kesi yake utakapotolewa isipokuwa vinginevyo kwa amri ya Inspekta Jnerali wa Polisi. Afisa ambaye amesimamishwa kazi hataruhusiwa kuchukuwa mkopo kantini bila idhini ya mkuu wa Polisi wa Wilaya ambaye atafanya maamuzi kulingana na uzito wa kosa ikiwa ni pamoja na majukumu ya familia husika. Hataruhusiwa kufanya kazi yoyote na atatakiwa kukabidhi vifaa vyote na mali zingine za Serikali kwa Mkuu wa Kituo.

38. Inspekta Jenerali wa Polisi ndiye mwenye mamlaka ya kumsimamisha kazi Afisa na hawezi kufuata mapendekezo kutoka kwa Makamanda wote wa Polisi na kwa kawaida yatahifadhiwa kwa ajili ya (angalia utaratibu uliyowekwa katika aya 41(a)(ii)).

39 Iwapo imeidhinishwa kusimamishwa kazi, itaoneshwa katika fomu ya Polisi namba 32.

Adhabu zilizoidhinishwa.

40. Cheo cha mshtakiwa, muda wa utumishi, utendaji wake wa nyuma, na masuala yote ya kesi yatazingatiwa kabla ya adhabu kutolewa. Askari wasiokuwa na Kamisheni wana wajibu kusimamia nidhamu ya wanatarajiwa kuonesha mfano mzuri,kwa hiyo, adhabu kali itatolewa iwapo watatenda makosa ya kinidhamu. Adhabu zilizoidhinishwa zimeoneshwa katika kanuni C.8.2 ya Kanuni ya Utumishi ya Jeshi la Polisi na hakuna adhabu nyingine yoyote inayoweza kutolewa. Kwa ujumla mfumo wa utoaji adhabu kali utaendelea kutumika na iwapo adhabu hizo zimeshindwa kuleta mafanikio ya kuzuiamakosa ya utovu wa nidhamu, mapendekezo kwa ajili ya kufukuzwa kazi yataidhinshwa na Inspekta Jenerali wa Polisi. Iwapo mshtakiwa atapatikana na hatia zaidi ya kosa moja, siyo lazima au kuamua kutoa adhabu kwa kila kosa endapo mapendekezo ya kufukuzwa kazi yametolewa.

41. Moja au zaidi yaadhabu zifuatazo zinaweza kutolewa kwa askari wasiokuwa na Kamisheni ambao watakiri au kupatikanana hatia kwa makosa ya utovu wa nidhamu ;-

(a) Kulipa faini isiyozidi siku saba

(i) Adhabu pekee iliyoruhusiwa ya kulipa fedha taslimu (ukiondoa malipo ya mali za Serikali zilizopotea au kuharibiwa) itakuwa faini ambayo inaonyesha malipo ya siku moja au zaidi na ataendelea kulipwamshahara isipokuwa

posho.

(ii) Adhabu ya mshtakiwa ya kukatwa mshahara haitafanyika mpaka adhabu hiyo itangazwe katika Amri za Kijeshi.

(iii) Hakuna mazingira yatakayo simamisha makato ya nusu mshahara wa mshtakiwa katika mwezi.

(iv)Katika hali maalum, makamanda wanaweza kuidhinisha malipo ya faini kwa awamu juu ya mapendekezo ya mahakama.

(v)Malipo yote yataingizwa katika mfuko wa Polisi wa tuzo na yatakatiwa stakabadhi ya Serikali na namba ya stakabadhi itaoneshwa marejesho ya faini ya idara.

(i) Kuzuiliwa kambini.

Kuzuiliwa kambini kwa muda usiyozidi siku saba. Kuzuiliwa kambini kutakuwa na idadi ya siku zile zilizoidhinishwa ambazo hazizidi siku saba.. askari aliyezuiliwa anatakiwa kupiga timamu katika chumba cha mashtaka au chumba cha walinzi kila baada ya masaa mawili ambayo ni kati ya saa 12:00 asubuhi hadi saa 2:00 usiku wakati hayupo kazini na mahudhurio yote lazima yaandikwe kwenye kitabu cha matukio.

(ii) Kufanya kazi za ziada kwa lazima au kwatwa,

(c) Kufanya kazi za ziada au kwata.

(i) Kufanya kazi za ziada kwa muda wa masaa manne

(ii) kila kwata ya ziada itakuwa ya muda wa saa moja na itafanyika chini ya usimamizi wa karibu. Askari asiyekuwa na Afisa hawezi kupewa adhabu ya kucheza taburu.

(d) Kazi za sulubu

Kila kazi ya sulubu itakuwa masaa mawili na itakuwa ya kukata nyasi, kufagia, kupaka rangi n.k. Askari hawezi kutumika kufanya kazi katika Idara zingine za Serikali au kwa watu binafsi. Askari asiyekuwa Afisa hawezi kupewa adhabu ya kazi za sulubu.) Kusim

(e) Kusimamisha marupurupu kwa muda.

Marupurupu ambayo yanaweza kusimamishwa kwa muda ikiwemo marupurupu ya kupumzika hayawezi kusimamishwa zaidi ya siku saba.

(i) Hakuna adhabu itakayotolewa na mahakama na kuanza

kutumika mpaka ithibitishwe na Kamanda. Kamanda anaweza kutofautiana na kuondoa adhabu iliyotolewa lakini hawezi kuongeza adhabu isipokuwa Kamanda huyo amepewa mamlaka ya kumsikilizwa mbele yake.

(ii) Kamanda anaweza kutautiana au kuondoa matokeo ya uchunguzi na adhabu iliyotolewa kwa mshtakiwa, Kamanda hana uwezo wa kutofautisha matokeo ya uchunguzi ya kutokuwa na hatia na adhabu isipokuwa Kamanda amepewa mamlaka ya kumsikiliza mbele yake.

(iii) Iwapo taarifa ya kumbukumbu zimefanyika kwa Kamanda, Kamanda anaweza kutoa adhabu moja au zaidi kama ilivyooneshwa katika aya 41)a) au badala yake, au kulazimishwa, anaweza kumfukuza au kusitisha uteuzi wa askari asiyekuwa Afisa na Afisa wa Polisi wa cheo chini.

(iv) Iwapo askari asiyekuwa Afisa atafukuzwa kazi, kwanza atashushwa cheo. Tarehe rasmi ya kufukuzwa itakuwa siku ambayo mshtakiwa amesomewa adhabu yake.

(f) Iwapo askari asiyekuwa na Kamisheni ametiwa hatiani mbele ya mahakamaya jinai kutokana na kosa, Afisa huyo atafukuzwa kazi. Maelezo yafuatayo yatatumwakwa simu ya upepo kwa Inspekta Jnerali wa Polisi yakionesha tarehe ya hukumu.

(i) Namba na jina

(ii) Kosan a kifungu cha sheria alichokiuka.

(iii) Maelezo ya mahakamailiyotoa hukumu na namba ya kesi ya jinai.

(iv) Tarehe ya hukumu

(v) Maelezo yote ya hukumu iliyotolewa.

(vi) Kupata nakala mbili za hukumu kutoka mahakamani na kuzipeleka kwa Inspekta Jenerali wa Polisi bila kuchelewa.

(vii) Iwapo kuna rufaa, matokeo ya mwisho ya rufa yatatoewa kama ifuatavyo;

Tarehe ya kutoa hukumu

Namba ya rufaa ya kesi

Matokeo kamili ya rufaa

(g) Kufukuzwa kazini kutafahamika mara tu toka tarehe ya hukumu au kuachishwa kazi na hatimaye kukata rufaa ikiwa moja ya maelekezo.

Adhabu ya kufukuzwa kazi.

42(a) Adhabu rasmi kwa ajili ya kufukuzwa kazi lazima kuwe na kumbukumbu muhimu za kuonywa kwa askari wa cheo cha chini.

(b) Adhabu ya kufukuzwa kazi itakuwa daima katika kumbukumbu za PF.32 na PF.32A katika jalada'

(c) Kama afisa wa Polisi atatenda kosa kubwa au baadhi y a makosa madogomadogo ndani ya miaka mitatu ya adhabu ya kufukuzwa kazi isipokuwa mazingira maalum ya kufukuzwa kwake.(d) Adhabu ya kufukuzwa kazi itafuatiliwa kama ushatenda kosa kubwa na kufuatia kumbukumbu za afisi ya polisi bado kama hajatenda zaidi ya miaka 3 baada ya tuzo la adhabu alishatenda kosa kubwa na kufuatia kumbukumbu za afisa wa Polisi bado kama hajatenda zaidi ya miaka mitatu bada ya tuzp la onyo.

Mashtaka dhidi ya nidhamu'

43(a) umefanywa chini ya Kanuni xs Utumishi katika jeshi la Polisi kwa kuutumia nguvu na baadhi ya makosa ya nidhamu kwa tafsiri ya mahakama na kwa ajili ya adhabu ya faini katika shilingi 400 hadi shilingi 2,000 au kiifungo cha miezi kumi na miwili kati ya miezi mitatu na miezi kumi na miwili kuadhibiwa kulingana na kosa, mashtaka hayataandaliwa chini ya kanuni hii isipokuwa makosa ya tabia mbaya au kuhakikiwa na Mkuu wa Polisi .

(b) Kamanda wa Polisi wa Mkoa atapewa taarifa mara moja kama askari yeyote wa cheo cha chini ametuhumiwa chini ya kifungu C.1(a) na wao ama ili kutolewa ndani ya masaa ishini na nne kama ameridhika kwamba upande wa mashtaka ni lazima umetoa tarifa kwa Kamishna na Utawala na Fedha kwa maashtaka kwa kuzingatia kuwa kesi za kinidhamu zitakuwa sahihi.

Makosa ya kulala ukiwa kazini.

44. (a) Katika utekelezaji wa kazi ukiwa kazini.

Afisa akiwa amelala akiwa kazini ni kosa kubwa zaidi na katika hukumu ni kama ifuatavyo;- Polisi yeyote ambaye amepatikana na hatia ya kulala akiwa kazini atachukuliwa hatua kwa mujibu wa aya ya 35 na ambayo imependekeza kwa ajili ya kufukuzwa kazi. Na vile vile askari wote watapatikana mara mbili kwa kosa la kulala akiwa kazini atafukuzwa kazi.

(b) Ulevi

Kama afisa wa Polisi atakuwa amelewa na hawezi kuwajibika itabidi afikishwe kwa Afisa wa polisi ambaye ametangazwa na gazeti la Serikali au Mkaguzi wa jeshi la Polisi ambaye atachukua kumbukumbu zake katika hali yake ya ulevi. Atafungiwa kambini au ndani ya mahabusu tupu na atakuwa chini ya ulinzi atakapata fahamu. Kama kuna uwezekano anapaswa ashtakiwe chini ya Kanuni C.19 mbele ya Hakimu, na iwapo huduma za hospitali zinapatikana,mtuhumiwa atapelekwa hospitali kwa ajili ya uchunguzi wa daktari. Kwa kesi zingine ndondogo za ulevi si mhimu kupata ushahidi wa daktari masharti ya aya ndogo (a) yatatumika sawa kwa atakayepatika na hatia ya kulewa akiwa kazini.Kulewa kupita kiasi pia ukiwa hauko kazini adhabu yake ni sawaswa na kosa la kulala kazi akiwa hana silaha.Iwapo afisa wa Polisi amelewa na vilevile amefanya kosa lingine la kinidhamu, atashitakiwa kwa kosa kubwa tu na kuwa mlevi na kushindwa kutekeleza wajibu wake.

(c) Kutoroka.

Afisa yoyote ambayeametoroka na atatenda kosa chini ya C.19(2)(c) ya Kanuni ya Jeshi la Polisi na atashitakiwa kama mtoro Jeshini.

(d) Shambulio ,vitisho au kutumia lugha ya matusi

Kumshambulia kumtisha au kumtolea lugha ya matusi afisa mwingine mwenye cheo cha juu au wakiwa na cheo sawa wakati akiwa kazini, au wakati afisa huyo anatekeleza wajibu wake anamtisha na kumshambulia afisa huyo itakuwa ni kosa na watashitakiwa ipasavyo.

(e)Kukataa amri halali uliyopewa na kiongozi wako.

Maafisa wanatakiwa kutii amri halali waliopewa na viongozi wao. Makamanda wanapaswa wafuatilie kesi zote zilizoripotiwa kwao katika himaya zao zinazohusiana na kutotii amri halali na wanakumbushwa kwamba kutotii amri halali ni kosa chini ya kifungu 124 sheria ya adhabuamabyo inasema; “ Mtu ambaye atakataa amri halali, hati au amri halali iliyotolewa na mahakama, Afisa au mtu yeyote mwenye uwezo wa umma na kuidhinishwa kwa niaba, atawajibika isipokuwa adhabu yoyote au mfumo au utaratibu wa wazi uliowekwa kuhusiana na kosa hilo, atahukumiwa kifungo cha miaka miwili jela”.

Likizo

45.(a) Hakuna askari wa Polisi na ambaye yuko chini ya uangalizi wa nidhamu au jinai kuruhusiwa kwenda likizo mpaka hatua dhidi yake ihitishwe

(b) Afisa yeyote wa Polisi anayetenda kosa kubwa la kinidhamu wakati

akiwa likizo ataitwa katika Kituo cha Polisi kilicho karibu ambapo Afisa ambaye ni wa Gazeti la Serikali na aliyepangiwa na kesi itasikilizwa bila kuchelewa na pia kesi haitaahirishwa hadi Afisa atapomaliza likizo yake.

Nyaraka.

46.Matokeo ya kesi ya mashtaka ya kijeshi yataingizwa kwenye kitabu cha makosa cha kituo hcho cha Polisi (PF.60) Kwa mujibu wa aya 49 hapa chini.

47. Adhabu zote za mashtaka ya kijeshi isipokuwa tu adhabu zilizotoewa kwa wanafunzi wa mafunzo ya awali ya polisi katika Chuo cha Polisi, yatachapishwa katika Amri ya Polisi.

48. Adhabu yote ambayo ichapishwa katika Force Order ataweka kumbukumbu bila kuchelewa katika nafasi sahihi juu ya PF.104 a kwenye kumbukumbu za kadi PF.104A.

Kitabu cha mashtaka PF.60

49(A) Kitabu cha mashtaka kitatunzwa kama ifuatavyo;-

(i) Vituo vya Polisi vyote ,Makao Makuu ya wilaya, kama vile;,TEKNOHAMA, Idara ya upelelezi,kwa madhumuni yafuatayo ;

(ii) Vikosi vyoye vya Kutuliza Ghasia

(iii) Makao Makuu ya Mkoa kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari wote ujuu ya uanzishwaji ikiwa ni pamoja na Kitengo cha Upelelezi

(iv) Vyuo vya Polisi na askari wote

(v) Kikosi cha Kutuliza Ghasia na askari wote

(vi) Polisi Makao Makuu ya mkoa kwa askari wote

(vii) Makao Makuu ya Upelelezi kwa asakari wote

(viii) Mkuu wa Bendi Dar es salaam

(ix) Mkuu wa Polisi Reli na aska4i wote Dar es salaam

(B) Kbl kussitisha kila kesi ya mashtaka ya kinidhamu matokeo yake ya mwisho yatatakiwa yaingia katika daftari la mashtaka ya kijeshi na Amri zote na idadi zote zimkatiwa katika hali husika na mstari mmojautaachwa wazi katika kila kuingiza mshtaka. Aambapo adhabu zilizowekwa ni faini/ili kulipa kwa ajili ya vitu vya mali zilizopote au kuharibiwa.Jumla ya mapato yataingizwa kwenye mstari huo.

(c) Rejista ya mashtaka ya kijrshi itakuwa inaorodheshwa katika kitabu.

Nakala haitakiwa kupelekwa Makao Makuu ya Polisi.

KIAMBATISHO “A”

Ya Kanuni za Jeshi la Polisi 106

Nguvu ya Kanuni ya Nidhamu

Orodha ya Makosa

Afisa wa Polisi atatenda makosa yafuatayo;

1. Kushawishi, kununua au majaribio ya kununua au kusaidia Afisawa Polisi au kutotoa taarifa zake kwa afisa wake’
2. Migogoro au matumizi inayotoa unyanyasaji dhidi ya Afisa wake.
3. Kutumia vitisho kwa Afisa wake
4. Ni hatia kufanya ukaidi
5. Kusababisha usumbufu katika mistari yoyote kambini au kituoni.
6. Kutojiheshimu eneo la kazi
7. Kukataa kutii amri halali ya viongozi wake.
8. Kushindwa kuzingatia amri yoyote halali aliiyopewa na kiongozi wake
9. Kushindwa kujitambua kutokana na ulevi
10. Kunywa pambe wakati ukiwa kazini
11. Kunywa pombe wakati wa kazi, au katika kambi yoyote ya Polisi kambi kubwa au Kituo au katika sare
12. Kujipa likizo
13. Kulala ukiwa kazini
14. Kuacha lindo kabla ya kutolewa isipokuwa kumkamata mhalifu yoyote ambaye una wajibu wa kumkamata.
15. Kuondoka au kutoroka chini ya ulinzi wa Polisi kabla hajaachiliwa huru na mamlaka husika.
16. Uzembe au kukataa kusaidia ukamataji wa askari yeyote anayeshtakiwa na kosa lolote wakati kuna amri halali ya kufanya hivyo
17. Uzembe umepelekea mahabusu anayekabiliwa na mashtaka ya kutoroka au abapo ni wajibu wako kumuangalia au kumlinda

18. Anatumia nguvu bila kibali
19. Kuwa mwoga
20. Kufyatua risasi bila amri au haki ya kufanya hivyo
21. Kushindwa kuhudhuria katika gwaride lolote ulilotakiwa na kiongozi wako bila sabau ya msingi.
22. Kuweka rehani,kuuza kupoteza au kuharibu kwa uzembe,kuweka mbali,uharibifu wa amakusudi au kushindwa kutoa taarifa ya uharibifu wowote wa silaha yoyote, risasi, accoutrement, wive,gari au vifaa vingine vilivyotolewa kwake u mali yoyote iliyopo katika ulinzi wake.
23. Kupatikana na mali ya umma isivyohalali,au mali yoyote ya askari, au kupatikana na mali yoyote ya mtu.
24. Kutenda kosa lolote la uporaji, au kuharibi mali
25. Kupokea na kushawishi rushwa au bakshishi.
26. Kutokuwa makini, kutokuwa mstaraabu na kuwa mgomvi .
27. Wakati wa gwaride, kuwa mchafu au uchafu wa mwili, silaha, mavazi au vifaa.
28. Kutoa taarifa bila idhini au kutoa taarifa yoyote ya uchunguzi au idara nyingine au jambo la Polisi.
29. Fanya au ishara yoyote ya taarifa ya uongo au hati.
30. Kufanya au kujihusisha na kutoa malalamiko bila kujitaja jina.
31. Maringo au kujisingizia ugonjwa wowote kwa makusudi au udhaifu
32. Tabia mbaya ya makusudi,au utovu wa nidhamu wa makusudi hospitali au mahali pengine au amri yoyote na kusababisha hali ya maradhi kuwa mbaya sana, mgonjwa kuwa dhaifu au ucheleweshaji wa tiba.
33. Kuwa na magonjwa ya zinaa au magonjwa mengine na kushindwa kutoa taarifa kwa daktari wa Serikali kwa ajili ya tiba.
34. Kujipatia deni ndani au nje ya Jeshi ambalo ameshindwa kuyalipa’
35. kuchukua kitu chochote bila idhini ya mtu binafsi au mamlaka husika.
36. Kupinga kumkamata, kumsindikiza au kumshitaki mtuhumiwa
37. Kuvunja kambi ya Polisi,kambi au makaazi wakati umezuiliwa kihalali.

38. Kutoa taarifa za uogozi wakati wa kujiunga na jeshi la Polisi.
39. Kukataa au kudharau kufafanua au kutuma taarifa yoyote au kufanya marejesho ambayo una wajibu kufanya au kutuma.
40. Kutoa mashtaka ya uongo dhidi ya askari

    Kufanya madai ya uongo dhidi ya askari
41. Kutoa malalamiko dhidi ya askari yoyote wakati ukijua kuwa taarifa hizo ni za uongo.
42. Kufanya kazi zozote bila idhini au Ofisi zaidi ya kazi za Polisi.
43. Kuwa mdhamini kwa mtu yoyote au kujishughulisha na mikopo yoyote pamoja na Afisa yoyote wa Polisi bila kibali cha Maandishi ya Inspekta Jenerali wa Polisi.
44. Kushindwa kutoa taarifa kamili ya kipato chako kwa viongozi wako.
45. Kushindwa kutii kwa makusudi kanuni na amri mbalimbali za jeshi
46. Ana hatia ya tendo lolote na tabia kutotii amri au dharau kutotekeleza utaratibu mzuri wa nidhamu ya Jeshi,au ukiukwaji wa wajibu katika ofisi yake au tabia nyingine mbaya akiwa nia askari wa Jeshi.

PGO - 107

NIDHAMU - UJEURI

1.Hakuna afisa wa polisi ama akiwa kazini au mapumzikoni anaeruhusiwa kutumia lugha ya matusi ukatili au ujeuri kwa raia yeyote,.

2. Gazzetted officers, Wakaguzi na ma-NCO wana wajibu wa kusimamia mwenendo wa tabia za maafisa walio chini ya kamandi zao na kuchukua hatua za haraka za kinidhamu dhidi ya polisi yeyote ambaye atakayetumia ukatili, kiburi au uonevu kwa raia. Matukio mabaya ya askari ni sharti yatapelekwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwaajili ya mchakato wa kufukuzwa kazi.

3. Raia yeyote hapaswi kuachwa akisubiri bila sababu yeyote katika kituo cha polisi. Wao wana haki ya kuhudumiwa haraka ipasavyo na afisa wa chumba cha mashitaka anawajibika kuhakikisha kwamba raia wanapata huduma haraka ipasavyo. Kama kucheleweshwa hakuepukiki, muhusika sharti ataarifiwe kwa lugha ya upole kwamba asubiri au arejee baadae katika urahisi wake. Hapaswi kwa namna yoyote kupuuzwa au kuendelea kusubirishwa bila kupewa taarifa kwa linaloendelea kuhusiana na jambo lililompeleka kituo cha polisi.

4. Mashahidi hawapaswi kusubirishwa kwa muda mrefu katika vituo vya polisi. Endapo raia watahitajika kutoa maelezo au kusaidia upelelezi ni lazima waelezwe muda wa kamili wa kufika na maelezo yao yachukuliwe bila kuchelewa kwa muda uliopangwa.Maafisa wa polisi wote ni.

5. Yafuatayo ni makosa makubwa kwa maafisa wa polisi: -
(A) ujeuri na tabia ya kutoa lugha ya matusi wakati wa kushughulika makosa ya usalama barabarani au wakati wa kufanya uchunguzi au ukamata.
(B) Kuchelewa, iwe kwa makusudi au vinginevyo, katika utunzaji wa taarifa, malalamiko, nk, yaliyotolewa na raia katika Vituo vya Polisi.
(C) Kushindwa kuwasaidia watu ambao wanahitaji msaada, yaani wazee au watoto wanaovuka barabara zenye msongamano.
(D) Kufafanya aina yoyote ya mbinu za uonevu.
(E) Kuendesha baiskeli au kuendesha magari kwa namna ya kutojali na ya hatari.
(F) Kuzurura ukiwa katika sare za kazi kwa namna itakayoleta usumbufu kwa wananchi.
6. polisi wanapewa mamlaka fulani maalum ili wapate kutumikia umma. Maafisa ambao watatumia vibaya mamlaka haya au kutaka kuwatisha au kuwaonea raia ni wajibu kufukuzwa kazi

PGO - 108

NIDHAMU - MICHANGO NA ZAWADI KUTOKA UMMA

1. Katika hali yoyote hakuna polisi yeyote atakayeruhusiwa kushawishi

kuchukuwa mchango au zawadi kutoka kwa raia, ama kwa ajili yake mwenyewe au kwa niaba ya Jeshi, au kwa kwa mtu yeyote yule, bila idhini ya kimaandishi ya mkuu wa Jeshi la Polisi.

2. Kama raia yeyote atahamasika kuchangia fedha au bidhaa kwa Jeshi la Polisi,anashauriwa kuandika moja kwa moja kwa Mkuu wa jeshi la Polisi kuhusiana na suala hilo.

3. Hakuna Michango au zawadi itakayo pokelewa katika kituo chochote cha polisi au ofisini, au na afisa yeyote wa polisi. Fedha au mali, kama ilitumwa kwa njia ya mkono au kwa njia ya posta, itarudishwa mara moja kwa mtoaji. Mtoaji atashauriwa kwamba anaweza kuandika moja kwa moja kwa mkuu wa Jeshi la Polisi, ambaye ndie pekee anaweza kushughulikia masuala hayo.

4. Katika hali yeyote ambapo mchango itatolewa kwa Jeshi la Polisi, au kwa askari Polisi,taarifa itafunguliwa katika kitabu cha taarifa cha kituo cha Polisi husika na ripoti fupi ya ukweli itatumwa kupitia Kamanda wa Polisi wa Mkoa husika kwenda kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi.

5. Kila mchango au zawadi itakayorudishwa kwa Mtoaji, lazima risiti ipatikane na Kuambatanishwa na taarifa iliofunguliwa katika kitibu cha taarifa cha Polisi rejea aya ya 4 hapo juu.

7. Ni marufuku kwa Maafisa wa polisi kupokea zawadi kutoka kwa raia kwa ajili yao wenyewe au kwa ajili ya familia zao. Endapo zawadi hiyo itakuwa imepokelewa itarudishwa mara Moja kwa Mtoaji,Na taarifa iliyokwisha Pokelewa na kuingizwa katika kitabu cha taarifa cha kituo husika itatatumwa kwa Kamanda wa Mkoa/kikosi.Naye kwa hiari yake anaweza kuituma kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi.

8.(a) ni marufuku kwa maafisa wa Polisi kupokea au kutoa zawadi za thamani zaidi ya zawadi ya kawaida kutoka kwa marafiki au mtu binafsi na jamaa zake iwe katika sura ya fedha, bidhaa, kusafirishiwa bidhaa bure au manufaa mengine ya kibinafsi. Amri hii itawahusu si tu kwa maafisa wenyewe lakini pia kwa familia zao na maafisa watawajibika kwa utunzaji wa familia zao.

(b) Hii ni muhimu hasa katika wale watu binafsi na makampuni ya kibiashara ambao husherehekea Krismasi, Id-el-Fitr, Id-el-Haj, Diwali, n.k kama hafla/matukio ya kutoa zawadi mara nyingi ya thamani kubwa kwa wateja wao au washirika.

kukubalika kwa zawadi hizo na afisa na familia yake, itapelekea kushusha hadhi na uadilifu katika jamii anayoishi, na kuwepo kwa uwezekano wa kuathiri imani ya umma katika uadilifu wake wakati wa kutoa huduma. Katazo hili halihusiani na zawadi zenye thamani kidogo, kama vile shajara, kalamu, nk iliyotolewa na muuza duka kwa wateja wake, kwa kawaida kama ishara ya nia njema katika hafla.

(c) Iwapo zawadi ya thamani itatumwa kwa afisa au kwa familia yake, wanapaswa kurudi mara moja kwa mtoajii, kwa maelezo kwamba kukubali zawadi hizo hairuhusiwi chini ya kanuni. Kama kurudishwa zawadi hizo itakuwa kosa na aibu, ni lazima kukabidhiwa kwa Serikali, na risiti itatolewa.

(D) Mkuu wa jeshi la Polisi anaweza kuidhinisha ufunguzi wa michango ya hiari kwa madhumuni yoyote aliona kuwa yana maslahi kwa utumishi wa umma kwa ujumla mradi tu masharti yafuatayo yamezingatiwa:
(I) michango hautakuwa nje ya huduma iliyo kusudiwa kwa jamii;
(Ii) orodha ya michango haitawekwa hadharani , ambayo huelekea kuweka kiwango cha michango haitatumika na kila msukumo wowote wa kulazimisha michango lazima iepukwe.

PGO - 109

MADENI

1. Amri za kudumu za Serikali F.11 zinasomeka kama ifuatavyo: -
(A) deni kubwa lenye usababisha aibu na fedheha, itokanayo na sababu yeyote ile itahesabika kama ukosefu wa fedha wa kijitakia unaotokana na kutokuwa makini kwa ofisa,na itapelekea kushtakiwa kwa makosa ya kinidhamu.

(B)Aibu itokanayo na madeni – inayohusu rehani na kukopa fedha katika viwango vya juu cha riba itakuwa kitachukuliwa kama kosa ambalo, litaadhiri heshima ya utumishi na uaminifu wa mtu binafsi na inaweza kuwa ni kikwazo cha kumkwamisha mtumishi kupandishwa daraja kazini au nyongeza ya mshahara wake. lolote la ukweli , atakalo kiri ofisa wa Polisi itakuwa sehemu ya maelezo yake au maelezo ya ahadi ama kwa madhumuni yake au kwa mtu mwingine, itachukuliwa kama mwelekeo ule ule. (C) Kwa kawaida, kila nafasi inayowezekana maafisa walio katika madeni watapewa ili kuwaokoa kutoka kwenye aibu ya madeni, lakini ni wazi kwamba lazima kuna kikomo ambacho afisa haiwezi kubakia katika utumishi wa umma, katika hali iwayo ile maanani inaweza kuchukuliwa ili kumuondoa kwa manufaa ya umma. Katika hali fulani, inaweza hata kuwa muhimu kufikiria kufukuzwa, lakini hatua hii itachukuliwa tu katika hali mbaya na ambapo madeni sio kigezo pekee kilichohusishwa.

(D) Iwapo afisa wa Polisi atolewa taarifa kama mdaiwa ataandikiwa barua na Katibu wake Mkuu / Mkuu wa Idara inayojitegemea au Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mkoa kumjulisha kwamba serikali inachukua mtazamo mbaya sana juu ya madeni yake na kuongeza kuwa yeye atawajibika na hatua za kinidhamu ambayo inaweza kusababisha kuondolewa katika huduma kama hatua za haraka hazitachukuliwa na yeye mwenyewe kurekebisha hali hiyo . Anapaswa, wakati huo huo, kuitwa kutoa orodha kamili ya madeni yake, iwe kama mdaiwa halisi au mdhamini, pamoja na mapendekezo yake ya kuyalipa. Kama inaonekana kuwa nafasi nzuri kwamba anaweza kuweka mambo yake katika mpangilio mzuri, atapewa nafasi ya kufanya hivyo na barua ya ziada ya onyo ataandikiwa kwamba kama atashindwa kupunguza madeni yake kama inavyotakiwa au kama atakopa madeni mapya, hatua za kinidhamu zitachukuliwa. Atatakiwa pia kuwasilisha taarifa ya robo mwaka kuonyesha hasa hali halisi ya fedha yake na kiasi ambacho kimekuwa kikilipwa kwa miezi mitatu iliyopita kufkia tarehe ambayo taarifa inawasilishwa.

(E) \iwapo afisa atakuwa mwenye madeni inahitaji kwamba hapaswi tena kutekeleza majukumu ambayo yeye angeshawishika kutumia kwa matumizi binafsi fedha za umma au vilivyohifadhiwa, inaweza kuwa muhimu

kumondoa kwa maslahi ya umma au kumuhamishia sehemu ambayo hatakutana na vishawishi. Hili wazo mbadala la baadaye si mara zote linawezekana kwa matokeo kwamba Serekali haitakuwa na chaguo bali kutaka aondolewe kwa manufaa ya umma. Afisa yeyote, kwa hiyo, mwenye kuonesha tabia hii ya kuwa na madeni lazima aonywe kwa maandishi.

2. Maafisa wakuu wa komandi watatoa taarifa kwa mkuu wa jeshi la Polisi za askari yeyote aliyepo chini ya himaya ambaye anajulikana kuwa na madeni makubwa.

3. Madeni huzaa rushwa. Hakuna Afisa wa polisi anaweza kuonekana mwaminifu kama atashindwa kulipa madeni yake. Madeni ni kikwazo katika kupandishwa cheo na hakuna afisa mwenye madeni makubwa anaweza kuwa na matumaini ya maendeleo katika Jeshi. Askari Polisi yeyote ambaye anaona mwenyewe atashindwa kulipa madeni yake atatoa haraka taarifa yake kwa Afisa wa komandi yake kupitia njia za kawaida kumtaarifu Mkuu wa Jeshi la Polisi.

4. Kila Askari wa cheo cha chini atatoa tamko la kweli na sahihi juu ya madeni yake kama alivyotakiwa na Afisa gazeti la serikali.

READ BACK	Used when sender requires message to be repeated back to him.
READABLE	Used to report signals. Means signals fairly good.
RELAY THROUGH	Used by control to instruct substation.

Proword	*Meaning*
RELAY TO	Instruction to relay a message.
REPORT SIGNAL	Used by control signal ascertain signal strengths
ROGER	Message received
ROGER ON	Message received so far. Carry on.
SAY AGAIN	Repeat all your message
SAY ALL AFTER	Repeat the message after word indicated
SAY WORD AFTER	Repeat the word after the word indicated.
SPEAKING	Used to indicate person speaking.
STANDING BY	Used by Control to indicate that Control is free to receive calls.
THROUGH ME	Send your message to me. I will clear it.
TIME SIGNAL	Am about to send a time signal.
VERIFY	Check text with originator and send correct version.
VERY WEAK	Used to report signal. Means voice communication impossible.
WAIT	Indicating a pause of a few seconds. Other stations not to interrupt.
WAIT OUT	Used by control station only, indicating wait and do not answer until I tell you.
WILCO	Instructions will be carried out.
WORD AFTER	Used when making a repetition or verification.
WORD BEFORE	Used when making a repetition or verification.
WORDS TWICE	Say every word or phrase twice, or used to indicate that every word or phrase will be sent twice. Used when conditions are difficult.
WRONG	What you have just said is wrong. The correct version is ..... Used in conjunction with read back procedure.

Proword	*Meaning*
ASSUME CONTROL	Used by Control when appointing a substation to assume control.

Reporting Signal Quality	
13.	The following prowords are to be used in describing signal quality: -

Proword	Meaning
LOUD AND CLEAR	Signal very good; perfectly readable.
READABLE	Signal fairly good; readable.
VERY WEAK	Signal very weak; voice communication impossible.
NOTHING HEARD	No signals heard.
INTERFERENCE	Used to report interference in conjunction with the words “slight” or “heavy”
DISTORTED	

Proword	*Meaning*
	Used in conjunction with the appropriate prowords.

PGO - 193
MAWASILIANO – 'TAARIFA ZA HATUA ZA HARAKA –MFUMO 'P'

1. Wakuu wa vituo wanaoshughulikia ufuatiliaji mpya wa wahalifu wanotafutwa wanawajibu kwamba taarifa yoyote waliyonayo ambayo inaweza kusaidia wahalifu kukamatwa inatumwa mara moja, ikiwezekana kwa simu au radio kwa:-

   (a) Kituo chochote cha polisi cha karibu ambacho kinaweza kuwa na nafasi ya kuwezesha kuzuiwa;

   (b) Makao makuu ya mkoa kwa wakati huohuo inapotoa maelekezo kuhusu vituo ambavyo tayari vimepewa taarifa angalia kipengele kidogo (a) hapo juu

2. Makao makuu ya mkoa tena yatakuwa na wajibu wa kupeleka taarifa kwa kituo kingine chochote ndani ya mkoa ambao waweza kushiriki vyema katika operasheni.

3. Makamanda wa polisi wa mikoa watajulisha makao makuu ya polisi, amra moja iwapo wanafikiri kwamba taarifa zinapaswa kusambazwa kwa vituo na mikoa yote au kwa mikoa na vituo Fulani. Hatua zitaendelea kwa kufuata kipengele cha 6 na kuendelea. Makamanda wa mikoa watahakikisha kwamba hatua inachukuliwa tu kwa maelekezo ya afisa muhusika.

4. Mkurugenzi wa upelelezi wa jinai anaweza kuingilia wakati wowote kwa kutoa maelekezo iwapo anafikiri kwamba udhibiti kamili au kiasi wa kioperesheni unapaswa kufanywa na makao makuu ya polisi (kama uwindaji wa kitaifa wa watu na kadhalika).

5. *Taarifa zote zitatumwa kwa radio au simu kwa kufuata vipengele* 1-4 zitajulikana kama taarifa "P"na zitakuwa zikitanguliwa na utaratibu huo.

Mtandao wa kitaifa

6. (a) Kila kituo cha makao makuu ya mkoa kitatumia kipindi cha dakika 3 (mfano. 0200 –0203) katika masafa 8010 k/cs. Aina ya utumaji taarifa MCW itatumika .

   (b) Kituo cha radio cha makao makuu ya polisi kitahifadhi saa katika mtindo 8010 k/cs. Kwa kukubali taarifa "P" isipokuwa wakati wa vipindi vya dakika 3 za kusikiliza .

(c) Wakati wa kuanza kwa kipindi cha usikilizaji cha masaa kituo cha radio cha makao makuu ya polisi kitarusha kwa kipindi cha wito cha sekunde 30 kusaidia vituo vya mikoa kurekebisha vipokeo vyao. Ishara ya marekebisho itafuatwa na kurudia rudia kwa wito wa ki-ishara wa kituo cha makao makuu, ikifuatiwa na muda na namba ya ukaguzi wa urushaji(namba iliyorushwa kwa kuandikwa katika batli za makao makuu ya mikoa kuthibitisha kwamba kipindi cha usikilizaji kimetumika) ikifuatiwa na QTC ikionyesha "nina taarifa" au QRU "sina taarifa."

(d) Radio ya makao makuu ya polisi kwanza itatuma/rusha taarifa "P"zozote ambazo itakuwa nazo, baada ya hapo vituo vya makao makuu ya mkoa vinaweza kutuma taarifa "P" yoyote iliyopo.

(e) Ishara za wito zitarushwa katika utaratibu wa kufuata herufi. Vituo vya makao makuu ya mikoa vinavyotumiwa taarifa vitakiri upokeaji wa taarifa hizo kwa kutuma "R" , ikifuatiwa na ishara zao za wito au "N" ikifuatiwa na ishara zao za wito

(f) wakati hazijapokelewa kwa kurudiwa.

Radio ya makao makuu ya polisi itadhibitiwa na mtu mmoja na itaandika taarifa zote zilizotumwa na vituo vya mikoa. Ikibidi radio ya makao makuu ya polisi itazituma tena taarifa hizo kwa vituo vya mikoa vyovyote ambavy haviwezi kutumia mtandao huu (3865 Kc/s) kwa utumaji wa kawaida uliotumwa ambao umeshindwa kunakili taarifa iliyorushwa kwa mara ya kwanza .

(g) Vituo haviruhusiwi kutumia mtandao huu (8010Kc/s) kwa utumaji wa kawaida au wa namna mbili.

7. *Mtandao wa mkoa* – makamanda wa mikoa watatunga kanuni kwa ushughulikiaji wa taarifa "P" zozote katika mitandao yao ya mikoa.

PGO-194
MAWASILIANO-VIFAA VYA REDIO-UTUNZAJI NA UANGALIFU

1. Mawasiliano ni kitu muhimu sana wakati wa hatari na inaunda sehemu muhimu katika Idara ya Polisi.Vifaa vyote vya redio vitunze katika mazingira ya kutumika.Hii inatumika zaidi katika vitu vinavyotembea na vilivyoegeshwa vipangwa kama vifaa vingine ambavyo havipo katika usimamizi wa moja kwa moja wa afisa mwenye mamlaka wa tawi la mawasiliano.

2 Maafisa wa Polisi wa vyeo vyote wanawajibika kulinda mali,kutunza,kutumia radio zote walizokabidhiwa ziwe zimefungwa,zinazotembea au zilizoegeshwa.

3 Simu sisizo tumia waya zilizopo Makao Makuu ya Mkoa,kituo kikubwa auMakao Makuu ya mawasiliano kwa kawaida majukumu ya maafisa wa vituo vidogo vya mawasiliano,lakini ni ukweli kwamba inawapunguzia majukumu maafisa kama para 1 na2 ya amri hii.Matandao hautakuwazi wakati wote isipokuwa kwa amri ya afisa idara ya mawasiliano isipokuwa waka wakutoa au kubadilisha betri.

4. Afisa mawasiliano wa ndani atashauriwa na afisa mkuu kwa dharula auharaka anapokuwa na tayizo kwenye simu zisizo kuwa na waya.Pale inapowezekana au kujaribiwa radio ya mkononi mbovu au vifaa vitarudiswa karakana cha kitengo husika mapema inavyo wezekana.

5. Afisa Mawasiliano au Mhandisi msimamizi atawajibika msimamo maelekezo kwa vituo vidogo namna ya kutumia injini ,utaratibu wa kuweka mafuta,matengenezo ya betri,na malekezo maalumu yanayohitajika kwa matumizi ya kifaa chochote. Ya maelekezo yaandaliwa na kubandikwa pembeni na kifaa husika.Msisitizo huu utasimamiwa na wahusika wote.

6. Bunda la vifaa vinavyobebeka kwa kawaida vitatunzwa katika karakana ya vifaa vya mawasiliano.Ambapo kivitendo haiwezekani vifaa hivyo vitatunza katika ofisi ya Mkuu wa Kituo au Idara.Vifaa vitatolewa stoo pale tu vitakapokuwa vinahitajika na vitarudishwa stoo mara moja baada ya mahitaji kusitishwa.Mkuu wa kitengo atatunza kumbukumbu ya kitabu cha kutunzia vifaa ,ataelezea kwa kina aina ya vifaa alivyotoa au vilivyorudishwa,ataonyesha tarehe na muda kwa kila jambo.Hali ya kifaa na upotevu wowote

utakaojitokeza untnukuliwa pia.

7. Stoo yenye vitu vilivyohifadhiwa kwenye mabunda,kubebeka nakuhamishika vitafungiwa sehemu ya usalama.Funguo wadharula utafungiwa kwenye kabati la kioo kwaurahisi wa kuuchukua.

8. Afisa msimsimamizi wa vifurushi,vinavyobebeka na vinavyo hamishika atazingatia yafuatayo:-

   (a) Vifaa vitunzwe katika chumba kikavu na kisipigwe na jua la moja kwa moja;

   (b) Vifaa vinapotunzwa stoo haraka betri zitolewe;

   (c) Betri ziwekwe kwenye chaji kwa muda kama ilivyoanishwa mkuu wa tawi la mawasiliano;

   (d) Vifaa havitakiwi viwekwe karibu na betri zinazo chajiwa;

   (e) Betri zinapochajiwa ni lazima zitolewa katika vifaa vyake;

   (f) Unyevunyevu nje ya betri nilazima upanguswe kwa uangalifuVichwa vitakavyo onyesha dalili ya kutu ni lazima visuguliwe na kupakwa mafuta kidogo. Terminals showing signs of corrosion should have same carefully scraped away and be lightly vaselined.Hakikisha betri inawekwa maji yasiyo na kemikali kabla ya kuichaji kadri itakavyoelekezwa mkuu wa idara ya mawasiliano;

   (g) Vifaa vyote lazima vikaguliwe na mhusika walao mara moja kwa wiki na kaguzi zote rasmi.Vifaa vitawashwa na kujaribiwa na maafisa watajiridhisha yakwamba vifaa vipo katika hali nzuri na betri zina moto tayari kwa matumizi;

   (h) Kifungu kinachuhusika reja yautoaji wa vifaa vya radio(kwa mujibu wa aya 6) itaandaliwa kwa ukaguzi na itasainiwa na afisa muhusika na ukaguzi;

   (i) Vifaa vyote vitapangwa kwa uangalfu vinapowekwa kwenye gari ili kuzuia mtiksko na uharibifu usio walazima wakati wakuvisafirisha.Vifurushi vya vifaa vitawekwa wima na kuchukua tahadhari za kila aina ili kuhakikisha haviharibiki au kupotea;

   (j) Vifaa vyote nilazima vifutwe vumbi kwa uangalifu baada ya kuvitumia,au kila wiki vinapokuwa stoo.

9. Watumiaji wa radio za mkononi lazima wafanye mazoezi ya kutumia hususani watumiapo betri za gari,Taa zisiachwe zinawaka wakati gari limesimama au limeegeshwa wakati wa usiku.Iwapo kuna uthibitisho kuwa betri aina moto gari libaki limesimama,dereva atatkiwa kuendesha gari likiwa linaonyesha kipima mwendo kama ishara ya hali nzuri ya betri kwa muda ufuatao:

Dakika kumi na tano	Injini iwe imewashwa
Dakika thelathini	Injini iwe imezimwa
Dakika kumi na tano	Injin iwe imewashwa
Dakiki thelathini	Injini iwe imezimwa

Maelekezo ya liyopita ni mara chache yatatumika katika magari ambayo yamefungwa vifaa vizito ya umeme.Vifaa vinapaswa kuzimwa baada ya kazi namtumiaji wa radio au dereva kama mtumiaji wa redio hayupo.

10. Dereva wanatakiwa kuwa makini wakati wanapo osha magari wahakikishe maji yasiingie kwenye vifaa radio au sehemu za kufungia.Iwapo kutakuwa na mashaka kuwa maji yameingia katika kifaa chochote jambo hili ni lazima litolewe taarifa kwa mkuu wa tawi la mawasiliano kifaa hicho kizimwe,vinginevyo uhalibifu mkubwa unaweza kutokea.Unyevu utakaopenya ndaini ya chombo unatakiwa kufutwa maramoja kwa kifutio kisafi.

11. Iwapo gari lenye redio ya mawasiliano itapelekwa karakana kwa marekebisho na dereva habaki muda wote na gari wakati wa marekebisho vifaa vya redio nilazima vitolewe katika gari hilo na mkuu wa tawi la mawasiliano au mtu mwingine aliye ruhusiwa kabla ya gari kuingia katika karakana.Kama mtu aliyeruhusiwa hayupo afisaa mwenye cheo cha juu kuwazidi wenzake atafungua kwa ungalifu vifaa vyote vya mawasiliano na kuvitunza katika usalaama.Kama vifaa vitakuwa zaidi ya kimoja vitawekewa alama kuonyesha mahaliau gari ambako kifaa kimefunguliwa.Kila kifaa cha mawasiliana kitafungwa tena kwenye gari ambako kilikuwakimefunguliwa.

12. Pale gari lenye radio ya mawasiliano litakakapomaliza safari ya kikazi ni lazima ichajiwe isipokuwa kama itakuwa imefungiwakifaa chenye umeme mkubwa.

13. Ni wajibu wa dereva kila anapofanya usafisha gari pia lazima aondoe vumbi katika vifaa vya redio kwa ungalifu kwa kitumia kitambaa kisafi,kikavu na ving'arisha iwapo itahitjika.

14. Mkuu wa kituo anawajibu wa kusimamiavifaa vya radio,injini na betri vinatumika na kutunzwa kwa utaratibu uliyowekwa na mkuu wa tawi la mawasiliano.Kabati na vifaa vilivyo fungwa vitafutwa kwa uangalifu na kung'alishwa kila siku na askari wa kituo.

15. Taarifa ya uhalibifuwowote au upotevu wa vifaa maramoja utatolewa taarifaa kwa Kamanda wa Polisi Mkoa na taarifa ya maandishi ikithibitisha namna ya uhaliribifu au upotevu ulivyotokea,nakala kwa mkuu wa mawasiliano wa tawi na nyingine kwa Chifu wa mawasiliano Tanzania.

PGO - 195

SIMU

Uunganishaji.

1. (a) Maombi yote ya uwekaji wa simu, simu za ndani na chum kuunganishia simu lazima ya pitie kwa Mkuu wa pc Wilaya(kwa njia ya simu ya upepo kama kuna umuhir Mkuu wa mawasiliano Makao Makuu ya ya Polisi na uunganishwaji utakaofanyika hadi hapoidhini yake itakap imepokelewa, kwa nyongeza Mkuu wa maw atashughulikia nyaraka zote na Kampuni ya simu Tanz huduma nyingine ya simu za mkononi ikiwa ni pamoja r zote zilizoko Dar es salaam.

   (b) Kamanda wa Polisi ana wajibika kama ifiatavyo: -

(i) Simu hazita unganishwa kwa Maofisa hawatakuwa na shughuli muhimu ya matumiz katika kazi zao;

(ii) Kiasi kidogo cha simu zinaweza zikaunganishwa nyumba ya makazi ya maofisa;

(iii) Uhamishaji usiowalazi kati ya nyumba za Maa Maofisi ya Polisi hayaruhusiwi kwa muunganil jitihada lazima zifanyike kuonyesha kunashughul ushawishi kiuchumi kamati za nyumba zinazosl kuweka idadi sahihi kwa makazi rasmi ya Maa polisi;

(iv) Usambazaji wa simu usiokuwa wa lazima wa vi hairuhusiwi kwenye nyumba za maafisa;

(v) Simu zote zinaweza kuondole katika nyumba za M wa polisi endapo hakutakuwa na umuhimu wa kama ilivyoainishwa kwenye kifungu (i) na (ii)hapo

(c) Mkuu wa Kikosi cha simu atamjulisha Mkuu wauu wa Polisi kupitia marejesho ya nusu mwaka nusu ya kwanza wa kwanza hadi wa sita na mwezi wa saba hadi wa k mbili ikieleza namba sahihi ya simu zote za Polisi na sahihi ya Maofisa wa Polisi waliounganishiwa simu hizo.

Matumizi ya simu

2. (a) Upigaji wa simu hautafanyika kihohela isipokuwa kunaj na mambo muhimu na yaharakaambayo hayawezi ku kutumwa kwa njia ya barua au kwa simu ya upepo. Mal upigaji wa simu na muda wa kumia simu lazima zidhibitiw

(b) Maswala yote yanayo husu Vituo vya Polisi lazima kwa julishwe kwa Mkuu wa Polisi wa Mkoa kwa njia ya k Wakuu wa vituo vya polisi hawata ruhusiwa k mawasiliano ya simu moja kwa moja na Makao Makuu y labda tu katika mazingira ya siyo kuwa ya kawaida.

(c) Simu hazitaruhusiwa kufanya mawasiliano ya Askari matatizo binafsi na Makao Makuu ya Polisi kama vile r

ya likizo,malipo,au madai ya mavazi n.k.,katika mazingi
matatizo hayo yata shughulikiwa kupitia utaratibu kwa M
Kituo hatimae kwa Mkuu wa polisi wa Mkoa.

(d) Umuhimu wa upigaji wa simu utafanywa na Mkuu w
katika mazingira ya hatari Maofisa wanaofanya maw
hayo lazima wawe tayari kuhakikisha kughalamia ma
simu ambayo haya kuwa ya lazima kikazi.

(e) Simu zote za nje lazima ziingizwe kwenye Rejesta ya m
ya simu kama inavyoonyeshwa hapa chini.

(f) Mawasiliano binafsi kupitia simu za Polisi zikiwepo s
Majumbani haziruhusiwi labda tu katika mazingira ya
,Ofisa yeyote atakae fanya mawasiliano ya binafsi atav
kulipa gharama hizo kwa mkuu wa kituo hati za
zitapokelewa zikiwa na namba za risiti za malipo zita
katika Rejesta ya matumizi ya simu .

Watumishi wanaoruhusiwa kumia simu

3. Mawasiliano kupitia simu za polisi yatafanywa na watu wafuata

(a) Maofisa wa Polisi

(b) Wakaguzi wa Polisi

(c) Wakuu wa vituo vya polisi

(d) Askari kiongozi wa chumba cha mashtaka walioko zamu
viongozi waliotajwa hapo juu hawatakuwepo.

(e) Askari wa cheo cha chini aliyeruhusiwa na Ofisa yeyote a
wa Kituo cha Polisi; au

(f) Askari yeyote katik mazingira ya hatari.

Rejesta ya simu

4 Rejesta za simu zitawekwa katika kila taarifa ya polisi panap
na mawasiliano.Rejesta hiyo itatunzwa na askari wa chum
simu au sehemu ambayo hakuna chumba cha simu ita
kwenye chumba cha mashtaka na ambae atahakikishak
taarifa sahihi zinandikwa kuhusiana na simu zinazopigwa
kituoni Rejesta hiyo pia itatumika katik katika simu za mo
moja kutoka maofisini na zile za kwenye majumba ya Maofi

mwisho wa mwezi nakala ya Rejesta ya simu zitatumwa kw
wa Polisi Mkoa ambae ataanda hati za malipo kupitia katika
ya malipo ya simu.

Malipo ya akaunti ya simu

5. Akaunti za simu zikipokelewa kwa malipo,Mkuu wa polis
atawajibika kukagua maingizo yote kwenye Rejesta ya simu
huo ataufanya katika zile simu za moja kwa moja na
majumbani kwa Maofisa.Akaunti za simu zitaidhinishwa ba
ukaguzi huo kama ni sahihi kwa malipo zitalipwa dosari
zitakazo tokea kati ya Rejesta na akaunti ya simu zitahitaji n
kutoka kwa mkuu wa kituo. au yeyote anaehusika na simu ilik
dosari hizo. Endapo itabainika kwamba tofauti hizo zinatok
shirika la huduma za simu Tanzania basi dosari hizo zitael
katikaa Ofisi ya malipo ya shirika la simu Tanzania na kama z
lipwa maombi yatafanywa na polisi ili kurudishwa malipo hayo.

Uchumi

6. Wakuu wa polisi wanawajibika kuhahakikisha kwamba kunal
na kubana matumizi katika matumizi ya simu, lazima wa ha
akaunti za malipo zina kaguliwa kwa usahihi na hivyo:

   (a) Watajirizisha kwamba simu zote zilizo unganishwa
   zinaingizwa aktika akaunti za malipo zimeruhusiwa kwa
   za para 1 (a);

   (b) Watahoji simu zote, za ndani na za nje , zilizo zilizosaba
   na matumizi ya utovu wa nidhamu na kupelekea ha
   kinidhamu kwa askari waliotumia simu hizo kwa m
   yasiyo sahihi;

   (c) Atapitia na kukagua idadi ya simu zilizotumika kati
   laini,ikiwa ni pamoja na maeneo yote yanayopokea hud
   simu na chumba cha simu ambazo hazikutumika
   matumizi sahihi.

7. Maofisa wote wanaotumia simu za polisi akiwepo Mkuu w
wana wajibu wa kutambua kuwa simu hizo haazitakiwi kutum
ulazima na kwamba kila mtumiaji lazima azingatie amri hii.

PGO - 196

USAFIRISHAJI-AJALI KWA MAGARI YA POLISI.

1. Ajali ikitokea inayphusisha magari ya Polisi (zikiwemo pikipiki) dereva wa gari hilo anatakiwa atoe taarifa ya ajali , bila kuchelewa kwa:-

   (a) Mkuu wa kituo cha Polisi kilicho jiranithe ; na kwa

   (b) Afisa ambaye amekabidhiwa gari hilo.

   Endapo dereva wa gari hilo hawezi kutoa taarifa yeye mwenyew (kwa mfano kutokana na majeraha aliyopata),itatolewa na abiria au na askari aliyepo kwenye eneo hilo.

2. Mkuu wa Polisi wa Wilaya au Kituo aliyepokea taarifa ya aja atwajibika kufanya upelelezi wa ajalki hiyo , kwa kuzingztia taratibu sahihi zilizopo (angalia Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi namba 250).

3. Mkuu wa Polisi wa wilaya , bila kuchelewa atamjulisha Kamanda wa Polisi wa Mkoa na Inspekta Jenerali wa Polisi, kwa simu ya upepo akitoa kamili za ajali nzima-

   (a) P.T. namba na aina;

   (b) Muda ,Tarehe na mahali;

   (c) Majeruhi husika (imeua,majeraha makubwa au madogo); na

   (d) Uharibifu kwenye gari (mkubwa au mdogo).

   Endapo gari hilo ni Mkoa mwingine ,Kamanda wa Mkoa husika pia atajulishwa

4. (a) Ajali ikitokea inayphusisha magari ya Polisi (zikiwemo pikipiki) ni muhimu kutoa taarifa inayojitegemea kwa Serikali ikiwa n nyongeza ya ile ya kawaida ya upelelezi wa polisi wa ajali .

   (b) Taarifa ya ajali iayoshughulikiwa na aya hii itatolewa endapo tu:-

      (i) Gari binafsi,mtambo au mali imehusika , bila kuja ukubwa wa uhalibifua ;

      (ii) Mtu yeyote amejeruhiwa;

      (iii) Thamani ya uhalibifu iliyokadiriwa kwa gari la Polis ianazidi shilingi 300,000/=.

   (c) Taarifa ya ajali itatolewa katika fomu TFN. 80 “Taarifa ya ajali Magari ya P.T. na Mitambo”, kwa nakala nne kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kupitia Kamanda wa Mkoa ndani ya masaa 7 tangu ajali itokee.

   (d) Makamanda wa Polisi watatoa ushauri wao katika aya ya 9 y fomu TFN. 80 na wanalazimika waweke mapendekezo mapendekezo yeyote ya mashtaka kama yapo.

5. Endapo kuna sababu za kuweza kuifanya Serikali ifunguliwe mada kutokana na uharibifu uliosababishwa na ajali, mpelelezi wa aja atatoa fomu ya Polisi namba 90,katika nakala nne , ikiambatana n Taarifa ya Ajali (TFN.80).

6. Makadirio ya gharama za matengenezo yatapatikana kutoka katik Karakana za E. Na M. , Wizara ya Miundombinu, na kupelekwa kw Inspekta Jenerari wa Polisi. Hakutokuwa na ucheleweshaji w utolewaji wa Fomu TFN. 80 na Fomu ya Polisi namba . 90 katik swala hili..

7. Endapo madai yatafunguliwa dhidi ya dereva au mmiliki wa gari l kiraia lililohusika katika ajali iliyohusisha gari la Polisi,Where makadirio kwa maandishi yatakuwa katika fomu iliyooneshwa katik kiambatanisho “A” yatapatikana toka katika Karakana ya E. and M Wizara ya Miundombinu.

8. Afisa Mnadhimu (Usafirishaji) katika Makao Makuu ya Polis atahusika na utoaji wa fomu za TFN. 80 na nyaraka nyingine katik Wizara ya Ulinzi na Usalama wa Raia kwa niaba ya Inspekta Jenera wa Polisi. Pia nakala zitzpelekwa Wizara ya Miundombinu n

kwenye Wizara ya Fedha.

9. Mkuu wa Polisi wa Wilaya ataamua kama dereva wa gari hil ashtakiwe , atfanya hivyo kutokana na matokeo ya Upelelezi n atachukua hatua bila kuchelewa. Kanuni za kufuatwa zimetolew katika aya inayofuata. Endapo kutakuwa na mashaka, Kamanda w Polisi Mkoa ajulishwe. Kama dereva atashtakiwa,matokeo ya kes pamoja na nakala ya hukumu iliyotolewa na Hakimu vitapelekw kwa Inspekta Jenerali wa Polisi na Kamanda wa Polisi wa Mko anayemiliki gari hilo mara tu baada ya kesi kuisha.

10. Madereva wa Polisi hawana msamaha wowote wa vifungu vya sheri na watashtakiwa endapo watafanya makosa ya Usalama barabaran Kama hakuna haki ya kushtaki ‘ Mkuu wa Polisi wa Wilay anayepeleleza ajali ataamua kama uharibifu uliofanyika ilikuwa n kutokana na uzembe au sababu nyinginezo ambazo ambaz zinaadhibiwa kwa kanuni za Kinidhamu ndani ya jeshi na atajulish uamuzi wake kwa Kamanda wa Mkoa.

11. Katika taratibu za kushughulikia makosa ya kinidhamu yanayotokan na ajali zilizosababisha uhalibifu kwenye mali za Serikali, afi anayetoa adhabu ni lazima amjulishe mshtakiwa kwamba adhab hiyo haihusiani na madai yeyote yanayoweza kutolewa kuhus gharama za matengenezo ya gari. Nakala ya hati ya mashtaka nay mwenendo wa masshtaka vitapelekwa kwa Inspekta Jenerali w Polisi.

12. Askari yeyote anayeendesha gari la Jeshi bila idhini atawajibika kw uharibifu wowote wa gari utakao tokea , bila kujali kwamba anawez kulalamika kutokana na ajali hiyo na vinginevyo atashtakiwa.

    Pindi dereva wa Polisi atahusika katika ajali kataka mazingira y kutatanisha,Kamanda wa Polisi wa Mkoa atamsimamisha derev huyo kufanyakazi za udereva mara moja na atachukua hatu kusitisha posho ya ya udereva katika kipindi chote ambacho atakuw hafanyi kazi za udereva.Katika makosa makubwa ya uzemb ,itakuwa ni muhimu kumzuia kufanyakazi za udereva.

Utoaji wa Taarifa za ajali pindi gari la kiraia likiwa linatumika kufanyia kazi

14. Taarifa ya Ajali katika fomu TFN. 80(kama inavyofanyiw marekebisho ya msingi) itatolewa na afisa yeyote wa Polis aliyehusika katika ajali hiyo akiwa kazini au akifanya kazi ya uderev , pamoja na kwamba alikuwa anatumia gari la kiraia ,kwa kuzingati

mazingira yaliyoainishwa katika aya ya O, taarifa itahitajika kama vile afisa alikuwa anaendesha gari la Polisi.

KIAMBATANISHO "A"

To P.G.O. No. 196

MFANO WA GHARAMA ZA MATENGENEZO KWA PT. 521

Ifuatayo ni taarifa kamili ya gharama za matengenezo kwagari P.T. 52 lililopata ajali.

	Shs.	Cts
Vipuri	245	94
Vibarua	50	00
	295	94

Endapo gharama za matengenezo zitafanywa na mtu yeyote gharama zifuatazo itabidi ziongezwe.

Jumla ya gharama za matengenezo	295	94
Asilimia 20 ya gharama za Usimamizi	59	19
Asilimia 10 ada ya uwakala	29	59
	384	72

PGO -197
USAFIRI-UDHIBITI NA UTUMIAJI

Udhibiti

1. Magari yote,pamoja na pikipiki,yatadhibitiwa na kusambazwa na makao makuu ya Polisi.

2. Ugawaji wa magari utafanywa kwa:-

   (a) Makamanda wa Mikoa na Makamanda wa vikosi.

   (b) Vikosi ya kutuliza ghasia.

   Magari yote yatakuwa chini ya usimamizi wa moja kwa moja waMakamanda wa Polisi Mikoa ambao watakuwa na wajibu wa kuyasimamia na kwa matumizi yaliyo sahii.

3. (a) Makamanda wa mikoa watatoa magari kwa kuzingatia para 1(a)kwa wakuu wa viyuo na mgawayo wote chini ya mikoa yao,lakini hawatagawa gari kwa matumizi binafsi isipokuwa kwa maelekezo maalumu kutoka kwa Mkuu wa jeshi la Polisi Tanzania.

   (b) Makamanda wa Polisi mikoa hawata hamisha au kugawa magari yaliyo gawiwa kikosi cha kutuliza ghasia,lakini katika tukio la dharula anaweza kilipangia gari aumagari hayo kazi nyingine kwa muda.Katika kila tukio madereva wa vikosi vya kutuliza ghasia wataendesha magari hayo na watarudi na magari hayo mara baada ya shughuli hiyo kwisha.

4. Gari hata gawiwa tena au kubadilishwa nje ya mkoa bila ya kibali cha mkuu wa jeshi la Polisi Tanzania.

Matumizi

5. Magari ya polisi kama yapo yatatumika daima kwa safari rasmi tu.Mail zote zilizotumika katika safari rasmi kwa kutumia gari binafsi yanapaswa yafahamike na kuandikiwa madai kukiwa na uthibitisho kwa kuandika “Nathibitisha kuwa hapakuwa na gari la polisi”Kamanda hatalipa madai yote ambayo hayana uthibitisho.

6. Magari yote ya polisi ya hifaziwa katika gereji au eneo maalumu ya maegesho pale yanapokuwa hayapo katika matumizi.Hayapaswi kutunzwa katika nyumba nyumba ya afisa isipokuwa kama kunajambo maalumu na kwa ruhusa ya Kamanda wa Polisi.

7. Magari ya Polisi hayatumika kwa shughuli ambazo siyo rasmi na shughuli binafsi,au kwa safari ambazo siyo za muhimu.Abiria

wasiyo ruhusiwa hawatakiwi kupakiwa.

8. Matumizi ya siyo ya muhimu ya magari ya Polisi au matumizi wa magari makubwa wakati magari madogo yapo yote yanakatazwa.Maafisa wa kuu wa kila mgawayo katika ngazi zote wanawajibu wa moja kwa moja kuhakikisha kuwa amri zote zinafuatwa bila kuzikwepa na magari yote yatumike kwa kuzingatia uchumi na faida .

9. Sheria kwa ujumla wake magari ya Polisi yataendeshwa na madereva walioruhusiwa au afisa mwingine atakaye ruhusiwa na afisa aliyetangazwa katika gazeti la serikali mwenye mamlaka na gari husika.Magari ya Polisi katika wakati wowote hayataendeshwa na dereva asiye na leseni halali ya daraja linalotakiwa.Madereva wenye leseni za muda wataendesha magari ya Polisi pale tu wanapokuwa katika mafunzo maaluum.

10. Hakuna gari la Polisi litakalo endeshwa katika mwendo wa usiyo wa kawaida,isipokuwa katika dharula ,au katika kukamata waalifu au katika hali inayo kubalika za kukimbia.

11. Wanyama wadogo au Mifugo haitabebwa kwenye magari ya polisi isipokuwa wakiwa katika vibanda au kantana.

12. Magari ya polisi hayatumika kusafirisha askari polisi kutoka ofisini hadi katika makazi yao au kituoni au katika eneo jingine la kazi isipokuwa tu itakapo amriwa naKamanda au Mkuu wa Polisi wilaya.

13. Pikipiki za Polisi hazirusiwe kupakia abiria kwa nyuma isipokuwa katika hali dharura au kwa ruhusa ya afisa aliye tangazwa katika gazeti.

14. (a) Hairuhusiwi kubeba mzigo kupita kiwango chake cha ubebaji.

    (b) Idadi ya abiria wa kupakiwa katika gari ya Polisi ukimtoa dereva itakuwa imelezwa na mtangenezaji.

15. (a) Kila safari inayofanywa na gari la Polisi nilazima iwe imeruhusiwa kabla gari halijaondoka na ngazi zifutazo za maafasa:-

        (i) Afisa aliyetangazwa katika gazeti;

        (ii) Mkaguzi wa Polisi;

        (iii) Staff Sajin and RSM;

(iv) Kiongozi wa chumba cha mashitaka (angalia(b) chini); au

(v) N.C.O kiongozi wa Tawi la matengenezo,

(b) Kiongozi wa chuma cha mashitaka atakaye amuru safari ya gari la polisi kama utaratibu wa kifungu (a) cha juu ataweka kumbukumbu ya taarifa katika kitabu matukio ya kituo muda aliyotoa amri:

(i) Namba za usajiri za gari iliyotumika;

(ii) Namba, cheo nza jina la dereva;

(iii) Lengo la safari;

(iv) Muda wa kuondoka; na

(v) Muda wakurudi.

16. (a) Kila gari la polisi litakuwa na log book(fomu E.M.I.(A))

(b) Kila afisa anaye amuru safari ataweka saini katika sehemu husika katika log Book(fomu E.M.I.(A)) kabla gari nhalija ondoka,Haita ruhusiwa gari kwenda safari au kazini bila kupata kibali au ruhusa kutoka kwa afisa mwenye malaka.

(c) Madereva watajaza kopi mbili za (fomu E.M.I.(A)) akielezea taarifa za kila safari.

(d) Kila mwisho wa mwezi kopi zote zilizo jazwa za(fomu E.M.I.(A)) zitatolewa katika Log book na afisa anayehusika na gari na kuzipelekwa kwa Kamanda wa Polisi Mkoa.Nakala ya bpili itabaki katika Log Book.

(e) Kamanda atahakikisha kuwa kila fomu iliyokamilika(fomu E.M.I.(A)) itatunzwa katika faili la kila gari baada ya kuifanyia ukaguzi wa wa kina katika makao makuu ya mkoa.(fomu hizi haziitajiki makao makuu ya Polisi).

(f) Maafisa ambao wamepewa magari watafanya ukaguzi wa kina kila mara kwenye Log Book na kwa kila mwisho wa

mwezi kwa lengo la kufanya mahesabu ya matumizi na uwezo wa kila gari na kila dereva.Watasainni kila kurasa ya mwisho kuonyesha kuwa kimekaguliwa.

Majalada ya Historia ya Magari

17. Jalada la historia ya gari litatunzwa makao makuu ya polisi kwa kila gari la Jeshi.Jalada linguine litatunzwa katika kila katika kila kikosi ambako kunagari la Polisi. Na Jalada la tatu liakuwa katika kila makao makuu ya Mkoa.

18. Mawasiliano yote kuhusu taarifa,utendaji kazina matengenezo ya gari yatatunzwa katika jalada la historia ya ya gari.

19. Iwapo gari linahamishwa kutoka utawala mwingine,jaladala historia ya gari nalo litamishwa pamoja na gari iwapo itakuwa ndani ya Mkoa jalada la Mkoa litahamishiwa makao Makuu ya mkoa unaopokea.

20. Jadala la historia ya gari litaharibiwa miezi mitatu baada ya tarehe gari kuondolewa katika matumizi na bodi ya ufuatilia juu ya magari.

21. (a) Maafisa waliogawiwa magari wata tuma taarifa kila mwezi katika nakala mbili katika fomu fomu M.V.R.I kwa Makamanda wa Mikoa .Taarifa itakuwa ya mwezi na iwafikie makamanda kila kabla ya tarehe 15 ya mwezi.

    (b) Fomu M.V.R.I.itajazwa kwa ukamilifu isipokuwa katika vifungu vifuatavyo:-

        (i) Grisi,maji nk.

        (ii) Mishahara ya Madereva’

        (iii) Matairi,tyubu,vipuri na mabadiliko,

        (iv) Jumla ya madeni.

22. (a) Makamanda watatuma nakala hailisi ya taarifa ya mwezi makao makuu ya jeshi,na inatakiwa ifike kila ifikapo tarehe25ya kila mwezi na atatunza nakala.

    (b) Kila Kamanda wa Polisi atahakikisha kuwa kila taarifa ya mwezi itakayokabidhiwa kwa kuzingatia kila gari lililo gawiwa kutaka tarehe iliyo gawiwa hadi siku yatakapo

ondolewa au kukoma kutukika na bodi ya uhakiki.

23 Log Bookfomu E.M.I. (A)na fumu M.V.R.I.ni fomu za kitaifa kwa kupata utambulisho na Makamanda kutoka serikalini.

PGO -198
USAFIRI-MASHINE

MAJUKUMU YA MADEREVA

1. Madereva wa polisi wana majukumu ya kuhakikishausafi na utunzaji wa katika hali nzuri wa magari yao na usalama wavifaa vilivyo tolewa kwaajili ya gari hiyo.

2. Madereva watakuwa na wajibu wa kufanya marekebisho kama ilivyo elezwa katika P.G.O.199.

3. Madareva wapolisi watatoa taarifa ya bilaya kuchelewa,uhalibifu atakaokuwa ameugundua.Hapaswi kufanya matengenezo au marekebisho yoyote isipokuwa yale tu aliyopewa kibali au iwapo atukuwa katika dharula ya safari.

4. Dereva wa Polisi muda wote akuwa:-

   (a) Wataendesha kwa usalama na kwa utaratibu kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani nakanuni zake zinazotoa alama za kuongoza madereva;

   (b) Wataendesha kwa upole na kuwa mfano katika jamii

   (c) Watahakikisha kuwa koti lefu litavaliwa tu wakati wa matengenezo);boot nilazima zivaliwe;

   (d) Watazui mtu asiye husikakuweza kuharibu magari yao;

   (e) Kuhakikisha kuwa mizigo ipakiwe isipite kiwango kilicho ruhusiwa nakuhakikisha usambazaji nakuhakikisha usalama wa gari;

   (f) Watahakisha log book za magari zitatunzwa kama ilivyo elekezwa katikan P.G.O. Na. 197;

   (g) Kutoa taarifa ya tukio la ajali hata kama nj dogo ambalo gari limehusika.

5. Madereva wa Polisi wanakatazwa kufanya yafuatayo;-

   (a) Kuruhusu mtu ambaye hajaruhusiwa kuendesha gari la polisi;

(b) Kuendesha gari lolote ambalo linamatatizo au bovu;

(c) Kupakia abiria wasioruhusiwa au mizingo isiyorusiwa;

(d) Kuacha gari bila uangalizi barabarani;

(e) Kuvuta wakati wa kazi au karibu na gari lake;

(f) Kutumia gari bila ya safari kuruhusiw katika log book au bila ya kuandika taarifa katika kitabu cha kumbu kumbu kituoni.

6. Maderva ambao hawajawa mahili na vifaa vya mawasiliano wanakaazwa kuingilia mawasiliano kwa vifaa vya mawasiliano visivyo na waya katika magari yao wakati wowote.Vifaa vya mawasiliano ni sehemu ya gari hivyo madereva wanawajibu wa kuangalia usalama wake.

7. Madereva wa Plisi wanaweza kuendesha magari yasiyo ya serikali ya daraja la leseni yake inavyoruhusu.

PGO - 211

TAHADHARI ZA AFYA

1. Tahadhari kubwa inatakiwa kuchukuliwa na askari wa vyeo vyote kulinda afya zao dhidi ya magonjwa ya kuambukizwa na magonjwa ya mlipuko

2. Wakuu wa Kamandi watashirikiana na Kitengo cha Afya cha Polisi kuhakikisha program za afya za askari Polisizinazingatiwa.

3. Kila Mkuu wa kamandi atahakikisha kwamba, kuna vifaa vya kutosha vinavyohusiana na masula ya afya.

MAGONJWA YA KUAMBUKIZA NA YA MLIPUKO

4. (a) umakini kwa askari wa vyeo vyote jeshini utazingatia sera, mipango na maelekezo ya kitaifa kuhusiana na magonjwa ya kuambukiza na mlipukokama vile sera ya ukimwi, malaria, kifua kikuu na kipindupindu. Sera ambazo ziliznzishwa na serikali kusaidia watu katika juhudi za kupambana na kuenea kwa magonjwa hayo.

(b) kuhusiana na gonjwa la ukimwi, Wakuu wa Kamndi watahakikisha juhudi zinafanywa ndani ya Jeshi la Polisi kuinua na kuendeleza sera na mipango ya kitaifa katika kamandi zao. Hili litafanywa kupitia elimu, program za uelimishaji na kupima maambukizi kwa hiari.

(c) mkuu wa Jeshi la POlisi ataendelea kutoa nyaraka za jinsi ya kupambana na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza kama ukimwi na madhara yake ndani ya Jeshi la Polisi.

PGO - 221

WAHALIFU WATORO, UREJESHWAJI WAO, MAAFIKIANO YA PANDE MBILI KATIKA MASUALA YA UHALIFU WA JINAI NA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU.

SEHEMU YA I

UKAMATAJI-WAHALIFU WATORO-MAELEZO YA JUMLA.

Kwa ujumla.

1.Utaratibu uliowekwa wa kukamata na urejeshwaji wa makundi mbalimbali ya watu wanaotafutwa na majeshi ya polisi ya nchi zingine umeelezwa kwa urefu katika aya zifuatazo kwenye amri hii.

2.Iwe kwa mazingira yoyote yale mtu yeyote hatakabidhiwa kwa mamlaka ya nchi nyingine isipokuwa na mpaka:-

Utaratibu kamili wa kisheria uliowekwa katika amri hii uwe umefuatwa,jalada la kesi liwe limeonwa na Mkurugenzi wa Upelelezi wa M akosa ya Jinai na mashitaka yawe yamefinguliwa na Mkurugenzi wa Mashitaka,na mshitakiwa awe amefika mbele ya hakimu na kuwe hakuna amri dhidi ya kujisalimisha kwake.

SEHEMU YA II

SHERIA YA WAHALIFU WATORO(WANAOFUATILIWA)SURA YA 57 MAREJEO YA 2002.

3.(a)Kazi ya ufuatiliaji na ukamataji unaofanywa na askari wa majeshi ya polisi ya nchi zinazopakana ambazo wahalifu watoro wamekimbilia nchini Tanzania wanaruhusiwa na sheria ya wahalifu watoro(wafuatiliwaji).

(b)Chini ya vifungu vya sheria hii waziri mwenye dhamana na mambo ya sheria kama ataridhika kwamba mipango ya kubadilishana imefanywa na nchi zinazopakana anaweza kulielezea eneo la Tanzania ambapo polisi wan chi zinazopakana wanaweza kuingia wakati wa ufuatiliaji wa wahalifu hao na ambalo ndani yake wanaweza kufuatilia na kuwakamata wahalifu hao.Hii itafanyika kupitia notisi ya serikali kuchapwa katika gazeti .

(c)Dhamira ya sheria hii ya wahalifu watoro sura ya 57 marejeo ya 2002 ni kurahisha kwa haraka ufuatiliaji wa mhalifu mipakani kutoka nchi moja kuingia nchi nyingine ili kuwakamata.Ufuatiliaji ni lazima uwe wa haraka.

(d)Hakutakuwa na mazingira yoyote ambayo afisa wa polisi anaweza kuvuka na kuingia nchi jirani ili kumkamata mtu anayetafutwa ambaye amekuwa akiishi huko kwa muda.Kesi zote hizo lazima zipitie kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na hukna hatua zozote zinazoweza kuchukuliwa bila kupata maelekezo kutoka kwake.

4.Kwa sasa,zifuatazo ni nchi ambazo zina utaratibu wa kubadilishana wahalifu watoro na Tanzania chini ya vifungu vya sheria hii.Jamhuri ya Kenya -wahalifu watoro(wafuatiliwaji)(Kenya na Uganda)Amri,kupitia notisi ya serikali namba 101/1938,178/1947,161/1957 na 222/1962.

Nguvu za ufukuziaji.

5.(a)Polisi wa Kenya-Askari wa Jeshi la Polisi la Kenya wanaruhusiwa kuingia Tanzania ili kufuatilia mhalifu ndani ya eneo maalum la kijiografia lilivyoainishwa kama ifuatavyo:-

“Ndani tu ya eneo lililokaa katikati ya –mpaka wa Kenya-Tanzania na mstari wa kubuni uliochorwa toka Tanga njia nzima ya reli mpaka Arusha,kuanzia barabara nzima ya Arusha-Makuyuni hadi Makuyuni,pia barabara ya Makuyuni-Oldean hadi maili 47,kuanzia barabara ya Ngorongoro-Ol Bal Bal(mbuga ya Serengeti)-mpaka wa Kenya(Ol Puss Imoru) mpaka makutano ya kituo cha kusini mwa Loliondo ambapo barabara ya kwenda kilima cha Banagi inakutana,barabara nzima ya Banagi hadi kilima cha Banagi,pia barabara nzima ya Ikoma-Natta-Buhemba-Busegwe hadi Busegwe,barabara nzima ya Mwanza-Musoma hadi Musoma”.

(b)Polisi wa Uganda-Askari polisi wa Uganda wanaruhusiwa kuingia Tanzania kufuatilia mhalifu ndani ya eneo la nchi linalokaa katikati ya mpaka wa Uganda/Tanzania na mstari wa kubuni uliochorwa wenye urefu wa maili 50 kutoka mpakani.

(c)Askari ywyote wa Jeshi la Polisi Tanzania au Majeshi ya Polisi ya nchi zinazopakana yanayofanya kazi chini ya vifungu vya sheria hapo juu watalazimika kuvaa sare wakati wa ufuatiliaji wa mhalifu.

Utaratibu wa ukamataji.

6.Askari yeyote wa Jeshi la Polisi Tanzania au Majehi ya Polisi ya nchi zinazopakana wanaowafuatilia na kuwakamata wahalifu watoro katika eneo lolote la nchi jirani ilivyoainishwa katika aya ya 5 watalazimika kumpeleka mhalifu bila kuchelewa katika kituo cha Polisi cha nchi ulikofanyika ukamataji.Polisi wan chi hiyo kwa haraka iwezekanavyo watampeleka mhalifu huyo mbele ya Hakimu kwa matazamio ya kumsalimisha katika nchi alikokimbia.

SEHEMU YA III

SHERIA YA UREJESHWAJI WA MKOSAJI ILI AHUKUMIWE KATIKA NCHI ALIKOFANYA MAKOSA,SURA YA 368 MAREJEO YA 2002.

Kwa ujumla

7.Usalimishwaji wa wahalifu watoro(ambao hawaguswi na sheria ya wahalifu watoro(wanaofuatiliwa)Sura 57 Marejeo 2002) kuja na kutoka Tanzania na nchi zingine ulimwenguni hutawaliwa na sheria ya urejeshwaji wa mkosaji Sura y 368.

8.Sehemu ya II ya sheria huelezea utaratibu wa makosa yanayofanyiwa urejeshwaji wa mkosaji.Sheria hutumika tu pale ambapo makubaliano yamefanywa na nchi yeyote kwa heshima ya kumrejesha mkosaji katika nchi alikofanya kosa,sambamba na amri ya waziri mwenye dhamana na masuala ya sheria iliyochapishwa katika gazeti,bila kuathiri hali yeyote,mambo yasiyofuata kawaida na sifa zitakazoainishwa katika amri.

Utaratibu chini ya sehemu ya II ya sheria ya urejeshwaji wa mkosaji kwa kumkamata mhalifu ambae amekim bia kutoka Tanzania kwenda nchi nyingine.

9.Ukamataji wa mhalifu(mkosaji) aliyekimbia kutoka Tanzania kwenda nchi nyingine atatafutwa kulingana na utaratibu uliowekwa au ulioanishwa katika aya ya 11.

10.Pale ambapo Mkuu wa kituo atajiridhisha kuwa mtoro ametenda kosa kati ya yaliyoorodheshwa katka jedwali la sheria hii katika kituo chake,atafanya yafuatayo:-

(a)Ataanzisha lalamiko au atafungua shitaka chini ya kifungu 128 cha Sheria ya mwwnendo wa makosa ya jinai,sura 20 marejeo ya 2002 mbele ya Hakimu

mwnye mamlaka ya kisheria mali pale.

(b)Atawaita mashahidi ambao wanaifahamu kesi mbele ya Hakimu ambaye ataweka kumbukumbu za ushahidi wao kwa ufupi sawasawa na kana kwamba anaendesha kesi hiyo kwa nia ya kumpeleka gerezani,isipokuwa mshitakiwa hatakuwepo.Uhahidi katika kuthibitisha ni lazima uguse mambo muhimu yatakayoonyesha kuwa mshitakiwa alitenda kosa hilo analoshitakiwa nalo.

(c)Atampa Hakimu wasifu wa mshitakiwa na pia taarifa zote muhimu zinazowezekana za nchi alikokimbilia ili kuwezesha kutambuliwa,mahali alipo na kukamatwa.

11.Kama Hakimu ataridhika kwamba kosa limeanishwa vyema dhidi ya mshitakiwa,atatoa hati ya kumkamata chini ya kifungu cha 130 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai ,sura ya 20 na katika majumuisho ya usikilizaji atapeleka kumbukumbu kwa msajili wa mahakama kuu.

12.Hakimu atapeleka nakala iliyothibitishwa kwa mkurugenzi wa mashitaka ambaye baada ya kupitia ushahidi,atapanga ushahidi na hati itakayo thibitishwa kwa mhuri wa serikali ya Tanzania.

13.Mkuu wa kituo kwa wakati huo atawasilisha taarifa kamili ya maelezo ya kesi na hatua zilizochukuliwa na poilisi kwa kamanda wa polisi wa mkoa na mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai.Kama inatarajiwa kuwa mhalifu mkimbizi anaweza kutoroka katika nchi aliyopo ambako hati iliyothibitishwa imepelekwa,maombi yatajumuishwa katika taarifa kwamba polisi wa n chi hiyo ambako mkimbizi huyo amekimbilia wataombwa waombe hati ya dharura ya kumkamata wakisubiri hati iliyothibitishwa na nyaraka zingine.

14.Baada ya hati na nyaraka zingine kuwa zimetibitishwa,zitatumwa na serikali ya Tanzania kwa nchi alikokimbilia mshitakiwa ili ziweze kutekelezwa.

15.Mkuu wa kituo atachukua hatua kuhakikisha kwamba mashahidi wa kwenda kumtambua na wasindikizaji wanapatikana kwa kipindi kifupi kinachowezekana ili kwenda katika nchi hiyo kama watahitajika.

16.Katika kukamtwa kwa mtoro/mkimbizi katika nchi alikokimbilia ,Hakimu au Jajiambaye alikuwa akisikiliza kesi hiyo,atampeleka gerezani akisubiri kurudishwa kwake,kama atajiridhisha kuwa mtoro huyo ametambuliwavyema na kwamba ushahidi dhidi yake umegusa na kuthibitisha mambo muhimu ya kosa alilotenda kama inavyoonyesha kwenye hati.

SEHEMU YA IV-UKAMATAJI WA MKOSAJI(MHALIFU)ALIYEKIMBILIA TANZANIA KUTOKA NCHI NYINGINE

17.Sehemu ya II ya sheria inashughulikia juu ya usalimishwajikati ya nchi

ambazo,kwa sababu ya sheria,yaweza hitaji usalimishwaji wa wahalifu kutoka kila nchi.

18.Mamlaka ya kisheria yanayojadiliwa na sheriahayashughulikiwi katika mipaka ya nchi aliyokimbilia lakini ni mipaka ya nchi aliyokimbilia na ile ambayo anahitji asalimishwe.Hii ni muhimu kwa vile ni mahakama pekee iliyo na mamlaka ya kuamua wakati wa usalimishwaji kutoka Tanzania kwa mujibu wa sheria.Ni muhimu kutambua kuwa mahakama ndiyo inayotakiwa kuchukua jukumu chini ya sheria,pia imepewa nguvu za kushughulikia jambo hilo.

Muda uliotengwa kwa ukamataji.

19.Wakati wowote ule ofisa wa polisi apokeapo taarifa kwa telegram,simu ya upepo au njia yoyote ile,kuwa mhalifu kutoka nchi ambayo sheria hii inatumika katika kituo chake cha kazi,atamwarifu ofisa aliyeko juu yake aliyepo katika kituo ambaye naye atamjulisha kamanda wa polisi mkoa kwa njia yoyote ya haraka.Kama kuna hatari yoyote ya kutoroka kabla ya hati ya mahakama kwa ukamataji haijapatikana,kamanda wa mkoa atamwamuru ofisa apate apate hati ya muda ya ukamataji kwa mhalifu kwa mujibu wa kifungu cha 13 cha sheria, hiyo hati ya muda ya ukamataji kutokana na kifungu 13 cha sheria,Hati ya ukamataji itatolewa na mahakama kutokana na maelezo ya kiapo kutoka ofisa wa polisi,au mtu yeyote,ambaye anaweza kuapa kuwa kutokana na maelezo aliyoyapokea anaamini mhalifu ametenda kosa ambalo usalimishwaji wake utekelezwe,na hati ya ukamataji kwa kosa lililotendwa imetolewa katika nchi,ambapo inasadikiwa kosa limetendeka.

20.Kama ofisa mwandamizi katika kituo anaona kuwa muda ni mfinyu wa kumwarifu kamanda wa mkoa,atahakikisha anapata hati ya ukamataji na kasha kumwarifu kamanda wa mkoa kwa uamuzi wake katika kipindi cha mapema mno.

TANBIHI:Hakuna nguvu ya kisheria ya kumkamata mhalifu mtoro pasipokuwa na hati ya ukamataji kutokana na kifungu cha 14(f)cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai,sura ya 20 isipokuwa aidha hati ya muda ya ukamataji bado inatumika,au hati iliyosainiwa muda wake wa kutumika umer

ejeshwa nyuma na mahakama ambayo kwa mujibu wa mamlaka iliyonayo kisheria kuwa mhalifu anakaribia kujificha.

21.Ofisa mwandamizi katika kituo au ofisa aliyeamuriwa na kamanda wa mkoa atachukua hatua muhimu kuhakikisha ukamataji wa mhalifu unafanikiwa na kumfikisha mapema mahakamani kabla haijatoa hati ya muda ya ukamataji,mkuu wa kituo na ofisa yeyote mara moja atatuma taarifa zifuatazo kwa mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai:-

(a)Taarifa za mhalifu (jina kamili na la bandia),kosa na mipaka yake.

(b)Tarehe na mahali alipokamatwa(kama ukamataji wake umefanyika mara tu baada ya kupata taarifa).

22.Kama ukamataji haukufanyika hadi muda mwingine baada ya hati ya ukamataji,mkurugenzi wa makosa ya jinai atajulishwa kwa simu ya maandishi.

23.Itambulike kuwa mahakama itamwachia mtu aliyekamatwa kwa hati ya muda ya ukamataji isipokuwa kama hati halisi ya ukamataji imewasilishwa na kusainiwa kwa muda muafaka kama itakavyoonekana inafaa.

24.Mkurugenzi wa makosa ya jinai katika kupokea taarifa kutoka kwa mkuu wa kituo au ofisa mwingine aliyeidhinishwa,atachukua hatua zote muhimu kuharakisha upokeaji wa hati iliyothibitishwa ikionyesha shahidi na msindikizaji kutoka nchi jirani inayohusika.Kama hati ya ukamataji haijapokelewa katika muda wa siku saba kutoka siku ya mwanzo ya kumweka mahabusu,ofisa atampeleka mhalifu mahakamani aiombe mahakama au aongezewe siku saba zaidi,akiitaarifu mahakama ya kuwa hati bado haijapokelewa kutoka jeshi la polisi la nchi inayomhitaji huyo mhalifu.

25.Katika kupokea hati iliyothibitishwa,mkuu wa kituo au ofisa mwingine aliyeteuliwa na kamanda wa mkoa atampeleka mtoro mbele ya Hakimu aliyempeleka rumande,au kama hakuwa amewekwa rumande,mbele ya Hakimu mwenye mamlaka ya kisheria wa eneo analoishi mtoro.Hakimu,kama ataridhika kwamba hati imetolewa na mtu mwenye mamlaka ya kutoa hati,anaweza kuidhinisha hati hiyo,na kama atajiridhisha kwa kiapo cha shahidi aliyetambua kwamba mahabusu ndiye mwenye jina hilo,au vinginevyo ilivyoelezwa kwenye hati,anaweza kutoa amri mahabusu arudishwe kwenye nchi ambako hati ilitolewa na kwa sababu hiyo atapelekwa chini ya ulinzi wa mtu ambaye hati ilikuwa imeelekeza,na na kuwekwa chini ya ulinzi na kasha kumpeleka nchi ya jirani ambako hati ilitolewa,ili atendewe kwa mujibu wa sheria.Mkuu wa kituo atamkabidhi mahabusu kwa msindikizaji kutoka jeshi la polisi la nchi jiranina kufanya mipango ya kuondoka kwao.

26.Kuondoka kwa mahabusu na msindikizaji kutoka Tanzania ni lazima mkurugenzi wa makosa ya jinai ajulishwe kwa njia ya simu ya maandishi kama kumbukumbu ya kuondoka kwao.

SEHEMU YA V-UKAMATAJI WA MHALIFU ALIYEKIMBIA TOKA TANZANIA KWENDA NCHI NYINGINE.

27.Mkuu wa kituo ambaye atakuwa na sababu za kuamini kwamba mtu aliyefanya kosa Tanzania amekimbilia nchi nyingine zinazotekeleza sheria

hii,mara moja atamjulisha kamanda wa mkoa,ambaye atamteua aidha mkuu wa kitu au ofisa mwingine kuchukua hatua zifuatazo:-

(a)Ataapia taarifa hizo mbele ya Hakimu Mkazi yeyote kumshitaki mshitakiwa na kosa hilo na kupata hati ya kumkamata katika utaratibu wa kawaida kana kwamba mshitakiwa yuko Tanzania.Hati hizo zitakuwa na wasifu kamili wa mtu anayetafutwa na uidhinishwaji utaonyesha endapo dhamana inaweza kukubaliwa na, kama ndivyo,kiasi cha dhamana.

(b)Atahakikisha kwamba hati imegongwa mhuri wa mahakama ya chini na kusainiwa na Hakimu Mkazi aliyeitoa.

(C)Kitengo cha simu za maandishi kwa ajili ya kumbukumbu cha CIDPOL,Dares Salaam,kitatoa taarifa zifuatazo:-

(i)Jina kamili na la bandia la mtoro/mkimbizi.

(ii)Kosa lililoanishwa katika hati.

Mahakama inayotoa hati.

Itaiandikia nchi jirani ambayo mtoro huyo anaishi(hii ni lazima ikamilike kwa haraka)

(d)Atapeleka hati, pamoja na jalada la kesi, kwa mkurugenzi wa makosa ya jinai kulipitia na kulipeleka kwa mwanasheria mkuu ambaye atatoa ushauri iwapo au kama siyo kesi ya msingi ya kushughulikiwa chini ya sheria ya Urejeshwaji wa Mkosaji.

28.Mkurugenzi wa makosa ya jinai katika kupokea simu hiyo kulingana na aya ya 27(c)haraka iwezekanavyo atawasiliana na mwanasheria mkuu na kuamua iwapo kuna uharaka wa kuomba jeshi la polisi la nchi jirani kuomba hati ya muda ya kumkamata au wasubiri kufika au jalada la kesi la polisi.

29.Pale ambapo Mwanasheria Mkuu ataamua kuwa kesi ni ya msingi ithibitishwe kwa hati,atapeleka hati kwa Waziri wa sheria kwa uthibitisho.

30.Mara tu hati itakapothibitishwa ,itarudishwa kwa mkurugenzi wa makosa ya jinai ambaye aidha:-

(a)ataipeleka kwenye nchi ambayo mshitakiwa amekamatwa kwa hati ya muda (angalia aya ya 28) na atamjulisha mkuu wa kituo au ofisa mwingine ambaye hati ya awali imetokea,kwa simu ya maandishi,kwamba hati imetumwa na kwamba atatakiwa kutuma shahidi wa kutanbua na msindikizaji katika kituo cha polisi cha eneo ambako mtoro yuko rumande.

(b)Atarudisha taarifa katika kituo kilichokuwa kikisubiri uamuzi toka polisi wa nchi jirani ambako mtoro yupo,au anakoaminika anakaa,kwamba

ameshakamatwa.Pale ambapo mkurugenzi wa makosa ya jinai atapokea taarifa kwamba ukamataji umeshafanywa,atatoa maelekezo kwa mkuu wa kituo,kutuma shahidi wa kutambua,sambamba na msindikizaji na hati kwa kituo cha polisiwaliomkamata mtoro/mkimbizi.

31.Polisi wan chi ambako mshitakiwa amekimbilia wanaweza kutoa hati kwa Hakimu ambaye kwa matakwa ya sheria ambaye ataidhinisha hati hiyo itumike katika eneo lake la mamlaka ya kisheria.

32.Mkosaji, katika kukamtwa au kama tayari yuko rumande,atapelekwa mbele ya Hakimu.Mtu wa kumtambua atatoa ushahidi wake kwa kiapo kwamba ndiye mtu aliyetajwa katika hati na Hakimu ataamuru mahabusu arudishwe Tanzania.Msindikizaji anaweza kumchukua mahabusu na kurudi Tanzania na mara tu afikapo anatakiwa kumpeleka mbele ya mkuu wa kituo cha polisi au ofisa mwingine aliyeteuliwa ambaye mara moja atampeleka mbele ya Hakimu aliyetoa hati halisi na kuwajulisha CIDPOL kwa simu ya maandishi.

SEHEMU YA VI-UREJESHWAJI-UKAMATAJI WA WAKOSAJI WATORO KATIKA NCHI ZA NJE NA KUJISALIMISHA KWAO NCHI ZA NJE.

33.Kujisalimisha kwa mkosaji ambaye amekimblia nchi za nje kutoka Tanzania (au kinyume chake) ni utaratibu mrefu na utazingatiwa tu kwa kesi za jinai ambazo ni makosa makubwa.

34.Majalada yote ya kesi yatapelekwa kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kwa ajili ya kuyapitia na kasha kuyapeleka kwa Mwanasheria Mkuu ambaye atatoa ushauri wa kina kwa kila kesi.

PGO - 222

MAPATANO YA PANDE MBILI NA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU.

SEHEMU YA I

SHERIA YA MAPATANO/MAAFIKIANO YA PANDE MBILI KATIKA MASUALA YA UHALIFU WA MAKOSA YA JINAI,SURA 254 MAREJEO YA 2002.

1.(a)utaratibu unaosimamia ushirikishwaji wa maofisa wa polisi katika mapatano/maafikiano ya pande mbili kwa masuala ya makosa ya jinai umeainishwa kwa kina na kwa mpangilio ufuatao katika sehemu hii.

(b)Mapatano hayo yanahusisha:-

(i)Upatikanaji wa ushahidi,nyaraka au makala zingine.

(ii)Uwasilishwaji wa nyaraka na kumbukumbu zingine.

(iii)Mahali na utambuzi wa mashahidi na watuhumiwa.

(iv)Utekelezaji wa maombi ya upekuzi na ukamataji.

(v)Mpangilio wa watu kutoa ushahidi au kusaidia katika upelelezi.

(vi)Utwaliwaji au utaifishaji wa mali kulingana na kosa lililotendwa.

(vii)Upatikanaji wa adhabu zinazohusu fedha kulingana na kosa.

(viii)Kupiga marufuku au kukataza udanganyifu katika mali,au kuganda kwa mali ,ambazo zinaweza kutwaliwa au kutaifishwa,au ambazo zinaweza kuhitajika kukidhi adhabu zinazohusiana na fedha zitolewazo kulingana na kosa,

Mahali mali ilipo kiasi kwamba inaweza kutwaliwa,au kwamba inaweza kuhitajikakukidhi adhabu zinazohusiana na fedha zitolewazo,kulingana na makosa,na huduma ya nyaraka.

2.Afisa wa polisi mwenye au juu ya cheo cha koplo tu ndio wanaoruhusiwa kushughulikia masuala ya mapatano ya pande mbili.

Maombi ya mapatano ya pande mbili kwa Tanzania.

3.Kama wakati wa upelelezi itaonekana kwamba ushahidi wa muhimu kuhusiana na kesi hauwezi kupatikana ndani ya Tanzania,jambo hilo kwa haraka litapelekwa kwa mkurugenzi wa makosa ya jinai.

4.Kama mkurugenzi wa makosa ya jinaiataona jambo hilo linapaswa kufuatiliwa ,anaweza kulipeleka kwa mkurugenzi wa mashitaka au kutumia njia zingine zlizopo.

Mapatano ya pande mbili kwa nchi zingine.

5.Kama wakati wa upekuzi kulingana na hati iliyotolewa kwa kufuata sheria ya mapatano ya pande mbili katika masuala ya uhalifu wa makosa ya jinai,ofisa wa polisi atapata kitu ambachoanaamini katika mazingira na sababu za msingi kuwa kinahusiana na mwenendo wa kesi au upelelezi katika nchi za nje,anaweza kukikamata kwa ujumla au sehemu yake na kukikabidhi haraka kwa ofisa aliyeko juu yake.

6(a)Mkurugenzi wa makosa ya jinai atafahamishwa haraka iwezekanavyo ukamataji huo na katika kujulishwa huko atatoa amri stahiki kwa heshima ya

kukitunza wakati maelekezo ya maandishi yakisubiriwa kutoka kwa mwanasheria mkuu kuhusiana na namna ya kushughulika na jambo hilo.

(b)Iwapo maelekezo ya maandishi hayatapatikana kutoka kwa mwanasheria mkuu ndani ya siku 21 mkurugenzi wa makosa ya jinai atatoa maagizo ya kukiharibu kulingana na kitu chenyewe kilichokamatwa ili yatekelezwe haraka.

7.Ofisa wa polisi ambaye atatekeleza hati ya upekuzi kulingana na aya ya 3 ya amri hii mara tu baada ya utekelezaji wa hati ,atampa mtu aliyepekuliwa,au mmiliki au mmiliki wa ardhi,jingo lililopekuliwa,au ataacha ikiwa imejitokeza kwenye hiyo ardhi au jengo,kama itakavyohitaji,notisi ilivyopangwa:-

(a)Jinan a cheo cha ofisa wa polisi.

(b)Jina la Hakimu aliyetoa hati na siku iliyotolewa.

(c)Maelezo ya kitu kilichokamatwa na kuondolewa kulingana na hati.

8.Ofisa wa polisi anayefanya kulingana na aya ya 3 ya amri hii atalindwa na kifungu cha 226 cha kanuni ya kudumu ya jeshi la polisi anapofanya upekuzi.

9.Utekelezaji wa mapatano kuhusiana na hati ya upekuzi unamkataza ofisa wa polisi kufanya upekuzi kwa njia ya kuingia uvunguni mwa mwili wa mtu unayempekua.

SEHEMU YA II

SHERIA YA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU,SURA 256 MAREJEO YA 2002.

10.Chini ya sehemu ya amri hii mapato yatokanayo na uhalifu maana yake ni mali yoyote ambayo imetafutwa,imechumwa au kupatikana,moja kwa moja na mtu yeyote kutokana na:-

(a)kufanya kosa lolote kubwa

(b)Kufanya kitendo chochote au kutofanya ambacho:-

(i)kimetokea nje ya Jamhuri ya Muungano.

(ii)kinahusiana na dawa za kulevya na,

(iii)iwe kama kimetokea ndani ya Jamhuri ya Muungano,ni miongoni mwa makosa ya kukamatwa au kosa kubwa la dawa za kulevya.

(c)Wajibu wa jeshi la polisi ni kupeleleza au kusimamia uharibuji wa mali zilizopatikana au kuzalishwa na mtu yeyote kutokana na kutenda kosa.

11.Pale ambapo mali inadhaniwa ni pato linalotokana na uhalifu na

kutwaliwa ,mkurugenzi wa makosa ya jinai au ofisa aliyeidhinshwa nay eye kwa maandishi atandaa kwa utunzaji wa mali na atahakikisha kuwa hatua zote za msingi zinachukuliwa kwa ajili ya matunzo.

12.Baada ya utwaaji kufanyika ,mkurugenzi wa makosa ya jinai atawasilisha shauri kwa mwanasheria mkuu kwa maombi ya katazo au amri ya kuhaka mali ilyotwaliwa.Pale ambapo ombi limekataliwa mkurugenzi wa makosa ya jinai atamwelekeza ofisa anayehuika kupanga utaratibu wa kurejesha mali kwa mwenyewe mapema kadri inavyowezekana.

13.Uangalizi wa mapato yanayodhaniwa yamepatikana kwa njia ya uhalifu ufanywao na polisi kwa kawaida unafanywa kwa amri ya mahakama kufuatiwa na maombi ya mkurugenzi wa mashitaka.Katika mazingira yoyote yale amri ya uangalizi haitatolewa kwa mtu yeyote (ikiwemo mahakama)isipokuwa askari polisi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

14.Katika mazingira yoyote,pale ofisa wa polisi atakapotakiwa na Hakimu kutoa taarifa ya amri ya uangalizi ,ofisa huyo atamkumbusha Hakimu juu ya jambo hilo kwa kurejea kifungu cha 66 cha sheria ya mapato yatokanayo na uhalifu ,sura 256 marejeo 2002 ambayo inakataza utoaji wa taarifa hizo.

15.Mkurugenzi wa makosa ya jinai bila kuchelewa atafanya mawasiliano na mwanasheria mkuu kwa taarifa yoyote ya amri ya uangalizi iliyotajwa kwa mahusiano ya kosa lililotendwa nje ya nchi.

PGO - 223

MALI ILIYOTAIFISHWA

UTUMIAJI

1.Mali zote ambazo kwa amri ya mahakama ambazo zimetaifishwa zinakuwa mali za serikali.Mali zilizo chini ya uangalizi wa polisi ambazo zinahusika na amri ya kutaifishwa lazima zitumiwe kwa mujibu wa amri hii.

Silaha na Risasi

2.Silaha na risasi ambazo zimetaifishwa kwa amri ya mahakama zitashughulikiwa kwa mujibu wa maelekezo yaliyo katika amri ya kudumu ya Jeshi na.276.

Milipuko

3.Milipuko iliyotaifishwa inayosubiri kuhalibiwa itatunzwa katika sehemu salama baada ya kushauliana na mkaguzi wa ndani wa milipuko.Milipuko kwa kawaida inaharibiwa kwa kutupwa katika kina kirefu ch maji,lakini pale ambapo hili haliwezekani kuharibiwa kwake kutafanywa kwa kufuata maelekezo ya mkaguzi wa milipuko.

Silaha Hatari

4.Maombi lazima yafanywe kwa Hakimu kwa ajili ya amri ya kuhari,kuondoa au kutumiwa silaha zilizotaifishwa katika mikono ya polisi. Katika masanduku mazuri,maofisa wataziwasilisha silsha kwa Mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai kwa ajili ya kuziweka katika makumbusho ya polisi.

Makosa ya uhujumu uchumi

5.Amri ya kutaifisha inayotolewa na Mahakama chini ya kifungu 60(5) cha sheria ya makosa ya uhujumu uchumi,sura 200 marejeo ya 2002,mahaka yaweza,chini ya kifungu hichi kutoa utaratibu wa utumiaji wa mali hiyo.

Hongo

6.Amri ya utaifishaji itafanywa chini ya kifungu 17 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa,sura 329 majeo ya 2002.Kifungu hiki kinaeleza kuwa fedha zote ambazo zimetaifishwa zitapelekwa katika mfuko mkuu wa hazina na zitakuwa sehemu ya pato la serikali.Amri ya kudumu ya Jeshi na.241 nayo pia itatumika.

Mali iliyochukuliwa na polisi chini ya sheria ya mwenendo wa makosa ya jina au sheria yoyote.

7.Mali zilizo chukuliwa na polisi chini ya sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai,sura ya 20 au sheria yeyote na utaifishaji wa mahakama utafanywa kw kumujibu wa sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai,sura 20 au sheria inayotumika.

Dawa hatari na sumu

8.Pale sumu na dawa hatari zinapotaifishwa,ofisa ayehusika atawajibika kupata amri ya mahakama ikimwiidhinisha kuyapeleka kwa ofisa madawa kwa ajili ya kuyateketeza.

Mali za wizi na zinazodhaniwa ni za wizi

9.Mali za wizi na zidhaniwazo ni za wizi ambazo zimechukuliwa na polisi zitatumiwa kwa mujibu kifungu cha 43 cha sheria ya jeshi la polisi na polisi wasaidizi,sura 322 marejeo ya 2002 kama mwenyenayo hawezi kutambulika.

Mali iliyookotwa

10.Maofisa wa plisi wanatakiwa kuchukua jukumu kwa mali zote zilizookotwa ambazo zaweza hamishika na kutengeneza orodha yake na kuiwasilisha kwa hakimu.Hakimu atatoa amri ya kutunza mali hizo na kutaka notisi iwekwe nje ya kituo cha polisi ikionysha orodha ya mali hizo na kuwataka watu waliopotelewa wawasilishe madai ndani ya miezi sita baada ya notisi.Kama mali itabaki bila madai ya mtu yeyote,mali itauzwa kwa amri ya mahakama na mara moja nusu ya pato hilo itaingizwa katika mfuko wa tozo na tuzo za polisi,uwiano huo wa baki kama ambavyo hakimu aweza elekeza kiasi kilipwe kwa muokotaji na baki nyingine iende kwenye mfuko wa hazina.Amri ya kudumu ya Jeshi na.304 nayo pia itatumika.

Rejista ya vielelezo

11.Mkuu wa kituo cha polisi atahakikisha kolamu ya 6 na 9 ya rejista ya vielelezo inajazwa kulinga na maelezo yaliyo kwenye amri ya mahakama.Sahihi ya ofisa anaetunza mali siku zote itawekwa katika kolamu ya 13.

Uhifadhi wa mali iliyotaifishwa

12.Mali iliyotaifishwa itachukuliwa kwa haraka,itahifadhiwa katika bohari vielelezo ya polisi ikisubiri kutumiwa au kuchukuliwa.Wakati mahakama itawajibika kwa uuzaji na haina sehemu ya kuhifadhi,mali hiyo yaweza kuhifadhiwa katika bohari ya vielelezo ya polisi na kushughulikiwa kwa mujibu wa amri ya kudumu ya Jeshi na.229 kwa vile sehemu salama na uwekaji alama ndio pekee inayohusika.

AMRI YA KUDUMU YA JESHI LA POLISI NA.224

UHAlLIFU NA MATUKIO-MAKUBWA

1.Maofisa wa kamandi wote wanawajibika moja kwa moja kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kwa:-

(a) utawala makini kwa maeneo kwa wao kuwajibika.

(b)kuhakikisha wanasimamia popote na kadri itapolazimu juu ya uzuiaji na utambuzi wa uhalifu.

(c)kuhakikisha kwamba upelelezi na uendeshaji wa kesi mahakamani

unafanywa kwa umakini na mafanikio.

2.Maofisa wa kamandi wanatakiwa kuzuru bila kuchelewa katika matukio yote makubwa yanayotokea katika kamandi ispokua pale ambapo watajilidhisha kwamba uwepo aidha si wa lazima au hauwezi kutekelezeka kutokana na majukumu mengine.

3.Wakuu wa upelelezi Mkoa na Wilaya wanatakiwa kufika wao wenyewe katika maeneo ya matukio yote ya mauaji,unyang'anyi wa kutumia silaha na uhalifu wowote mkubwa isipokuwa pale tu watakapokuwa wamesamehewa kufanya hivyo na wakuu wao wa kamandi.

4.Wakuu wa polisi wilaya na vituo wao watafanya hivyohivyo kuwa watafika eneo la tukio na katika matukio mengine makubwa yenye kufanana na hayo yakiwemo makosa makubwa ya ajali za usalama barabarani,moto na majanga,isipokuwa kama uwezekano wa kufika ni mdogo.

5.Wakuu wa kikosi cha usalama barabarani watafika katika matukio yote makubwa ya ajali za usalama barabarani.

6.Maofisa wote ambao amri hii inawahusu watachukua hatua zote muhimu kuhakikisha kwamba wanakuwa karibu na makao makuu yao wakati wa kutokuwepo kwao katika maeneo ya matukio au uhalifu.

PGO - 225

MIILI YA MAREHEMU

SEHEMU YA KWANZA

1. Iwapo Afisa wa POlisi atakuta mwili wa marehemu katika maeneo ya miji ukiwa katika eneo la wazi au ndani ya jengo na endapo mazingira ya kifo hicho yametokana na, au inakisiwa kuwa sababu za kifo hicho sio cha kawaida, atatuma taarifa katika kituo cha Polisi kilicho karibu. Afisa anayesubiri kuwasili kwa Afisa wa upelelezi atafanya:-:-

(a) Atauacha mwili wa marehemu bila ya kuugusa katika sehemu uliokutwa;

(b) Atabakia sehemu ulipo mwili na kama inawezekana ufunikwe;

(c) atahakikisha sehemu kuzunguka mwili inabakia kama ilivyo;

(d) Alama za nyayo za miguu alizozikuta zitafikwa bila ya kuharibiwa;

(e) Atakagua eneo lote la karibu kuzunguka eneo la tukio kuona kama kuna silaha lakini hapaswi kuzigusa au kuziondoa

(f) Kukusanya pamoja ushahidi wowote unaoweza kuwepo katika eneo la tukio

2. Katika maeneo ya Vijijini ambayo yapo mbali kituo cha Polisi, Afisa wa atakayekuta mwili wa marehemu katika mazingira yanayofanana na ufafanuzi uliotolewa hapo juu, atachukua hatua kama zilivyoainishwa kwa mwili uliokutwa katika mazingira ya mjini, isipokuwa kama inaaminika kutakuwa na uchelewaji katika kumpata afisa wa

upelelezi,kwanza atatuma taarifa katika kituo cha Polisi kilicho karibu au katika mamlaka ya serikali ya mtaa na kisha atachukua hatua za kufanya upelelezi yeye mwenyewe kuhusiana na mazingira ya kifo.

3. Mara baada ya kupokea taarifa katika kituo cha Polisi kuhusu kupatikana kwa mwili wa marehemu katika mazingira ya kutatanisha,Mkuu wa kituo cha Polisi atachukua hatua za haraka kama zilivyoelezwa katika P.G.O. NO. 311.

4. Katiaka eneo la tukio, afisa wa upelelezi atafanya jitihada za kutafuta sababu za kifo. Kama anadhani kuwa mtu huyo amekufa kutokana na sababu ambazo sio za kawaida.ikiwa ni;

(a) Amejiua yeye mwenyewe; au

(b) ameuawa kwa bahati mbaya; au

(c) amekufa katika mazingira ambayo yanaonyesha kuwa kunaweza kuwa na kosa ambalo limetendeka, atafanya:-

(i) atafanya taratibu za kuchukua picha ya eneo la tukio na mwili wa marehemu kabla mwili aujafanyiwa uchunguzi au kuondolewa sehemu ulipo.

(ii) atachukua kumbukumbu ikieleza hali na namna mwili wa marehemu ulivyokutwa kuhusiana na maeneo ulipokutwa na mazingira mengine kulingana na kesi yenyewe;

(iii) atachunguza kuwapo kwa silaha na ushahidi mwingine katika eneo la tukio na kuandaa taarifa ya kina kuhusiana na vitu vilivyokutwa na mahali vilipokutwa katika kuoanisha na mwili wa marehemu;

(iv) Mwili uchunguzwe kwa umakini na kuandaa orodha kamili ya vitu vyote vilivyokutwa kwa marehemu au vilivyo chini ya Polisi ambavyo vinahusiana na kesi. Vitu hivi vitaorodheshwa katika kitabu cha mkononi cha afisa husika na baadaye kuingizwa katika kitabu cha taarifa na faili la kesi. Kama mwili utakuwa tayari ulishafanyiwa uchunguzi kabla ya Polisi kuwasili na kukuta vitu na nguo za marehemu vimeondolewa vitachukuliwa na afisa muhusika vikiorodheshwa katika risiti , na atabaki na nakala moja ya risiti ya vitu hivyo;

(v) Atakusanya pamoja ushahidi wote katika eneo la tukio na kuweka kumbukumbu zao na majina yao kwenye kitabu chake cha kumbukumbu.

(vi) Katika eneo la tukio lolote la kujiua,atafanya uchunguzi kuona kama kuna barua yoyote iliyoachwa na marehemu. Barua hiyo itahifadhiwa kama ushahidi kama ushahidi katika uchunguzi rasmi wa kisheria,Such letter will be put in as evidence at the inquest, lakini hairuhusiwi katika mazingira yoyote yaliyomo katika ushahidi uliokusanywa kusambazwa kwenye vyombo vya habari;

(vii) Atachukua hatua zote zinazostahili kuhakikisha mwili umetambuliwa.Ikiwa haiwezekani kutambuliwa kabla ya kuondolewa sehemu ulipo, mwili utachukuliwa alama za vidole na kupigwa picha ukiwa na mavazi yaliyokutwa nao na kwa kadiri itakavyowezekana uwe katika hali ya kawaida kama akiwa hai. Picha zitakazopigwa zionyeshe moja uso kamili na moja ionyeshe umbo kwa upande. Negativu, pamoja na picha moja, na fomu za alama za vidole maabara ya kitengo cha

uchunguzi.Nakala zingine za picha zitaambatanishwa na maelezo yake ambazo zitasambazwa katika vituo vya Polisi vilivyo karibu.

(viii) Kabla ya mwili kuondolewa katika eneo la tukio,lebo ya sababu za kifo cha marehemu (P.F.165) itafungwa katika kifundo cha mguu au sehemu nyingine ya mwili.

(ix) Atahakikisha mwili wa marehemu umeondolewa na kupelekwa sehemu ya kuhifadhi maiti, Kituo cha Polisi au sehemu nyingine muafaka,na kama inawezekana katika jeneza la kuhifadhia maiti ikisubiri kufanyiwa uchunguzi wa kidaktari.

5 Iwapo mwili umekutwa na hakuna mazingira yanayotiliwa mashaka,afisa aliyeko katika eneo la tukio atatuma taarifa kwa simu au maneno katika kituo cha Polisi kilicho karibu na atachukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuweka kumbukumbu ya maandishi ya eneo sahihi ulipokutwa mwili;

(b) Atabakia sehemu mwili ulipo hadi kitakapowasili kifaa cha kubebea maiti au sanduku na kuuondoa;

(c) Mwili upelekwe kituo cha Polisi kilicho karibu na atatoa taarifa afisa wa chumba cha mashitaka aliyeko kazini

(d) Mkuu wa Wilaya ajulishwe.

6. Iwapo baada ya uchunguzi wa awali, Polisi itabainika kuwa marehemu amekufa kutokana na vurugu au kifo ambacho sio cha kawaida au amekufa akiwa jela au mahabusu ya Polisi, Mkuu wa kituo husika cha

Polisi, bila ya kuchelewa ataanda taarifa ya kifo katika fomu “B” kwenye sheria ya uchunguzi, sura namba 24 iliyofanyiwa mapitio 2002, na kutumwa kwa Korona mwenye mamlaka ya kisheria katika eneo husika kuandesha uchunguzi, akianzia na taarifa zozote zinazohusiana na sababu za kifo zilizogundulika katika upelelezi na kutoa maoni yake iwapo au sivyo kuwa kifo kimetokana na kutenda au kuacha kutenda kitendo chochote kinyume na sheria.

7. Korona baada ya kupata fomu “B” na baada ya kuona kwamba upepelezi kuhusiana na mazingira ya kifo ni muhimu aweza, kuamuru kwa maandishi katika fomu “C” ya sheria ya uchunguzi sura namba 24 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002, akimtaka Daktari yeyote wa Serikali au kama hayupo Daktari, Mtaalamu yeyote wa afya katika eneo lake la kazi, kuufanyia uchunguzi mwili na kutoa taarifa kwake.

8 Katika hali ya dharura ambapo haitakuwa rahisi kwa Mkuu wa Polisi wa Kituo kupata amri ya Korona, Mkuu wa kituo aweza kutekeleza mamlaka ya Korona kama yalivyoelezwa katika aya ya 7 hapo juu(P.F. 99).

9 Mtaalamu wa afya, baada ya kupokea fomu “C” Sheria ya Uchunguzi Sura ya 24 mapitio ya mwaka 2002 inamtaka kuufanyia uchunguzi haraka mwili wa marehemu ili kubaini sababu za kifo cha marehemu na kuelezea mazingira yanayohusiana na tukio hilo.

10 Endapo amri ya kuufanyia uchunguzi mwili wa marehemu imetolewa afisa wa upelelezi atafanya:-

(a) Atakuwepo wakati wa uchunguzi, na atampa taarifa mtaalamu wa uchunguzi kuhusu mazingira ya kifo ambayo itamsaidia wakati wa

kuufanyia uchunguzi mwili wa marehemu;

(b) Atahakikisha mwili umetambuliwa ipasavyo na mtaalamu anayeufanyia uchunguzi, na kama inawezekana awepo mtu aliyeshuhudia tukio hilo au asipopatikana, awepo mtu au afisa wa Polisi aliyegundua mwili kw mara ya kwanza;

(c) Atahakikisha nguo alizokuwa amevaa marehemu zinaondolewa akiwepo na nguo hizo zijumuishwa katika vitu vilivyokutwa kwa marehemu ataandika kumbukumbu kamili katika kitabu chake cha kumbukumbu. Taarifa ya alama zozote,alama za miburuzo, mfano nguo kuwa na unyevu, pia ataziingiza katika kitabu chake cha kumbukumbu na kasha kuhamishiwa kwenye jalada la kesi. Vitu vingine vyote ambavyo havihitajika kuwa vielelezo, vitakabidhiwa kwa mtu anayestahili kuwa navyo, au vitaharibiwa kulingana na P.G.O. namba 306.

11 Baada ya kukamilisha uchunguzi wa mwili wa marehemu mtaalamu aliyefanya uchunguzi atawasilisha taarifa, ya maandishi, kwa Korona aliyetoa amri ya kufanya uchunguzi katika fomu “C” ya sheria ya uchunguzi wa marehemu Sura ya 24 mapitio ya mwaka 2002. Fomu hii itaainisha sababu za kifo na kuwekwa saini na tarehe na Daktari. Nakala moja itapelekwa kwa Mkuu wa Kituo husika cha Polisi ambaye baada ya kupokea nakala ya fomu “C” atawasiliana na Korona ili kupanga tarehe muafaka kwa ajili ya kuendesha uchunguzi.

SEHEMU YA PILI

UCHUNGUZI WA DAKTARI NA UCHUNGUZI WA KISHERIA WA MAREHEMU
UCHUNGUZI WA KISHERIA (Inquests)

12 Korona hawabanwi na sheria za ushahidi na Polisi, wanapofanya kazi kama maafisa wa Korona wanapaswa kukusanya ushahidi na kuziwasilisha taarifa zoet zilizopo ambazo zitamsadia Korona katika maamuzi kuhusu sababu za kifo.

13 Iwapo, wakati wa uchunguzi wa Korona, itadhihirika ushihidi uliopo unaonyesha kuwa kuna kosa la jinai limetendeka kuhusiana na jambo linalochunguzwa na Korona na akiona kuwa mazingira yafaa kuendelea na taratibu za mwenendo wa mashitaka,anatakiwa chini ya kifungu cha 8 (1) cha Sheria ya Uchunguzi wa Korona Sura ya 24 mapitio ya mwaka 2002 kusimamisha uchunguzi unaofanyika hadi matokeo ya mwenendo wa mashitaka utakapojulikana.

14 Endapo uchunguzi wa Korona utasitishwa kuwezesha taratibu za mwenendo wa mashitaka ya jinai kufanyika na iwapo katika mwenendo huo wa mashitaka ukapelekea mtu au baadhi ya watu kutiwa hatiani, kutopatikana na hatia, kuachiwaau kama wamefutiwamashitaka, Korona aweza:-

(a) ataendelea na taratibu za uchunguzi na kusikiliza ushahidi wa nyongeza au atazingatia ushahidi uliokusanywa katika mwenendo wa mashitaka na kuwa ndio msingi wa kufikia maamuzi ya mwisho au;

(b) Endapo kwa maoni yake ataona kuendelea na uchunguzi hakuna manufaa yoyote kwa umma, atayathibitisha maoni hayo katika mwenendo huo wa uchunguzi,atafunga uchunguzi chini ya kifungu cha 28 cha sheria ya uchunguzi wa Korona Sura ya 24 mapitio ya mwaka 2002 na kuwasilisha nakala ya mwenendo mzima kwa Mkurugenzi wa Mashitaka.

15 Endapo Korona atagundua kuna kosa la mauaji lililofanywa na

mtu au watu wasiojulikana nakala ya mwenendo mzima utapaswa kutumwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi kulingana na kifungu cha 28 cha sheria ya uchunguzi wa Korona Sura ya 24 mapitio ya mwaka 2002.

16 Uongozi wa Reli utapewa tahadhari na nafasi ya kuwezesha kutuma mwakilishi katika uchunguzi wa Korona unaofanyika kwa kifo cha mtu yeyote kilichosababishwa na ajali ya gari moshi.

17 Maombi ya kuairisha uchunguzi wa Korona yatafanywa kwa kesi zote ambazo vifo vimetokana na shughuli za uchimbaji madini mpaka uchunguzi chini ya sheria ya madini Sura ya 123 mapitio ya mwaka 2002 utakapokamilika.

18 Kwa kawaida uchunguzi hauwezi kufanyika bila ya mwili kuonekana. Ukweli kwamba kuna taarifa ya mtu kupotea katika mazingira yanayoleta mashaka hayatoshelezi kuanzisha uchunguzi wa Korona. Hata hivyo, endapo, kuna ushahidi usiotiliwa shaka kuwa kuna mtu amefariki lakini mwili wake hauwezi kuonekana, ndipo ucuhunguzi wa Korona unaweza kufanyika. (Mfano kuzama baharini).

UCHUNGUZI

19 Amri ya Hakimu kulingana na kifungu cha 5 cha sheria ya uchunguzi wa Korona Sura ya 24 mapitio ya mwaka 2002 ni sharti ipatikane kabla uchunguzi wa Korona haujaanza kufanyika. Ni lazima shahidi awepo kutambua kaburi na kama inawezekana kuutambua mwili. Ni muhimu Daktari awepo wakati mwili unafukuliwa kutoka kaburini. Endapo inadhaniwa kifo kimesababishwa na sumu, sampuli ya masalia karibu na ilipozikwa maiti au sanduku zichukuliwe na kuwekewa lakiri na

kuwekwa kwenye chupa ambayo itawekewa lebo kuonyesha ni sehemu gani katika maiti au sanduku sampuli hiyo iepatikana, mfano “juu” “chini”. Endapo kwa maoni ya Afisa wa Polisi au Daktari itaonekana kuwa kusafirisha maiti kutoka sehemu ilipokuwa imezikwa kupelekwa chumba cha kuhifadhia maiti ni hatari kwa afya ya jamii, uchunguzi utafanyika ndani ya kaburi na mwili kuzikwa sehemu ulipokuwa umezikwa. Katika hali yoyote ambapo ni muhimu mwili kusafirishwa hairuhusiwa katika mazingira yoyote kuomba kutumia gari la kusafirishia wagonjwa ili litumike kusafirishia maiti. Gharama za kusafirisha maiti zitagharamiwa na Polisi na Kasma ya Usafiri.

KUINGIA NDANI NA KUFANYA UPEKUZI

SEHEMU YA KWANZA

MAMBO YA MSINGI

1. Kuingia na kufanya upekuzi ndani ya nyumba kutafanyika tu, endapo: -

(a) Kuna hati ya Upekuzi iliyotolewa; au

(b) Katika kutekeleza nguvu za kisheria zilizotolewa kwa maafisa Fulani wa Polisi kuingia ndani na kufanya upekuzi bila ya hati ya kupekulia.

(c) Hakuna mazingira yoyote ambayo polisi aweza kuingia ndani ya majengo binafsi labda tu ana hati ya kufanya upekuzi au amepewa nguvu maalum zinazopatikana katika sheria mbalimbali za Tanzania kuingia na kufanya upekuzi.

KUINGIA NA KUFANYA UPEKUZI UKIWA NA HATI

2. (a) Endapo Mkuu wa Kituo cha Polisi, Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya au Afisa wa Upelelezianadhani ni muhimu kuingia katika majengo binafsi ili kupata mali au kitu chochote ambacho, au kuhusiana na kosa lililofanyika, au kitu chochote ambacho ni muhimu katika upelelezi wa kosa lolote, ataomba mahakamani hati ya upekuzi chini ya kifungu cha 38 cha Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, Sura ya 20 mapitio ya mwaka 2002. Mtu aliyetajwa katika hati ndiye atakayefanya upekuzi.

(b) Kama upekuzi utafanyika kati ya masaa ya machweo ya jua au mawio, Hakimu ataombwa kuidhinisha kufanyika kwa upekuzi huo saa yoyote ya mchana au usiku(kifungu cha 40 cha Sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 mapitio ya 2002).

(c) Iwapo Afisa aliyeelezwa katika aya (a) hapo juu amepata taarifa

na anazo sababu za kuamini kuwa mtu anayetafutwa kuhusiana na kutenda kosa la jinai yupo ndani ya nyumba yoyote, ataomba hati ya kumkamata kwa Hakimu wa eneo husika.

(d) Iwapo kitu chochote kimechukuliwa kutokana na upekuzi uliofanyika, afisa aliyechukua vitu hivyo atatoa risiti kuonyesha kuwa vitu hivyo vimechukuliwa, ikiwa na sahihi ya ya mmiliki wa jingo au ndugu wa karibu au mtu mwingine anayemiliki jingo kwa wakati huo, na sahihi za mashahadi wakati wa upekuzi kma yupo yeyote.

(e) Maafisa wa Polisi wanakumbushwa kuwa kifungu cha 38 (4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai mapitio ya mwaka 2002, inaeleza kuwa Mtu yeyote, aliyepewa nguvu ya kisheria kutoa, kuidhinisha au kufanya upekuzi au mtu yeyote, mahali, jengo, chombo cha moto, behewa,au chombo chochote, Kwa kjiamulia na bila sababu za msingi za kufanya hivyo, kutoa amri, idhini au kufanya upekuzi wa namna hiyo an hatia ya kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu tatu au kifungo kwa muda usiozidi mwaka mmoja.

SEHEMU YA PILI

KUINGIA NA KUFANYA UPEKUZI BILA HATI

3. Iwapo Hakimu awezi kupatikana, au kuchelewa katika kupata hati ya upekuzi kunaweza kuharibu upelelezi wa kesi, kuingia kwa madhumuni ya kufanya upekuzi kunaweza kufanyika chini ya vifungu mahususi ya Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 mapitio ya mwaka 2002, kwa kuzingatia kuwa mambo yote ya msingi yaliyoelezwa katika sheria yamekamilishwa

4. (a) Vifungu vya msingi vya sheria vinavyoelezea kuingia ndani kwa madhumuni ya kufanya upekuzi bila ya hati inapatikana katika kifungu cha 34 (1) ya Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 mapitio ya mwaka 2002, kama yalivyonukuliwa hapa chini: -

"Iwapo afisa wa Polisi mwenye cheo sio chini ya Mkaguzi msaidizi wa Polisi anazo sababu za msingi kuamini kuwa kitu chochote muhimu kwa au kwa madhumuni ya kufanya upelelezi wa kosa lililotendeka ambalo ana mamlaka ya kulipepeleza endapo afisa wa Polisi mwenye cheo sio chini ya Mkaguzi msaidizi wa Polisi ana sababu za msingi kuamini kuwa kitu chochote muhimu kwa au kwa madhumuni ya upelelezi wa kosa lililotendeka ambalo an mamlaka ya kulipeleleza chaweza kukutwa mahali popote katika ndani ya mipaka yoyote au kituo cha polisi ambacho yeye ni kiongozi, au alipopangiwa, na kwamba kitu hicho kwa maoni yake hakiwezi kupatikana bila ya kuchukua hatua za haraka, afisa huyo baada ya kuweka kumbukumbu ya maandishi kuhusiana na mazingira ya maoni yake na kuelezea katika maandishi hayo kwa kadiri inavyowezekana kitu kinachopelekea upekuzi kufanyika, bila ya kuathiri yaliyomo katika kifungu cha 38 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai Sura ya 20 mapitio ya 2002, atafanya upekuzi au ataruhusu upekuzi kufanyika ili kutafuta kitu hicho katika eneo lolota lililopo ndani ya mipaka ya kituo hicho cha Polisi".

JAMBO LA KUZINGATIA: "Sababu za Msingi za kuamini" ni jukumu la mahakama kuamua, baada ya kuzingatia mazingira yote ya msingi yaliyofanya afisa aamini hivyo.

(b) Iwapo Afisa anatekeleza upekuzi chini ya yaliyomo katika

kifungu cha 34(1) cha Sheria ya Polisi na Polisi wasaidizi, Sura ya 322 mapitio ya 2002 kama ilivyonukuliwa hapo juu, anapaswa kuandika amri ya upekuzi katika Fomu ya Polisi namba 91 na, kama yawezekana , kufanya upekuzi kwa mtu ambaye hawezi kumpekua na hakuna afisa mwenye cheo cha, au zaidi ya Mkaguzi msaidizi wa Polisi aliyepo kwa wakati huo, aweza, baada ya kuweka kumbukumbu ya maandishi, sababu za kufanya hivyo, na kumtaka Afisa yeyote wa Polisi kufanya upekuzi na atatoa amri ya kufanya upekuzi kwa maandishi katika P.F.91 kwa Afisa huyo, akifafanua eneo linalofanyiwa upekuzi na, kwa kadiri inavyowezekana, vitu vinavyotafutwa.

(c) Nakala ya kila amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 34 (1) itapelekwa kwa Hakimu aliye karibu haraka iwezekanavyo.

5. Mamlaka ya kuingia na kufanya upekuzi bila ya hati ya upekuzi yaliyomo katika kifungu cha 34 (1) cha Sheria ya Polisi na Polisi wasaidizi, Sura ya 322 mapitio ya mwaka 2002 yanaongozwa na, kwa kadiri vifungu vilivyomo vyaweza kutumika, vifungu vya 40, 43, na 44 vya Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai Sura ya 20 mapitio ya mwaka 2002. Vifungu hivi ndivyo vinavyosimamia ni muda gani upekuzi utafanyika, namna utakavyofanyika na jinsi ya kuhifadhi mali zilizochukuliwa kwenye upekuzi. Vifungu hivi vimenukuliwa hapa chini: -

(a) “KIFUNGU CHA 40 CHA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI SURA YA 20 MAPITIO YA 2002.

Kila hati ya upekuzi yaweza kutolewa na kutekelezwa siku yoyote(ikijumuisha Jumapili) na yaweza kutekelezwa kati ya masaa ya mawio na machweo ya jua lakini mahakama yaweza baada ya maombi

ya Afisa wa Polisi au mtu mwingine ambaye ameidhinishwa na kumruhusu atekeleze hati ya upekuzi katika muda wowote".

(b) "KIFUNGU 43 CHA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI SURA YA 20 MAPITIO YA 2002

(i) Endapo jengo lolote au eneo jingine linalopaswa kupekuliwa limefungwa, mtu yeyote anayeishi ndani ya jengo hilo, au kiongozi wa jengo au eneo hilo anapaswa, kwa matakwa ya Afisa wa Polisi au mtu mwingine anayetekeleza hati ya upekuzi, na baada ya kuonyesha hati, atamruhusu aingie, na kumuwezesha kufanya upekuzi ndani na kumruhusu kutoka baada ya upekuzi.

(ii) Iwapo idhini ya kuingia ndani au kutoka nje ya jengo au eneo jingine haiwezi kupatikana, Afisa wa Polisi au mtu mwingine anayefanya upekuzi aweza kuendelea na upekuzi kama ilivyoelezwa katika vifungu vya 19 au 20,

(iii) Endapo mtu yeyote katika au kuhusu jengo hilo au mahali anadhaniwa kumficha kitu chochote ambacho upekuzi ni sharti ufanyike,mtu huyo aweza kapekuliwa. Kama mtu huyo ni mwanamke, masharti ya kifungu cha 26 kitazingatiwa. Kifungu cha 26 kinaeleza kuwa endapo anayepekuliwa ni mwanamke, upekuzi ufanywe na mwanamke mwingine kwa kuzingatia heshima na utu."

JAMBO LA KUZINGATIA: Kwa ufafanuzi zaidi wa (ii) hapo juu, tazama aya ya 8 na9yautaratibuhuu.

(C) "KIFUNGU CHA 44,SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI SURA YA 20 MAPITIO YA MWAKA 2002.

(i) Endapo kitu hicho kimechukuliwa na kutolewa mbele ya Mahakama,

chaweza kuzuiliwa mpaka mwisho wa uchunguzi wa kesi, uangalifu wa hali ya juu uchukuliwe katika uhifadhi wake.

(ii) Iwapo kuna rufaa iliyokatwa,au kama mtu yeyote ameshitakiwa, Mahakama inaweza kuamuru vitu hivyo kushikiliwa kwa madhumuni ya kukata rufaa au kesi kusikilizwa.

(iii) Kama hakuna rufaa iliyokatwa, au kama hakuna mtu aliyeshitakiwa kwa ajili ya kesi kusikilizwa, Mahakama itaelekeza mali/vitu kurejeshwa kwa mtu ambaye vitu vilichukuliwa, labda tu kama Mahakama yoana inafaa au ina mamlaka au kwa mujibu wa sheria inatakiwa kuviharibu au vinginevyo".

6. Iwapo upekuzi umefanyika chini ya kifungu cha 34cha Sheria ya Jeshi la Polisi na na Polisi Wasaidizi,Sura ya 322 mapitio ya 2002 au chini ya kifungu cha 38 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai Sura ya. 20 mapitio ya mwaka. 2002, polisi wanalazimika na kifungu kidogo cha 34 (6) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya .322 mapitio ya mwaka 2002 kuruhusu mkazi, au mtu mwingine kwa niaba yake, kuwepo wakati upekuzi uafanyika, kama waona yafaa.

Kuingia na kufanya upekuzi ketekeleza ukamataji bila Hati

7. Kila inapowezekana Afisa Polisi atafanya ukamataji akiwa na hati, lakini katika hali ya dharura, au pale ambapo hati haiwezi kupatikana kwa muda muafaka, anaweza kukamata bila ya hati, kama ameajiriwa kisheria kufanya hivyo. Mamlaka ya kukamatwa bila hati ni kama ifuatavyo:

-

"KIFUNGU CHA 14 –SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI. SURA YA 20 MAPITIO YA MWAKA 2002"

Afisa Polisi yeyote anaweza, bila amri kutoka kwa Hakimu na bila ya hati, kumkamata: -

(a) mtu yeyote ambaye anatenda uvunjaji wa amani mbele yake;

(b) mtu yeyote ambaye kwa makusudi anamzuia Afisa Polisi wakati katika utendaji wa kazi yake, au ambaye alitoroka au anajaribu kutoroka chini ya ulinzi halali;

(c) mtu yeyote ambaye anamiliki kitu chochote kinachoaminika ni mali ya wizi au anayedhaniwa kutenda kosa linalihusiana na mali hizo;

(d) mtu yeyote ambaye yeye anaona anadanganya au kuzurura katika barabara kuu, yadi , au sehemu nyingine wakati wa usiku na ambaye katika mazingira ya msingi anamhisi ametenda kosa au ana nia ya kutenda kosa au ambaye anamiliki silaha bila ya halali vifaa vya kuvunjia nyumba;

(e) mtu yeyote ambaye ana sababu ya kuamini hati ya kukamatwa imetolewa;

(f) mtu yeyote ambaye anatuhumiwa katika mazingira ya msingi kuwa anahusika kutenda kitendo chochote katika sehemu yoyote nje ya Tanzania ambapo, kama kimetendeka Tanzania, angeweza kuadhibiwa kwa kutenda kosa hilo, na kwa mkosaji wa kosa lililo chini ya Sheria ya Makosa yanayotakiwa mtuhumiwa arejeshwe akashitakiwe kwao Sura ya 368 (Extradition Act) au vinginevyo, anapaswa kukamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi nchini Tanzania;

(g) mtu yeyote ambaye anafanya kitendo chochote ambacho ni cha kudharau nembo ya Taifa au Bendera ya Taifa;

(h) mtu yeyote ambaye anatuhumiwa kuwa ni Mzururaji".

"KIFUNGU CHA 28 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya . 20 MAPITIO YA MWAKA 2002"

Nguvu ya ziada ya kukamata imetolewa kwa afisa yeyote Mkuu wa kituo cha Polisi ambae anaweza kukamata au kusababisha kukamata bila ya Hati ya kukamata:

(a) mtu yeyote ambaye anachukua anachukua tahadhari ili kuficha uwepo wake ndani ya mipaka ya kituo hicho katika mazingira ya kuwa na sababu ya kuamini kwamba anachukua tahadhari hiyo kwa lengo la kutenda kosa ambalo aweza kukamatwa bila ya hati ya kukamata;

(b) mtu yeyote ndani ya mipaka ya kituo hicho ambaye hana njia halali ya kujikimu au ambao hawawezi kutoa sababu ya kuridhisha ya jinsi anavyoishi ,

(c) mtu yeyote ambaye ana sifa za unyang`anyi mzoefu, mvunjaji wa nyumba au mwizi au mpokeaji mzoefu wa mali za wizi, wakati akijua kuwa zimeibiwa au mwenye sifa za mazoea ya uhalifu wa unyang'anyi wa kutumia nguvu, au ili kutenda uhalifu wa unyang'anyi wa kutumia nguvu, mhalifu mzoefu wa kuwatisha watu na kuwaweka katika hofu ya kuwajeruhi".

8. Ni Lazima kwa mhalifu ambaye hati ya kukamatwa inatekelezwa,au watuhumiwa ambao wamefanya kosa ambalo Afisa wa Polisi anaweza kumkamata bila ya hati, ameingia, au yupo ndani ya jengo au sehemu yoyote, basi, Afisa Polisi aweza, chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai Sura ya. 20 mapitio ya mwaka 2002 baada ya kutimiza masharti fulani, ataingia kwa nguvu katika jengo au eneo hilo kama yafaa.

9. Kifungu cha 19 cha Sheria mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya. 20 mapitio ya mwka 2002 imenukuliwa hapa chini:

"(1) Kama mtu yeyote anatekeleza hati ya kukamata, au Afisa Polisi mwenye mamlaka ya kukamata, ana sababu ya kuamini kwamba mtu anaepaswa kukamatwa ameingia katika au yumo ndani ya nyumba yoyote au mahali popote, mtu huyo au Afisa Polisi atamtaka mtu anaeishi katika nyumba au kiongozi wa nyumba au sehemu kumruhusu kuingia ndani, na mtu anayeishi ndani ya nyumba au kiongozi wa eneo hilo anapaswa kmruhusu bila kikwazo kuingia na kumuwezesha kwa msaada uaohitajika kufanya upekuzi ndani ya nyumba au eneo hilo.

(2) Kama ruhusa ya kuingia katika nyumba hiyo au mahali haiwezi kupatikana chini ya kifungu kidogo kilichotajwa awali, itakuwa halali katika hali yoyote kwa mtu yeyote anayetekeleza hati, na katika hali yoyote ambayo hati yaweza kutolewa, lakini haiwezi kupatikana bila ya kutoa nafasi ya kutoroka kwa mtu huyo, Afisa Polisi ataingia mahali hapo na kufanya upekuzi, na ili kuwezesha kuingia ndani au mahali hapo, atavunja sehemu yoyote ya ndani au nje ya mlango au dirisha ya nyumba au sehemu hiyo, ili kufanikisha ukamataji wa mtu huyo au mtu mwingine au kuwezesha kuingia katika nyumba au eneo, ikiwa baada ya kueleze ya mamlaka yake na madhumuni na mahitaji ya kuingia kihalali kufanywa, hawezi kupata idhini vinginevyo, kulingana na kifungu kidogo cha (3).

(3) Kama nyumba yoyote ile au mahali ni katika ghorofa inamilikiwa na mwanamke (si mtu anayepaswa kukamatwa) ambae, kulingana na desturi, hapaswi kuonekana katika jamii, mtu huyo au Afisa wa Polisi atalazimika, kabla ya kuingia katika ghorofa, kutoa notisi kwa mwanamke kuwa ana uhuru wa kuondoka atapewa kila msaada wa kumuwezesha

kutoka, na kisha anaweza kuvunja uwazi katika ghorofa na kuingia ndani . "

MPANGILIO WA UPEKUZI.

10. Iwapo hati ya upekuzi au kukamata imetolewa, Afisa Polisi ambaye hati imeelekezwa aitekeleze atalazimika kupanga mapema operesheni ya kufanya upekuzi, kwa kuzingatia yafuatayo: -

(a)Madhumuni ya kufanya upekuzi;

(b) hali ya nyumba au majengo yatakayofanyiwa upekuzi;

(c) Tabia ya wakazi wa nyumba au majengo, na

(d) kama mali inayotafutwa inaweza kutupwa nje ya madirisha wakati wanaofanya upekuzi wanawasili, au kama kuna uwezekano kwamba mtu yeyote katika majengo atajaribu kutoroka, wanaofanya upekuzi wanapaswa kuwa idadi ya kutosha ili kuweza kuizunguka nyumba au eneo linalofanyiwa upekuzi na wafanyakazi waliowekwa kwenye nafasi hizo waweze kuona madirisha na milango ya majengo na kuzuia mtu yeyote kutoroka kutoka ndani.

Njia ya kufanya ili kuingia ndani

11. Kiongozi wa maafisa-wanaofanya upekuzi, au Afisa Polisi atakayefanya upekuzi, anaweza kwa hiari yake kuomba kiongozi wa eneo husika wenyeji wawili wa eneo hilo kuongozana nao isipokuwa kama hakuna muda wa kutosha kupata huduma zao.

12. Endapo majengo yanayofanyiwa upekuzi ni nyumba ya kuishi,Kiongozi wa maafisa wanaofanya upekuzi atabisha hodi, kujitambulisha, kutoa notisi ya mamlaka yake na kazi ambayo yeye amekuja kufanya na kuwaeleza nia ya kuingiandani lakini kwa lugha ya heshima. Kama amakataliwa kuingia au ombi limepuuzwa, afisa, baada

ya kujaribu mara mbili au tatu kupata ruhusa kawaida, anaweza kuingia katika majengo kwa kuvunja uwazi eneo lolote la nje la mlango au dirisha.

13. ikiwa kuingia kunahitajika ili kutafuta ushahidi ambao unaweza kuharibiwa na wakazi, afisa kiongozi wa timu ya upekuzi ataendelea na upekuzi kwa mujibu wa aya. 12, isipokuwa kwamba yeye aweza kuvunja mara moja kama mahitaji yake ya kwanza kuomba idhini ya kuingia yalikataliwa au kupuuzwa. Endapo inawezekana, hati ya upekuzi au mamlaka nyingine lazima ionyeshwe kwa mkazi.

14. Endapo kuingia kunahitajika ili kuwakamata washitakiwa hatari au wenye silaha au endapo inaaminika wakazi wana silaha au wamekata tamaa na upinzani wa kutumia silaha unaweza kutokea, tahadhari ya kutosha lazima zichukuliwe ili kupunguza hatari ya majeruhi au kupoteza maisha. Afisa kiongozi wa timu ya Polisi kwa kawaida atendelea kwa mujibu wa aya. 13, lakini anaweza kuvunja bila ya kutoa onyo mapema kama yeye anaona kuwa itakuwa ni hatari sana kufanya vinginevyo. kupatikana kwa Kasi ya kuingia ndani kutegemea kiwango cha hatari kinachotarajiwa kutoka wakazi.

15. Kwa kuzingatia kwamba kama sehemu yoyote ya eneo hilo ni ghorofa ambalo linakaliwa na mwanamke (si mtu anayepaswa kukamatwa) ambae, kulingana na desturi, hatakiwa kuonekana kwa umma, Afisa wa Polisi, atatoa notisi kabla ya kuingia kwenye ghorofa,kuwa yuko huru kuondoka katika jengo na atampatia msaada unaohitajika kwa yeye kuondoka na kisha aweza kuvunja uwazi katika jengo na kuingia ndani.

16. Ieleweke kuwa polisi ana mamlaka sawa ya kuvunja uwazi kwenye milango na madirisha kwa ndani au kuvunja milango na madirisha kwa

nje na kuingia ndani.

Njia ya kutekeleza upekuzi ya majengo

17. Endapo nyumba au majengo yanatakiwa kupekuliwa, ni muhimu kwamba upekuzi ufanywe bila ya usumbufu kwa wakazi kwa kadiri iwezekanavyo na kwamba hakuna uharibifu usoi na sababu unaofanyika kwa mali, na kwamba upekuzi uliofanywa ni kwa faida kamili ya ushahidi unaoweza kupatikana.Upekuzi utafanyika baada ya kuzingatia mambo yafuatayo: -

(a) Pale ambapo nafasi ya kuingia kwenye nyumba au eneo, mmiliki atapewa taarifa ya sababu za kufanya upekuzi na kuonyeshwa hati ya upekuzi (kama upekuzi huo ni kwa mujibu wa hati). Anapaswa kisha kuulizwa kama ana vitu au mtu anayetafutwa kwenye majengo. Afisa anapaswa kuweka kumbuka ya jibu katika daftari lake.

(b) Huduma ya kiongozi wa mtaa au mashahidi wawili wa kujitegemea, ambao wanapaswa kuwapo wa kufanya upekuzi, lazima ipatikane. Hii ni kuhakikisha kwamba yeye au wanaweza kuwa katika nafasi ya kutoa ushahidi wa kusaidia kama kitu kinachounganishwa na kosa kimepatikana na kukanusha madai kwamba ulifanywa bila ya uangalifu na mali kuharibiwa.

(c) mmiliki wa nyumba lazima kuulizwa kama ana vito vyovyote au fedha kwenye majengo. Kama anavyo, anapaswa kuvionyesha na kama si mali inayotafutwa) anapaswa kurudishiwa mmiliki yeye mwenyewe. Hii itasaida kuzuia madai yoyote baadae kwamba fedha saa, au vito ziliibwa na mmoja wa waliofanya upekuzi.

(d) Upekuzi ni lazima kufanyika kitaalamu ili kuhakikisha kwamba hakuna sehemu ya majengo imesahaulika.

(e) ikiwa vyumba vyote vya jengo vimepekuliwa, nje ya nyumba, paa, bustani, juu ya miti, nk, lazima basi vipekuliwe.

(f) Kama kitu kinachohusika na kosa kimepatikana, kumbukumbu zitawekwa za mahali kilipopatikana, yaani, kabati, sanduku, nk, katika daftari la afisa. Hii ni muhimu kwani inaweza kasaidia baadae kama kutakuwa na madai kwamba vitu vilipatikana katika chumba cha mpangaji au mtu mwingine au, pengine, kupandikizwa katika nyumba na adui. afisa atakayekuta kitu wakati wa upekuzi lazima pia aweke kumbukumbu kadirio la eneo kitu kilipokutwa kuhusiana na dirisha au mlango kutoka nje.

(g) Tahadhari lazima ichukuliwe wakati wa kufanya upekuzi ili kuhakikisha kuwa hakuna uharibifu unaofanyika wa mali na mali zisihamishwe kama hakuna ulazima wa kufanya hivyo. Iwapo Kwa mfano mavazi, nk, ni vimeondolewa kutoka kabati au masanduku, ni lazima kurudishwa kama ilivyokuwa kabla ya kuanza upekuzi kabla ya kuondoka kwenye majengo.

18. Baada ya kukamilisha upekuzi, taarifa ya upekuzi zitafanywa nje eneo la tukio, kutoa maelezo ya vitu vyote vilivyokamatwa, na nakala itakabidhiwa kwa mmiliki.

19. Taarifa ya upekuzi itaeleza wazi kwamba hakuna kitu chochote zaidi ya vituvilivyoorodheshwa kwenye taarifa ambavyo vimechukuliwa na kwamba hakuna uharibifu uliofanyika. Mmiliki anapaswa kuulizwa kama ameridhika na upekuzi ulifanyika kwa njia sahihi, na kama anajibu kuwa umefanyika sahihi, ukweli lazima uandikwe katika taarifa ya upekuzi.

Afisa wa Polisi aliyefanya upekuzi, mmiliki wa majengo, kama yupo tayari, baada ya kuulizwa, kiongozi wa mtaa au wakazi wenyeji wawili wanapaswa kusaini Taarifa.

Upekuzi wa chombo, ndege mashua, au gari

20. Maafisa wa polisi pia wamepewa mamlaka na kifungu cha 25 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai Sura.ya 20 Mapitio ya mwaka 2002 kusimamisha,kuzuia na kufanya upekuzi wa chombo, mashua, ndege au gari. Kifungu kinaelezi kama iuatavyo: -

(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 50 na 51 cha Sheria hii (CPA), Afisa wa Polisi yeyote anaweza kufanya lolote au yote ya mambo yafuatayo yaani, kusimamisha, kupekua na kushikilia: -

(a) chombo chochote, mashua, ndege au gari katika au ambapo kuna sababu msingi kuhisi kwamba kuna: -

(i) bidhaa yoyote iliyoibiwa;

(ii) vitu vyovyote vinavyotumika au nia ya kutumika katika kutenda kosa;

(iii) bila ya halali, silaha yoyote yenye madhara, vitu vilivyofichwa au vitu vyovyote vivyozuiliwa na sheria yoyote;

(b) mtu yeyote ambaye kuna sababu za kumhisi kuwa ana au amechukua kwa namna yoyote yoyote ya vitu viliyotajwa katika aya ya (a).

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Kifungu kidogo (3), kama wakati wa kumalizika kwa muda kama ulivyotajwa katika kifungu cha 50 kwa ajili ya kumhoji mtu hakuna maombi kwa ajili ya upanuzi wa muda yaliyofanywa au kama maombi ni yamefanywa na yamekataliwa, chombo, mashua , ndege, gari, au mtu, kwa namna itakavyokuwa, itaachiliwa na katika hali hii, bidhaa yoyote iliyokamatwa kutoka kwake atarejeshewa.

(3) Iwapo muda kwa ajili ya kumhoji mtu ni umeongezwa kwa mujibu wa

maombi sahihi yaliyotajwa katika Kifungu kidogo (2), Hakimu, endapo ataona ni muhimu, atatoa amri ili chombo chochote, mashua ndege, au gari kuwekwa kizuiliwa ili kuwezesha uchunguzi zaidi au kwa ajili ya matumizi kama vielelezo katika mashauri mahakamani.

PGO - 227
UPELELEZI-HATI ZA MASHITAKA

1. (a) Iwapo mtuhumiwa ambaye amekamatwa bila hati na kuletwa mbele ya Hakimu, hati rasmi ya mashitaka, zenye maelezo ya kosa na ambayo mtuhumiwa ameshtakiwa, itasainiwa na kuwasilishwa na Afisa Polisi kutanguliza hati ya mashitaka.

(b) Hati za mashitaka zitakazo wakilishwa mbele ya Mahakama ya chini zitaandaliwa kwenye PF 9 katika nakala mbili, kwa uangalifu maalumu na kwa mujibu wa maelekezo yafuatayo: -
(i) Jina, kabila, / utaifa; anwani, umri na kazi ya mtuhumiwa itaingizwa katika nafasi juu ya PF 9.
(ii) Maelezo ya kosa yataandikwa katika lugha ya kawaida kwa kufuata maneno yaliyotumika katika kifungu ya sheria, kwa kadri itavyowezekana kuepuka maneno yenye utata, kwa mfano,
"Wakaivamia Afisa wa Polisi wakati akitekelezaji wajibu wake, kinyume na kifungu cha 243 (b) cha Kanuni ya Adhabu, RE Cap.16 2002 ".

(iii) maelezo ya kosa (makosa) yaandikwe katika lugha ya kawaida, kuepuka utata, kwa mfano,
"John s / o Salim ..... alifanya shambulio (au iliishi) (au kwa makusudi alimzuia) mtu moja ..... afisa wakati anafanya "....

(iv) Kila kosa litatenganishwa na kosa jingine kwa kupewa namba tofauti na kujumuisha shitaka linalomkabili na maelezo ya kosa.

(v) sahihi ya mwendesha mashtaka, Tarehe na kituo itawekwa chini ya hati ya mashitaka.
(vi) nakala duplicate ya malipo (PF 9) itakuweka katika jalada la kesi kwa makosa madogo (vide para 7. (G) ya PGO No 286).

2. Mkuu wa Polisi wa Wilaya na Vituo vya itahakikisha kwamba: -

   (a) maelezo ya kosa yenye maelezo ya kutosha kuunga mkono ushahidi;
   (b) maelezo ya kosa yatarejewa katika shitaka;
   (c) Shitaka na fomu ya maelezo ya kosa yataunda msingi pekee kwa upande wa mashtaka (yaani yaliyoma katika hati ya mashitaka utakuwa ndio msingi wa maafisa waendesha mashtaka ili kuthibitisha

kosa linalobishaniwa).

3. (a) Maafisa watazingatia masharti ya kufungu cha 138 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai Sura ,. 20. UMakini wa kipekee uzingatiwe kwa hoja zifuatazo: -
(i) umuhimu wa kubainisha katika kila shitaka la wizi mmiliki wa kila kitu cha mali zilizoibwa na thamani yake.

(ii) Pale ambapo kuna kufungu kinachobainisha adhabu, ni lazima kinukuliwe katika mashitaka na pia kifungu cha kosa kifafanuliwe.

(iii)Muda ambao kosa limefanyika uelezwe ambapo hiki ni kitu muhimu katika hati ya mashitaka na kutilia maanani ufafanuzi wa neno "usiku" chini ya kifungu cha 5 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya.16 MAPITIO YA 2002.

(iv) Tahadhari lazima zichukuliwe kuepuke kuacha maneno "kwa nia kutapeli (au kudanganya)" kwenye mashitaka kama vile kufanya udanganyifu/ uongo.

(v) Katika kuandaa mashtaka kuhusiana kutoroka chini ya ulinzi halali, Mahakama zinahitaji kuona mazingira ambayo mtuhumiwa alitoroka lazima kuwekwa katika mashitaka, kwa mfano, kama kutoka mahabusu, chini ya hati ya Mahakama, baada ya kukamatwa kihalali na kabla ya kupelekwa mahakamani, au baada ya kutiwa hatiani na Mahakama.

(vi) Katika kesi za kusababisha majeraha mabaya mwili, aina ya majeraha na madhara ya uchungu alioupata mlalamikaji lazima uonyeshwe katika hati ya mashitaka kwa mfano ,, yalileta mpasuko mbele ya mkono wa kushoto, nk

(vii) Mashitakayanayoangukia katika wigo wa vifungu vya 266-275 vya Kanuni ya Adhabu, Sura ya .16 mapitio ya 2002 (yote yakiwemo), lazima pia kurejea kifungu 265 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya .16 mapitio ya 2002 vile vile iwapo wizi unahusisha makosa mengine, kwa mfano, uvunjaji jengo usiku, basi ni lazima hati ya mashitaka kurejea kifungu cha 265 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya .16 mapitio ya 2002.

(viii) Pale ambapo kuna madai ya nia ya kufanya kosa la jinai, kosa hilo la jinai lazima litajwe, kwa mfano, kuvunja na kuingia nyumba ya kukaa, kwa nia ya kutenda ubakaji.

(b) Endapo tendo moja limehusisha idadi ya makosa mbalimbali, kwa mfano, tendo moja la kuua bila kukusudia zaidi ya mtu mmoja, kila mtu aliyeuawa litahesabiwa ni kosa tofauti na mashitaka yote yatawekwa katika fomu moja ya mashitaka. Mfano kama ingekuwa unyang'anyi ambapo vitu vilivyoibwa vilikuwa almasi ambayo bado haijasafishwa na kukatwa. Mshitakiwa atakuwa ametenda kosa la unyang'anyi na kukutwa na almasi bila halali.

(c) mtu ambaye atamjeruhi mwingine kwa nia ya kuiba atashtakiwa kwa kosa la unyang'anyi na katika kosa la mbadala, kujeruhi kinyume cha sheria. Hivyo, kama Hakimu anaona kwamba ushahidi hautoshi kuthibitisha wizi, anaweza kumtia hatiani kwa kosa mbadala la kujeruhi kinyume cha sheria. Njia sahihi ya kuwasilisha mashitaka hayo ni kunza na shitakakubwa (yaani,

wizi) na kisha kueleza katika hati ya mashitaka kuwa kosa la pili la kujeruhi kinyume cha sheria ni mbadala kwa kuingiza maneno "katika mbadala" mara moja baada ya kosa la pili . Hii itaweka wazi kwa Mahakama kwamba shitaka hili ni mbadala na mwendesha anaweza kwenda zaidi, iwapo ni muhimu, kwa kuileza Mahakama kwamba kama hatia itapatikana kwenye kosa mbadala hakuna hatia nyingine itakayotolewa kwenye shitaka lililopo katika kosa jingine mbadala. Kama kesi imepelekwa kwenye Rufaa, na Mahakama ya Rufaa inaona kuwa moja ya mashtaka mengine mbadala yana sababu ya kuachiwa huru na Mahakama ya Chini. Endapo ipo wazi kwa Mahakama ya kutia hatiani kwa makosa madogo chini ya kifungu 181-187 cha Sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai, kosa dogo kamwe lisiwekwe kama shitaka mbadala.

(d) Iwapo kuna mapendekezo ya kuleta mashtaka mawili au zaidi dhidi ya watuhumiwa na moja ya shitaka linahitaji ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka, mashtaka yaliyobaki hayataendelea mpaka maelekezo ya mkurugenzi wa mashitaka ya jinaiyamepatikana. Barua yenye maelezo au muhtasari utapelekwa kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai na na jalada la kesi ni lazima lieleze hali ya halisi ya mashtaka yoyote ambayo yanasubiri.

(e) Mshtakiwa anaweza kushitakiwa chini ya kifungu cha 311 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya .16 Mapitio ya mwaka 2002, kwa kosa la kupokea au kuhifadhi.

(f) Iwapo mtu ametenda kosa la kuchoma nyumba kwa nia ya kuua au kutojali uwezekano kwamba kifo kinaweza kutokea, shitaka litakuwa mauaji. Kama kifo kilisababishwa tu katika tukio lenye nia ya kuchoma nyumba na hakuna shaka kwamba hakukuwa na kutojali kwamba kuna uwezekano kifo kitatokea, Jalada la kesi litawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai kwa ushauri kama mashtaka gani yaandaliwe. Endapopo mtu anaweka moto kwenye majengo yanayokaliwa na kuna ushahidi ushahidi kwamba kulikuwa na nia ya kuua mtu, hata kama hakufanya hivyo, shitaka litakuwa kujaribu kuua na shitaka la pili la kuchoma nyumba litaongezwa. Endapo mtu amejeruhiwa kutokana na matokeo ya kuchoma nyumba, shitaka la kujeruhi kinyume cha sheria kifungu cha 222 kitaongezwa, kwa kuzingatia ushahidi ulivyo, kwenye shitaka la kujaribu kuua na shitaka la kuchoma nyumba.

UCHUNGUZI - TAMKO LA KIFO NA UTHIBITISHO

TAMKO LA KIFO

1. Tamko la kifo ni tamko linalotolewa na mtu anayekufa akieleza ukweli na mazingira ambayo yana uwezekano wa kusababisha kifo chake. Kwa mujibu wa kifungu cha 35A cha Sheria ya Ushahidi Sura,ya 6 mapitio ya mwaka 2002 taarifa hizo zinakubalika katika ushahidi katika kesi yoyote ambayo sababu ya kifo cha mtu ndicho kitu kinachozungumziwa na inakubalika hata kama mtu alikuwepo au hakuwepo wakati kauli inatolewa, akiamini kuwa atakufa.
2.Afisa wa Polisi yeyote ambae ameridhika kwamba mtu anataka kutoa tamko la sababu za kifo, kama muda unaruhusu,atamuomba Hakimu kuhudhuria na kuchukua tamko.
3. Kama Afisawa Polisi ana maoni kuwa Hakimu hawezi kuhudhuria kwa wakati yeye mwenyewe ataandika tamko hilo.

4. Afisa wa Polisi ataweka taarifa ya tamko la kifo katika daftari yake au kwenye fomu kuandikia maelezo (PF 2A) katika maneno yanayotamkwa na mtoa tamko mwenyewe.
5. tamko lichukuliwe katika lugha ambayo inatamkwa, kama si kauli ya kuendelea lakini ilitolewa katika njia ya maswali na majibu, maswali na majibu halisi lazima yaandikwe.
6. iwapo tamko limeandikwa, Afisa wa Polisi atamsomea mtoa tamko na kumtaka aweke saini yake au dolegumba.
7. Kisha Afisa wa Polisi ataweka saini yake kwenye tamko pia mtu mwingine yeyote aliyekuwepo na kusikia tamko hilo.
8. Tamko la kifol inaweza kuandikwa na mtu yeyote, ingawa ni vyema likachukuliwa na Hakimu au Afisa wa Polisi.
9. Kama mtu yeyote yupo, anayetuhumiwa kusababisha kifo, hahitajiki kuwepo wakati tamko linatolewa, lakini kama yupo, mtu aliyejeruhiwa apewe nafasi ya kumtambua na kitu chochote kitakachosemwa na mtuhumiwa lazima pia kiwekwe katika maandishi.

UTHIBITISHO WA WATU WALIO MAHUTUTI

10. Kifungu cha 252cha Sheria yaMwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya. 20 Mapitio ya mwaka 2002, kinasema kwamba: -
"Endapo inaonekana kwa Hakimu yeyote kwamba mtu yeyote ambaye ni mgonjwa mahututi au ameumia na hakuna uwezekano wa kupona na anataka kutoa maelezo ya ushahidi kuhusiana na kosa lolote, na si rahisi kuchukua ushahidi wa mtu huyo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Hakimu anaweza kuchukua kwa maandishi,maelezo ya kiapo au tamko la dhati la mtu huyo naye ataandika humo sababu ya kufanya hivyo akionyesha tarehe na mahali wakati na eneo ambalo ushahidi umechukuliwa na kuthibitisha kwamba yamechukuliwa kwa usahihi, maelezo yote ya tamko lililotolewa na mtu huyo na ataihifadhi taarifa hiyo na kwenye faili kwa ajili ya kumbukumbu, isipokuwambapo taarifa imetolewa na mtu ambaye umriwake ni mdogo au matakwa ya imani ya kidini, kwa maoni i Hakimu au imani za kidini haifai, kuapishwa au kupitiwa, kauli inaweza kuchukuliwa bila kiapo au tamko la dhati ".
11. endapo mtu yoyote ameshitakiwa au ameletwa kwa kesi kusikilizwakuhusiana na kosa ambalo linahusiana na maelezo yalichukuliwa, ilani itatolewa ya nia ya kupeleka taarifa ile kwa mwendesha mashitaka na kwa mtu huyo. Kama mtu yupo chini ya ulinzi, anaweza na atapaswa kwa maombi, kuletwa na afisa ambaye mashitaka yapo kwake, chini yaamri,ya Hakimu, kwa maandishi, mahali ambapo taarifa imechukuliwa. (Kifungu cha 253 cha Sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya. 20 Mapitio ya mwaka 2002).
12. Kila taarifa hiyo, inatakiwa kuhalalishwa na kuthibitishwa na Hakimu, kwa namna inavyotakiwa katika aya ya 10, na bila ya kuhitaji uthibitisho zaidi wa ushahidi,utakubaliwa muhtasari wa kesi, uchunguzi wa awali au mbele ya Mahakama Kuu, ambayo mshtakiwa ameshtakiwa kwa kosa ambalo taarifa hizo zilizotolewa zinahusiana kwa msingi kwamba:-
(a) Mahakama imeridhika kwamba mtu ambaye alitoa kauli hiyo amefariki, au kwamba kupatikana kwake hakuwezekani bila uwezekano wa kuchelewa, gharama au usumbufu ambao katika mazingira ya kesi utakuwa hauna maana;
(b) Mshtakiwa amepokea taarifa ya nia ya kuchukua maelezo yake kama

ilivyoelezwa katika aya ya 11 hapo juu na alikuwa na au anaweza kuwa alikuwa, kama angeruhusiwa, kupewa nafasi kamili ya kumhoji shahidi mlalamikaji. (kifungu cha 255 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Mapitio ya mwaka 2002.)
13.Sheria juu yaliyoelezwa yanapatikana katika vifungu vya 252-255 vha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya. 20 Mapitio ya Mwaka 2002.
14. Uthibitisho huo utakubaliwa kama ushahidi juu ya: -
(a) uthibitisho kwamba mlalamikaji amekufa au kwamba kwa sababu yoyote nyingine ya kutosha kuhudhuria kwake hakuwezekani;
(b) ushahidi kwamba taarifa ya kuridhisha, kwa maandishi, ya nia ya kuchukua uthibitisho huo alikuwa amepewa mtu ambaye alitakiwa kuingiza kama ushahidi na kwamba mtu huyo alikuwa na haki na fursa zote za kumhoji mlalamikaji.

PGO - 229

VIELELEZO VYA UPELELEZI

AINA YA VIELELZO

1. Vielelezo kutokana na madhumuni maalum

a. Mali zilizoibiwa pamoja na mali zinazohusishwa na upelelezi wa wahalifu.

b. Mali inayounganishwa na mhalifu kutokana na kuonekana alama za vidole za mhalifu, alama za miguu, damu, nywele na nyusi.

c. Vifaa vilivyohusika katika tukio (kosa), visu, bunduki, wino.

d. Karatasi zinazofanana na kosa linalopelelezwa.

2 (a) Askari wanahusika vilelezo pale tu vinapohitajika kwa upelelezi na mwisho hupelekwa mahakamani kawa ushahidi, au kurudishiwa mhusika mwenyewe au kuharibiwa kutokana na melekezo.

(b) Usalama na utambulisho sahihi wa kuhifadhi vilelezo nio jukumu la afisa kiongozi wa upelelezi mtililiko wa vielelezo vilivopatikana hadi kuhifadhiwa utapangwa na kufanywa na askari wachache kama itakavyowezekana, na askari polisi wa kwanza kukusanya vilelezo atahusika kutoa mahakamani kama kielelezo.

(c) Hakuhitajiki afisa wa juu, kituo kitawajibika kuhakikisha

umakini na usimamizi wa kuhifadhi vielelezo kutokana na umhimu kunatakiwa maelekezo na umakini katika kihifadhi vielelezo na maelekezo yake.

UWEKAJI WA VIELELEZO

3. Vielelezo ni ushahidi, uwekaji au upoteaji unategemea mara nyingi uwekaji na upimaji. Polisi akiwa katika eneo la tukio la uhalifu mjini au karibu na kituo cha polisi anatakiwa kuhakikisha vielelezo haviguswi na eneo la tukio haliingiliwi wala kukanyagwa hadi afisa wa upelelezi atakapofika.

4. (a) Afisa wa polisi atakapofika katika eneo la tukio la uhalifui kitu cha kwanza ni kulinda vielelezo labda ni mhimu kuviondoa katika eneo hilo kiusalama na kuvilinda visiharibike hadi mpelelezi atakapofika. Vielelezo vinavyohusiana na alama za vidole lazima vilindwe kwa umakini mkubwa.

   (b) Kama eneo la tukio lipo wazi na hali ya hewa sio nzuri, afisa wa polisi anakiwa achukue hatua ya kuzuia vielelezo, hasa alama za miguu kwa kuzifunika na maboksi ambayo hayana kitu, ndoo au kitu chochote cha kufunikia.

5. Afisa wa upelelezi anapaswa kuchukua hatua anazofikiri ni za mhimu pindi tu anapofika katika eneo la tukio:- (a) Kupiga picha eneo la tukio pamoja na sehemu yenye kielelezo

   Wataalama wa alama za vidole wanapaswa kuhusishwa ili waweze kuhakiki tukio pamoja na vielelezo.

   (c) Vielelezo vingine ni muhimu vikatafutwa kwa umakini katika tukio na iwapo kama ni lazima picha ziendelee kupigwa kuhusiana na tukio.

   (d) Chukua vipimo vya mpango

   (e) Chukua maelezo kuhusina na mazingira ya namna kielelezo kilivyopatikana.

   (f) Ondoa kielelezo na kihifadhi eneo salama au kilinde kielelezo ndani ya eneo tukio.

6. Tahadhari za makusudi ni lazima zichukuliwe katika kushughulikia vitu vinavyohusu alama za vidole katika eneo la tukio na hasa kabla ya kuwasili kwa mtaalam wa alama za vidole kwa mfano;- (a) Vitu kama bilauri au vinavyofanana na hivyo ni lazima vikashikwa kwa kidole kimoja.juu ukingoni na dole gumba likashika chini kwenye kitako .(b) Kipande cha bilauri ni lazima kikashikwa kwenye kiungo pasipo kugusa kwenye upawa.(c) Chupa ni lazima ikashikwa kwa mkono mmoja kwenye ukingo wa kufungulia na mkono mwengine ukashika chupa hiyo eneo la kitako. (d) Kisu ni lazima kishikwe kwa kidole kimoja kwenye ncha na kidole kingine kishike mwisho wa mpini. (e) Bunduki ni lazima ishikwe pasipo kuharibu alama za vidole kwa hiyo kwa mazingira kama hayo kipande cha kitambaa chaweza kutumika kushika eneo la mtutu. Kwa ujumla bunduki ni lazima iachwe pasipo kufaulisha risasi, hata hivyo tahadhari za makusudi ni lazima zichukuliwe ili kuepusha ajali. Hairuhusiwi kufanyiwa majaribio bunduki hiyo au kuiruhusu. (f) Chombo cha usafiri cha mtuhumiwa kwa haraka kishikiliwe na kuhifadhiwa eneo salama mpaka hapo kitakapohakikiwa. Wakati fulani ni muhumu kuhakiki chombo hicho sehemu ili chombo hicho kipopatikana ili kuepusha kupotea au kuharibika kwa ushahidi(alama za vidole n.k). (g) Unapotafuta nguo za mtuhumiwa umakini uwekwe kwenye zipu za suruali, kwenye pindo, kingo za mikunjo, kwenye mifuko, au ndani ya viatu. Maeneo hayo ni lazima yakahakikiwa iwapo kama kuna madoa au alama zinazohusiana na tukio . Umakini pia ni lazima ukawekwa kwenye kucha za vidole.

7. (a) Vielelezo ambavyo vina alama za vidole, alama au chochote kile chenye thamani kuhusiana na upelelezi wa tukio ni lazima kilindwe kielelezo hicho pasipo kufuta kwa kutumia kitambaa,karatasi au kitu chochote isipokuwa kitu hicho kishikwe kwa kutumia mipira(glove). Umakini ni lazima ukazingatiwa katika kuhifadhi kielelezo hicho na hasa kinapopelekwa katika kituo cha Polisi. (b) Vielelezo vinavyohitaji uhakiki wa kisayansi ni lazima uchukuliwe tofauti kwa kufuata sampuli na hairuhusiwi kuvigusanisha.

KUVIPA MAJINA VIELELEZO

8. Afisa wa Upelelezi ni lazima akaweka majina kwenye kila kielelezo (PF.145). Utaratibu wa kuweka majina kwenye vielelezo unatofautiana kulingana na aina ya kielelezo. Kwa ujumla majina lazima yawekwe kwenye vilelezo ili kuepusha mwingiliana wa vielelezo hivyo.

9. Wakati fulani kipande cha mti hutumika katika kubandika jina la kielelezo.

Kwa mfano kwa bilauri, chupa au kipande cha chupa. Umakini ni lazima uzingatiwe kuhakikisha kwamba jina haliwezi kuziba alama za mtuhumiwa 10.

11.Alama/jina la kielelezo ni lazima likawekwa kwa kutumia kipande cha

karatasi pini haziruhusiwi kutumika. Makabrasha ni lazima yakakunjwa na kuwekewa alama kwa kutumia namba.

12. Alama za vidole wakati wote ni lazima ikawekwa kwenye kielelezo hicho.

13. Iwapo kama kielelezo hicho kipo kwenye wingi wa poda au kimiminika kama vile bangi, sukari, unga,m gongo nk. Kama upo uwezekano anza kupima uzito wa hicho kielelezo pamoja na kibebeo chake kabla ya kuhifadhi kielelezo hicho.

14. (a) Namba ya usajili ya kielelezo ni lazima iwe namba ya jalada la kesi au namba ya kumbukumbu za shtaka. (b) Kwa nyongeza ni kwamba mtiririko wa namba za usajili wa kielelezo ni lazima pia iingizwe kwenye kitambulisho cha kielelezo husika.

15. Iwapo kama kielelezo/vielelezo kitaondolewa kutoka chini ya uangalizi wa afisa mmoja kwenda kwa afisa mwingine,afisa anayekabidhi kielelezo hicho ni lazima akaandika jina/cheo na namba ya afisa anayekabidhiwa kielelezo naye pia akiwepo. Kadhalika tarehe na muda wa makabidhiano itaonyeshwa nyuma ya kelelezo PF.145.

UANDIKISHAJI WA VIELELEZO

16. Kumbukumbu za kila kielelezo ni lazima ziandikwe kwenye kolamu ya kwanza mpaka ya tano katika kitabu cha kumbukumbu za vielelezo PF.16 c ha mkuu wa kituo au afisa yeyote wa polisi aliyekasimiwa na mkuu wa kituo kuhifadhi kitabu hicho.

17. (a) Kolamu ya sita leja ya kielelezo ni lazima ikajazwa na afisa anayepokea na kuhifadhi kielelezo hicho kwenye sehemu salama na maalum ya kuhifadhia.(b) Usafirishaji wowote wa kielelezo hicho ni lazima kiandikwe kwenye kolamu ya 7 na 11 ya leja. (c) Kolamu ya 12 ni lazima ijazwe wakati kielelezo hicho kinapokabidhiwa mahakama kwa risiti (PF.137) (d) Kolamu ya `13 ni lazima ikajazwa iwapo tu kielelezo hicho kinaporudishwa kwa mmiliki au kuharibiwa na mkuu wa kituo na hasa kinapokuwa hakina thamani au kwa amri ya mahakama au mmiliki.

18. (a) Kila kielelezo katika eneo la tukio ni lazima kikaandikwa kwa namba tofauti ndani ya kolamu namba 4 ya leja ya vielelezo/isipokuwa kwa vile vinavyofanana vinaweza vikaandikwa kwa ingizo moja na wingi wak ukaandikwa. (kwa mfano paketi 20 za maziwa zenye majina na ukubwa unaofanana zimeokoewa katika tukio la wizi katika eneo moja na muda unaofanana). (b) Mstari mweusi ni lazima uchorwe chini ya ingizo za mwisho la kielelezo kila kimoja lakini bakisha nafasi ya kutosha ya kuandika hatua za utoaji wa kielelezo.

UHIFADHI WA VIELELEZO

19. Funguo za chumba cha kuhifadhia vielelezo ni lazima zihifadhiwe na mkuu wa kituo au afisa yeyote aliyeteuliwa na mkuu wa kituo ambaye atawajibika kuhifadhi vitu vya chumba hicho, hairuhusiwa funguo hizo kushikwa na afisa yeyote aliye chini ya cheo ya sajenti meja isipokuwa kwa mazingira fulani kwa mujibu wa taratibu za kudumu za kituo husika.

20. Vielelezo vyenye thamani kubwa kama vile vito na pesa ni lazima vifungwe vizuri katika bahasha ya kuhifadhia vitu (PF>166) na kuhifadhiwa kwenye kasiki au sanduku la pesa. Kumbukumbu ni lazima ziingizwe kwenye leja ya kasiki au sanduku la pesa.

21. Mpangilio maalum ni lazima uwekwe na mkuu wa kituo kuhifadhi mafuta pamoja na vitu vyote vya mripuko au vielelezo vya hatari.

22. Bunduku na risasi ni lazima kadri iwezekanavyo vihifadhiwe katika chumba cha kuhifadhia silaha za kituo.

23. Kadri itakavyowezekana wanyama watashikiliwa na mmiliki mwenyewe isipokuwa kumbukumbu kama vile rangi, alama, n.k ni lazima ziandikwe na iwapo kama itawezekana picha ni lazima zichukuliwe. Kabla ya kurudisha wanyama hao kwa mmiliki makabidhiana ya kimaandishi ni lazima yachukukuliwe na afisa anayepeleleza kosa ili wanyama hao watakapo hitajika muhusika aweze kufanya hivyo. Iwapo kama wanyama hao watashikiliwa kwa uangalizi wa polisi basi wanyama hao wawekwe kwenye viwanja vya serikali. Iwapo mnyama ataugua kutokana na majeraha au magonjwa, hakimu akaarifiwe ili atoe maelekezo juu ya namnna ya kufanya..

24. Vielelezo vyenye upana na ukubwa visivyowezekana kuwekwa kwenye chumba cha kuhifadhia vielelezo ni lazima viwekwe salama. Vielelezo vyote ni lazima viwekwe kwenye chumba cha

kuhifadhia vielelezo.

25. Vielelezo vyenye kuharibika haraka na ambavya si rahisi kuhifadhiwa mpaka washauri ni lazima viwasilishwe kwa hakimu pamoja na mtuhumiwa kama yupo na hii itawezesha hakimu kuandika vielelezo pamoja na utaratibu wa kuharibu. Kama upo uwezekano vielelezo hivyo ni lazima vipigwe picha kabla ya kuharibiwa.

26. Iwapo kama kielelezo kitaondolewa kwa muda mfupi na kurudishwa kwenye chumba cha kuhifadhia ingizo la kielelezo hicho ni lazima liandikwe kwenye /leja ya vielelezo PF.16.

UFUNGASHAJI WA VIELELEZO

27. Iwapo kama kielelezo au kupelekwa sehemu yenye umbali fulani, ni lazima kielelezo/vielelezo hivyo vikafungwe kwa uangalifu ili kuepusha mwingiliano wa ushahidi. Afisa anaehusika na ufungashaji wa kielelezo ni lazima ajiridhishe mwenyewe kwamba njia ya usafirishaji iliyochaguliwa inakidhi kuepusha:-

    (a) Upotevu wakati wa usafirishaji

    (b) Mwingiliano unaotokana na ufungashaji

    (c) Kuharibika kutokana na mikwaruzano

    (d) Kuharibika kutokana na kuvuja, kutoonekana, kulipuka n.k

28. (a) iwapo kama afisa wa upelelezi atahitaji masuala ya upasuaji au uhakiki wa viwatilifu (chemicals) kama kielelezo ni lazima akaandaa vitu hivyo a kuvituma kwa copi PF 180 na kuwasilisha vihusika kwa wataalam wa upasuaji au Mkemia wa Serikali. (b) kwa utafiti wa vielelezo vya maandishi, milipuko alama za vidole, nyayo za miguu, sehemu ya kwanza na ya pili ya PF.118 ikajazwa na sehemu ya pili na tatu ikapelekwa kwa idara ya forensic pamoja na kielelezo husika. Sehemu ya kwanza ni lazima ibaki katika kitabu kwa kumbukumbu kitakapofanyiwa kazi na idara ya forensic sehemu ya tatu ya PF.118 kitarudishwa sehemu ilipotoka pale kituoni kikiwa na majibu ya uchunguzi. Baada ya hapo majibu/matokeo yataingizwa kwenye jalada la shauri pamoja na kuingiza kumbukumbu hiyo kwenye kitabu cha upelelezi ikionesha tarehe ya utoaji pamoja na tarehe ya urudishaji ikiwa na nambari ya PF.118. (c) Ni jukumu la afisa mpelelezi kufungasha na kutuma kielelezo kwa njia sahihi ikizingatiwa kwamba kielelezo hicho kina thamani. Kielelezi kinachotumwa kwa ajili ya uhakiki ambacho pia

ni chenye kuharibika haraka ni lazima kisafirishwe kwa njia ya haraka kikiwa kwenye mikono ya askari ambaye amapeewa jukumu la kufanya hivyo. (d) Ikiwa kielelezo kitatumwa kwa njia ya posta ni lazima kisajiliwe stakabadhi ya usajili itaingizwa kwenye kitabu cha kumbukumbu za upelelezi na hiyo stakabadhi itatumwa ikaandikiwe barua au PF.180. (c) Afisa atakayepeleka kielelezo Dar es salaam ataelekezwa kujitambulisha kwa idara ya forensic pindi tu atakapofika ili aweze kupanga utaratibu za kufikishwa kielelezo hicho kwa mtaalam wa upasuaji au mkemia. Ikiwa majibu ya kielelezo yatarudishwa kwa njia ya posta, afisa aliyesindikiza kielelezo ataelekezwa kurudi kituoni kwake haraka. Afisa atapewa risiti ya kielelezo au amri ya kurudi ambayo pia itaonesha usalama wa risiti au vinginevyo kuhusu kielelezo ikieleza njia ya urudushwa wa kielelezo. (d) Uchunguzi kama itakavyoonesha itafanywa kama ifuatavyo:-

(i) Madoa ya damu pamoja nayote yanahusu uchunguzi huo kwa mkuu wa upasuaji, maabara ya kitabibu Dar es salaam

(ii) Madawa ya kienyeji, sumu ikiwemo sumu ya kwenye mshale au sumu yoyote inayotiliwa shaka itapelekwa kwa mkemia wa serikali au maabara ya kitabibu.

(iii) Alama za vidole au nyayo, /maandishi, miripuko itapelekwa kwa idara ya forensic, CID HQ P.O. Box 9094 Dar es salaam

29. Kila kielelezo kifungwe tofauti.

30. \Alama ya ufungaji ambayo ni lakiri ni lazima iwekwe katika kila kielelezo kwa namna kwamba kielelezo kimoja hakiwezi kuingiliana na kingine labda tu endapo alama hiyo ya ufungaji itakapokatika. Mtu yoyote atakaypokea kielelezo ni lazima ahakikishe kuwa uwepo wa alama ya ufungaji ili kuona kama wakati wa upokeaji kila kitu kimekaa mahala pake.

31. Ni muhimu sana kuweka kumbukumbu za kila mtu anayekabidhiwa kielelezo. Hii ni kwa sababu ushahidi utahitajika mahakamani, ushahidi ambao hautakuwa na mashaka katika mwingiliano wa vielelezo kutoka polisi. Kumbukumnbu hizo zitachuukuliwa kwa mujibu wa alama za kielelezo PF.145. Hata askari aliyekabidhiwa kielelezo atalazimika kuweka kumbukumbu katika kijitabu chake cha kumbukumbu ikionesha tarehe, muda na mahala pamoja na jina la mtu aliyemkabidhi kielelezo hicho. Anawajibika pia kuchukua risiti ambayo ataiweka kwenye kijitabu chake cha

kumbukumbu ikionesha namna alivyokabidhi kielelezo.

32. (a) Kielelezo kilichoenda kwa mtaalam wa upasuaji au mkemia wa utafiti kitapelekwa kikiwa ndani ya PF.180. (b) Iwapo uchunguzi zaidi wa kitaalam utahitajika kutafiti kielelezo taarifa sahihi itolewe ikionesha shauri, na mchanganuo wa kielelezo pamoja na kielelezo chenyewe vyote vipelekwe huko kwa mtaalam. Nakala ya taarifa itapelekwa huko kwa mkono au kwa posta zikiwa tofauti.

33. Orodha ya vielelezo vya kesi iliyochapishwa itajumuishwa katika kila jaladala kesi,

HATUA ZA MWISHO ZA KUHARIBU VIELELEZO

34. Ikiwa kielelezo kitatolewa kama ushahidi katika mahakama za chini au kwa hakimu ili kuhakiki kielelezo hicho ni jukumu la mwendesha mashtaka kuandaa kielelezo hicho na kukiwasilisha kwa risiti ya kielelezo cha mahakama PF.137 kwa hakimu kwa lengo la kupata saini ya hakimu kwenye risiti hiyo ya mahakama wakati kesi ikiendeshwa au kipindi cha uahirishaji kesi au wakati wa uendeshaji kesi katika hatua za awali (b) Mwendesha mashtaka anawajibika kuhakikisha kwamba mtirirko wa nambari za risiti unaingizwa kwenye kolamu ya 12 ya daftari la vielelezo vya mahakama na haswa vielelezo hivyo vinaporudishwa kituo cha Polisi.

PGO – 230

UPELELEZI WA ALAMA ZA VIDOLE

MUHIMU:

Mamlaka ya kuchukua alama za vidole kwa watu walio mahabusu inaelezwa chini ya kifungu 35 cha Sheria za Jeshi la Polisi na Askari Wasaidizi Sura 322 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2002 na kifungu cha 59 cha sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura 20 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002. Nakala ya kifungu cha 35 na kifungu 59 zinaambatanishwa kwa kiambatanisho A

1. Mkuu wa kituo atachukua au atamwambia mtu kuchukua alama za vidole kwenye fomu (PF 14B) alama za vidole za mtu yeyote.

   (a) Aliyeko mahabusu anayetuhumiwa au ambaye amefungwa kwa kutokana na kosa fulani

   (b) Aliye chini ya uangalizi wa polisi.

2. Mkuu wa kituo atatakiwa wakati wa kumuweka mahabusu mtu (ambaye hajafikishwa mahakamani) kuchukua au kumwambia mtu achukue alama za vidole vya mtu huyo katika fomu namba 14 B

PALE AMBAPO SHAURI LA KESI LINASIKILIZWA NA MAHAKAMA ZA CHINI YA MAHAKAMA KUU.

Nakala moja ya fomu 14Bpamoja na fumu namba 75 zikiwa zimejazwa kikamilifu zitatumwa kwa idara ya Utambulisho bila kuchelewa kama fomu hiyo itahitaji namba za vifungo vya nyuma vya kwa alama “T” itawekwa kwa wino mwekundu kushoto kwenye kona kwa fomu za alama za vidole. Kama matokeo toka idara ya uUtambulisho yatasema mtuhumiwa apelekwe mahakama Kuu kwa ajili ya kesi, mkuu wa kituo atatoa seti nyingine ya alama za vidole katika fomu ya alama za vidole akioanisha na namba TCRO na namba ya cheti cha vifungo vya nyuma.

B. WAKATI KESI INASIKILIZWA NA MAHAKAMA KUU

Nakala mbili na fomu ya alama za vidole PF 14B ikiwa imewekwa alama nyekundu ya “HC” kona ya fomu hiyo pamoja na PF 75 ikiwa imekamilika, na vyote vitatumwa kwenye Idara ya Utambulisho bila kuchelewa .

3. Endapo mtuhum,iwa aliyepelekwa shaurini na akahukumiwa na mahakama za chini na ikizingatiwa kwamba alama hazikuchukuliwa kama aya ya pili ya

mwongozo huo inavyoeleza, mkuu wa kituo bila kuchelewa atachukua au atamwambia mrtu achukue alama za vidole za mtuhumiwa huyo na ataziwasilisha kama kawaida kwenye idara ya uchunguzi, pamoja na PF 75 na fomu ya matokeo ya kesi PF 102 na hati ya kifungo pale inapohitajika.

4. Pale ambapo itaaminika kuwa mtu aliyewekwa chini ya ulinzi au aliyehukumiwa aliwahi kuhumiwa kabla nje ya nchi ya Tanzania, mkuu wa kituo atachukua au atamwamuru zichuliwe alama za vidole kwenye nakala mbili zaidi za alama za vidole za mtu huyo katika fomu PF 14B kawa kila nchi ambapo inachukuliwa kifungo kilifanyika.

   Alama za vidole za mara moja moja – hatua za kuchukuliwa na mkuu wa kituo

5. Wakati ambapo mtuhumiwa yupo mahabusu na anatuhmiwa na:-

   (a) Kuvunja na kuingia kwenye jengo au

   (b) Wizi wa gari au kuiba kutoka kwenye gari au

   (c) Kosa lolote ambalo inahisiwa mtuhumiwa aliwahi kufungwa kwa kosa moja ya hayo hapo juu kati ya a na b na kwa nyongeza seti ya alama za vidole zitachukuliwa katika fomu moja ya alama za vidole PF 15 na kutumwa pamoja na fomu ya alama za vidole PF 14B kwa Mkuu wa Idara ya Utambulisho kwa kuzingatia maelekezio ya aya ya 2 na 3 ya mwongozo huu.

   Maingizo mhimu ya kuwekwa katika fomu ya alama za vidolea ya PF 15 ni:-

i. Jina la mtuhumiwa/mtu

ii. TCRO namba (kama inajulikana)

iii. Tarehe

iv. Kituo

v. Sahihi ya afisa anayechukua alama hizo za vidole

6. Pale ambapo mtu aliyewekwa mahabusu au kufungwa na siyo mtanzania kwa asili, nakala zaidi za

fomu ya alama za vidole PF14B ikiandikwa na nchi ya asili ya mtu huyo zitatumwa Idara ya Utambulisho. Kwa minajili ya agizo hili mtu ahesabiwa kuwa siyo mtanzania kwa asili kama alikuwa mtanzania kwa uasili.

7. Mtu yeyote atakayekataa kuchukuliwa alama zake za vidole kulingana na aya ya kanza (i) atashtakiwa chini ya kifungu 35 shria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura 322 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002 na baada ya kuhumiwa nguvu ya kadri inaweza kutumika ili kupata alama za vidole.

8. Alama za vidole zitachukuliwa kwa lililooneshwa kwenye kiambatanisho “B” cha Mwongozo huu. Afisa anayechukua alama za vidole atahakikisha kuwa mtu ambaye alama zake za vidole zimechuliwa ameweka saini aua alama ya dole gumba la kulia kwenye sehemu husika nyuma ya fomu ya alama za vidole iliyochapwa PF 14B vilevile ataweka alama ya kidole cha shahada kwenye eneo husika chini ya saini au dole gumba.

   UTARATIBU KATIKA IDARA YA UTAMBULISHO KATIKA KUPOKEA FOMU PF 14B

9. Wakati wa kupokea fomu ya alama za vidole PF 14B Mkuu wa Idara ya Utambulisho atasababisha upekuzi kufanyika katika kumbukumbu za alama za vidole na kuchukua hatua kulingana na aya zifuatazo:-

   Alama za vidole kwa mtu aliye mahabusu (ambaye bado hajafikishwa mahakamani)

   10 (a) kama hakuna kumbukumbu za vifungo / hukumu za nyuma zilizoweza kupatikana kituo kitajulishwa kwa :-

   i. Fomu ya uchunguzi wa matokeo PF 102 A kwa nakala

   ii. Fomu ya matokeo ya shauri PF 102 ikizingatiwa namba ya kesi, jina la mshtakiwa na namba ya muda ya TCRO

   (b)kama kumbukumbu za nyuma zinachunguzwa , Mkuu wa Idara ya Uchunguzi atatuma kituoni:-

i. fomu ya uchunguzi ya matokeo PF 102A kwa nakala

ii. fomu ya matokeo yakesi PF 102 akizingatia namba ya shauri ya jalada lake, jina la mshtakiwa na namba ya TCRO.

iii. Kumbukumbu za mtu/mtuhumiwa PF 18B

iv. Nakala ya fomu ya vifungo/hukumu za mtu za nyuma PF 18C

v. Nakala ya THERMOFAX ya fomu ya polisi kwa watu ambao waliwahi kuhukumiwa.

ALAMA ZA VIDOLE ZA WATU WALIOSHTAKIWA NA KUHUMIWA

11(a) Kama hakuna kumbukumbu zilizopatikana, kituo kitajulishwa kwa matokeo ya fomu ya upekuzi PF 102B ikiwa na nakala.

(b)Kama kumbukumbu za nyuma zitakuwepo Mkuu wa Maabara atajulisha kituo na mamlaka ya magereza kwa :-

i. matokeo ya fomu ya upekuzi PF 102B ikiwa na nakala.

ii. atadurufu hatia za mhusika katika fomu ya polisi namba 18C baada ya kupokea fomu ya alama za vidole za mtu mmoja ambaye ni PF15 Mkuu wa kitengo cha Maabara atachukua hatua zifuatazo:-

12. atazipanga chini ya mfumo wa mikono miwili na kuzifaili katika hatua atakazochukua mkuu wa kituo baada ya kupokea fomu za polisi namba 102A, 102B,18B,18C kutoka kwa Mkuu wa kitengo cha Maabara.

13(a) kwa waliotiwa hatiani

i. Kama hakuna kumbukumbu za kutiwa hatiani atapata nakala ya hati ya kifungo kama itahitajika na kuipeleka kwa mkuu wa kitengo cha maabara kupitia kwa mkuu wa upelelezi wa mkoa, pamoja na fomu ya matokeo ya shauri PF 102 kutoka kitengo cha maabara iliyojazwa kikamilifu.

   Nakala ya fomu 102A itapelekwa kwa mkuu wa gereza ambalo mfungwa pamoja na hati ya kifungo.

ii. kama kuna kumbukumbu za kutiwa hatiani atapata nakala ya hati ya kifungo kama itahitajika na kuipeleka kwa mkuu wa kitengo cha maabara kupitia kwa mkuu wa upelelezi wa mkoa pamoja na fomu ya matokeo ya shauri PF 102 kutoka kitengo cha maabara.

Nakala ya fomu ya polisi PF102A na hatia zilizomo kwenye fomu ya polisi zitapelekwa kwa mkuu wa gereza ambalo mfungwa amepelekwa pamoja na nakala halisi ya hati ya kifungo kama mtuhumiwa amewahi kutiwa hatiani nakala ya THERMOFAX ya PF 18C itapelekwa Hakimu ili kuitunza.

b.kama ataachiwa fomu ya matokeo ya shauri PF 102 kutoka kitengo cha maabara itaambatanishwa na matokeo ya shauri na itarudishwa kwenye kitengo cha maabara pamoja na nyaraka zote kutoka kwenye kitengo hicho PF 18B na 18C.

AKIKANA HATIA ZA AWALI

14(a) kama akikana hatia alizopatikana nazo katika mahakama za chini mwendesha mashtaka atafanya yafuatayo:-

i. Ataomba mhusika awekwe rumande

ii. ataomba jozi za alama za vidole za mhusika zichukuliwe kwenye fomu za alama za vidole PF 14B na kuzipeleka kitengo cha maabara kwa maombi ya kupewa cheti ya kutiwa ambapo mhusika anakana.

(b)baada ya kupokea alama za vidole na maombi kama yalivyoombwa katika (a) ii hapo juu.

Mkuu wa kitengo cha maabara ataanda cheti kutoka kituoni kwenye fomu ya alama za vidole PF 18A kwa njia ya simu ya upepo na kwenye jozi nyingine ya alama za vidole kutoka kituoni.

KUTHIBITISHA HATIA ALIZOPATIKANA NAZO AWALI

15 Hatia za awali zinathibitishwa kwa kutoa hati ya kupatikana na hatia hizo PF18A pamoja na joziya alama ya vidole PF14B ambazo zimechunguzwa katika kitengo cha maabara. Alama za vidole kwenye PF14B lazima zitolewe na mtu aliyechukua alama hizo.

WASHTAKIWA WALIOHUKUMIWA KIFO

16. Ikiwa mtu atatiwa hatiani na kuhukumiwa kifo ofisa kuanzia mrakibu msaidizi wa polisi aliyepo zamu Mahakama Kuu wakati hukumu hiyo ikitolewa, atafanya yafuatayo:-

(a) atachukua alama za vidole vya mtu aliyehukumiwa kwenye PF14B jozi moja

(b) atajaza fomu ya matokeo ya shauri kwenye PF 102 kutoka kitengo cha maabara

(c) apate nakala ya hati ya kifungo

(d) atapeleka fomu zote zilizotajwa kwa mkuu wa kitengo cha maabara ANGALIZO hayo yote yafanyike kabla mahakama haijamaliza shughuli zake.

MTUHUMIWA KUKATA RUFAA AU KUOMBA SHAURI LIFANYIWE MAPITIO

17 Kama katika maombi hayo yamekubalika na hukumu ya awali imepitiwa upya , kitengo cha maabara watamjulisha mkuu wa kituo juu ya suala hilo.

MAJUMUISHO

18 FOMU ZA KUMBUKUMBU (FP 18B) NA FOMU ZA HATIA ZA AWALI (FP18C)

(a) Kwa namna yeyote ilie fomu ya kumbukumbu za mhalifu PF 18B au fomu ya hatia PF18C hazitatolewa mahakamani kama kielelezo. Pia kwenye fomu ya kumbu PF18B hakutaingizwa kitu kipya wala kubadilishwa au kuongezwa kitu chochote.

(b) Alama za vidole za watu hawajatiwa hatiani hazitabakia katika kitengo cha maabara balizitaharibiwa na kumbukumbu kuwekwa katika kitabu cha orodha ya alama za vidole na mkuu wa kitengo cah maabara baada ya kupokea taarifa hizo/

(c) Alama za vidole za ambao hawajashtakiwa zitaharibiwa na kitengo cha maabara.

(d) Fomu ya alama za vidole hazitapelekwa sehemu yeyote nje aya Tanzania bila kupitia kwa mkuu wa kitengo cha maabara Dar es salaam.

(e) Alama za vidole za washtakiwa zilizopelekwa kitengo cha maabara hazihitaji barua ya maelekezo.

(f) Alama za watu wengine wasio washtakiwa kwa mfano polisi, wafanyakazi wa serikali au taasisi nyingine zinapopelekwa kitengo cha maabara lazima ziambatanishwe na barua ya maelekezo.

(g) Kama namba ya TCRO inajulikana lazima inakiliwe.

(h) Kumbukumbu za alama za vidole, picha gazeti la polisi nakadhalika, vitapelekwa kwa mkuu wa kitengo cha maabara kwa anuwani hii:-

Mkuu wa Kitengo cha Maabara,

S.L.P 9094,

Dar es salaam.

(i) Mawasiliano yeyote yanayohusu watu waliohamishishiwa sehemu kwa nguvu, waliofukuzwa, waangaliwa, alama za vidole za wafungwa , picha za wafungwa, hatia za awali, na mashauri ya waharifu yaliyorejewa, kuachiwa nakadhalika, mara zote yatafanywa kwa kuangalia kumbukumbu ya namba ya TCRO.

VIFO VYA WAHARIFU WALIOORODHESHWA

19. Kama kifo cha mharifu aliyeorodheshwa atafahamika mkuu wa kituo atatuma taarifa kitengo cha maabara akiambatanisha alama za vidole za mharifu huyo huku akinakiri namba ya TCRO inayohusika na mazingira ya kifo na alama za vidole za watu waliokufa.

Kata fomu za alama vidole vipande vipande ukifuata mistali iliyokujwa, usikate namba na tarakimu zinazomaanisha kitu fulani. Weka kipande cha kwanza mkono wa kulia kwenye mabano katika kijijko kwa kulegezwa nati na kusukuma juu klampu. Upande wa juu wa kipande utakuwa umeingia chini ya klampu na upande wa chini wa kipande utakuwa umeingia kwenye uwazi wa kijiko. Sukuma kipande ndani ya kijiko mpaka nafasi yote ya dole gumba ya kulia ipo katika nafasi wakati nati itakapokazwa mpaka klampu itakaposhika vizuri kipande hicho. Paka wino dole gumba la kulia na kizuunguushio. Weka dole gumba ndani ya mubonyeo wa kijiko na gandamiza kwenye karatasi. Nati italegezwa tena na kipande kusukumwa mpaka nafasi ya pili iwe kwenye nafasi baada ya mikono yote kuchukuliwa, vipande lazima vibandikwe kwenye fomu ya lama za vidole iliyowazi.

SHERIA YA JESHI LA POLISI NA POLISI WASAIDIZI KIFUNGU CHA 35 SURA 322 KAMA ILIVYOFANYIWA MAREJEO 2002. MAMLAKA YA KUCHUKUA ALAMA ZA VIDOLE NA KUPIGA PICHA N.K ZA WATUHUMIWA AU WALIOPATIKANA NA HATIA.

1. Kila mkuu wa kituo cha polisi au polisi yeyote anayepeleleza kosa, anaweza Kuchukua au kusababishwa kuchukuliwa kwa vipimo au alama za mikono, vidole, nyayo au kuweka kumbukumbu ya sauti, picha au sampuli za mwandiko wa mtu yeyote anayetuhumiwa kutenda kosa awe ameshikiliwa na polisi au vinginevyo kama inaaminika kuwa vipimo, alama, kumbuku picha au sampuli hizo zinaweza kutumika kumtambua aliyefanya kosa hilo au kutumia kama ushahidi wa kosa analoshikiliwa nalo au analoshtakiwa nalo.

2. Kila mkuu wa kituo cha polisi au yeyote anayepeleleza shauri lolote, anaaweza kuchukua au kusababisha kuchukuliwa kwa vipimo, alama za mikono, vidole, nyayo au vidole, kumbukumbu za sauti picha , au sampuli za mwandiko wa mtu yeyote ambaye hajashtakiwa na kosa lolote ikiwa vitu hivyo ni muhimu katika katika kuwezesha upelelezi wa kosa lolote

3. Mtu yeyote awe chini ya ulinzi kisheria, au awe ameshtakiwa lakini hayuko chini ya ulinzi haruhusiwi kukataa kuchukuliwa vipimo, alama, kumbukumbu ya sauti, picha au sampuli za mwandiko wake. Iwapo atakataa, afisa wa polisi anayehusika anaweza kuchukua hatua zinazofaa ikiwa ni pamoja na kutumia nguvu ya kadri ili kuwezesha vitu hivyo vichukuliwe.

4. Mtu yeyote akikataa kuchukuliwa vipimo, alama, kumbukumbu, picha au sampuli za mwandiko kama zinavyotakiwa chini ya sehemu (1) na(2) atakuwa anafanya kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyozidi shini elfu kumi au kufungwa kwa kipindi kisichozidi miezi 24 au vyote, faini na kifungo.

5. Licha ya kuwepo maelekezo katika kifugnu kidogo (10), mtu anayeshikilia vipimo, alama, kumbukumbu, picha au sampuli za mwandiko na kila aliye na nakala za vipimo, alama, kumbukumbu, picha au sampuli ataviharibu ikiwa

(a) Kwa mtu aliyechini ya ulinzi kwa kutenda kosa;-

(i) Kama mashtaka ya Yule mtu hayataendelea

(ii) Kama mashtaka yanaendelea na ameshinda shauri.

(b) Kwa mtu aliyeongelewa katika kifungu kidogo (2) kama vipimo, alama, kumbukumbu, picha au sampuli hizo hazitahitajika tena kwa lengo la kuwezesha upelelezi.

6. Kutakuwa na ofisi itakayoitwa Ofisi ya Kumbukumbu za Wahalifu ambayo itapitishwa na waziri anayehusika na mambo ya upelelezi wa makosa ya wahalifu kwa lengo la kutunza,kulinganisha…… fomu za alama za vidole.

7. Ofisi ya kumbukumbu za wahalifu pamoja na kusimamiwa moja kwa moja na Mkuu wa Jeshi la Polisi na itaongozwa na ofisa wa polisi mwenye cheo

cha juu mtaalam wa kulinganisha alama za vidole atakayeteuliwa mara kwa mara na mwanasheria mkuu wa serikali kwa kumtangaza kwenye gazeti.

8. Fomu za alama za vidole zilizokamilika zitakuwa na kutunzwa katika ofisi ya kumbukumbu za mahalifu.

9. Fomu zote za alama za vidole zitakuwa na mfumo maalum.

10. Pamoja na maelekezo yaliyotolewa katika sehemu ya (5) itakuwa na halali kubaki na kumbukumbu zilizopatikana kufuatana na maelekezo ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya sehemu hii za mtu yeyote aliyeondolewa chini ya sheria ya kuondoa watu wasumbufu au kufukuzwa chini ya sheria ya kufukuza watu wasumbufu sura ya 39 kama ilivyorejewa mwaka 2002 na amri hiyo inafutwa au kusitishwa.

Sheria ya mwenndo wa makosa ya jinai sura ya 20 sehemu ya 59 kama ilivyorejewa ,wala 2002. Mamlaka ya kuchukua alama za vidole, picha n..k za watuhumiwa.

1. Mkuu wa kituo cha Polisi au polisi anayepeleleza kosa anaweza kuchukua au kusababisha kuchukuwa vipimo, alama za mikono, vidole, nyayo au vidole vya miguuni, au kumbukumbu ya sauti au picha au sampuli za mwandiko wa mtu yoyote anayetuhumiwa kutenda kosa awe chini ya ulinzi wa polisi au vyenginevyo. Iwapo ataamua kuwa vitu hivyo vitamsaidia katika utambuzi wa mtu aliyehusika kutenda kosa au kuwa ushahidi kosa analotuhumiwa kutenda.

2. Mkuu wa kituo au polisi anayepeleleza shauri anaweza kuchkua au kusa babisha kuchukuliwa vipimo, alama za mikono, alama za vidole, nyayo, alama za vidole vya miguuni au kumbukumbu ya sauti, picha au sampuli ya mwandiko wa mtu yryote ambaye hajastakiwa na kosa lolote ikiwa

11. Kila mkuu wa kituo anayepokea taarifa ya ukamataji wa mtu anayetafutwa kama ilivyooneshwa katika kipengele cha 10 hapo juu, atasitisha uingizaji wa taarifa za mtu anayetafutwa katika rejesta kwa kuandika neno “amekamatwa” kutoka kona moja hadi kona nyingine ya kurasa akiwa amenukuu rejea ya taarifa ya ukamataji. Nakala mbili za FP.179 zilizowekwa kwenye ubao wa matangazo ya Polisi na utawala zitaondolewa na kuharibiwa.

12. Mkuu wa kitengo cha uchunguzi akipokea taarifa ya ukamataji wa mtu anayetafutwa, atafuta kadi ya jina katika gazeti la polisi, kwa kuzingatia kuwa mtu anayetafutwa ameshakamatwa na kuhusishwa na kesi anayotuhumiwa nayo. Kama atakuwa na shtaka lingine, taarifa katika gazeti la polisi haitafutwa mpaka atakapokamatwa.

13. Mkuu wa kituo ataondoa kadi ya jina katika orodha na kuiharibu. Mkuu wa kitengo cha upelelezi atahifadhi kadi za majina ambazo zina picha tu.

DAFTARI LITAKALOTUNZWA NA KITENGO CHA UCHUNGUZI

14. Mkuu wa kitengo cha uchunguzi atatunza daftari la watu wote wanaotafutwa. Daftari litagawanywa katika sehemu ili kupangwa kwa majina ikionesha tabia zao. aliyeondolewa mjini chini ya sheria ya kuondoa watu wasumbufu au kufukuza watu chini ya sheria ya kufukuza watu wasumbufu Sura ya 39 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002 na amri hiyo ikafutwa.

ALAMA ZA VIDOLE NA ALAMA ZA VIGANJA

UCHUKUAJI WA ALAMA ZA VIDOLE

Vifaa na malighafi

1. Sahani ambamo wino utasambazwa. Hii inaweza kuwa
   (a) sahani ya bati iliyopakwa rangi yenye nchi 4 kwa 12 ambayo itashikwa kwenye .....tofauti la mbao.
   (b) Kipande cha sahani ya vioo yenye vipimo sawa na tajwa hapo juu.
2. Kizunguushio kwa ajili ya kusambaza wino
3. Wino wa lama za vidole
4. Fomu za alama za vidole
5. Vifutio kwa lengo la kufutia
6. Benzine, petroli au spiriti yeyote
7. Meza au stendi kwa mfungwa wa wastaniurefu wa meza au stendi ambayo alama za vidole zitachukuliwa uwe futi tatu na inchi 6. Juu

lazima kulingane na kuwe hakuna vishimo vishimo. Vitofali vya mbao vinaweza kutumika kuinua meza ya kawaida mpaka urefu unaohitajika.

KUWEKA WINO KWENYE SAHANI

(a) Minya matone kadhaa kutoka kwenye tubu katika sahani ya yatawanye mpaka yawe yameenea kwa usawa wa sahani. Wakati wa kutawanya kizunguushio kitolee kwa mbele au nyuma mwisho wa sahani.

(b) Kama wino wa ,majaribio utafifia ongoza mwingine. Kama utakuwa mwingi chukua karatasi weka juu yake na pitisha kizunguushio utapungua.

(c) Wino uwe wa kutosha kiasi kwamba vidole vikizunguushwa juu ya kisahani unaandika bila matatizo.

(d) Kifuniko cha tubu ya wino lazima kiwekwe mara tu baada ya kutumia.

(e) Sahani na kizunguushio lazima kioshwe baada ya matumizi vyombo vichafu huleta matokeo mabaya.

UTAYARISHAJI WA VIDOLE

(a) Vidole vya mtuhumiwa vitaangaliwa na kufutwa jasho na uchafu kwa kutumia kifutiokilicholoweshwa kwa mbali na petroli au sipiriti nyingine majimaji kwenye vidole huzuia wino kujiandika kwenye vidole.

(b) Kama ngozi ni ngumu na kavu lowesha vidole kwenye maji ya vuguvugu na futa kidogo ili usikaushe kabisa.

UWEKAJI WA FOMU ZA ALAMA ZA VIDOLE

(a) Kunja fomu ya alama za vidole kwenye mstali wa kwanzawenye alama “mkunjo” weka sehemu iangalie juu ya meza, na kunja sehemu ya chini yake itazame chini ikaze vizuri kwenye ukingo wa meza unaweza kuwa kitu kizito kidogo ili kuzuia isitoke mezani.

(b) Baada ya kuchukua alama za vidole vya mkono wa kulia fomu hiyo ikunjwe katika mstali wa pili wenye alama “mkunjo” na sehemu ya juu ya fomu iwe juu ikiwa mezani.

(c) Alama za vidole za kulia zikichukuliwa fomu yote iwekwe juu ya meza tayari kwa kuchukua plain impression.

ALAMA ZA MZUNGUUKO

(a) Mchukuaji husimama mwisho wa meza mchukuliwa akiwa mbele yake.

(b) Kidole cha kuchukulia kizuungushwe huku kikiwa kimegusana na kibao chenye wino. Kidole chenye wino kizunguushwe kwenye karatasi ili kuweka alama usigandamize kwa nguvu ili kuhakikisha ngozi inakutana vizuri na kibao chenye wino na karatasi. Kidole cha pili toka dole gumba cha uchukuaji kilale kwa mbali juu ya mwisho wa kidole cha anayechukuliwa iwe nyuzi tisini kwenye ubao na ikunjwe kwenye kiwiko,

(c) Dole gumba na vidole zunguusha upande tofauti dole gumba zunguusha kwa ndani kuelekea kwenye mwili na vidole vingine uzunguushe kwa nje kuelekea nje ya mwili kwa vidole vigumu na vikavu wakati mwingine ni mhimu kuzunguusha vidole mara mbili kwenye kibao chenye wino kabla ya kuchukua alama hii ifanywe kwa uangalifu.

(d) Kama alama itachukuliwa kuanzia juu ya mstali wenye alama “mkunjo” kutakuwa na nafasi ya kutosha kwa alama nyingine kama ya kwanza itakuwa haifai.

(e) Usizunguushe vidole katika kibao kilichotumika kabla hujapitisha tena kizunguushio.

ALAMA TUPU

Alama tupu hupatikana kwa kuchukua kila mkono kuweka vidole vinne kwenye kibao chenye wino hakikisha mkunjo wa mwisho wa kidole unakuwa kwenye ukingo wa kibao hii irudi iwe kwenye fomu ya alama za vidole.

Mkono wa mtuhumiwa uwe umelala sawasawa na vidole viwe pamoja.

ALAMA ZA VIGANJA

(a) Alama za kiganja lazima zioneshe mikunjo yote iliyopo kwenye kiganja kizima.

(b) Alama za kiganja zinapatikana vizuri kwa kutumia PALMA PRINTER.

(c) Safisha kiganja kwa ufasaha na pitisha kizunguushio chenye wino kwenye kiganja. Katikati ya kiganja lazima wino upite vizuri kwani alama zinatakiwa zioneshe mpangilio wote wenye kiganja.

(d) Mwanga wa vidole uwekwe juu ya karatasi iliyoko juu ya kizunguushio, gandamiza kidogo kuhakikisha vimekutana vizuri halafu sukuma kwa mbele na kwa nje kutoka kwenye mwili huku vidole na dole gumba vikiwa vimeachana kidogo.

(e) Kipande cha karatasi chenye ukubwa wa full cap inatosha kwa mikono yote miwili kila upande mkono mmoja.

PGO 231

UPELELEZI – UTAMBULISHO WA PICHA

1. Utambulisho waweza kutumika kwa makusudi mawili:-

   (a) Kumtafuta mhalifu au mtu aliyepotea ambaye utambulisho wake unajulikana

   (b) Kueneza utambulisho wa mtu aliyetenda kosa

2. Picha haitaweza kutumika kutambulisha endapo:-

   (a) Mtuhumiwa yuko chini ya ulinzi au amezuiliwa

   (b) Wakati mtuhumiwa anajulikana na aweze kukamatwa haraka na kufikishwa kwenye gwaride la utambulisho

3. Kuna mbinu mbili za utambulisho wa mtuhumiwa kwa kutumia picha nazo ni:-

(a) Wakati picha pekee/ moja ya mtuhumiwa /watuhumiwa inapopatikana

(b) Wakati picha ya mtuhumiwa inapodhaniwa imo katika albamu ya picha ya watu wenye tabia ovu.

Utaratibu wa utambulisho kwa Albamu ya wenye tabia ovu

4. (a) Wakati polisi inahodhi picha ya mtuhumiwa ambaye hajakamatwa picha yake yaweza kuoneshwa kwa shahidi pamoja na picha nyingine za watu zisizopungua nane zenye kuwiana kwa mazingira yoyote yale shahidi asioneshwe picha moja tu.

(b) Picha yenye majina au utambulisho wowote kwa mbele au nyuma isioneshwe kwa shahidi.

(c) Ofisa anayeendesha gwaride la utambulisho la picha ataingiza jumla ya picha za mtuhumiwa na picha nyinginezo kama ilivyo katika para ya 3 ya gwaride la utambulisho (P.F.136)

(d) Picha zitawekwa mbele ya shahidi na hakuna jaribio litakalofanywa kusaidia utambuzi

(e) Gwaride litasimamishwa mara tu baada ya kukamilishwa kwa utambuzi. Picha hizo, zitawekwa mbali na mashahidi waliosalia na mtuhumiwa atakamatwa na kuwekwa kwenye gwaride la kawaida la utambulisho mble ya mashahidi waliobakia, kwa mujibu wa PGO No. 232.

(f) Picha zote zilizooneshwa mbele ya mashahidi zitatuzwa vyema ili zije kutolewa mahakamani ikibidi/mahakama ikizihitaji.

5. (a) Endapo haijapatikana picha ya mtuhumiwa, shahidi aweza kuoneshwa albamu ya picha ya watu wenye tabia ovu. Picha hizo hazitakiwi kuwa na alama yoyote ya utambulisho wala nafasi ya picha katika albamu hiyo wala ukurasa haupaswi kuwa na alama yoyote.

(b) Albam hiyo itawekwa mbele ya shahidi na hakuna ishara yoyote ya kueleza utambuzi itakayoruhusiwa

(c) Shughuli hiyo itakoma mara tu utambuliso utakapokamilika. Kisha albam hiyo itawekwa mbali na mashahidi waliosalia, na mtuhumiwa atakamatwa na kuwekwa kwenye gwaride la kawaida la utambulisho kwa mashahidi mbalimbali kwa mujibu wa PGO No. 232.

6. (a) Wakati gwaride la utambulisho litakapofanywa kwa utaratibu wa picha moja au albamu ya watu wenye tabia ovu, utaratibu tumika utajazwa katika regista ya gwaride la utambulisho para ya 3.

   (b) Kama kila alivyoitwa shahidi katika kuchunguza picha, jina la kila shahidi pamoja na matokeo na kila jambo lililoelezwa na shahidi litaandikwa katika sehemu ya pili ya para ya 4 ya regista ya gwaride la utambulisho.

   (c)Katika kuhitimisha gwaride, ofisa mwendeshaji atakagua na kutia sahihi yake katika kila eneo elekezwa.

   Nakala ya pili katika regista ya gwaride la utambulisho itatolewa na kuwekwa kwenye jalada la kesi au katika jalada la makosa madogo

P.G.O - 232

UPELELEZI - GWALIDE LA UTAMBULISHO

1. Wakati itakapokuwa muhimu kuhakikisha kwamba mtu aliye chini ya ulinzi wa polisi anaweza kutambuliwa na mashahidi polisi wanalo jukumu la kuhakikisha kuwa taratibu zinafanywa ili kuhakikisha kwamba kulikuwa hakuna upendeleo uliofanyika ili kutambua mtuhumiwa , vinginevyo uhalali wa utambuzi kama ushahidi utakuwa umeondolewa wakati huohuo mashahidi wanatakiwa wapewe wasaa mzuri na wa kutosha kufanya utambuzi wao katika mazingira mazuri, na kiongozi wa Gwaride la utambulisho atahakikisha uwezo wa mashahidi katika kuwatambua watuhumiwa/mtuhumiwa kwa hiyo wanatakiwa kuwasikia mashahidi wakiongea kuwaona wakiwa wamevaa kofia na wakiwa wamevua kofia, kuwaona kwa mbele na nyuma na wakiwa wanatembea au kwa namna yoyote ile ambayo itaonekana inawapa mashahidi uwezo wa kuwatambua watuhumiwa
2. Gwalide la utambulisho litafanyika kwa kufuata taratibu zifuatazo:
   a) Afisa wa Polisi anayehusika na shauri hilo ataandaa mipango ya awali ya kufanya Gwalide la utambulisho na ataingiza idadi ya mashahidi wanaoshiriki katika Gwaride hilo, na idadi ya

watuhuiwa katika nafasi chini ya Jedwali la 3 la fomu ya Gwalide la utambulisho **(P.F.186)** Ataingiza majina ya maashahidi chini ya jedwali namba 4 ya Fomu/Rejesta ya Gwaride la utambulisho kwa utaratibu atakaoutumia kuwaita kuatambua watuhumiwa. Atatengeneza nakala ya rejesta huyo kwa kuweka karatasi nakilishi (carbon paper) katikati ya karatasi halisi na karatasi ya kurubuni zinazofuatia

b) Japokuwa kiongozi wa upeleleziatakuwepo katika shughuli hiyo, lakini hatahusika kufanya Gwalide la utambulisho. Afisa anaeendesha Gwalide la utambulisho anatakiwa asihusike na shauli hilo na inapowezekana anatakiwa awe ni afisa wa kuanzia mratibu msaidizi wa polisi afisa aliye chini ya cheo cha mkaguzi msaidizi wa polisi hataruhusiwa kuendesha gwalide la utambulisho.

c) Kwa muda muafaka kabla ya Gwalide la utambulisho, afisa msimamizi atamfahamisha watuhumiwa/mtuhumiwa kuwa ata/watawekwa katika gwalide la utambulisho. Na kama kuna kipingamizi kitakachotokea litaandikwa na mawasiliano yafanywe kati ya afisa mpelelezi na afisa anaeendesha gwalide la utambulisho kabla ya kufanya gwalide hilo.

d) Kama mtuhumiwa atapendelea kuwepo Kwa marafiki zake, matayalisho yatafanywa ili nao wawepo; na watatakiwa kukaa sehemu na kuangalia tu bila kutamka chochote.

e) Sehemu itakayochaguliwa kufanya Gwalide la utambulisho itatakiwa iwe sehemu yenye mwanga wa kutosha na mtu yeyote asiyehusika haruhusiwi kuhudhuria wala kuwa shahidi wa Gwalide hilo. Shahidi watajipanga chini ya afisa wa Polisi ambae hahusiki na shauri hilo katika chumba au sehemu ambayo hawezi kuona au kusikia yanayoendelea kwenye Gwalide hilo la utambulisho na watakuwa wakiitwa na afisa anaeendesha gwalide hilo. Mashahidi hawataruhusiwa kuwaona au kuwaasikia watuhumiwa kabla hawajawekwa kwenye utambulisho pia hawataachiwa kwa picha au kwa namna yoyote ile. Afisa aliyefanya ukamataji au upelelezi hataruhusiwa kuwa na mawasiliano moja kwa moja na mashahidi kabla ya gwalide kufanyika.

f) Matayaarisho yatafanywa kuhakikisha kuwa mashahidi hawana nafasi ya kuona au kuonwa na watu waliopo katika Gwalide hilo.

g) Hakutakuwa na pingamizi kwa nguo aliyovaa mtuhumiwa wakati akitenda kosa lililofanyika japokuwa nguo hizo

hazitakuwa zinaonyesha madoa ya damu, au alama zozote au kuchanika ambayo itabainisha /itakayomtofautisha na watuhumiwa wengine waliopo katika gwalide la utambulisho na nguo alizokuwa amevaa wakati wa kutenda kosa.

h) Watu watakaochaguliwa katika Gwalide la utambulisho wanatakiwa wawe wa umri unaolingana, urefu, muonekano jumla na aina ya maisha na nguo zinazofanana wanazovaa.

i) Wanatakiwa wawepo watu wanane au zaidi Kwa mtuhumiwa mmoja, watu kumi au zaidi kwa kwa watuhumiwa wawili, kama watakuwa zaidi ya watuhumiwa wawili, kufanyika zaidi ya gwalide moja kukiwepo watu tofauti watakaoshiriki gwalide hilo.

j) Wakati afisa anaendelea na Gwalide atakapofika na kuchukua nafasi ya kuendesha gwalide hilo watuhumiwa wataletwa kwenye gwalide na Afisa atawaeleza madhumuni ya kufanya Gwalide hilo, na atawauliza watuhumiwa kama wanalopingamizi lolote kuhusiana na watu walioshiriki Gwalide hilo na kama kunapingamizi lolote litatokea litaandikwa katika Rejesta ya gwalide la utambulisho **(PF 186)** na hatua za haraka zitachukuliwa kuwabadilisha wale waliokataliwa na mtuhumiwa. Mtuhumiwa ataalikwa kusimama katika mstari sehemu atakayoitaka kusimama na sehemu hiyo itawekwa alama katika Rejesta ya Gwalide la utambulisho

k) Tahadhali kubwa itachukuliwa kuona kwamba mtuhumiwa atakuwa amevaa pingu au kitu chochote ambacho kitamtofautisha na watu wengine, na hakuna jaribio lolote litakalo fanyika kuwatofautisha.

l) Shahidi wa kwanza ataitwa na Afisa anayesimamia Gwalide la utambulisho, ambaye atamweleza sababu za kufanya Gwalide hilo la utambulisho mbele ya wote waliopangwa na kuwataka/kuwaalika kumgusa mtu yeyote atakaye mtambua bila shahidi kuguswa au kuulizwa maswali yoyote.

m) Kama shahidi atahitaji mtu yeyote katika Gwalide la utambulisho kutembea au kuongea, kumuona akiwa amevaa kofia au akiwa amevua, haya yatafanyika na watu wote waliopo katika Gwalide hilo wataambiwa wafanye hivyo Afisa anayeendesha Gwalide la utambulisho ataandika kikamilifu katika Rejesta yake ya Gwalide la utambulisho utambuzi wowote utakaofanywa na kama kuna kipingamizi chochote au utambuzi wowote usio Sahihi na kama kuna pingamizi toka kwa watuhumiwa au mashahidi wengine na kama mashahidi

walitambua mtuhumiwa , atawauliza ni kwa njia gani waliweza kumtambua na ataandika kila aliyesoma aliyomtambua mtuhumiwa na kujaza katika Reesta ya gwalide la utambulisho, hakuna maswali mengine nje ya hayo yatakayoulizwa.

n) Shahidi anapoondoka katika Gwalide hilo, atatakiwa apelekwe katika sehemu ambayo hataweza kusikika au kuwa na mawasiliano na mashahidi wengine au maafisa wengine wa upelelezi na atakuwa chini ya Afisa mwingine wa Polisi ambaye hahusiani na shauri hilo; na atakaa hapo hadi Gwalide la utambulisho litakapomalizika.Mashahidi wanaofuatilia watafuata utaratibu huohuo uliotajwa hapo juu kuwatambua watuhumiwa.

o) Mwisho wa Gwalide la utambulisho, picha ya pamoja itachukuliwa kwaajili ya kuwakilisha mahakamani kwa ajili ya kielelezo. Wote walioshiriki katika gwalide la utambulisho wanatakiwa wapewe na kuangaliwa kwa uangalifu, na kwa upole.

p) Afisa anayefanya Gwalide la utambulisho atatakiwa kutoa ushahidi Kwa matokeo ya Gwalide alilolifanya katika mahakama yoyote ambayo shauri hilo litasikilizwa kumbukumbu yake itakuwa ile nakala halisi iliyoachwa katika Rejesta ya Gwalide la utambulisho, ambayo ilijazwa siku ya Gwalide la utambulisho.

4. Afisa mpelelezi wa shauri atatoa ushahidi wa jinsi alivyopanga watu wengine katika Gwalide la utambulisho.

5. Kanuni hizi za Jeshi la Polisi hazipunguzi ulazima wa afisa wa polisi kutoa taarifa ya sehemu alipo muda wote kulingana na maelekezo ya kanuni za polis 277.

PGO - 280

VITABU

KITABU CHA KAZI (PF59A) NA KITABU CHA KAZI NA MAJINA.

Kila mkuu wa kituo atatakiwa kuandaa mpango wa kazi ili kila askari wa vyeo mbali mbali wanaofanya kazi katika himaya yake wanapangiwa kazi zitakazoainishwa katika kitabu cha kazi (PF59A).

Kitabu cha kazi kitakuwa katika kila kituo cha polisi na taarifa zote zitaandaliwa kabla ya mpango kazi.

3) (a) Katika vituo daraja B na C askari wote wa vyeo mbali mbali (R&F)wataorodheshwa katika kitabu cha kazi.

(b)Utaratibu huo utatumika kwa vituo vya daraja A isipokuwa

i) Idara ya upelelezi wa makosa ya jinai na kikosi cha intelijensia hawataorodheshwa katika kitabu cha kazi cha kituo.

ii)Vitabu vya kazi vitatofautishwa kwa askari wa usalama barabarani vitakuwepokatika vituo daraja A ambavyo vina afisa.

4) Vitabu vya kazi vitatumika si chini ya masaa 24 na sio zaidi ya siku saba kwa kuanzia na vitawekwa chumba cha mashtaka. Orodha madhubuti ya kazi itatolewa kwa mpango kambini,vyumba vya malindo n.k ili kuwafanya askari wa vyeo vyote kufahamu kazi wanazotakiwa kuzifanya.

5) Vitabu vya mpango kazi vitajazwa kama ifuatavyo

a) Kazi zote muhimu za mara kwa mara katika kituo na majukumu yataingizwa kolamu ya kwanza sambamba na nguvu kazi iliyopona inavyojitosheleza.

b) Muda wa kazi utaonyeshwa katika kolam ya pili.

c) Idadi (na majina kama inalazimu) ya askari waliochaguliwa kwa kazi yataingizwa sehemu ya juu nusu ya sehemu mkabala ya kazi azifanyazo katika kolamu husika (yenye kichwa JUMATATU,JUMANNE n.k).

6)Nusu ya sehemu ya chini mkabala na kila kazi katika kolamu(zenye kichwa JUMATATU,JUMANNE n.k)zitatumika kurekodi kwa wino mwekundu,maelezo ya kazi na hasa zile zifanywazo. Kwa kawaida kuna sehemu ndogo ya mwisho hubadilishwa kabla ya mpango kazi kutokana na ugonjwa,utoro n.k na ni muhimu kwa afisa kufahamu namna askari walivyopangwa kwa muda huo. Alama zifuatazo zitatumika kwa kazi hiyo

v—Kazi azifanyazo kama zilivyoonyeshwa katika kitabu cha kazi.

X—Kazi kama zilivyoonyeshwa katika kitabu cha kazi hazijafanywa.

a—Mtoro.

s—Mgonjwa.

c—Amebadilishwa kazi.

r—Siku ya mapumziko.

av—Utoro na amepangwa P.c50

ax—Mtoro na hakuna aliyepangwa.

Sv—Mgonjwa na amepangwa PC 50.

Sx—Mgonjwa na hakuna aliyepangwa.

cv—Amepangwa kazi nyingine badala yake amepangwa pc50.

cx—Amepangiwa kazi nyingine na hakuna aliyepangwa badala yake.

rv—Amepumzika na kubadilishana na pc 50.

Rx—siku ya kupumzika na hakuna aliyepangwa.

7) Mfano wa ukurasa umeonyeshwa chini kama muongozo.

Mfano wa ukurasa

TOKA HADI JUMATATU JUMANNE

CHU MBA CHA MASHTAKA 0001 0800
Sgt50 Stg50

v

CHUMBA CHA MASHTAKA 0800 1600
Sgt 51 Sgt 51

V v

CHUMBA CHA MASHTAKA 1600 2359
Sgt 52 Sgt 52

V SV54

NO.1 ULINZI 0001 0600
PC1 PC1

V ax

No.1 ULINZI 0600 1200
PC2 PC2

V V

NO.1 ULINZI 1200 1800
PC3 PC 3

v v

NO.1 ULINZI 1800 2359
PC4 PC4

v v

NO.2 ULINZI 0001 0600
PC5 PC5

v v

NO.2 ULINZI 0600 1200
PC6 PC6

rvpc10 v

NO.2 ULINZI 1200 1800
PC7 PC7

v v

NO.2 ULINZI 1800 2359
PC8 PC8

CX CVPC

SEHEMU YA PILI----KITABU CHA JUMLA.

8) Kila mkuu wa kituo na kikosi atakuwa na kitabu cha jumla kwa kazi za askari wa vyeo mbalimbali(PF59) ambapo kumbukumbu za kila siku za kazi zinazofanywa zitaandikwa mf .wagonjwa,watoro n.k. Kumbukubu hizi ni muhimu ili afisa msimamizi aweze kupanga kazi kwa haki wakati anapotengeneza vitabu vya mpango kazi. (PF59A)

9) Alama za herufi hapa chini zitatumika katika kitabu cha jumla. Maingizo yote yatakuwa kwa wino wa bluu au mweusi isipokuwa nyakati za usiku (1800 hadi 0600) ambayo yatakuwa kwa wino mwekundu.

B---- Kazi za ulinzi

G--- Kazi za malindo

SD--- Kazi za kituo (zikiwemo amri mbali mbali.

P-----Doria

SL---- Mstari wa wagonjwa na likizo ya ugonjwa.

H----Hospitali.

A---- Utoro bila likizo.

R---- Mapumziko.

C---- Utoro mfululizo.

Nyongeza ya herufi za alama zinaweza pia kutumika katika mazingira mahsusi.

VITABU- KITABU CHA KUMBUKUMBU ZA KIOFISI

1. Kila mrakibu wa polisi, mkaguzi na mkuu wa kambi wanatakiwa kuwa na kitabu cha kumbukumbu za ofisi

2 Kitabu cha kumbukumbu kinatakiwa kuwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili.Kumbukumbu zinatakiwa kuingizwa kila siku

3 Maelekezo sahihi ya yafuatavyo lazima yaingizwe kwenye kitabu cha kumbukumbu.
   (a) Masaa ya mahudhurio ofisini, mizunguko ya kawaida na masaa nje ya ofisi
   (b) Kazi maalum au upelelezi uliofanywa au uliofanyika.
   (c) Mpangilio wa doria, kutembelea vituo, na mizunguko ya usiku
   (d) Mahojiano
   (e) Magwaride ya mashtaka ya kijeshi
   (f) Magwaride na mazoezi yaliyofanywa au yaliyofanyika
   (g) Mahudhurio ya Mahakamani
   (h) Misako
   (i) Shughuli nyinginezo zilizofanyika nje ya ofisi; mfano mikutano ya wakuu wa mikoa.
   (j) Idadi ya kilomita kwa safarinza kikazi kwa gari au magari la au ya serikali.
   (k) Shughuli nyinginezo zenye mvuto.

4 Mapendekezo ya shughuli zinazotarajiwa kufanywa baadaye zinaweza kuandikwa pembeni mwa kitabu cha kumbukumbu.

5 Kitabu cha maingizo lazima kiwe na mpangilio sahihi ambao utamwezesha kila afisa wa polisi kurudia kumbukumbu za nyuma kwa muda wowote kwa kumbukumbu sahihi za wajibu na shughuli zake.

6 Vitabu vya kumbukumbu vitatolewa kwa ajili ya kaguzi zote za kawaida na mkuu wa polisi wa wilaya (OCD) na wakuu wa vitengo. Hatakama afisa hatakuwepo kwa wakati wa ukaguzi anatakiwa kuacha kitabu chake cha kumbukumbu ofisini ili kiweze kukaguliwa.

7 Warakibu wa polisi ambao wanatakiwa kukagua vitabu hivyo . Watakuwa wanapewa jukumu la kuangalia shughuli zilizopangwa kuangalia kaguzi, mizunguko na misako iliyofanyika. Kwa ujumla watakiwa kutoa taarifa kwa kila tukio ambalo limetendeka au kutokea na iliyo kawaida kwa viongozi wao

8 Vitabu ambavyo tayari vimekaguliwa vitatunzwa kwa muda wa mwaka mmoja.

PGO 284

VITABU SHAJARA ZA KITUO

1. Kitabu cha shajala za kituo (PF. 51) kitadumishwa katika chumba cha mashitaka cha kila kituo cha polisi na katika sehemu nyingine yoyote ya uttendaji kama ilivyoagizwa kamanda husika wa polisi .
2. Askari polisi kiongozi wa chumba cha mashitaka atakuwa na wajibu wa kudumisha/kutunza kitabu cha kumbukumbu za kituo.
3. Kitabu cha kumbukumbu za kituo ni kitaandikwa kwa wino na kitakuwa na rekodi sahihi na kamili za kila kitu ambacho kinachofanyika/tokea katika eneo la kituo au ndani ya kituo kuhususiana na utawala wa polisi, ukiondoa matukio ambayo kumbukumbu zake zimerekodiwa katika vitabu vingine rasmi vya kumbukumbu za kituo au kumbukumbu.
4. Maingizo kuhusu matukio yafuatayo yatawekwa kumbukumbu katika kitabu cha kumbukumbu za kituo: -

(a) kuingia au kutoka kazini kwa askari wote wa ulinzi, walinzi wa vituo, doria na watumishi wengine wote katika kazi nyingine yeyote.

(b) kuondoka kwa mkuu wa kituo kutoka kituoni na jina la Afisa Polisi kaimu kama wa kituo cha polisi wakati mkuu wa kituo hayupo kituoni. Kurudi kwa mkuu wa kituo kutarekodiwa kwenye kitabu cha kumbukumbu za kituo.

(c) Ziara za kuwaona wafungwa katika seli,walinzi wa malindo, na walinzi wa vituo zinazofanywa na mkuu wa chumba cha mashitaka au afisa mwingine yeyote.

(d) Masuala ya kutolewa na kurudishwa kwa pingu, baiskeri, tochi, vifaa vya kutuliza ghasia na mali nyingine za kituo, isipokuwa silaha na risasi.

(e) Katika Vituo vya Polisi vinavyohama tu, maelezo kwa kifupi yataingizwa katika kitabu cha taarifa cha kituo cha polisi kinachohama ya kuingia kila kufanywa katika Kitabu Mkono Polisi Station Ripoti (vide General Order No. 7)

5. Maingizo yatafanywa katika utaratibu ufuatao

(a) Katika Safu ya kwanza ya mpangilio, kila ingizo litapewa namba zenye mtiririko zitakazoanza usiku wa manane na kumalizika na ingizo la mwisho saa 2359.

(b) Katika Column pili ingizo linalohusianisha taarifa moja na nyingine iliyopitayoyote katika kitabu cha kumbukumbu ya kituo na vitabu vingine rasmi vya kituo itaingizwa.

(c) Katika Safu ya tatu muda sahihi wa ingizo la taarifa; utaratibu wa masaa ishirini na nne utatumika. Namba husianisho ya maingizo mengine katika kitabu cha kumbukumbu ya kituo na maingizo mengine katika kitabu za kituo zitafanywa na namba itaandikwa juu ya tarehe. kumbukumbu ya ingizo No 513 ya Novemba 15, 2004 itasomeka: -

_ 513__
15.11.04

(D) Katika Safu ya nne rekodi fupi lakini sahihi ya tukio kuwa kumbukumbu.

(E) Katika safu ya tano saini ya afisa anayefanya ingizo.

6. Kila marejeo yanayofanywa na N.C.Os. na konstebo yatajumuisha vyeo na namba zao za kijeshi.
7. Maingizo yote yatafanywa yakiwa nadhifu na yanayosomeka, na, kama inawezekana, kwa Kiingereza. Inakatazwa kufanya maingizo yeyote kwa kutumia karamu ya mkaa.
8. Maingizo yatafanywa katika mpangilio kuanzia namba ndogo kwenda kubwa na bila kuchelewa.
9.Hakuna ingizo lililokwisha fanywa linaweza kubadilishwa, kuondolewa au kuongeza na hakuna ingizo linaloweza kufanywa katikati ya mistari iliyokwisha andikwa. Na pia hakuna kufuta ingizo.

10. Kama ingizo kamili linahitaji marekebisha au nyongeza, ingizo jipya litafanywa katika namba mpya na rejeo la ingizo lililorekebishwa. Dokezo litaandikwa kwa wino mwekundu itarekodiwa mbele ya ingizo la zamani.
11. Hakuna nafasi tupu itaachwa kati ya maingizo au mstari wowote katika ingizo. Mstari utacholwa kutoka katika neno la mwisho la kila ingizo lamwisho hadi kwenye column ya 4 upande wa kulia.
12. Ifikapo saa 23:59 kila siku mstari mmoja mwekundu utacholwa kwa karamu ya wino. Tarehe ya siku inayofuata itaandikwa kwa karamu nyekundu mara baada ya mstari uliocholwa kwa herufi kubwa. Ingizo linalofuata litafanywa katika mstari unaofuata mara baada ya mstari wa tarehe.
13. Ingizo la mwisho la mwizi litakuwa ni lile ingizo la mwisho kabla ya kuisha kwa siku ya mwisho ya mwezzi. Mistari miwili mwekundu itachorwa chini ya ingizo la mwisho kuanzia mwanzo kushoto kuishia kulia mwa kitabu.

14. (A) Wakati wa kukabidhiana majukumu ya chumba cha madaraka, ingizo litafanywa kwa kuzingatia mfumo na litasainiwa na wanaotoka na kuingia kazini katika chumba cha mashitakakatika kituo cha polisi: -
"Ninakabidhi wajibu katika chumba cha mashitaka kwa Konstebo .....
No ....pamoja silaha na risasi zifuatazo ....
mali zote za Serikali na vifaa vya kituo vilivyopo, fedha katika mkono, Sh. ..... wafungwa waliopo chini ya ulinzi ..... "
(B) mapungufu yote ya silaha na risasi, mali juu ya kituo, fedha, au wafungwa chini ya ulinzi itakuwa kumbukumbu. Afisa wa Polisi anayetoka kazini hataondoka kituoni mpaka maingizo kwa upande wake na anayekabidhiwa yamefanywa na kutiwa saini na yeye mwenyewe na yule anayekabiidhiwa. Katika vituo ambavyo havifunguliwi kwa masaa ishirini na nne, afisa wa polisi anayefunga kituo atafanya ingizo kuonyesha muda ambao anafunga kituo. Ingizo linalofuata litaonyesha muda ambao anafungua kituo.

15. Mkuu wa kituo chaa polisi ataangalia kitabu cha kumbukumbu za kituo angalau mara moja kwa siku kati ya saa 08:00 na masaa 09:00 na kufanya ingizo la ukaguzi husika kwa wino mwekundu.
16. Maafisa wanaokagua na wanaotembelea vituo watachunguza kitabu cha kumbukumbu za kituo na na kuhakikisha kwamba kinatunzwa ipasavyo. Pia watatizama maingizo katika vitabu vingine vinavyohusiana na kitabu cha kumbukumbu za kituo.
17. nakala ya sheria hizi wakati huo.
18. Vitabu vya kumbukumbu za kituo vitatunzwa kwa miaka miwili kabla ya kuharibiwa.

PGO 285.

VITABU ,WITO WA MAHAKAMA.

1.Kila mkuu wa kituo lazima atenganishe kitabu cha wito wa mahakama (PF55) kwa hati ya wito wa mashahidi na watuhumiwa.

2. Kila shahidi (Mlalamikaji) wito na wito kwa watuhumiwa wanaowasilishwa kituoni kwa huduma lazima uingizwe kwenye kitabu husika cha wito huo.

Wito wa madai hautaingizwa katika kitabu hicho .Kutakuwa na kitabu cha matukio ya wito wa kesi za ajali Barabarani zitakazowekwa katika Kituo daraja A chini ya maelekezo ya Mkuu wa Polisi wa kitengo husika.

3.Mahingizo ya kumbukumbu za wito wa mashahidi utaingizwa kwa mtiririrko wa namba kuanzia moja January hadi 31 desemba lazima ufanywe bila kucheleweshwa na nkwaa mujibu wa taratibu zifuatazo :-

(a)Kila wito lazima upewe namba katika kolamu namba moja na lazima uwe na mhuri wa kituo kwa upande wa juu wa kona ya kulia ikiwa na namba ya kitabu cha kumbukumbu hiyo.

(b) Anuani ya kila wito lazima iandikwe katika kolamu namba 2,3,4,8,9 na 11mapema iwezekanavyo baada ya kupokelewa kutoka mahakamani.

© Afisa naayekabidhi qwito huo kwa ajili ya kufanyiwakazi zitaingizwa katika kolamu namba 5na kuandika jina lake katika kolamu namba 6.

(d) Afisa anayepokea wito huo lazima asaini katika kolamu namba 7.

(e) Mapema wito huo unapokuwa umefanyiwa kazi ,jina lla mtu aliyepewa wito huo ,tarehe na muda wa kupokelewa wito huo,lazima viandikwe katika

kolamu namba 10 na nakala ya wito huo utarudishwa katika mahakama ilotoa na kuthibitishwa na afisa aliyehusika.

(f) Kama wito huo haukufanyiwa kazi,lazima iandikwe 'Haujafanyiwakaz' na kuingizwa katika kolamu namba 10 na tarehe ambayo nakala mbili za wiuto huo zitarudishwa mahakamani na mahakama ilotoa iutaziingiza katika kolamu namba 12.

4.Sahihi ya karani wa mahakama na mhuri wa mahakama ,inapa tikana katika kolamu namba 13. Pale wito unaporudishwa katika mahakama iliyotoa kwa barua ni vyema kunukuu kumbukumbu ya barua katika kolamu namba 13 isipokuwa katika mazingira risiti lazima ipatikane kutoka ka karani wa mahakama na kutunzwa sehemu salama.

5.Wito ambao ambao ulisha tolewa kwa mtu ambaye amesafiri kwenda wilaya nyingine utarejeeshwa katika mahakama iliyotoa chini ya barua ya uambatanisho ikionyesha mahali,makazi (kama yanafahamika) ya mtu aliyetajwa katika wito huo . Mahakama itaombwa kushukuru na kupokea risiti hiyo na ingizo litaingizwa katika kolamu namba 12 ya nukuu itaingizwa kolamu namba 13.

6.Mkuu wa kituo na wa Wilaya wanawjibika mojakwamoja na:-

(a) Vitabu vya kumbukumbu vya witokuwa vimeandaliwa kwa usahihyi na maingizo muda wote yanaingizwa kwa wakati.

(b) Wito wa mahakama unafanyiwa kazi pasipokucheleweshwa .

(c) Nakala a wito wa mahakama na nakala mbili ambazo hazikufanyiwa kazi zirejeshwe katika mahakama iliyotoa kabla ya tarehe ya shauri kusikilizwa.

(d) Kifungu cha 91-99 ikijumuishwa na kifungu 145 vya Sheria ya Mwenendo wa makosa ya Jinai Cap n20 maerekebisho ya 2002 viakikishwe vinazingatiwa.

7.Maafisa wakaguzi lazima wawe makinin na kolamu namba 10,12 na 13kwenye vitabu vya wito wa mahakama na lazima kuhakikisha kwamba hitimisho la kila wito ulokwishatolewa unashughulikiwa kwa usahihi unaotakiwa.

PGO 286

MAJALADA YA KESI NA TAARIFA ZA MAKOS A MADOGO

UTAYARISHAJI

1. Taarifa zitakazoshughulikiwa kama majalada ya kesi kwa kila taarifa yenye kiwango kifuatacho litafun

2. guliwa jalada (PF.2C)

   (a) Makosa chini ya sheria ya makosa ya jina cap 16 iliyofanyiwa marekebisho 2002 mbali na;-

      (i) Makosa ambayo huwezi kukamata bila hati ya kukamatia

      (ii) Makosa chini ya kifungu 176 na 177

      (iii) Wizi na uvunjaji ambapo thamani ya mali iliyoibiwa haizidi sh. 100,000/=

      (iv) Shambulio chiniya kifungu 241 kati ya watu wa kabilamoja endapo tu hakuna aliyezuiliwa hospitali.

   (b) Makosa chini ya sheria zifuatazo;-

      (i) Sheria ya Madawa ya Kulevya na Usafirishaji Haramu wa Madawa namba 95 Marekebidho ya mwaka 2002.

      (ii) Sheria ya Madini Cap 123 Mrekebisho ya mwaka 2002

      (iii) Sheria ya Rehani Cap 1275 Marekebisho ya mwaka 2002

      (iv) Sheria ya Udalali Cap 227 Marekebisho ya mwaka 2002

      (v) Sheria ya Usonara na Uhunzi Cap 778 Marekebisho ya mwaka 2002

      (vi) Sheria ya Utulivu ya Umma Cap 385 Marekebisho ya mwaka 2002

      (vii) Sheria ya Watabibu na Madaktari wa Menoi Cap 15 Marekebisho ya mwaka 2002

      (viii) Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Ziada cap 322 Marekebisho ya mwaka 2002

      (ix) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) ya mwaka 1982

      (x) Sheria ya serikali za Mitaa(Mamlakaya Wilaya) Cap 287 Marekebisho ya Mwaka 2002

      (xi) Sheria Ndogo za Wanunuzi na Qauzaji wa Vyuma

      (xii) Vikuukuu na Vyuma Chakavu Cap 329 Marekebisho ya mwaka 2002

      (xiii) Sheria ya Umoja wa Wafanyakazi Cap 244 Marekebisho ya

mwaka 2002

(xiv) Sheria ya Kuzuia Rushwa Cap 329 Marekebisho ya Mwaka 2002

(c) Vifo vya mashaka na vya ghafla

(d) Ufyatuaji wa risasi na mabomu ya machozi wa Polisi (wakati ambao sio wa mazoezi)

(e) Utorokaji wa watuhumiwa chiniya ulinzi halali wa Polisi

(f) Migomo, mikusanyiko isiyoo halali na kupigana hadharani

(g) Upotevu wa mali ya serilkali iliyo chini ya uangalizi wa Polisi iliyo na thamani au zaidi y ash 50,00/=

(h) Malalamiko yoyote dhidi ya Askari Polisi.

(i) Uchunguzi wowote mwingine wa muhimu wa makosa ambayo Afisa atafikiria kuyaweka katika jalada.

3. Mashauri yasiyoangukia ndani ya kikundi kilichotengwa katika sehemu 1 yatashughulikiwa kama makosa madogo kulingana na sehemu 2 ya kanuni hii.

4. Maofisa wenye jukumu la kutayarisha majalada ya kesi, majalada yatatayarishwa na Mkuu wa Kituo au Afisa au afisa mwengine kama itakavyopangwa na Kam anda wa Polisi wa Mkoa au Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

Matayarisho ya Makava ya Juu ya Jalada(PF.2C)

5. (a) Kila afisa ambaye ana jukumu la kutayarisha jalada la kesi atahakikisha kila kava la jalada limejazwa kwa usahihi kwa kuwekwa nambari na kusajiliwa katika rejesta ya upelelezi ya kituo (PF.221).

(b) Mambo yote muhimu yanahitajika juu ya kava la jalada yanakiliwe kwa usafi na usahihi baada ya kuthibtishwa taarifa zote zilizopo. Habari zisizo na ithibati ziandikwe kwa penseli ukweli utakapopatikana ziingizwe kwa wino. Hii itafanyika katika kesi zenye shaka mwanzonikuhusu kosa halisi nakifungu cha sheria.

Usajili wa Majalada ya Kesi

6. Kila kiuo kiamiliki rejesta ya upelelezi (PF.221) kuligana na PGO 281 majalada yote ya kesi kubwa kesi ndogo na majalada yua usalama

barabarani yataingizwa katika rejesta hii na maafisa wanaowajibika kuyatayarisha. Hatima ya mwisho ya kila kesi itaoneshwa katika safu ya mwisho ya rejesta kwa kutumia herufi

C - amefungwa

A - ameachiwa huru

U - haijapelelezwa

T imehamishiwa kituo kiiiiiingine cha Polisi

NFA - hakuna hatua nyingine ya kuchukuliwa (limekataliwa)

NOD - hakuna kosa lililobainika

D - ameachiliwa chini ya kifungu 3B kanuni ya adhabu

OD - kaachiliwa kwingineko

Kuyapa Namba Majalada

7. Kila taarifa yenye ulazima awa kufunguliwa jalada la mashtaka, mashtaka madogo nay a usalama barabarani yatapewa rejesta ya uchunguzi mbele ya mstari wa 15 wa Kitabu cha taarifa kulingana naibaraya ya 19(g) ya Kanuni ya Mwenendo wa Polixi 309. Rejesta za uchunguzi hizi zitakuwa namba za kudumu za rejea za majalada, majalada ya mashstaka madogo,na majalada yausalama barabarani yaliyofunguliwakuhusiana na taarifa ya rejesta ya uchunguzi hiyo. Namba za rejesta ya uchunguzi zitaingizwa baada ya mstarei wa kwanza wa daftari la upelelezi (PF,169. Namba za kesi ziandikwe baada ya herufi za siri za ikituo ikifuataiwa na mkwaju, herufi “CF” n m kwaju mwengine. Mkwaju na namba mbili za mwaka zitafuata namba hiyo (mfano DC/CF/1/04 sawasawa na jalada nambari moja la mwaka 2004 la kituo cha Polisi Kati (Central) mkoa wa Dar es salaam.

Yaliyomo Katika Jalada

8. Yaliyomo katika kila jalada yapewe nambari kwa wino wa bluu na kupangwa kwa mpangilio na afisa anayehusika na matayarisho yake, kulingana nautaratibu ufuatao;

(a) Upande wa kulia wa jalada

(i)Taarifa ya awali (PF.162A) isipewe namba

(ii) Kumbukumbu za upelelezi PF 2B zipewe namba A,A1 n.k. na

kuwekwa baada ya taarifa ya awali. Kumbukumbu za upelelezi zitabakia za kudumu jaladani

(iii) Maelezo ya mlalalaikaji (kama yapo) yapewe nnambari B,B1 n.k na yawekwe baada ya kumbukumbu ya maelezo

(v) **Maelezo ya shahidi yapewe namba(kwa kadri inavyowezekana kwa kufuatana) C,C1 nk na kupangwa kama folio C, C1 n.k baada ya maelezo ya mlalamikaji.**

~~(vi)~~ **Maelezo ya mshtakiwa yapewe namba D.D1 n.k na kupangwa**

baada ya maelezo ya mashahidi.

(vii) Hati na michoro pamoja na taarifa za madaktari, taarifa za vifo, kumbukumbu za makosa ya nyuma n.k yapewe namba E,E1 n.k. na kupangwa baada ya maelezo ya mshtakiwa.

(viii) Vielelezo vilivyo fungwa visipewe nambarilakinikumbukumbu iwekwew katika kurasa yaoneshe mpangilio wa jalaka.

(ix) Vilelezo vya makala ambavyo havihitajiki kufungiwa na vinaweza kujumuishwa bila tatizo jaladani (kama hati n.k) vipewe namba F,F1 n.k na kupangwa baada ya hati na michoro.

(x) Nakala ya nakili ya hatia ya mshtaka itapewa namba G n.k. na kupangwa baada ya vielelezo.

(xi) Mawasiliano mengineyo ya maandishi na telegram n.k yatapewa namba H,H1 n.k na kuwekwa baada ya hati ya mashtaka

(xii) Karatasi ya namna yha mpangilio wa jalada ulivyo, ulioorodhesha folio zote itawekwa (na kubaki siku zote)juu ya folio ya mwisho lakini haitapewa namba. Kama tolio ziliongezwa moja baada ya nyengine jaladani, itakuwa inaendelea kupangwa juu ya folio itakayokuwa ya mwisho mkono wa kulia wa jalada.

(xiii) Taarifa ya maendeleo ya kesi itawekwa mara zote juu ya karatasi ya mpangilio wa jalada na haitaandikwa namba. Na itabaki katika nafasi hii mara zote ////////////////// na minutes sheet kwa kumbukumbu za maafisa wanaochunguza jalada

(b) upandwa wa kushoto wa jalada

Minutes sheet peke yake **Iwekwe upande wa jalada**

Matayarisho ya hati jaladani

9. Hati tofauti tofauti zilizotajwa katika ibara iliyopita ya 7 zitayarishwe kwa utaratibu ufuatao;-

(a) Taarifa ya awali (PF.162A)

Taarifa ya awali itayarishwe na kutumwa kulingana na Kanuni za Jeshi la Polisi 311.

(b) Maelezo

Maelezo yote yaandikwe katika fomu PFR.2B kulingana na Kanuni za Jeshi la Polisi 236

(c) Hati na michoro zijazwe katika bahasha tofauti tofauti na vilivyomo viandikwe juu ya bahasha

(d) Hati ya mashtaka

Hati ya mashtakaipewe kulingana na Kanuni za Jeshi la Polisi 227

(e) Dayari ya uchunguzi (PF.28)

Kila afisa ambaye kwa njia moja au nyengine anahusika na upelelezi ataandika katika dayari ya uchunguzi kwa usahihi, bila kukosea kwa tarejhe zilizokuwepo kila alichofanya kuhusiana na upelelezi, pamoja na hapo kabla kumbukumbu ya simu alizopiga, alikotembelea, maandishi, mahojiano upelelezi n.k.

(f) Coveringi report

Afisa anayehusika na kila jalada ataandika taarifa ya maendeleo ya kesi (covering report)akipangilia jinsi matukio yalivyotokea na upelelezi, na kuelezea kwa kifupi jinsi ushahidi ulivyokusanywa. Covering report inaweza kuwa ndefu au fupi, kulingana nauzito wa mkusanyiko wa kesi (au tikio) na kutoa taarifa ya kesi bila kukosea . Taarifa ya maendeleo ya kesi itumbukizwe juu ya dayari ya uchunguzi mchoro wa upande wa kulia mwa jalada.

(g) Minutes sheet

Maelekezo na maoni ya afisa aliye/////////////////jalada yatatolewa na afisa mpelelezi na kuandikwa juu ya minutes sheet, pamoja na mapendekezo kwa kufikiriwa ngazi za juu. Mara zote minutes sheet iambataniswe upande wa kushoto mwa jalada.

(a) Isipokuwa vituo vinavyoongozwa na Askari wavyeo vya chini ambao wana jukumu la kutayarisha majalada, kilajalada lirudishwe ndani ya masaa 48 ya kuyafungua kwa uchunguzi wa awali ……..

i. Mkuu wa Polisi wa Wilaya kama jaladalinatokea vituoni ambavyo yeye ana makao makuu yake

ii. Mkuu wa Kituo cha Polisi ambacho Mkuu wa Polisi wa Wilaya hawezi kupatikana kwa haraka

(b) Maofisa na Wakaguzi watakaochunguza majalada kwa mara ya kwanza wataelekezwa cha kufanya na linimajalada hayo yarudishwe tena kwao kwa uchunguzi zaidi.

(c) Ucheleweshaji usio wa lazima wa majalada uepukwe. Maafisa wanaohusika na kazi hiii wahakikishe maafisa wengine wenye uzoefu

wanafanya upelelezi kwa niaba endapo kama wanaohusika hawatakuwepo kwa muda mrefu.

Uchungui baada ya kukamilika

10. Isipokuwa ilivyo ibara ya 13 au hatua ya mahakamani tayari inangojew a kila jalada litapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya lichunguzwe na yeye kabla ya mwezi mmoja kwisha baada ya kufunguliwa (au ////////////// Ikiwa na moja kati ya haya maingizo ndani yake.

(a) Matokeo ya kesi kwa mahakama imemaliza au

(b) Taarifa (katika minutes sheet) kuhusu maendeleo ya upelelezi bado haijatakiwa, kama kuna dalili kufatilia au

(c) Mapendekezo (kwenye dokezo sahihi na sababu za kufanya hivyo)

Wa jalada lifungwe kwa kuwa upelelezi umefikia mwisho bila nafasi ya kufaniki wa

11. Mkuu wa Polisi wa Wilaya atachunguza majalada yote yaliyopelekwa mbele yake na

(a) Kuweka jalada makao makuu yake makuu ya Wilaya kama

mahakama imemaliza baada ya kuhakikisha vielelezo vyote vimeondolewa ipasavyo na taarifa zote zimerudishwa Ofisi ya utambulisho.

(b) Kuhakikisha kwamba majalada yote ya uchunguzi wa awali yamepelekwa kwa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa kwa kupitiwa na maoni mara baada ya upelelezi kukamilika, na baada ya kufikia mwisho kesi yote ya mauaji hufikishwa jalada bila ya kuchelewana katika wakati wowote isizidi masaa 48 baada ya tarehe kwisha, kwa Mkuruenzi wa Upelelezi wa ajili ya kulipeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia kwa wakili wa serikali anayehusika na zoni hiyo.

(c) Kuchelewa uchunguzi zaidi kama anafikiria uchunguzi zaidi ni wa lazimana nyakati zote aelekeze linijalada lirudishwe kwake kwa kuchunguzwa au

(d) Kupeleka jalada makao makuu ya mkoa kama ametaka Mkuu wa Polisi wa Mkoa atoe ushauri huu kwa simu au signal (ibara hii haihusu ushauri wa mwanasheria wa Serikali, utaratibu umeelezwa ibara 13(b)) au

(e) Kuamuru jalada lifunguwe kama hakuna hatua yoyote yenye faida inayowezekana a kesi haiagukii makosa yliyoorodheshwa hapa chini kwenda makao makuu ya mkoa sio zaidi ya miezi 2 baada ya kufunguliwa na kuomba maelekezo au hatua zaidi au mamlaka kufunga jalada kama hakuna hatua yoyote ya maana inaweza kuchukuliwa.;-(i) Makosa dhidi ya Jamhuri (ii) Mauaji vifo vya mtu vitokanavyo na na mtu vinawezekana (iii)Migomo, mikusanyiko isiyokuwa ya halali na vipigo (iv) Makosa yasiyo ya kawaida yahusuyo matabaka (v) Ufyatuaji silaha polisi (vi) Makosa yote ambapo silaha, miripuko au tindikali zimetumika. (vii)Rushwa (viii) Unyanyasaji wa aina zote (ix) Mali bandia (x) Kugushi kwa hali ya juu (xi) Wizi au hasara ya fedha za Serikali (xii) Utoro au kutoroshwa chini ya ulinzi halali wa polisi (xiii)Kesi zote za vifo vya ghafla au vya , mashaka mbali navile ambavyo ushahidi unaonesha hakuna kosa lililotendeka. (xiv) Kubaka,ambapo tabaka zaidi ya moja au watoto wanahuska (xv) Usaliti (xvi) Kupiga askari Polisi

Kesi zote kama hizi zitafungwa kwa maelekezo ya kimaandishi ya Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa. Afisa ambaye kama ana shaka atapeleka jalada kwa Mkurugenzi wa Upelelezi .

12. (a) Majalada yote ya kesi muhimu yapelewe makao makuu ya mkoa ndani ya miezi 2 kulingana na ibara ya 119F. Majalada yote

kama haya yatachunguzwa na Kamanda wa Polisi wa mkoa (au Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa kwa niaba yake) ambaye ataelekeza hatua gani za ziada za kuchukuliwa. Majalada yapelekwe tena Makao Makuu ya Mkoa kila baada ya mwezi 1 hadi yafanikiwe au Kamanda wa Polisi wa Mkoa aelekezwe yafungwe.

(c) Majalada yote yaliyofungwa yataondolewa kulingana na ibara 14

Matukio maalum

13. Kama ushauri wa kisheria ni wa lazima, jalada litatumwa, bila kuchelewa kupitia kwa Mkuu wa upelelezi wa mkoa kwa wawakilishi wa Mkurugenzi wa Mashtaka, waendesha mashtaka, isipokuwa kesi zote (pamoja na kesi za usalama barabarani) ambapo polisi atatakiwa kushtakiwa. Majalada yote ya aina hii yatatumwa kupitia kw Kamanda wa Polisi wa mkoa kwenda wa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa amabyo atayaingiza kwa Inspekta Jenerali wa Polisi.

Utunzaji wa Uendeshaji wa Majalada ya Kesi

14. Majalada ya kesi yenye vifungo na yaliyofungwa yashughulikiwe kama ifuatavyo;-

(a) Mauaji na Uhaini

(i)Kesi zenye vifungo. Majalada yepeleke kwa afisa wa makao makuu ya upelelezi kwa mwaka mmoja kuanzia tarehe lilipofungwa. Ndani ya muda huu atayachunguza majalada kila baada ya miezi 6 kwa malengo ya kuhakikisha kama njia yoyote nyengine ya uchunguzi italeta tija. Baada ya mwaka mmja jalada lipelekwe makao makuu wa upelelezi Dar es salaamkuhifadhiwa.

(b) Makosa yenye adhabu miaka 7 au zaidi (isipokuwa mauaji na uhaini)

(i) Kesi zenye vifungo. Jalada litumwe makao makuu ya wilaya na kuzuia pale kwa mwaka mmoja halafu litaharibiwa kwa moto naMkuu wa polisi wa wilaya

(ii) Kesi zisizo na vifungo. Jalada litazuiwa na kituo kilichotoa jalada kwa mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kuflifunga na litachunguzwa.

(iii) Kesi zisizo na hatia. Majalada yatazuiliwa na vituo vya awali

kwa muda wa mwaka mmoja katoka tarehe ya kulifungua halafu liharibiwe kwa moto na mkuu wa polisi wa wilaya.

SEHEMU 1

Majalada ya makosa madogo

15. (a) Kila kosa ambalo halihusiani na sehemu ya kwanza ya kanuni hii litachukuliwa kama kosa dogo

(b)Kama hakuna maelezo ya kusaidia au makaratasi ya kesi yanayohitajika kuendesha mashtaka kwa ufanisi, afisa mpelelezaji ataandika yaliyotokea katika upelelezi katika sehemu husika katika fomu ya taarifa ya awali (first information report) (PF.162A) na fomu itapelelekwa mahakamani na ofisa mwendesha mashtaka kama kunahitajika karatasi za kusaidia zitawekwa ndani ya fomu PF.162A ambayo zitakunjwa katikatina kubadilishwa kuwa jaketi la jalada. Maafisa wahusika wa matayarisho ya majalada madogo

16. Majalada ya kesi ndogo zitatayarishwa na mkuu wa kituo au afisa yeyote atakaypangwa na Mkuu wa upelelezi wa mkoa au mkuu wa polisi wa wilaya.

Matayarisho ya majalada madogo

17. (a) Kila afisa ambaye anahusika na utayarishaji wa majalada madogo atahakikisha kuwa kila jalada limejzwa kwa usahihi, kupewa namba, na kusajiliwa katika daftari la upelelezi la kituo (PF.221)

(b) Kila taarifa mhimu inayotakiwa katika majalada ya kesi ndogo yataandikwa kwa usafi na usahihi baada ya ku kuthibitisha taarifa zote zilizomo. Kila kunapokuwa na shaka, taarifa iingizwe kw penseli isiyokoza na kunakiliwa kwa wino baada ya ithibati ya mabo. Hii itatumika katika kesi ambazo kuna shaka kuhusu kosa halisi na kifungu cha sheria.

Kusajili Majalada

18. Majalada yote ya makosa madogo yataingizwa katika daftari la upelelezi la kituo station investigation register) kulingana na utaratibu uliowekwa ibara ya 5 ya kanuni hii

Kuyapa Nambari Majalada Madogo

19. Majalada yote ya makosa madogo yatapewa nambakulingana na utaratibu uliowekwa ibara ya 6 ya kanuni hii, isipokuwa kwamba kila jalada la makosa madogo yataandikwa herufi "DIC"(mfano DC/DIC/2/04 ni sawasawa na jalada la makosa madogo namba 2 ya mwaka 2004 ya kituo cha polsi kati mkoa wa Dar es salaam.

Yaliyomo kwenye doketi

20. Yaliyomo (kama yamo) ya kila jalada dogo yatayarishwe kwa usafi na kujazwa kwa njia ambayo kesi itafahamika kiurahisi na kuwasilishwa mahakamani bila matatizo.

Kurudisha na kuchunguza majalada madogo

21. (a) Isipokuwa vituo vidogo vilivo chini ya askari wa cheo cha chini ambao wenyewe wanahusika na utayarishaji wa majalada madogo, kilajalada liwasilishwe kwa mkuu wa mkuu wa kituo kwa uchunguxi au afisa aliyeidhinishwa kumwakilisha, isipokuwa linapohitajika na mwendesha mashtaka.

(b) Afisa atakayechunguza uchunguzi uliotajwa, hapo juu ataelekeza katika kila kesi juu ya jalada au dokezo sabili hatua gani za ziada zitachukuliwa na ni lini lirudishwe kwa uchunguzi.

(c) Ucheleweshwaji usio wa lazima wa uchunguzi wa majalada uepukwe Mkuu wa kituo mwenye dhamana atahakikisha kuwa afisa mwengine au Mkaguzi anayekaimu kwa ajili yao kama anaweza kutokuwepo kituoni mwao kwa muda mrefu.

Uchunguzi baada ya kumaliza

22. Kila jalada lipelekwe kwa mkuu wa kituo alichunguze sio zaidi ya siku 7 baada ya kulifungua (au mapema kama inawezekana) na moja ya maingzo yafuatayo ndani yake;-

(a) Matokeo ya kesi kama mahakamani imemalizika

(b) Taarifa fupi kuhusu maendeleo ya kesikama bado haijafanikiwa ingawa inaonesha kuwa uwezekano wakufanikiwa ni mdogo

(c) Maoni kuwa jalada lifungwe kwa kuwa upelelezi unaonekana

umemaizika bila mafanikio

(d) Mkuu wa kituo atachunguza majalada yote yatakayoletwa mbele yake na;

(i) Aamrishe uchunguzi zaidi au

(ii) Aelekeze kuwa kesi ifungwe kama akiridhika kuwa hakuna hatua zozote za ziada za kipolisi zinazoweza kuchukuliwa.

Utunzaji na Uondoshaji wa Majalada ya Makosa Madogo

23. Majalada yote ya makosa madogo ambayo upelelezi umemalizika litazuiwa nakituo cha awali kwa muda wa miezi 3 halafu yatahariib iwa kwa moto kwa maelekezo ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya mwezi wa Januari wa kila mwaka.

PGO 287.

CHUMBA CHA MASHITAKA – OPARESHENI.

Taratibu kwa ujumla;

1.Chumba cha mashitaka laizima kiwepo kila kituo cha polisi.

2(a) Daraja' A na B' lazima view wazi masaa yote ya mchna na usiku katika mazingira ya kudumu.

(b) Kituo daraja C chumba cha mashitaka kinaweza kufungwa usiku kama itakuwa imeelekezwa na Kamanda wa Polisi wa mkoa kwa mujibu wa sheria za kituo ,ikielekeza askari kontabo lazima awe kazini kujibu simu za dharura zinazopigwa usiku na kuliunda mahabusu kwa mujibu wa kifungu namba 9 (c) (11).Askari wa Jeshi la Polisi katika kazi hiyo wanaweza kuruhusiwa kulala katika nchumba cha mashitaka kama kutakuwa hgakuna mahabusu ndani ya kituo.

3.Chumba cha mashitaka lazima kiwe kisafi muda wote .Thamani lazima zipangwe kwa usahihi na ziwe katika idadi inayostahili . Vitabu na kumbukumbu zilizokwisha tumika zisiwekwe katika chumba cha mashitaka.

4.Uvutaji wa sigara katika chumba cha mashitaka ni marufuku.

5.Maofisa pekee waliopo kazini au wenye kazi maalum ndio wanaoruhusiwa kuingia katika chumba cha mashitaka.

6.Maofisa walioko zamu katika chumba cha mashitaka lazima waondoke haraka iwezekanavyo mara tu baada ya muda wao wa kazi kwisha.

MAOFISA WA CHUMBA CHA MASHITAKA.

7.Kila chumba cha mashitaka lazima kisimamiwe na mkuu wa chumba hicho (CRO) ambaye atakuwa mwenye mamlaka katika chumba hicho na atawajibika moja kwa mmoja kwa mkuu wa kituo kwa ufanisi nwa kazi zote katika chumba hicho na majukumu.Askari wote katika chumba cha mashitaka lazima wawajibike na kupokea amri zote kutoka kwake .

8.Askari wanaofanyia kazi chumba cha mashitaka wanapaswa kufanya kazi zote kwa mujibu wa majukumu yao.Ni Stafu Sagenti pekee na kuendelea au askari mwenye cheo cha Copolo au Sagenti anaweza kuongea lugha ya Kiingereza atapangwa katika chumba hicho wakati wote wa mchana kwa vitu daraja A na B .

9.Askari wafuatao ndio watakaopangwa kazi muda wote katika chumba cha mashitaka:-

(a) Vituo Daraja A,

(i) Afisa mmoja msimamizi katika chumba cha mashitaka.

(ii) Idadi ya askari wawili konstabo kama wasimamizi wa chumba cha mashitaka.

(iii) Askari mmoja konstebo wa kusimamia chumba cha mahabusu.

(b) Vituo Daraja B,

(i) Afisa mmoja chumba cha mashitaka.

(ii) Askari mmoja konstebo katika chumba mahabusu kama kina watuhumiwa wamewekwa mahabusu kwa mstari (siyo walioko nyuma ya kituo au karibu na kituo cha Polisi)

10.Askari wote wa chumba cha mashtaka wanapaswa kuzingatia amri zote za kipolisi ambazo kimsingi zinawahusu wao nan watalazimika katika:-

(a) Kupokea na kuandika taarifa zote katika kitabu cha matukio (RB) kwa mujibu wa PGO 309.

(b) Kuhakikisha kwamba hatua za haraka zinachukuliwa na ofisa husika

kushughulikia kila taarifa inayopokelewa katika chumba cha mashitaka.

© Kushughulikia ujumbe wowote unaopokelawa kituoni na msimamizi wa chumba cha mashitaka na kuufikisha taarifa hiuyo kwa ofisa muhusika hivyo hatua muhimu zichukuliwe pasipo kuchelkewa.

(d) JKusimamika kitabu cha mahudhurio na matukio kwa mujibu wa PGO 284.

(e) Kusimamia vutabu vungine vyote katika chumba cha mashitaka na kuingizaa kumbukumbu kwa mujibu wa kanuni wa kazi za polisi .

(f) Kutunza funguo za mahabusu na kusimamia kitabu cha mahabusu kwa mujibu wa PGO 353.

(g) Kusimamia ulinzi katika ghala la silaha la kituo na silsha zilizomo ndanikwa mujibu wa PGO 152.

(h) Kutoa silaha na risasi kutoka katika ghala la kituo kama itakavyokuwa imeamuriwa na mkuu wa kituo.

(I) Kuhakikisha kwamba silaha zote zilizotolewa kutoka ghalani zinarudishwa bila kucheleweshwa.

(j) Kukagua askari wote wa doria na kazi zingine wakati wakiwa katika foleni/gwaride nje ya kituo mwanzo na mwisho wa kazi na kutoa taarifa na kitu chochote kitakacho kiukwa kwa mkuu wa kituo.

(k) Kusimamia mali zote za mahabusu ,Vielelezo vilivyopotea na mali za kuokotwa na nyingine zozozte zilizo kabidhiwa katika chumba cha mashitaka mpaka hapo mkuu wa kituo atakapokuwa ameridhishwa na hayo majukumu yua kazi.

(l) Kuhakikisha nidhamu ya askari katika chumba cha mashitaka inadumishwa na hakuna uvunjivu wa sheria za kazi.

KUKABIDHI CHUMBA CHA MASHITAKA

11.Askari wa chumba cha mashitaka lazima wabakie kazini kwa muda wa masaa nane .Hawataweza kuondoka katika chumba hgicho baada ya muda wao kwisha isipokuwa mpaka pale watakapokabidhi majukumu yao yote kwa shifti inayoinga .

12.Kila shifti ya chumba cha mashitaka inayoingia kazini lazima:-

(a) Kukagua mahabusu wote na kuhakikisha wamehesabiwa kwa

mujibu wa kifungu 13(a) cha PGO namba 353.

(b) Kuangalia/Kukagua ghala la silaha la kituo linalofanyakazi pamoja na silaha na risasi zilizomo kwa mujibu wa para 11(a) cha PGO Namba 152.

(c) Kukagua mali zote za mahabusu ,vielelezo,mali za kuokota na mali nyingine ambazo zilikwisha pokelewa katika chumba cha mashitaka na zile ambazo hazijakabidhiwa kwa mkuu wa kituo.

(d) Kukagua saa ya ukutani ya chumba cha mashitaka kama inafanyakazi ipasavyo na kuhakikisha simu ya kituo inafanyakazi.

(e) Kuangaalia kitu kingine chochote kama kinahusiana na kanuni za sheria za polisi.

Atakaporidhika kwamba kila kipo kwa usahihi ataingiza ingizo katika kitabu cha kituo (SD) na atachukuwa majukumu ya chumba cha mashitaka ,ghala la silaha ,mahabusu na kadhalika.Shifti iliyopokelewa inaweza kuondoka kwa ajili ya mapumziko.

13.Kama mmkuu wa chumba cha mashitaka hataridhgika na kwamba kazi zipo sawa ,atakataa kupokea majukumu ya chumba cha mashitaka na lazima amjulishe mkuu wa kituo . Wote wanaokabidhi na wanaopokea watabakia chumba cha mashitaka mpaka mkuu wa kituo amalize uchunguzi na kasha aelekeze kwamba makabidhiano yaendelee.

PGO 288

MAJUKUMU YA ASKARI WA VYEO VYA CHINI

Kwa kawaida:

1. Kila askari atawajibika kwa kazi wakati wote na atafanya kazi wakati wowote atakaoamriwa, haitajaisha ni wakati again amepangiwa kazi hiyo.

2. (a) Kila askari wa cheo cha chini atatakiwa kufanya kazi masaa 8 katika kila muda wa saa 24. paredi na mafunzo mengine vitahesabika kuwa ni moja wapo ya kazi.

(b) Kwa nyongeza kamanda atatoa kwa utaratibu idadi ya askari watakaokuwa mapumziko katika kila kituo au idara kufoleni wakati wowote wa dharura.

3. Bila upendeleo kutoka kwenye anya ya 1, kwa kawaida kazi maalum zitafanywa kama ifuatavyo:

(a) Kazi za doria masaa 6 mfululizo.
(b) Lindo masaa 8 zamu za mgawanyo. Ulinzi watakuwa zamu sio zaidi ya masaa 2 kwa wakati mmoja.
(c) Doria fupi - masaa 6 mfululizo
(d) Zamu za chumba cha mashtaka vituoni vya daraja A na C – masaa 8 mfululizo
(e) Zamu za chumba cha mashtaka kwa vituo vya daraja C – masaa 12 mfululizo (12.00Asubuhi hadi 1200 jioni) vinginevyo iwe imepangwa tofauti kutokana na utaratibu uliowekwa kwa manufaa ya kituo husika.

4. Mkuu wa kituo atapanga maofisa wa chumba cha mashitka watakaopokezana wakati wa chakula na atamruhusu askari wa zamu ya usiku kwenye vituo vya daraja C kulala kati ya saa 4.00 hadi 6.00 usiku kama ulinzi wa jengo la kituo umeimarishwa. Huu utakuwa ni utaratibu wa binafsi wa kitu husika.

5. Taratibu za kila siku za kazi za muda wa masaa 8 zitaanzia saa 6.01 usiku, 2,00 asubuhi na 10.00 jioni, mida ya masaa 6 itaanzia saa 6.01 usiku, 12.00 asubuhi , 6 00 mchana na 12.00 jioni, Askari wa jeshi la Polisi wenye kazi maalum au dharura watapangiwa kazi nyingine kwa vipindi fulani.

Kazi za askari wa kike:

7. Askari wa kike watafanya kazi za polisi kwa ataratibu zifuatazo

(a) Hatofanya kazi za usiku isipokuwa wameitwa au kubakia kazini kwa sababu maalum.
(b) Hawatafanya doria za mitaani wakati wa giza, labda tu wawe na ulinzi wa kutosha.
(c) Hatafanya kazi za kutuliza ghasia au kazi za fujo labda tu ziwe zinawahusu wanawake au watoto.
(d) Hawatafanya kazi za kukaa au zinazohusu masuala ya dini.

8. Wakiwepo askari wa kike wa kutosha watafanya kazi zifuatazo:-

(a) Upekuzi wa wanawake na majengo yao nyumba zao.
(b) Kusindikiza wanawake
(c) Uangalizi wa wanawake waliopo kwenye vituo vya polisi ikiwa ni pamoja na kuwaangalia wakiwa mahabusu.
(d) Kuhoji wanawake kwa makosa ya kijinsia.
(e) Kuhoji watoto, mfano watoto waliopotea, watoto waliofanya makosa.
(f) Kuwasaidia watoto wanakatiza barabara na kuwaelekeza watoto wa shule mambo muhimu ya Usalama Barabarani; na
(g) Kufuatia uwepo wa askari wa kike na umuhimu wao; wanapaswa kuwepo mahakamani wakati wa mashauri dhidi ya watuhumiwa wakike yanaendelea au wakati mashahidi wa kike wameitwa mahakamani kutoa ushahidi.

KUSINDIKIZA MILIPUKO, SILAHA NA RISASI ZA JESHI

1. Usindikizaji mara zote utatolewa kulingana na ombi lililotolewa. Wakati usafiri wa maji au anga utakapotumika, mzigo utasindikizwa hadi kwenye ndege au meli na kukabidhiwa kwa nahodha. Utapelekwa katika eneo wanakokwenda na kusindikizwa hadi mwisho wa safari. Hakuna malipo yatakayofanywa kwa usindikizaji wa mzigo huo.
2. Usindikizaji wa milipuko utatolewa kwa matukio yafuatayo
    (a) Uingizaji wote mkubwa toka nje kwa njia ya Reli
    (b) Masuala yote makubwa yahusuyo milipuko zidi ya 100 toka ghala la kuhifadhia milipuko Dodoma.
3. Silaha na risasi za jeshi zima zitasindikizwa zinaposafirishwa katika mazingira yoyote hazititolewi kutoka bohari kuu bila kusindikizwa. Hii pia itatumika wakati wa kuhamisha baina ya kitengo na kitengo.
4. (a) Nguvu yoyote ya kusindikiza ni jukumu la offiasa anayesimamia shughuli hiyo; atapaswa kuzingatia:-
        i. Ukubwa wa mzigo
        ii. Njia itakayotumika/Barabara
        iii. Idadi ya silaha zinazotumika katika safari
        iv. Aina ya usafiri
        v. Mapumziko
    (b) Nguvu kazi isipotezwe katika usindikizaji wa mara kwa mara inapowezekana maofisa wanaokwenda likizo, uhamisho au doria za kawaida watumike
    (c) Kuhakikisha kila askari ana kitabu kidogo cha kuandika mambo atakayokumbana nayo yaani (Note Book)
    (d) Kuwapa maelekezo mfano watuhumiwa wanaotafutwa, mali za wizi au taarifa nyingine za muhimu za kazi za polisi.
    (e) Maelekezo kuwa kila askari kuhusu wajibu wake kama ulivyoanishwa kwenye kitabu cha kazi na kuhakikisha anaeleweka kwa kila askari kuhusu wajibu na majukumu yao.

5. Afisa anayesimamia usindikizaji atahakikikisha kwambe wahusika wana chakula cha kutosha, pesa vya kujikimu mpaka watakaporudi kituoni.

6. Amri ya kusafiri PF. 58 itakamilishwa na ofisa anayepanga usindikizaji na maelekezo yafuatayo na taarifa yao:-
   (a) Vyombo vyote masanduku yafungwe kabla ya kuchuliwa na ofisa mtoaji.
   (b) Namba ya vyombo vinavyosindikiwa vitatiwa saini na wasindikizaji; yaliyomo katika vyombo haitakuwa wajibu wa wasindikizaji.
   (c) Katika suala la silaha idadi lazima ionyeshwe katika amri ya kusafiri na itasaniwa na msindikizaji.
   (d) Kabla usindikizaji kukoma, lazima risiti ya kupokea ipatikane toka kwa afisa mpokeaji.
   (e) Hatua za kulinda mzingo wakati wa safari zichukuliwe hususani wakati wa usiku.
   (f) Hatua zichukuliwe ikiwa pana tukio la kuvunjika kwa usafiri/msafara.
   (g) Jina la afisa mpokeaji.
   (h) Maelekzo ya silaha yachukuliwe na msindikizaji na wakati gani yatatumika kulinda mzingo. Wakati inapoonekana inafaa maagine zitajazia risasi tano “bolt itabaki imefungwa na hakuna risasi itawekwa katika chember usalama utafanywa. Kama maofisa atakuwa na revolver risasi tano zitajazwa katika culinder. Risasi saba zitaachwa katika Punch.

7. (a) Mkuu wa Polisi wilaya ambaye maombi ya usindikizaji yametumwa kwake atawajika kuandaa usindikdizaji. Atapaswa kuwahusisha na kamanda wa polisi na Mkoa wake ikiwa hana askari wa kutosha

   (b) Ikiwa kuna wingi wa mabomu/milipuko bandari ya Dar es salaam, Kamanda wa polisi Reli na kanda ya Dar es salaam watawajibika kutoa wasindikizaji.

(c) **ULINZI KATIKA OFISI ZA SERIKALI**:

1. Ulinzi wa polisi utakuwa katika ofisi za serikali ambazo zitakazohitaji ulinzi. Makamanda wa mikoa wanao wajibu wa kuamua kwa makubaliano na Wakuu wa mikoa ni ofisi zipi za serikali zinahitaji ulinzi na namna zitakayolindwa. Ukamakini utazingatiwa ili kuepuka kupoteza nguvukazi katika ulinzi ambao zi wa lazima.

2. Makamanda wa mikoa watahakikisha kwamba amri muhimu za jukumu zinatolewa katika vituo vyote ambavyo vinatakiwa mara kwa mara kutoa ulinzi katika ofisi za serikali.

3. Walinzi katika ofisi za serikali kwa kawaida watatakiwa kubeba /kuwa na bunduki na risasi tano kwa mujibu wa PGO. 274.

4. Walinzi wanapaswa kukaa katika hali ya tahadhari wakati wote wawapo lazini na hawaruhusiwa kukaa au kulala chini isipokuwa kama wameruhusiwa rasmi kufanya hivyo.katika amri ya kudumu ya kituo (wakati wa usiku na k..)

5. Wakati ulinzi aingiapo kazini atatakiwa kuchunguza maeneo, madirisha, kasiki na kitu kingine chochote alichoaminiwa kukiangalia na asiruhusu mlinzi (kama yupo) aliyekabidhi kuondoka kazini hadi atakapojiridhisha kwamba kila kitu kipo sawasawa.

6. Kwa mazingira yoyote mlinzi yeyote hataondoka katika eneo lake la kazi mpaka apokelewe Man zote walinzi watatakiwa kuripoti chumba cha mashtaka kilisho karibu wanapingia na kutoka kazini na maingizo yatafanywa katika kitabu cha matukio.

7. Maofisa wa doria watakagua walinzi katika majengo ya serikali

ili kuhakikisha kwamba wanazingatia mashart ya utaratibu huu na taratibu zingine za amri za kudumu.

PGO 292

UWASILISHWAJI TAARIFA

TAARIFA MAWASILIANO YA

1. Taarifa zote zinzowaslishwa kwa au kumiliwa na polisi zijaliwe zitakuwa ni siri. Askari wa vyeo vyote pamoja na watumishi raia hawaruhusiwi kunakili, kufupisha au kuchuka nyaraka za kiofisa au sehemu yoyote ya nyaraka hizo kwa matumizi binafsi au kwa matumizi ya watu wengine, ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari bila idhini rasmi ya kiofisi. Katazo hili lazima litatumika kwa taarifa zilizopokelewa kwa maneno au kwa simu au radio.

2. Kifungu cha 4 na 5 cha sheria ya usalam wa taifa sura ya 47 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002 inasomeka kama ifuatavyo:-

   (i) Mtu yeyote anayemiliki au chini ya utawala wale, alama ya mfucho, neno la siri, mchoro, mapango , muundo, hati , makala, habari au taarifa inayohusiana na au ilyotumika kulingana mahali au kitu chochote mahali pale au imefanywa au kupatikana kinyume cha sheria hii au ambacho ameaminiwa kwa siri na mtu yeyote mwenye madaaka ya umma, au ambacho amepata au ambacho amekuwa nacho kwa mujibu wa madaraka yake au alikuwa sehemu ya mkataba na serikali au alikuwa na madaraka maalumu

au mkataba mzima au sehemu yake katika mjukumu aliyokuwa nayo kuhusiana na sehemu inayolindwa au ni mtu ambaye au alikuwa ameajiriw ana au chini ya mtu mwenye madaraka au aliyekuwa na madaraka ya umma au aliye au alikuwa sehemu ya mkataba na ambaye:-

(a) Anayatumia kwa namna au kwa madhumuni yenye madhara kwa usalama au maslahi ya usalama wa Jamhuri ya Muungano au;
(b) Anatoa mawasiliano kwa mtu asiyeruhusiwa au asiye na maslahi kwa Jamhuri ya Muungano badala ya mtu anayewajibika kuwasiliana naye; au
(c) Ameshindwa kujiheshimu mwenyewe au anafanya matendo yanayoharisha usalama wa nchi; au.
(d) Ameshikiria mchoro, mpango, muundo, hati , makala au habari katika miliki yake au chini ya utawala wake wakati hana hati ni kinyume na jukumu lake au ameshindwa kuzingatia na maelekezo ya kisheria kuhusiana na mrejesho au uhifadhi wake atakuwa na kosa na akipatikana na hatia atawajibika kutumikia kifungo kisichozidi miaka 20.
(e) Mtu yeyote anayemiliki au chini ya utawala wake mchoro woeote mpango, muundo, au makalla nyingine habari au taarifa zihusianazo na zana za vita na ambaye anafaya mawasiliano moja kwa moja au kupitia kwa mtu yeyote kwa namna ambayo na kwa sababu zenye madhara kw ausalama au maslahi ya Jamhuri ya Muungano. Atakuwa ametenda kisa na akipatikana na hatia atatumikia kifungo kisichozidi miaka 20.

3. Mtu yeyote anayepokea alama ya mfucho, neno lasiri, mchoro, mapangu, muundo, hati au makala nyingine, habari, au taarifa huku akijua au ana sababu za msingi kuamini katika kipindi ilichopokea

mawasiliano, kumetokea upinzani na sheria hii, lazima vinginevyo ithibitike mawasiliano kwenda kwake haikuwa dhamira yake, atakuwa na kosa na akatiwa hatiani atapaswa kutimikia kifungo kisichozid miaka 20.

4. mtu yeyote anayetoa mawasiliano kwa mtu tofauti na mtu aliyeruhusiwa na ofisi , mwenye mamlaka kutoa taarifa zenye maslahi kwa Jamhuri ya muungano, taarifa zinazohusu ulinzi au usalama wa Jamhuri ya Muungano, lazima atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatumikia kifungo kisichozidi miaka 20.

5. Kwa mahumuni ya kifungu kidogo cha (4) “taarifa zinazohusu ulinzi au usalama wa Jamhuri ya Muungano “ inajumuisha taarifa zinazohusu mwenendo au mahali polipo na vikosi vya jeshi la ulinzi, Jeshi la Polisi, hatua zinazochuliwa kulinda maeneo nyeti maeneo yanayolindwa, upatikanaji na uhifadhi wa zana za vita”.

KIFUNGU CHA 5 – UTUNZAJI WA TAARIFA MUHIMU

1. Mtu yeyote anayetoa taarifa kuhusu jambo la siri au amesababisha uvunjifu wa jambo hilo kwa mtu asiye na mamalaka nalo au kwa mtu asiye na maslahi kwa Jamhuri ya Muungano lazima atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatumikia kifungo kisichozidi miaka ishirini.

2. Kwa mashitaka kwa kikuka kifungu kidogo cha (1) haitakuwa kinga kwa mtuhumiwa kuthibitisha kuwa aliokuwa akitoa taarifa za jambo la siri hakujua na kwa sababu namjua lile lilikuwa la siri.

3. Kila ofisa wa polisi aelewe wazi kwamba vifungu vilivyopo hapo juu vinamhusu pamoja na adhabu zilizopo bila kujali yupo jeshini au hayupo iwapo atatoa taarifa za siri kwa makosa.

4. Hairuhusiwi kwa hali yoyote kwa ofisa wa polisi kutoa maelezo kwa kauli au maandishi kwa jamii nje au ndani ya Tanzania kuhusu mambo ya kisiasa au kuhusu sera na mambo ya Jeshi la Polisi au Serkali. Umakini umewekwa kwa vyeo vyote kuhusu kifungu cha 35 na 36 Amri za jumla za seikali.
    - “Ofisa haruhusiwe kuandika au kutoa matangazo ya mazungumzo kuhusu suala la kisiasa au kiutawala, ingwa anaweza kutoa habari iliyosainiwa kuhusu jambo lenye maslahi ya wengi. Masharti haya yanazihusu pia familia za askari /ofisa”

    - “ Ofisa haruhusiwi kuhojiwa akiwa kazini au likizo kuhusu sera ya nchi au mambo yanoyweza kuathiri ulinzi na rasilimali za jeshi la Tanzania.”

5. Maudhui ya amri za polisi , maelekzo na taarifa za siri za uvamizi, ukamataji/ushikiliaji, upelelezi na upeo wake na mambo yanayofanana hayaruhusiwe kupitishwa kwa vyombo vya habari hata kwenye jamii.

MAWASILIANO KUTOKA KUMBUKUMBU ZA KIOFISI

6. Nyaraka za kiofisi haziruhusiwi kuonyeshwa kwa watu walio nje ya jeshi .nyaraka hizo ni vitabu au kumbukumbu. Mwenye mamlaka hayo ni Mkuu wa Kikosi au Idara. Majalada ya polisi hayapaswei kupitishwa kwa idara za nje ya Jeshi. Majalada ya kesi yanaweza kupelekwa kwa Mkurugenzi wa mashitaka kulingana na amri No. 286. Nakala za maelezo ya mtuhumiwa na mashahidi yanaweza kutolewa kwa mtuhimiwa au wakili wake kulingana na amri No.245

ya Jeshi la Polisi.

TAARIFA KWA MAAFISA WA VYOMBO VYA HABARI (MAGAZETI, RADIO NA TELEVISHENI) NA UTANGAZAJI

7. Taarifa kuhusu matukio ya kawaida ya uhalifu, majanga ya moto na matukio kama haya yanaweza kutolewa na ofisa wakaguzi kwa maofisa wa vyombo vya habari wanaokubalika. Mkaguzi atatoa taarifa iwapo tu katika kituo husika hakuna ofisa. Maelezo ya taarifa yatahusu:
    (a) Aina ya tukio- wizi, kubaka, mauaji, moto, ajali ya gari n.k.
    (b) Mahali na muda wa tukio.
    (c) Waliokamatwa bila kutaja majina yao, isipokuwa idadi, utaifa, jinsia, umri.
    (d) Majina na anwani za wahusika, mfano waliouawa, waliojeruhiwa, waliopelekwa hispitali n.k.
    (e) Majina ya walalamikaji isipokuwa:-
        i. Kesi za kubaka na makosa ya kujamiiana
        ii. Kama mlalamikaji ameomba jina lihifadhiwe.

    ANGALIZO: Kwa kifo au majeruhi haarishi polisi anakubali jukumu la taarifa ya awali liwe la mrithi. Majina ya anwani za marehimu hayatatolwa kwa vyombi vya habari hadi jukumu hilo limetekelezwa. Mrithi ambaye hatapatikana haraka ajulishwa kwa barua pepe au simu kuptia wilaya iliyokaribu na anwani yao. Taarifa ipewe muda unaokubalika kumfikia mlengwa kabla majina na anwani za marehemu hajakabidhiwa vyombo vya habari. Ni muhimu kuchelewesha kutangaza taarfa iza tukio hadi ithibitike kwa mrithi amepokea taarifa ndipo itangazwe Radioni au gazetini siku inayofuata.

8. wawakilishi wa vyombo vya habari wapewe nafasi ya kupata taarifa wenyewe katika eneo la tukio. Awanapaswa kuheshimu amri za ofisa wa polisi aliyepo kazini na wataingia ndani ya kizuizi cha polsi kwa ridhaa yao hatakiwi kijihusisha na mjadala na wawaelekeze kwa afisa wa polisi aliyepo eneo la tukio kwa maelekezo.

TAARIFA YA AJALI

9. Maombi kuhusu taarifa za ajali za barabaani zinazopokelewa kutoka makampuni ya bima au wawakilishi wao wa kisheria zishughukiwe na ofisa wa polisi Trafiki au Mkuu wa Polisi wa Wilaya kama ifuatavyo:-

(a) (i) Iwapo hakuna kosa la jinai lililogundulika au hakuna ushahidi wa kutosha kuendelea na taratibu za kimahakama mwmbaji anaweza kupatiwa taarifa hiyo katika PF. 90 kwa gharama zilizoekezwa. Taarifa hizo zitatolewa iwapo zipo polisi, Uchunguzi maalum kuhusu kutafuta taarifa hautashughulikiwa na polisi.

(ii) Polisi haitakubali kuwajibika kuhusu usahihi wa majina na awani yaliyotolea polisi na mashahidi pamoja na watu walihusika na ajali.

(iii) Barua zote zinazoripatiwa zilipelekwe kabla ya kutumwa sehemu husika

(b) Kama kuna kosa la jinai hakuna taarifa zilitotolewa isipokuwa kwa amri ya mahakama kesi iliposajiriwa. Hii pia itahusu uchunguzi wa habari za kifo.

TAARIFA YA MOTO:

10. maombi toka kampuni ya bima au mmiliki wa mali ziiiilizoungua yatashughulikwa sawa na taarifa ya ajali ya barabarani kifungu Na 9 hapo juu. Taarifa zitakuwa kwa njia ya barua. Hakuna malipo .

UTHIBITISHO WA KOSA LA WIZI KWA KAMPUNI YA BIMA

11. (a) Kufuatana na masharti na sera za baadhi ya makampuni ya bima ni muhimu kwa mtu aliyekatiwa bima mali kutoa taarifa polisi kuhusu wizi wa mali hiyo katika hali hii mhusika anaweza kuomba uthibitisho wa taarifa aliyotoa polisi kwa mali iliyoibiwa.

(b) Maombi ya aina hii yatashughulikiwa na mkuu wa polisi wa wilaya. Uthibitisho utakuwa na uundo ufuatao:-

Nathibitisha .....(jina la mtoa taarifa) ametoa taarifa hapa kituoni tarehe .....kuwa vitu vifuatavy vimeibwa kwake:-

1..... 2..... 3..... 4..... 5..... 6.....

Sahihi :..... Mkuu wa Polisi

Wilaya ya :.....

ANGALIZO:-

Ieleweke wazi kwamba uthibitisho huu siyo ushahidi kuwa taarifa iliyotolewa

polisi na malalamikaji inakubalika kuwa ni kweli.

(c) Nakala na uthibitisho itawekwa kwenye faili la kesi ioyoripotiwa polisi na mlalamikaji.

12. Wakati mwingine maelekezo ya mlalamikaji yanaombwa polisi na makampuni ya Bima na watu wengine. Kwa kuwa taariffa zitolewazo polisi ni siri, hairuhusiwi kutoa taarifa za mlalamikaji kwa mtu mwingine, isipoliuwa mlalamikaji mwenyewe akiziomba kwa polisi.

PGO - 293

TAARIFA

NJIA YA SAHIHI YA UTOAJI

1. Kila afisa wa polisi anawajibi wa kufikisha taarifa za uhalifu au usalama kwa mkuu wake hata kama ni mdogo sana.

2. Kama ofisa wa polilsi akiwa kazini au hayuko kazini, akkaona kitu chochote kinachotia mashaka au si cha kawaida , atarekodi kwenye kidaftari chake kidogo cha mfukoni kuhusu jambo hilo, na kama itawezekana atatoataarifa mara moja kwa mkuu wake wa komandi na kuomba maelekzo, Kama hakuna simu atatoa taarifa haraka iwezekanavyo kwa kituo cha polisi kilicho karibu. Amri hii haimzuii afisa wa polis kuchukua hatua zinazofaa kama za kukamata na kufanya uchunguzi wa tukio kama ataona kufanya hivyo ni muhimu.

3. (a) Kama utaratibu wa kawaida, kila kitu chenye umuhimu kitariotiwa kama ifuatavyo:-

i. Askari wa cheo cha chini ataoa taarifa kwa mkuu wake wa kituo au

kwa afisa mwingine wa juu kama mkuu wake wa kituo hayupo.

ii. Kila mkuu wa kitu atatoa taarifa kwa mkuu wake wa polisi wa Wilaya.

iii. Kila mkuu wa polisi wa Wilaya atatoa taarifa kwa mkuu wake wa polisi wa Mkoa

iv. Kila mkuu wa polisi wa Mkoa atatoa taarifa Mkao Makuu ya Jeshi la Polisi.

4. Taarifa itakuwa kuelekezwa bila kuchelewa kwa wake wenye haki ya kuupokea. Wahusika wote ni lazima wafahamishwe kikamilifu kilichotokea katika maeneo yaliyo chini yao. Wakuu wa komandi vile vile watahakikisha kwamba wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na atendaji wengine wa idara za seikali wanashauriwa na maombo yote yanayowahusu.

5. Afisa yoyote atakayeshikilia habari au kuchelewesha usambaaji wake atakabililwa na adhabu kali.

PGO - 294

UTOAJI WA TAARIFA/MAELEZO KWA VYOMBO VYA HABARI NA REDIO

1. Maafisa wafuato ndiyo to wenye mamlaka ya utoaji wa taarifa juu ya masuala ya polisikwa vyombo vya habari

(a) Inspekta jenerali wa polisi katika masuala yote yanayohusu sera za jeshi na usalama.

(b) Mkuu wa upelelezi wa makosa ya jinai - Taarifa za uhalifu,

matangazo ya watu wanaotafutwa na vifaa kuhusiana na uhalifu, ajali n.k

(c) Mkuu wa polis mahusiano ya umma makao makuu ya jeshi la polisi- Taafifa za mara kwa mara kuhusiana na jeshi zima.

(d) Makamanda wa Polisi mkoa - Taarifa za mara kwa mara zinazohusu mikoa.

2. Taarifa zote zitolewazo kwenye vyombo vya habari na redio lazima ziwe zimechapwa au kuandikwa. Taarifa zitolewazo kwa mdomo zitaruhusiwa wakati wa dharura na zitatakiwa kuthibitishwa kimaandishi maa moja

3. Taarifa zote zitatolewa chini ya mamlaka au (jina) ya inspekta jenerali wa polisi bila sahihi . Mamlaka na sahihi binafasi zimezuiliwa

4. Amri hii itasomwa kwa kushirikiana na PGO Na 192 kwa hali yoyote ile hakuna taarifa zozote za polisi ambazo zitatolea kwa vyombo vya habari au jamii na afisa mabaye hana mamlaka ya kufanya hivyo.

MAJENGO YENYE LESENI – UDALALI PGO NO. 295

1. Madalali zaidi ya madalali wanaohamahama wanatakiwa na sehemu ya 4 (1) ya sheria ya udalali sura 227, kupata leseni kutoka kwa afisa wa wilaya au afisa mapato ya wilaya ambaye anakaa au anakusudia kuanzisha kama

nafasi yake kuu ya biashara.

2. Dalali anayehamahama ina maana ya mtu ambaye hana sehemu yeyote ya kudumu ya biashara na ambaye ameidhiniwa na Afisa wa Wilaya kwamba yeye anauza na kutoa huduma kwa mali zinazohamishika na mauzo ya vitu vilivyotengenezwa kwa asili au isiyozidi shiling mia moja kwa thamani.

AINA YA LESENI:

3. Kuna aina mbili za leseni:

(a) Leseni kuu ambayo inaidhinisha mwenye leseni kuendelea na biashara ya udalali mahali popote nchini Tanzania

(b) Leseni za mtaa ambayo inaidhinisha mwenye leseni kuendelea na biashara ya udalali tu ndani ya wilaya ambayo ameidhiniwa kufanyia biashara.

FOMU YA LESENI:

4. Leseni lazima itakuwa moja ya aina fomu katika sehemu ya kunza ya sheria. Leseni ya kila mwaka itakuwa inaishai siku ya juni, 30 katika mwaka na nusu lrdrni kila mwaka itakuwa inaishia siku ya Desemba 31 au siku ya Juni 30 ijayo baada tarehe kutolewa.

DAFTARI LA KUTOA LESENI

5. (a) Mamlaka ya kutoa leseni itatunza daftari la watu wote waliowapa leseni

(b) Mkuu wa kituo atayaandika majina na anwani ya madalali wote wenye leseni ndani ya kituo cha eneo lake ambalo anasimamia kwenye daftari la leseni ya majengo (PF. 214) kwa mujibu wa PGO namba 301.

VIGEZO JUU YA KUKUBALIWA KUUZA MALI

6. (a) Kila dalali mwenye leseni, juu ya ombi la mmiliki, ana wajibu wa kukubali kuuza mali yake ambayo si marufuku kwa sheria kutoleana na kuuza, ambayo inatolewa mjini au mahali ambapo anafanya biashara yake kama dalali. Hawezi kuhitajika kuuza mali ambayo amekabidhiwa mapema baada ya siku saba baada ya kukabidhiwa kwa ajili ya kuuza, lakini ukizingatia mali zingine ambazo amekabidhiwa kuuza ndani ya muda ambao mmiliki anahitaji au mapema baada ya hapo kama inawezekana.

(b) Dalali anaweza kuuza mali ya mmiliki zaidi ya mojakatika uuzaji huo, inahitajika kwamba bidhaa zitakuwa mpangilio mzuri kwa namna ya kwamba hakutakuwa na mchanganyiko wa mali ya mmiliki mmoja na mwingine.

(c) Leseni ya dalali haitaidhinisha uuzaji wa vitu au kitu chochote ambacho hakijaidhinishwa kwenye leseni hiyo.

MUONO WA LESENI

7. Kila Dalali mwenye leseni kabla ya mwanzo wa mnada na wakati wote wa mnada anahitajika kuonesha kwa wazi tiketi au bango lenye jina lake kamili, makazi, mchoro, machapisho au maandishi yenye herufi kubwa hadharani yanayoonekana vizuri na kusomeka.

Kumbukumbu zinavyotunzwa na Dalali mwenye leseni

8. Kila Dalali lazima atatunza leseni yake katika nafasia yake ya biashara au ikiwa hana nafasi hiyo katika mahali ambapo yeye ana mnada, rekodi ya mali yote inayotolwewa na yeye kwa ajili ya kuuza kwa mnada wakati wa kipindi cha leseni yake.

WAJIBU WA POLISI KUTOA HABARI KUHUSU MALI ILIYOIBIWA

9. (a) Mkuu wa kituo aliye pokea taarifa ya hasara, wizi au ulaghai wa mali

yoyote iliyotambulika au kuthaminiwa baada ya kupata maelezo kamili mali, hatasambaza kwa madalali wote katika kituo chake. Ni muhimu sana kutoa orodha ya mali, tarehe ya mali zinazotambulika au mali ya thamani ni lazima kutolewa kwa madalali haraka inavyowezekana baada ya wizi, hasara n.k baada ya kuripotiwa.

(b) Mkuu wa kituo ana wajibu wa kutembelea madalali wenye leseni katika kituo cha eneo lake kama jambo la kawaida angalau mara mpja kwa mwezi. Afisa mkaguzi lazima atatoa mwenyewe orodha ya mali iliyotambulika kuibiwa au kupotea na lazima atafanya ukaguzi wa mali alizokabidhiwa dalali kwa ajili ya kuuza dhidi ya kitabu chake.

Wajibu wa dalali kwa polisi

10 (a) Kila dalali wenye leseni lazima ataruhusu afisa wa polisi kukagua mali yoyote aliyokabidhiwa kwa ajili ya kuuza na lazima atatoa maelezo kuhusu mali anayomiliki na jina na anwani ya mmiliki wa mali hiyo,

(b) Wakati wowote wa kufanya mnada , Dalali lazima ataonyesha leseni yake kwa afisa wa polisi kwa ukaguzi kama kitalazimu kufanya hivyo.

(c) Kumbukumbu yoyote iliyotunzwa na dalali lazima itakuwa wazi kwa ukaguzi kama afisa yeyote wa polisi mzadizi itahitajika.

PGO - 295

MAJENGO YANAYOLIPIWA LESENI

1. Kumbi za semina, kumbi za michezo ya maigizo na majengo mengine yaliyolipiwa leseni kwa ajili ya burudani ya umma yanatakiwa kutembelewa na afisa wa polisi mwenye cheo cha mkaguzi au zaidi angalau mara moja kila mwezi. Rekodi za kila ziara zitawekwa kwenye kitabu cha usimamizi wa majengo yaliyolipiwa leseni kwa masharti ya

PGO Na. 301.

2. Afisa atayezuru atahakikisha kwamba majengo yako chini ya lezeni ya sasa. Atakagua jengo na kujihakikishia kwamba mahitaji yote ya leseni yametimizwa. Tahadhali maalum zitachukuliwa kwa usalama :-

   (a) Sehemu za kuingilia au kutokea lazime iwekwe wazi kabisa bila kizuizi na kuendana na masharti ya leseni.

   (b) Msongamano

   (c) Ishara za taa zinazoashiria njia za kutoka lazime ziwasher muda wote wa maonyesho.

   (d) Vichororo ambavyo watu hawaruhusiwi kukaa au kusimama.

   (e) Vifaa vya kuzimia moto ambavyo ni lazima viwekwe katika hali nzuriya utendaji

   (f) Tahadhari ya moto ambayo ni lazima kufanyika hasa katika chumba cha maonyesho,

   (g) Jenereta iwekwe tayari endapo umeme utakatika

3. Afisa atayezuru atahakikisha kanuni za manispaaa au sheria ndogo za miji kuhusiana na udhibiti wa maeneo ya starehe ya umme zinaeleweka na kufutwa vizuri na utawala

4. Pamoja na uwepo wa kanuni hii lakini ni lazima ieleweke hakuna hatua zitakazo chukuliwa ndani ya jingo kwa jinai isipokuwa pale ambapo hatua za haraka ztahitajika kwa ajili ya usalama wa umma. Afisa atakae tembelea maeneo hayo atamwita meneja ofisini kwake na atamfulisha juu ya jinai ilivyotoea na atamjulisha mkuu wa kituo afisa atakayetembelea maeneo atahakikisha kwamba.

   (a) Watu wakisubiri uingiaji katika ukumbi wa seinema au ukumbi wa michezo ya maigizo wawe na mwenendo mwema na kwamba mwenendo ambao atapelekea uvunjifu wa

amani hautatokea.

(b) Hakuna uzibaji wa barabara kuu ya umma sehemu ya kuingilia wakati watu wanaiagia au kutoka ukumbini.

(c) Upitaji magari kuingia na kutoka katika kumbi za sherehe utawezeshwa muda wote.

PGO - 297

MAJENGO YA BIASHARA

MILIPUKO NA STOO

(a) Sehemu yenye lesini ya kuhifadhi mlipuko - Mlipuko yenye uzito zaidi ya 10,000 kila au milipuko mingine ya uzito wa kilo 1,000 unaweza kuhitadhiwa katika stoo iliyojengwa kulingana na maelekezo ya kamishna wa migodi. Kufungu Na, 28 ya sheria ya milipuko sura 45 marekebisho ya sheria ya mwaka 2002.

(b) Katika stoo yenye leseni milipuko yenye uzito wa kilo 10,000 au chini yake au milipuko mwingine yenye uzito wa kilo 1.000 au pungufu inaweza kuhifadhiwa katika jengo lolote ambalo limekatiwa leseni ya kuhifadhi milipuko au mkaguzi wa migodi (kifungu 28 cha sheria ya milipuko sura 45 marekebisho ya sheria ya mwaka 2002.

(c) Kutunza ndani ya maboksi milipuko isiyozidi kilo 1,000 katika idadi ya milipuko isiyozidi kilo 100 inaweza kutunzwa ndani ya maboksi yaliyoidhinishwa na kamishna wa migodi kwenye eneo husika kama itavyoidhishwa na mkaguzi migodi kifungu 28 cha sheria ya milipuko sura ya 45 marekebisho ya sheria ya mwaka 2002.

MAJUMUISHO

2. Katika hali yoyote milipuko inaweza kuhifadhiwa pamoja na milipuko mingine sehemu moja isipokuwa usalama wa fyuzi

3. Katika swala la kuhifadhi milipuko na stoo, nakala ya leseni, lazima ionekane katika jengo kwa rejea ya afisa mkaguzi (kifungu 37 cha sheria ya milipuko Na. 56 cha mwaka 1963.

4. kitabu cha kutoa na kurejesha milipuko sharti kitunzwe na mmiliki wa kuhifadhi milipuko au stoo. Kitabu hiki kinaweza kutunzwa ndani ya jengo au kwa mmiliki wa jengo la biashara (kifungu 37 cha sheria ya milipuko sura 45 marekebisho ya sheria ya mwaka 2002.

HIFADHI YA MILIPUKO

5. Milipuko inaweza tu kulipuliwa kukiwa na leseni na kibali cha maandishi kinachotolewa na kamishna wa migodi kulingana na mipango na uhalisia ulioidhinishwa na yeye.

Mambo ya kuzingatia katika usalama wa kuhifadhi milipuko.

6. (a) Kila hifadhi ya milipuko kwa pande zote izungushiwe na kingo za undongo zenye urefu angalau futi tatu katika wembamba kama juu,

(b) chini ya miteremko ya ndani isipungue futi tatu au kuzidi futi sita kutoka kwenye ukuta isipokuwa mahali pa kuingilia ambapo patakuwa na mstari uliyovunjika au kulindwa kwa ukuta wa udongo kwa nje .

(c) Eneo lote lizungushwe na fensi, ambayo haizidi futi tatu. Kutoka kwenye kingo ambalo litaidhinishwa na kamishina wa migodi ambayo kutaingilika kupitia lango ambalo kama halitumiki litafungwa kwa kufuli.

(d) Lango la nje la kuhifadhi milipuko sambamba na mlango utakaonyesha ishara ya neno (hatari) na chini yake neno Baruti explosive au “Baruti Detonators” kama itakavyokuwa.

(e) Kila hifadhi ya milipuko itakuwa na angalau maunganisho kushawishi kuwasiliana moja kwa moja na nje yatayotumika kwa kupokelea na kutoa milipuko na chumba cha kuhifadhia ambavo upatikanaji unaweza kutoka kwa ushawishi.

(f) Upatinaji wa kipima joto cha juu na chini lazima kitunzwe ndani ya chumba cha kuhifadhi milipuko na pindi joto litazidi centigrade 35 nyuzi (au 95 F) mmilliki au msimamizi atoe taarifa kwa mkaguzi wa migodi.

(g) angalau jozi moja ya viatu vya kujikinga milipuko yenye mpira feliti au solezenye kamba itatunzwa kwa ushawishi ya kila hifadhi ya mlipuko na hakuna mtu atakayeingia ndani ya chumba mlipuko isipokuwa awe amevaa viatu vya aina hiyo

STOO ZENYE LESENI.

7 Upekee wa jambo hili haukuwekwa bayana na sheria isipokuwa muundo na mahali mpango uliopo kwa kuzingatia uthibitisho wa mkaguzi wa milipuko ya eneo husika. Upekee unahitaji kutakaa milango , kufuli na bawaba ni sawa na kuhifadhia milipuko isipokuwa tu mlango mmoja ambao hauna pungufu ya kufuli mbili. Kufusi cha udongo, uzio sio lazima isipokuwa inaweza kuhitajika katika mazingira fulani na kamishina wa migodi. Baadhi ya stoo za awali zilikuwa na mteremko wa C.GI. au mabati ya aluminium na vyuma vilivoachana kwa chini. Mabati lazima yaunganishwe kikamilifu ili kuzuia zisitolewe kutokea nje na paa la mbao na vyuma vinene kwa usalama lazima vijengewe kwenye ukuta.

KUHIFADHI KWENYE MABOKSI/MASANDUKU

8. Kuhifadhi kwenye maboksi yaliyotengenzwa kwa mbao yatahakikishwa na mkaguzi wa milipuko ya eneo husika. Eneo linalohusu kuhifadhi maboksi lazima litambulikane na liwe salama, lakini maboksi yatajengewa sementi na kufungwa minyororo kwenye jengo na kukaa yamefungwa. Udongo na uzio zi lazima maboksi yaliyothibitishwa kujengwa kwa chuma aina ya chubbi ili yafungwe haraka kwa ajili ya kutumika kwa matarajio ya operesheni yanaweza kutunzwa kwenye jengo ambalo ni salama kidogo kwa kuzingatia kwamba imejengwa kwe zege au kufungia minyororo yasihamishwe na kitu chochote.

9. kila kihifadhi milipuko na stoo lazima vikaguliwe kwa nje angalau mara

moja ya robo na mkuu wa polisi wa wilaya au mkaguzi atakayeteuliwa na yeye. Eneo la kila mahali pa kutunza milipuko penye leseni na stoo katika kila kituo pataandikwa kwenye kitabu cha usimamizi wa majengo ya biashara, fomu ya polisi 214 kulingana na PGO N. 301. Kila atakapotembelea eneo la kuhifadhi milipuko au stoo ataandika kwenye kitabu /leja.

10. Afisa atakayejua mahali pa kuhifadhi milipuko au stoo ataangalia mambo yafuatayo:-

(a) Ardhi umbali wa yadi 40 kwa pande zote za jengo na patakuwa safi na wazi kutokuwepo na nyasi ndefu au mmea

(b) Kingo za ardhi na uzio vitakuwa katika hali nzuri iliyorekebishwa

(c) Mlango wa jengo utafungwa kwa kiwango cha mifungo ya aina mbili.

(d)Mabati ya paa yataunganishwa kutopitika.

Kwa suala la hifadhi ya milipuko, lango kwenye ulinzi wa uzio utakuwa umefungwa

Jengo kwa ujumla litakuwa katika hali nzuri iliyorekebishwa.

11. Kwa nyongeza makamanda wa mikoa wataandaa utaratibu wa ukaguzi wa ghafla utakaofuatwa kwenye leja na yaliyo kwenye hifadhi ya milipuko na maafisa ambao sio chini ya cheo cha Mratibu Msaidizi. Mratibu atajiridhisha kwa tahadhari ya usalama uliowekwa na kifungu 36 na 37 cha sheria ya milipuko sura ya 45 marekebisho ya sheria 2002 kabla ya kuingia eneo la kuhifadhi milipuko

12. Afisa mkaguzi mara moja anatatoa taarifa ya ukiukwaji wa sheria na uhalifu ya usalama wa jengo na ataandika uchunguzi wake katika leja ya usimamizi wa majengo ya biashara. Mkuu wa polisi wilaya atatoa taarifa kwa mkaguzi wa milipuko wa eneo husika kuhusu ukiukwaji wa sheria au uharibifu kuhusiana na usalama wa milipuko.

PGO - 298

MAJENGO MAALUMU – POMBE ZA KIENYEJI

1. Sheria ya Vileo, Namba. 77 R.E. 2002 inatumika nchi nzima ya Tanzania. (Angalia G.N. 372/62 ya tarehe 31.8.62)

2. Mamlaka ya kutoa leseni katika Mamlaka za mtaa husika. Halimashauri zote za Wilaya ni Mmlaka za kutoa vibali/leseni katika maeneo ya burudani na biashara. (Angalia G.N. 377/62)

3. Mkuu wa Polisi Wilaya wakati anashughulikia maombi yaliyopelekwa kwake na Mamlaka za leseni atazingatia vigezo vifuatavyo :-

   (a) Tabia ya muombaji.

   (b) Uwezo wa kifedha na mtazamo wa kijamii unaomuhusu muombaji.

   (c) Muonekano na hali ya eneo linalotakiwa kupewa leseni. Kama eneo limejitosheleza kwa vifaa kufikika.

Mkuu wa polisi wa wilaya baada ya kujiridhisha kuhusiana na vigezo vilivyoanishwa katika aya hii atawasilisha mapendekezo yake kwa maandishi kwenye Mamlaka ya Leseni.

4. Kila eneo la biashara za vileo lililo mjini katika himaya ya kituo cha polisi litaandika katika Rejista ya Ukaguzi wa Maeneo ya Burudani na Kibiashara (P.F 124), kwa mjibu wa Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi P.G.O. Namba. 301.

5. Mkuu wa kituo cha polisi atakagua maeneo yote ya biashara za vileo katika eneo la mjini mara moja kila wiki na zaidi ya hayo atahakikisha maeneo hayo yanafanyiwa doria ya mara kwa mara wakati wa masaa ya biahara. Baada ya ukaguzi mkuu wa kituo ataandika taarifa ya ukaguzi kwenye rejesta ya Ukaguzi wa maeneo ya burudani na Biashara.

6. Kila askari atahakikisha anailewa vyema Sheria Vileo, Cap. 77 R.E. 2002.

7. Kila afisa wa polisi ana mamlaka ya kuingia bila hati muda wowote mchana au usiku eneo lolote la burudani kwa mjibu wa Sheria ya Vileo au eneo lolote endapo atakuwa na sababu za msingi za

kushuku ulevi haramu au kamali vinafanyika ndani au uhuni au waharifu wameingia ndani (kifungu 27 (3) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Askari wasaidizi, Cap. 322 R.E. 2002.

PGO - 299

MAENEO YA BURUDANI NA BIASHARA

BOHARI YA SILAHA ZA BINAFSI

1. Mtu yeyote anayetaka kuwa na Bohari binafsi ya kutunza silaha na risasi Kifungu cha 16 cha Sheria ya Silaha na Risasi Cap 223 R.E. 2002 kinamtaka apate na kuwa na leseni.

Muundo wa Maombi ya Leseni

2. Maombi ya kupatiwa leseni kwa ajili ya Boharia binafsi ya silaha yanapopokelewa na Mkuu wa polisi Wilaya yatapelekwa kwa Kamanda wa polisi Mkoa pamoja na mapendekezo/maoni ya Mkuu wea polisi Wilaya na Mkuu wa Wilaya husika. Kamanda wa Polisi Mkoa atahitaji kujua tabia ya muombaji pamoja na kujua endapo eneo husika linafaa kujenga na kuweka Bohari ya silaha.

3. Kamanda wa Polisi wakati wa kuangalia kama eneo linafaa atazingatia yafuatayo :-

    (a) Kama jingo ni la kibiashara, paa ni imara na milango ni ya chuma.

    (b) Mahitaji ya Bohari katika eneo kwa kuzingatia :-

        (i) Idadi ya watu na silaha;

        (ii) Kama kuna bohari binafsi nyingine katika eneo hilo.

4. Baada ya kumaliza uchunguzi kama ilivyoainisha katika aya 2 Kamanda wa Polisi Mkoa atayapeleka maombi hayo kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai pamoja na ramani ya Bohari iliyopendekezwa hiyo (au mapendekezo ya mabadiliko ya jingo lililopo) na taarifa ambayo itakuwa na maelezo yafuatayo:-

    (a) Jina kamili la muombaji, aina ya biashara na mapendekezo kama biashara ya silaha na risasi inahitajika/inafaa.

    (b) Namna bohari inayotarajiwa kujengwa itakavyokuwa ikionesha ukubwa wake.

    (c) Ukubwa wa vitu au silaha na risasi za aina zote zinazotarajiwa kuhifadhiwa.

    (d) Maelekezo mhimu yaliyopendekezwa yakiwa

yameambatanishwa na leseni.

(e) Maelezo halisi ya eneo. Mfano ploti namba, block namba kwa ajili ya kutangaza katika Gazeti la serikali.

(f) Mapendekezo ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

Hatua za Mkurugenzi wa Upelelezi anapopokea maombi

5. Baada ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kupokea maombi na taarifa, kama inavyoonesha aya ya 4 ataomba idhini kwa IGP na kumshauri Kamanda wa Polisi kuhusu matokeo.

Hatua za Kamanda wa Polisi kama maombi yamepitishwa

6. Kamanda wa polisi, kama maombi yamepishwa atamtaarifu muombaji jinsi jingo litakavyojengwa au kubadilishwa jinsi itakavyokuwa kama ambavyo imeoneshwa kwenye maombi, leseni itakavyotolewa. Baada ya kukamilisha ujenzi na Kamanda wa polisi kuridhika muombaji atatakiwa ada ya leseni kwenye ofisi za idara ya Mapato/Hazina ndogo na kupeleka ERV kwa Kamnda wa polisi ambaye atamjulisha Mkurugenzi wa Upelelezi maelezo ya ERV. Mkurugenzi wa Upelelezi atafanya utaratibu ili suala hilo la Bohari binafsi litangazwe katika Gazeti la Serikali, kamanda wa polisi atampatia muombaji wa bohari binafsi leseni kwa fomu namba 1 kwenye jedwali la Kanuni za Silaha na Risasi.

7. Kamanda wa polisi atawajibika kumjulisha mkuu wa kituo kuhusu leseni hiyo mpya na mkuu wa kituo ataingiza maelezo ya leseni husika kwenye Rejista za Burudani na maeneo ya Kibiashara (PF. 214).

Kumbukumbu kutunzwa na bohari binafsi la silaha

8. Mtu ambaye anamiliki leseni ya bohari binafsi la silaha anatakiwa na kifungu 17 cha Sheria kutunza rejesta ya Maingizo na Matoleo kwenye fomu mahsusi iliyoainishwa. Kila ingizo katika rejesta hiyo itakuwa :-

(a) Inafanyika mara baada ya kuingiza au kutoa;

(b) Andikwa tarehe;

(c) Iwekewe namba zinazofuatana;

(d) Imejumuisha maelezo ya silaha na risasi jinsi zilivyotengezwa kwa kumbukumbu za namba na alama zilizopigwa mhuri na

kusajiliwa kwa mjibu wa sheria ya Silaha na Risasi;

(e) Imejumuishwa kumbukumbu ya kibali cha kinachoruhusu kuweka na kutoa;

(f) Isainiwe na mmiliki ikijumuisha maelezo mengine kama yalivyoelekezwa na sheria.

Kuweka

9. Kifungu 18 cha Sheria ya Silaha na Risasi inaelekeza kwamba risasi na silaha zitakuwekwa kwenye Bohari isipokuwa kwa ombi la maandishi kwenye fomu maalum na kwa mjibu wa kibali kilichosainiwa na Gazetted officer aliyepo makao makuu ya wilaya.

Kutoa

10. Kifungu cha 18 na 19 cha Sheria ya Silaha na Risasi Cap.223 R.E 2002 kinaelekeza kwamba :-

(a) Hakuna silaha au risasi itakayotolewa kwenye bohari binafsi isipokuwa kwa ombi la maandishi katika fomu maalum na kwa mjibu wa kibali kilichosainiwa na Senior Gazetted Office ambaye kwa wakati huo anapatikana makao makuu ya wilaya;

(b) Kibali kuchukua silaha na risasi kutoka kwenye bohari binafsi kitatolewa katika mazingira yafuatayo :-

(i) Endapo itatolewa kwa ajili nya kuuza au kuhamisha, ambapo kibali cha kuuza na kuhamisha na kibali cha silaha ya mnunuzi au Yule anayehamishiwa lazima zitolewe na muombaji ikizingatiwa kwamba manunuzi au uhamisho huo ni wa ni mlipuko kwa mamlaka za mtaa au caps kwenye mamlaka za mtaa au kwa mtu anayewakilisha mamlaka za mtaa, utoaji wa kibali hicho kwa kuuza au kuhamisha itakuwa imekamilika;

(ii) Kwa madhumuni ya kuuza nje ya nchi, kwa namna ambayo leseni na kibali kinatakiwa kutolewa;

(iii) Ka kuhamisha kutoka kwenye bohari moja kwenda nyingine au kwenda bohari ya Umma. Na

(iv) Kwa madhumuni ya maonyesho katika eneo hilo kama kibali kitakavyokuwa kimeonesha.

usimamizi

11. (a) Mkuu wa polisi wilaya atasimamia kwa kwa karibu bohari za silaha binafsi kawa mjibu wa aya 4 (g) of P.G.O. No. 301 vile vile atahakikisha kumbukumbu zinatunzwa vizuri kwa mjibu wa aya 8 ya Amri hii.

(b) Ukiukwaji wowote wa mashariti ya leseni lazima yatolewe taarifa kwa kamanda wa ploisi mkoa na mkuu wa polisi wilaya.

PGO - 300

MAJENGO MAALUMU YENYE LESENI ZA HUDUMA YA BURUDANI ZA KIBIASHARA

VITU VYA ZAMANI NA VYUMA CHAKAVU

1. Sheria ya Vyuma Chakavu ina wajibu wa kusimamia taratibu za kushulika na vyuma chakavu pamoja na vitu chakavu imewekwa ili kusaidia polisi kuthibiti wizi wa vitu hivyo.

maana

2. Kwa mjibu wa kifungu cha 2 cha sheria, vitu ambavyo vihusiana na sheria hii vinatafsiriwa ifuatavyo :-

   (a) “vyuma chakavu” vyuma vya zamani, vyuma chakavu chuma chochote kilichotengenezwa,vyuma vya zamani, lakini bila kujumlisha dhahabu, fedha au madini ya chuma yenye kundi la platinoid.

   (b) “vifaa ambavyo ni Second-hand goods” maana yake ni vitu chakavu amb avy Rais ametangaza kuwa chakavu katika kifungu namba 3 katika sheria hii ikiwa ni pamoja na component parts, spaces and accessories of any such Second-hand goods. Rais, kwa mjibu wa (Tangazo) Amri, 1957, ametangaza kuwa chakavu kwa mjibu wa sheria :-

      (i) Baiskeli na vifaa vya baiskeli

      (ii) Cherehani.

      (iii) Vipuri vya gari.

      (iv) Waya aina ya Non-ferrous.

      (v) Chuma aina ya ingots and metal type (printers).

      (vi) Locomotive and rolling stock spare parts.

      (vii) Brass taps.

      (viii) Mita za maji.

      (ix) Stop cocks.

      (x) Non-ferrous joints and unions.

(xi) Non-ferrous piping

3. Mtu yeyote anayetaka kufanya biashara ya vyuma chakavu kifungu namba 4 kinamtaka kupata leseni.

4. Leseni zinazotolewa kwa sheria hii ni aina mbili :-

(a) Leseni Kuu inayotolewa na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, kupitia Tangazo la Serikali 540/57; na

(b) Leseni ya Mtaa inayotolewa na Mkuu wa Wilaya kwa wilaya ambayo muombaji anaishi.

Muundo wa maombi ya leseni

5., Maombi ya kupata au kuhuisha- renewal kwa leseni kuu au ya serikali za mtaaitawekwa kwa PF. 121, kwa toleo mbili - in duplicate, katika ofisi za uhasibu. Malipo stahiki yataambatanishwa kwenye maombi.

6. Baada ya kupokea maombi, PF. 121na ada, Hazina watakamilisha sehemu 1 ya pf 119 au PF 120, inategemea aina ya leseni inayohitajika, na aina ya maombi :-

(a) Leseni kuu – itapelekwa nakala ya PF. 121 na PF.121 na PF. 119 kwa mkuu wa polisi wilaya ambapo maombi yanaonesha kushughulikia biashara ya vyuma chakavu; au

(b) Leseni ya serikali za mtaa – itapelekwa nakala ya PF. 121 na PF. 120 kwa mkuu wa wilaya.

Leseni kuu

7. (a) Mkuu wa polisi wilaya baada ya kupokea PF. 121 na PF. 119kutoka Hazina, kama ilivyoainishwa kwenye ibara ya 6 (a) juu, atachuguza tabia ya muombaji na na kama eneo la biashara linafaa kwa matumizi na kutoa taarifa kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa kwa mjibu wa pro forma iliyoainishwa kwenye Jedwali “A”.

(b) Endapo ni kuhuisha, itatosha endapo mkuu wa polisi wilaya ataandika “imependekezwa” ikizingatiwa kwamba mmiliki wa leseni anaendelea na biashara kwa kipindi cha

mwaka. Maombi na leseni vitapelekwa kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa.

8. Mkuu wa Upelelezi Mkoa, baada ya kupokea nyaraka zilizoainishwa kwenye ibara ya 7 (a) na (b), baada ya kuangalia historia ya muombaji, atapeleka nyaraka husika kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya jinai kwa hatua zaidi.

9. Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai atashughulikia kila maombi na atatoa leseni kwa muombaji kwa mjibu wa Sheria ya Vyuma Chakavuya mwaka 1957. Atatunza pia kumbukumbu ya leseni zilizotolewa. Leseni zitatumwa kwa Mkuu wa upelelezi Mkoa kwa kuziwasilisha kwa muombaji leseni.

10. Mkuu wa Upelelezi Mkoa atawajibika kumtaarifu mkuu wa kituo kuhusiana na leseni mpya zinazotolewa na mkuu wa kituo ataingiza taarifa za leseni hiyo kwenye rejesta ya leseni za maeneo maalum PF. 214.

Leseni za zinazotolewa na serikalim za Mitaa

11. Mkuu wa polisi wilaya mara baada ya kupokea PF. 121 kutoka kwa Mkuu wa Wilaya, atafanyia uchunguzi maombi hayo na kuwasilisha taarifa fupi kwa maelezo yaliyoainishwa kwenye Jedwali “A”.

Kumbukumbu kuhifadhiwa na mmiliki wa leseni

12. Kila mmiliki wa leseni anatakiwa kwa mjibu wa kifungu13 cha sheria kutunza kumbukumbu kwenye fomu maalum na kwa ufasaha atafanya maingizo kwa kiingereza na Kiswahili ndani ya masaa 24 ya manunuzi na mauzo kwa maelezo yafuatayo :-

    (a) Akaunti ya vyuma vyote chakavu au mali za zamani anazozimiliki. Akaunti hiyo itaonesha :-

        (i) Jina la mtu aliyenunua, hitaji au pokea bidhaa.

        (ii) Tarehe na saa ya ya nmauzo;

        (iii) the consideration (fedha au kitu) kwa mauzo;

        (iv) Jina anuani, na kazi/shughuli za mtu ambaye bidhaa imepatikana.

    (b) Akaunti ya vyuma chakavu vinavyouzwa au kutolewa au

kuachilia umiliki, akaunti hiyo itaonesha :-

(i) Tarehe na muda wa tukio;

(ii) Jina, anuani na kazi ya mnunuzi, au mmiliki wa bidhaa.

(iii) Mmilikik wa leseni atatakiwa kila tukio litasainiwa na kuweka dule gumba.

makatazo

13. Chini ya kifungu 15 cha Sheria kinazuia mhusika wa vyuma na vitu chakavu asifanye majukumu :-

(a) Isipokuwa kati ya saa mbili asubuhi na saa kumi jioni;

(b) Endapo ana umri chini ya miaka 16;

(c) Mtu ambaye atashindwa kujitambulisha vyema na uhalali wa kununua bidhaa;

(d) Katika maeneo ambayo hayajaainishwa kwenye leseni

(e) Ikizingatiwa kwamba hakutakuwa na ununuzi au uchukuaji wa vyuma chakavu unaozidi uzito wa 200 lb.

Marufuku ya kuondoa alama ya utambulisho

14. Hairuhusiwi kwa mmiliki kubadilisha kwa namna Fulani muundo, namba za utambulishoau alama za utambulishokwenye vyuma chakavu au vitu chakavusiku kumi na tano baada ya kumiliki chuma hicho ckavu isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi ya afisa wa polisi mwenye cheo kisichopungua mrakibu msaidizi wa polisi.

Usimamizi wa leseni

15. (a) Mkuu wa polisi wa wilaya maeneo yote yanayojihusisha na vyuma chakavukwa mjibu wa ibara 4 (d) of P.G.O. No. 301na atahakikisha kumbukumbu zinahifadhiwa kwa mjibu wa ibara 12 ya amri hii.

(b) Ukiukwaji wowote wa leseni lazima utolewe taarifa kwa Mkurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai na mkuu wa polisi wilaya.

Kununua na kuuza vyuma chakavu nje ya nchi

16. Mkuu wa polisi wilaya, ikizingatiwa kuwa si chini ya cheo cha Mrakibu Msaidizi wa Polisi, anaweza kutoa baada ya kuombwa, “Cheti cha Kisheria Cha Umiliki”, PF. 122, kwa mmiliki wa leseni kuu anayetaka kusafirisha au kutoa vyuma chakavu nje ya nchi. Uangalifu utachukuliwa kuhakikisha kwamba vyuma chakavu ambavyo vinavyohusika vinamilikiwa kihalali na mwenye leseni.

KIAMBATANISHO “A”

(To. P.G.O. No. 300)

(a) Nini mchanganuo wa maeneo ambao biashara zinatakiwa kufanyika? Je ni eneo la nyuma ya duka la muombaji lina vyumba vingapi?

(b) Je eneo ni la makazi?

(c) Eneo lina hali gani, je ni la kibiashara au la viwanda?

(d) Je ni muombaji anamiliki bohali la kuhifadhia vyuma chakavu?

(e) Je ni yadi au ni store ya kuhifadhia vyuma kama ni kweli nini ukubwa wa eneo?

(f) Je vyuma ni tegemeo la muombaji au ndiyo chanzo chake cha kipato?

(g) Je kuna bidhaa nyingine zinahifadhiwa katika eneo hilo ambalo linategemea kuhifadhi vyuma chakavu?

(h) Je ana tabia gani amewahi kuhumiwa siku za nyuma?

(i) Kadiria mtaji wake, anaweza kutoa taarifa za kibenki?

PGO - 301

MAJENGO MAALUM YENYE LESENI ZA BURUDANI ZA KIBIASHARA

USIMAMIZI WA

1. Mkuu wa polisi wa wilaya anawajibika kukagua kwenye maeneo maalum ya huduma za kibiashara yafuatayo :-

   (a) Hoteli, nyumba ya wageni na sehemu ya mgahawa

   (b) Maeneo ya pombe za kienyeji

   (c) sinema.

   (d) Vyuma chakavu second-hand na wauza baiskeli.

   (e) Pawnbrokers.

   (f) Vifaa vya milipuko.

   (g) Bohari binafsi za kuhifadhia silaha.

2. Kila mkuu wa kituo mwenye maeneo ya burudani za kibiashara atakuwa na jalada linalotunza taarifa za ukaguzi maeneo ya burudani (PF. 214) ambapo atandika taarifa za ukaguzi wa maeneo husika. Ukurasa wa kwanza (Fomu PF. 214) kila jalada litatumika kwa kila aina moja ya eneo.

3. Maeneo yaliyoorozeshwa kwenye jalada yatakuwa yanakaguliwa na ofisa aliyeidhinishwa kufanya ukaguzi angalau mara moja kwa mwezi, isipokuwa kama ilivyoelezwa chini.mkaguzi atatoa taarifa kwa mkuu wake jambo lolote linalohisiwa kuwa ni uvunjifu wa sheria analokuwa amegundua kipindi cha ukaguzi.

4. Wakaguzi wanawajibu wa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

   (a) Hoteli, nyumba za wageni na sehemu ya mgahawa

   Kifungu 60 (1) cha Sheria ya Vileo, Cap. 77 R.E. 2002 kinampa mamlaka askali polisi yeyote kukagua eneo lolote linalouza pombe. Mkaguzi atakagua kama kuna waharifu, wanaotafutwa na polisi,Malaya nkna kuandika taarifa ya jambo lolote la uvunjifu wa sheria.

   (b) Eneo la pombe za kienyeji

Chini ya Sheria ya Vileo askari polisi yeyote nyumba zinazouza pombe za kienyeji. Afisa huyo atatoa taarifa za walevi, rowdyism, au hali yeyote ambayo inaashiria mkutano wa kiharifu wa watiliwa mashaka. (angalia P.G.O. No. 298).

(c) Sinema

Cap. 230 Kifungu 15, inawapatia nguvu askari polisi wote kukagua sinema, mkaguzi atahakikisha kwamba vifaa vya kuzima moto. nk vinafanya kazi hakuna msongamano wa watu na njia za kuingia na kutoka zipo wazi. (angalia pia P.G.O. No. 296).

(d) Vyuma chakavu, second –hand na wafanyabiashara ya baiskeli

Kifungu 18 (1) ya Cap. 345 inampa mamlaka afisa wa polisi wa cheo la Mrakibu Msaidizi wa Polisi au zaidi kukagua maeneo hayo. Mkaguzi ataangalia orodha ya mali zilizoibiwa na vitu vilivyopo na kwenye kitabu cha mauzo kujiridhisha kama mali za wizi zimepitia kwenye mikono yao. (angalia pia P.G.O. No. 300).

(e) Vifaa vya milipuko – Quarterly

kifungu 55 of Cap. 224 kinampa mamlaka afisa wa polisi wa cheo cha mkaguzi wa polisi na zaidi kukagua maeneo haya. Mkaguzi atakagua idadi ya milipuko akilinganisha na rejesta ya milipuko au taarifa yeyote ya mapungufu na usalama wa jengo na kutoa taarifa za namna ya matengenezo (angalia pia P.G.O.297).

(f) Bohari ya silaha binafsi – Quarterly

Kwa mjibu wa Sheria ya Silaha na Risasi hakuna haki ya kuingia bila Hati.kifungu 16 afisa wa leseni (mrakibu yeyote wa polisi au afisa Tawala) ana haki na mamlaka ya kuingia. Atakagua silaha ziliyoko ndani ya bohari akilinganisha na zilizoandikwa kwenye rejesta ya kuingiza na kutoa na kutoa taarifa ya mapungufu. Jingo lazima lipimwe usalama wake na kutoa taarifa za mapungufu. (angalia pia P.G.O. No. 299).

5. Majukumu ya afisa mkaguzi kama yalivyoainishwa kwenye aya 4

juuyamefafanuliwa na Amri nyingine. Kamanda wa polisi mkoa kwa nyongeza atatoa Amri hizo kama atakavyoona inafaa kwa ajili ya ukaguzi maeneo ya leseni za burudani na biashara katika mikoa yao.

PGO - 302
DORIA

VIJIJINI

General

1. Kila kituo cha polisi kina wajibu wa ulinzi na usalama wa sehemu ya nchi. Kitatimiza wajibu huu kwa kufanya doria za mara kwa mara ambazo zitapitia kila kijiji na maeneo ya watu na kuimalisha mawasiliano na watu. Kamanda wa polisi mkoa atahakikisha kuwa kila kituo cha polisi kitaonesha jedwali lenye ratiba doria (na kuambatanisha kwenye amri za kudumu za kituo) ambayo itatakiwa kufuatwa bila kukosa. Doria hii itafuata mfumo wa ulinzi katika maeneo ya ulinzi.

2. Aya zifuatazo inaonesha muundo wa doria ambao unatakiwa kufuatwa na vituo vyote.

   (a) Doria ya masaa sita kwenye maeneo ya watu karibu na kituo cha polisi;

   (b) Doria ya masafa marefu nay a kati ya siku moja au siku nyingi.

3. Doria za ziada zinatakiwa kufanya kwa kituo chenye eneo kubwa lenye msongamano.

4. Mpango kazi wa doria utaandaliwa kama ifuatavyo :-

   (a) Ramani itatolewa kwa kila kikundi cha doria pamoja na alama za njia yake.

   (b) Maelekezo ya kina yatatolewa, kuonesha muda, eneo watakalosimama, kitabu cha ukaguzi nakadhalika. Itachapwa kwa Kiswahili na kiingereza. Muda utakaotumika kutoka kijiji kimoja kwenda kingine kwa doria itakuwa ni masaa sita ikiwezekana kwa doria za masafa marefu pia.

   (c) Namba zitapangwa kwa kila doria.

5. Jedwali la doria itakayotengenezwa itakuwa na muundo ufuatao:-

   (a) Doria ya masaa sita

Doria namba 1 – kipindi– masaa 6.

x-masaa	Kuondoka kituoni.
x + ½ saa	Kufika kijiji “A” alama kitabu cha ukaguzi.
x + 2 masaa	Kufika kijiji “B”
x + 3 masaa	Kufika makao makuu serikali za mtaa. “C”. Alama kitabu cha ukaguzi kupumzika dakika 30.
x +4 ½ masaa	Kufika kijiji “D”
x + 5 masaa	Kufika kijiji “E”
x + 6 masaa	Kurudi kituoni.
(b) doria ya masafa marefu	
Doria namba. 3 muda siku tatu	
x-masaa	Kuondoka kituoni.
Siku ya kwanza	Kutembelea kijiji “A”; kijiji “B”, kijiji “C” na kulala kijiji “C”
Siku ya pili	Kutembelea misheni “A”, Misheni “B”, Misheni “C” na kulala Misheni “C”.
Siku ya tatu	Kutembelea kijiji “X”, kijiji “Y” na kijiji “Z” na kulala kijiji “Z”.
Siku ya nne	Kurudi .

ZINGATIA: A “Kitabu cha Visiting ” (PF. 187 – kiwango kidogo) kitatunzwa katika kituo kikuu cha doria (P.G.O. No. 303 yahusika)

6. Kitabu au jalada au mchanganuo wa doria pamoja na maelekezo ya njia na ramani ya kila doria vitanzwa kwenye chumba cha mashtaka ya vituo vyote vya polisi. Nakala itaandaliwa na kupatiwa wakuu wa vikundi vya doria.

Taratibu za kila siku za doria

7. Doria za mara kwa mara zitafanyika katika maeneo yenye msongamano wa watu kwa mjibu wa jedwali la doria linalooneshwa kwenye aya ya 1. Doria ya masafa marefu itahusisha askari angalau wawili. Doria fupi za masaa sita zitafanyika karibu na kituo cha polisi itafanya kama shughuli za beat.ukaguzi utafanyika kwenye vijiji, serikali za mitaa na eneo la mashamba na njia za doria.

8. Mamlaka za serikali za mitaa zitakuwa zinaulizwa,uangalifu utafanywa kwa wagonjwa mahututi na kuomba msaada wa serikali. Msaada unaowezekana utafanywa na polisi waliopo doria au mkuu wa kituo anapopokea taarifa.

9. Kila askali aliyeko doria atasimamiwa na mkuu wao ambaye atakuwa ameteuliwa mkuu wa polisi wilaya au mkuu wa kituo cha polisi kabla doria haijaondoka. Kama kwa sababu maalum mkuu wa doria hajateuliwa mwenye namba kubwa miongoni ndiye ataongoza kikundi. Mkuu wa kikundi cha doria ndiye atakayewajibika kwa matendo, nidhamu na tabia njema za askari walioko chini yake.

10. (a) Doria itafanyika kwa silaha kam mazingira yataruhusu, kwwa mfano eneo la michezo au eneo la kupitishia mifugo, mkuu wa kituo ataongeza maelekezo ya kuchukua bunduki na risasi, katika mazingira hayo askali watachukua silaha. Bunduki hazitakuwa na risasi isipokuwa dharura itatokea.

    (b) Kila askari anawajibika binafsi kwa silaha anayokuwa amechukua wakati wa doria.

    Silaha haitaachwa kulindwa. Kwenye vituo vya ulinzi wa usiku kila askari atalala akiwa na silaha pembeni yake.

11. Mavazi rasmi ya doria yatatumika, kwa mjibu wa PGO. Mavazi ya kiraia au viatu wakati wa doria hayaruhusiwi.

12. Askari wote wawapo doria watachukua tahadhali za kiafya na kam marelia ni tatizo mkuu wa polisi wilaya au kituo atahakikisha kuwa vidonge vimechukuliwa kwa mjibu wa kiwango cha matumizi ya kitabibu.

13. Askali polisi wanapokuwa doria hawaruhusiwi, katika mazingira yeyote kupatiwa chakula na takirima kutoka kwa wananchi. Chakula kitanunuliwa au kuchukuliwa kama inavyotakiwa. Kama ni lazima kwa usafiri wa jumla, feri, au meri malipo yatafanyika haraka.

Watarejeshewa na mkuu wa polisi wilaya ikizingatiwa kwamba taarifa kamili zimetolewa na zikithibitishwa na nyaraka za ushahidi wa malipo.

14. Kabla ya askari kuondoka mkuu wa polisi wilaya au kituo atatelekeza yafuatayo:-

    (a) Atateua mkuu wa msafara ambaye atakuwa anaongoza kikundi na kutoa maelekezo kama inavyooneshwa kwenye PF 62 itakayobaki kwenye kitabu cha doria. Kitabu kitachukuliwa na mkuu wa kikundi kikiwa kimejaladiwa lazima kitunzwe katika hali ya usafi na kifanyiwe matengenezo.

    (b) Elezea sababu za kwenda doria na kuhakikisha kuwa wote wanajua muda, njia na madhumuni ya doria.

    (c) Kagua bunduki na dhana nyingine;

    (d) Andika muda wa kuondoka na kurudi kwenye station diary.

15. Kila mkuu wa kikundi cha doria atatakiwa :-

    (a) Kikundi cha doria kinafuata njia kilichopangiwa;

    (b) Tarehe na muda wa kufika na kuondoka kwa kila kijiji, serikali za mitaa, nakadhalika. Inaingizwa katika eneo linalotakiwa kwenye amri ya doria, ikiungwa mkono na saini ya viongozi wa mitaa.;

    (c) Kila kitu muhim kinaandikwa kwenye notebook; uangalifu utafanywa kwenye kutoa msaada kwa wagonjwa nakadhalika.

16. Hali ya kila kikundi cha doria, mkuu wa kikundi atamaliza kwa kuandika taarifa na kuiwasilisha kwa mkuu wa kituo ambaye ataandika hatua zilizochukuliwa, kama inawezekana kufidia mapungufu au malalamiko yalioneshwa kwenye taarifa. Mkuu wa kituo vilevile atachukua taarifa iliyopo kwenye kitabu cha doria na kuhifadhi kwenye jalada maalumu. Taarifa hizo zitakaguliwa nma mkuu wa polisi wilaya na maafisa wengine wakati wa ukaguzi kituoni. Taarifa mhimu zitatolewa mara moja kwa afisa tawala wa wilaya na makao makuu ya mkoa.

17. Ukaguzi wa mara kwa mara utafanyika. Maofisa wakuu na NCOS watakapokuwa wanakagua doria na kuchukua hatua ya kusubili

kwenye eneo la doria mpaka doria itakapofika eneo hilohii itafanyika kwa doria za muda mfupi.

18. Doria lazima zitofautiane na na askali hatakiwi kupangwa eneo moja mara kwa mara. Ratiba lazima itofautiane kama ikilazimika.

.

PGO - 303
DORIA NA UKAGUZI KWA MAOFISA WAKUU

1. Wakuu wa polisi wilaya na maofisa na wakaguzi wa GD watapitia maeneo ambayo yapo kwenye himaya yao . ikizingatiwa ukaguzi wa kawaida kama ulivyoainishwa katika PGO namba 47 mchanganuo ufuatao utazingatiwa:-

   (a) Makao makuu wa wilaya yatakaguliwa kila baada ya masaa 24. Kuanzia saa 01.00 na 05.00 kila wiki.

   (b) Vituo vingine vilivyo katika wilaya vitakaguliwa mara kwa mara ikiwekana mara moja kwa mwezi labda kama kutakuwa na maelekezo ya C.O. ukaguzi huu utafanyika kati ya saa 22.00 na 05.00 hrs.

2. Maofisa hao watafanya doria ya miguu mara mbili kwa wiki kwa maeneo ya mjini. Watakuwa wanakagua askari wa lindo na walioko doria.

3. Ofisa anapokagua kituo ataangalia vitabu, mahabusu, viwanja na kambinikuhakikisha kuwa kila kitu ni kisafi. Kila kitu chenye umhimu kitaandikwa katika kitabu cha ukaguzi (PF. 187) na kuelezea kwa mkuu wa kituo au ofisa yeyote aliyepo.

4. Kila ukaguzi utaandikwa kwenye kitabu cha ukaguzi (PF. 187) kitakachokuwa kwenye chumba cha mashtaka na chumba cha askari wa kutuliza ghasia na eneo ambalo askari wanafanya kazi za kudumu. Mfano Ikulu, ofisi za serikali nakadhalika.kitabu cha ukaguzi kitawekwa kwenye eneo ambalo kuna ukaguzi wa mara kwa mara usiku na maafisa na wakaguzi kati ya saa 22.00 na 06.00 hrs itaadikwa kwa wino mwekundu.

5. Kamanda wa polisi anao wajibu wa kuhakikisha kuwa maofisa na wakaguzi wa polisi wakifanya doria ya miguu ya masafa marefu, na ikiwezekana kwenye makampuni kuwawezesha kufika kufika maeneo ya watu kwenye wilaya zao wakati huohuo wakijifunza jiografia ya wilaya zao.

6. Sare za kijeshi zitavaliwa kwenye doria isipokuwa ukaguzi unaofanywa na gazetedi ofisa anaweza kuwa kiraia baada ya saa 22.00 usiku.

7. Taarifa za kila ukaguzi na doria zitaandikwa kwenye diary ya ofisa.

Doria itaoneshwa kama ni za miguu na radio nakadhalika.

8. Hutaondoka kufanya ukaguzi na doria isipokuwa :-

(a) Kama ofisa anatalii;

(b) Anapokuwa anashughulikia kazi za dharura, au kazi za kimahakama;

(c) Kwa ruhusa ya kamanda wa polisi mkoa. Shinikizo la kiutendaji halitakuwa kigezo cha kutokutimiza wajibu wa amri hii.

Maofisa wa kikosi cha kutuliza Ghasia

9. Kamanda wa kikosi cha kutuliza ghasia pamoja na watakagua kambi yao ikiwezekan na mara moja kwa wikikati ya saa 01.00 na 05.00 na kuona kama kazi zinafanyika ipasavyo. Ukaguzi wa mara kwa mara utafanyika katika muda wowote.

Kikosi cha Intelijensiama maofisa wa C.I.D

10. maofisa wa intelijemsia na CID wanapokagua kituo kwa uchunguzi, au kwa madhumuni mengine, wataandika kwenye kitabu cha cha ukaguzi cha maofisa.

Mkuu wa kituo

11. Kila mkuu wa kituo atakwenda doria kila siku angalau saa moja katika maeneo ya biashara na makazi kkaribu na kituo chake. Atafanya doria mara mbili kwa wiki kati ya saa 20.00 na 01.00 na kati ya saa 01.00 na 05.00

12. Atafanya doria kwenye maeneo yake na kumfan ya afamike kwa wakazi wa eneo lake.

13. Atavaa sare za polisi muda wote awapo doria.kituo daraja C ataongozana na askari kufanya doria ya mbali angalau mara mbili kwa mwezi.

14. Vilevile, mkuu wa kituo daraja C ataongozana na askari kufanya doria ya mbali angalau mara mbili kwa mwezi.

PGO - 304

MALI ZA KUOKOTA

1. Kila Afis wa Polisi, aidha akiwa kazini au hauypo kazini, lazima awajibike na mali zote zinazoamishika za kuokota ambazo amekabidhiwa kwake (na watu wengine) au zilizookotwa na yeye. Iwapo atakabidhiwa kwake,ni lazima apate majina kamili na anwani ya aliyeokota na kuingiza taarifazote za mali katika kitabu cake wakati akiwepo aliyeokota ambye ataweka sahihi au ataweka dole gumba katika maandishi. Maelezo ye fedha yoyote au vitu vya thamani avichukulie kwa uangalifu. Ali hiyo lazima ikabidhiwe kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi kilichopo karibu.

2. Wakuu wa Vituo wao binafsi watawajibika kupokea na kuhifadhi katika sehemu ya usalama kwa kila bidhaa iliyookotwa au haina mwenyewe ambayo wamekabidhwa katika vituo vyao.

3. Maelezo kamili ya bidhaa iliyopatikana au iliyookotwa na kuletwa kituoni lazima taarifa ziandikwe kwenye kitabu cha mali za kuokotwa(PF.53) na kuondolewa kulingana na utaratibu uliopo.

4. Mali ya kuokota au isiyolalamikiwa iliyokabidhiwa katika Kituo cha Polisi na raia mwema au askari yoyote lazima ipokelewe na Mkuu wa Kituo, kama hayupo askari yeyote wa chumba cha mashtaka atapokea na;

   (a) Ataingiza maelezo mafupi katika kitabu cha matukio atakadiria thamana ya mali hiyo, na ataingiza tena taarifa fupi katika kitabu cha mali ya kuokota au isiyolalamikiwa.

   (b) Toa risiti kwa mtu yoyote au Polisi aliyeokota mali ya kuokota au isiyolalamikiwa na ingiza namba ya risiti katika kicha cha namba 2 katika daftari.

(c) Weka alama ya vifaa, katika PF.57 katika mtiririko wa vifaa au mali lazima kuingiza mtiririko wa namba katika mali ulizookota zilizoko stoo.

(d) Hifadhi mali yote ya thamani ktika bahasha (PF.166) na kufungia katka sanduku ililopo kituoni.

(e) Lazima ulipe fedha yoyote ambayo imepatikana kwa Afisa wa mapato aliyekaribu/au muhasibu ERV kwa ajili ya mikopo amana ya 'mali ya kuokota/isiyolalamikiwa katika mfuko 428/03' na pata ERV na uiweke kwa ajili ya usalama kwenye jalada kwenye mtiririko namba 9 ya daftari.

(f) Kuandaa mara moja katika rejesta ya mali yakuokota (PF.12) ya mali yoyote iliyoharibika au mali nyhingine, na hapo lazima mauzo yafanyike haraka ambayo itakuwa manufaa kwa mmliki kupitia kwa hakimu kwa kuadika mapendekezo ya mauzo ya mali hiyo. Mara nakala hiyo itakayorudi toka kwa hakimu na mara baada ya kuuza nakala nyingin ya mauzo lazima urudishe kwa hakimu na lazima iuzwe kwa dalali kama inawezekana na mwenendo wa malipo hayo yapitie kwa dalali wa zamani kama inawezekana na malipo hayo yalipwe kwa Afisa wa mapato/muhasibu kwa malipo ya mali isiyolalamikiwa katika amana kuu 428/03 ERV lazima itolewe na lazima kitunze katika usalamana ERV hiyo lazima uiandike mauzo hayo na uingize katika daftari na orodha namba 9 ya daftari.

Taarifa lazima itolewe kwa maandishi mali iliyo na thamani ya Tsh.50,000/= na ambapo mali ambayo ni silaha au risasi lazima iripotie kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai kupitia kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa na Mkuu wa Polisi waw Wilaya ndani ya miezi 6.

mamlaka ya kupokonya silaha atarishi

26. Afisa au mtu mwingine aliyefanya anaweza kupokonya silaha hatari kutoka kwa mtu aliye kamatwa ambazo zipo maungoni kwake, na atavitoa vitu hivyo Mahakamani, au Ofisi ambayo Afisa aliyekamata anatakiwa na sheria kumpeleka mtu huyo aliyekamatwa".

2. Vitu vyote vitakavyo kusanywa na afisa mkamataji toka kwa Mahabusi kabla ya kufikishwa kituoni vitakabidhiwa haraka iwezakanavyo kwa afisa aliyeko zamu chumba cha Mashtaka.

3. Kila afisa wa Polisi aliyekabidhi mali ya Mahabusu kulingana na aya ya pili, atamtaka afisa wa chumba cha mashataka kuthibitisha mapema chini ya orodha ya vitu hivyo katika kitabu chake cha kumbukumbu kwamba kila kitu kimekabidhiwa kwa usahihi. DOKEZO: Afisa ambaye amechukua vitun hivyo wakati anakamata mahabusu anahitajika kwa mujibu wa aya 6 (6) ya PGO no 272 kuorodhesha vitu hivyo katika vitabu vyao vya kumbukumbu.

4. Kila mshtakiwa ambaye anatakiwa kuwekwa mahabusu atapekuliwa kikamilifu mapema mara afikishwapo kituoni na mali alizokutwa nazo zionyeshwe. Afisa aliyeko zamu chumba cha mashitaka anawajibika kuona kwamba upekuzi huu umefanyika vizuri na kila kitu kimechukuliwa kutoka kwa mshtakiwa. Kila inapowezekana afisa mkamati ndiye afanye kazi hiyo ya upekuzi huo.

5. Washitakiwa watapekuliwa katika chumba cha Mashtaka. Washtakiwa wa kike watapekuliwa na Askari wa Kike au wanawake mwenzake sehemu ya faragha na kuzingatiz utu wake’

6. (a) Afisa wa Polisi ambaye atapekuwa mshtakiwa katika chumba cha mastaka atachukua kila kitu isipokuwa nguo alizovaa pamoja na mkanda, tai, sindilia viatu kamba viatu au vitu vingine vya aina ya nguo ambavyo anaweza kutumia kujiuwa kwa kujinyonga, vitu hivyo pia vitakabidhiwa kwa afisa aliyeko zamu chumba cha mashitaka.

(b) Afisa aliyeko zamu chumba cha mashtaka atakagua mali za mshatakiwa mbele yake na mbele ya afisa mkamataji. Na kila kitu kitaingizwa kwa kalamu au Penseli katika kitabu cha stakabadhi ya mali ya washtakiwa katika nakala mbili (PF 63). Atasaini nakara zote mbili na kumtaka afisa mmoja wa Polisi kuwa shahidi hati halisi ya stakabadhi ya mali ya mshtakiwa atakabidhiwa mshitakiwa na nakara itabaki katika kitabu cha stakabadhi,

(c) Kama mshitakiwa hajui kingereza maelezo ya vitu vilivyochukuliwa vitaandikwa kwa Kiswahili. Atasomewa na kuelezwa mbele ya afisa alikuwa shahidi.

(d) Endapo mshitakiwa hana malizozote zaidi ya hizo alizoruhisiwa kuwa nazo stakabadhi itatolewa kwake ikiwa imeandikwa hakuna, sahihi ya shahidi ni muhimu katika risiti za mali ya mshitakiwa.

(e) Mali zote ambazo zimechukuliwa kutoka kwa mshitakiwa zitafungwa pamoja na kuwa kewa lebo ya stakabadhi ya mali mshitakiwa (PF 167) Ikionyesha namba ya stakabadhi na jina la mshitakiwa na vitu hivyo vitahifadhiwa sehemu ambayo ni salama vilivyo kila fedha taslimu au vitu vya dhamani vilivyo chukuliwa kutoka kwa mshitakiwa vitawekwa kwenye bahasha ya mali za thamani (PF 166) na kukabidhiwa kwa mkuu wa kituo kwa hifadhi salama katika kasiki au sanduku la.

(f) Vitu kutoka mali ya mshitakiwa ambavyo vitahijika kama kielelezo katika kesi pia vitaingizwa kwenye rejesita ya vielelezo na maingizo hayo yaonyeshe kwenye nakara zote za sitakabadhi.

7. Wakati mshitakiwa atakapoondoka kwenye ulinzi wa Polisi kwa kuhukumiwa au kupelekwa rumande au kuachiwa mali zake isipokuwa zile ambazo zinaitajika (kama kielelezo kama ilivyo aya 6 (f)) atarudishiwa na kukiri upokeaji kwa kusaini kwenye stakabadhi au kuweka dore gumba ya nakara ya stakabadhi iliyopo kwenye kitabu cha stakabadhi chini ya maofisa wawili wa Polisi ambao pia watasaini nakara ya stakabadhi kama mashaidi kuwa mali hizo zimekabidhiwa kwa usasahihi. Stakabadhi halisi zitachukuliwa kutoka kwa mshitakiwa na kuambatanishwa na nakala ya stakabadhi iliyopo kwenye kitabu .

8. Afisa aliyeko zamuni chumba cha mashitaka anawajibika kwa usalama wa mali za washitakiwa waliopo kituoni. Mwisho wa zamu yake atakabidhi ulinzi wa mali zote za washitakiwa kwa anayepokea zamu ambaye atakagua mali hizo kwa kulinganisha na nakala za stakabadhi za mali za washitakiwa na kuingiza kwenye kitabu cha kituo cha kumbukumbu, kama mali hizo zitakuwa sahihi. Afisa anayepokea zamu kama kutakuwepo na mapungufu atatoa taarifa afisa wa juu katika kituo na hatakubali kulinda mali hizo bila kupata maelezo zaidi.

9. Afisa wa Polisi wa ngazi ya juu katika kituo baada ya kupokea taarifa za

mapungufu ya mali za washitakiwa ata:-

a) Ataandika taarifa kwenye kitabu cha kutolea taarifa.

b) Atafungua jalada la kesi.

c) Ataanzisha mara moja upelelezi kuhusiana na taarifa hiyo na

d) Atamjurisha mkuu wa Polisi wa wilaya.

e) PGO 402

f) VYAMA VYA SIASA - kampeni za uchaguzi

g) Maadili ya jumla wakati wa kampeni
1. Wakuu wa Polisi wa Wilaya wanakumbushwa kwamba tamko la kipindi cha kampeni za uchaguzi chini ya sheria, bila ya uhakika zaidi, kuanzisha kibali kwa ajili ya wagombea na vyama vya siasa kudhamini wagombea vile kuitisha mikutano ya hadhara na kushughulikia kwa madhumuni ya kuendeleza uchaguzi mgombea au jambo lolote umma au mlango kwa kufanya kampeni ya mlango.
2. Mkuu wa Polisi wa Wilaya ni wajibu amefungwa kuhakikisha kuwa vyama vyote vya siasa na wagombea kufurahia haki sawa kuhusiana na kampeni za uchaguzi. Mikutano ya kampeni, maandamano au kampeni za uchaguzi nyingine ya wapinzani haiwezi kuvurugika au kuwekewa pingamizi na chama kingine.
3. Haki ya kila mtu binafsi kwa ajili ya maisha ya amani na salama nyumbani vitaheshimiwa, hata hivyo, vyama vya siasa au wagombea wake wanaweza kuwasilisha maoni ya kisiasa au shughuli. Maandalizi ya maandamano au vizuizi kabla nyumba za watu binafsi kwa njia ya kupinga maoni yao au shughuli wala kuwa wameamua kwa hali yoyote.
4. Hakuna chama cha siasa au mgombea atakuwa na kibali yeye binafsi au wafuasi wake cha kufanya matumizi binafsi ya ardhi yoyote, jengo nk, kiwanja ukuta bila ruhusa yake kwa kuweka bendera kwenye miti-, kuweka mabango, matangazo, kuandika itikadi nk,
5. (a) Maafisa wa polisi lazima kumkamata mtu

yeyote ambaye kujenga vizuizi katika au kuvunja mikutano ya maandamano na yaliyopangwa na vyama vya siasa.
(b) Wafanyakazi au wafuasi wa chama kimoja cha kisiasa hawataruhusiwa kuleta misukosuko katika mikutano ya hadhara ulioandaliwa na chama kingine cha kisiasa kwa kuweka maswali ya mdomo au kwa maandishi au kwa kusambaza 'vipeperushi vya chama chao wenyewe.
(c) maandamano hayataruhusiwa ya chama kimoja maeneo ambayo mikutano inaendeshwa na chama kingine. Mabango ya chama kimoja yasiondolewe na wafanyakazi wa chama kingine.
Mikutano.
6. Chama au mgombea atatoa taarifa kwa mamlaka ya polisi kuhusu eneo na wakati wa mkutano, ili kuwawezesha polisi kufanya mipango muhimu kwa ajili ya kudhibiti usalama na kudumisha amani na utulivu.
7. Chama au mgombea atakuwa kujua mapema kama kuna vikwazo au amri ya zuio katika eneo waliloomba kufanyia mkutano. Kama amri hiyo ipo,wanapaswa kuitii. Kama msamaha wowote unahitajika dhidi ya amri hiyo, inapaswa upatikane mapema.
8. Kama ruhusa ya kibali inatakiwa kupatikana kwa ajili ya matumizi ya spika au kituo chochote kingine kuhusiana na mkutano uliopendekezwa, chama au mgombea aombe kwa mamlaka husika mapema na kupata ruhusa hiyo au kibali.
9. Waandaaji wa mkutano anatakiwa kutafuta msaada wa polisi juu ya wajibu wa kushughulika na watu wanaotaka kuvuruga mkutano au vinginevyo kujaribu kuleta machafuko. Waandaaji wenyewe wasichukue hatua dhidi ya watu hao.
10. Wakuu wa Polisi wa wilaya lazima kuhakikisha kuwa ripoti inatolewa kituoni juu ya watu walioleta vurugu/usumbufu katika mkutano wa hadhara, au programu nyingine na kuchunguzwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Waandaaji wa mkutano wasichukue sheria mkononi dhidi ya wakosaji hao, vinginevyo watatenda kosa chini ya sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16.

11. Wakuu wa Polisi wa Wilaya watawatahadhalisha waandaaji wa mikutano au makongamano mikutano ya kampeni, juu ya ukweli kwamba ardhi ya majengo, au mali nyingine inayohamishika au isiyohamishika ya mtu yoyote haitaharibiwa au kuvunjwa kutokana na shughuli au tabia isiyopaswa ya wanachama wa chama au wale katika mahudhurio.
12. Mgombea kwa vyovyote vile asiendeshe mkutano nje ya ule muda alioruhusiwa kufanya mkutano. Maandamano.
13. Chama au mgombea anaeandaa maandamano ataamua kabla wakati na mahali pa kuanzia maandamano, njia ya kufuatwa na wakati na mahali ambapo maandamano yataisha. Kutakuwa kawaida kuwa hakuna kupotoka kutoka mpango.
14. waandaaji watatoa mapema dokezo kwa mamlaka za polisi wa mpango ili kuwawezesha kufanya mipango muhimu.
15. waandaaji wanatakiwa kujua kama kuna amri yoyote ya zuio katika maeneo ambayo njia ya maandamano ina kupita, na atatakiwa kuzingatia amri hiyo isipokuwa kama kuna masamaha kuoka mamlaka husika. Kanuni yoyote kuhusu usalama itatakiwa kuzingatiwa.
16. waandaaji watachukua hatua za mapema ili kupanga njia kwa ajili ya maandamano, hivyo kwamba hakuna kuzuia au kizuizi kwausalama. Kama maandamano ni marefu sana, itabidi kupangwa katika makundi ya urefu wa kadri, ili kuruhusu kupita kwa urahisi, hasa katika maeneo ambapo maandamano yanapopita katika makutano ya barabara, yatapita kwa mafungu ili kuepuka msongamano wa magari.
17. Maandamano yatapita upande wa kushoto barabara kadri inavyowezekana na ushauri utakaotolewa na polisi utapaswa kuzingatiwa.
18. Kama vyama viwili vya siasa au wagombea watapendekeza maandamano juu ya njia moja au sehemu katika wakati huo huo, Mkuu wa Polisi wa Wilaya atawataka kuwasiliana vizuri mapema na kuamua juu ya hatua za kuchukuliwa ili kuona kwamba maandamano hayatasababisha kizuizi kwa watumiaji wa barabara. Msaada wa polisi utahitajika ili kufikia katika utaratibu wa kuridhisha. Kwa lengo

hili, vyama vitatakiwa kuwasiliana na polisi katika kwanza.
19. vyama vya siasa au wagombea watadhibiti kwa kadri iwezekanavyo katika suala la waandamanaji kubeba makala ambayo inaweza kutumika vibaya na mambo ya haramu, hasa katika dakika za msisimko.
20. Maafisa wa polisi wanakumbushwa kuwa macho dhidi ya makosa ambayo yanaweza kutokea katika mikusanyiko kama yalivyoainishwa na kifungu 37 (uchochezi wa vurugu) na 63B (kuinua kutoridhika na nia mbaya kwa madhumuni haramu) vya Kanuni ya Adhabu.
Siku ya Kupiga kura
21. Mkuu wa Polisi wa Wilaya anaweza, angalau wiki moja kabla ya siku ya kupiga kura, kuandaa mkutano na wawakilishi wa vyama vya siasa kushiriki katika uchaguzi katika maeneo yao ya mamlaka na kusisitiza juu yao kwamba viongozi wa chama, wanachama na wagombea watapaswa;
(a) kushirikiana na maafisa wa polisi juu ya wajibu wa uchaguzi ili kuhakikisha amani na utaratibu wa kupigia kura na kukamilisha uhuru wa wapiga kura na zoezi bila ya kuwa wanakabiliwa na kero yoyote au kizuizi;
(b) Kuwagawia wafanyakazi wao eneo la kupigia kura beji ya kufaa au vitambulisho;
(c) kushirikiana na mamlaka katika kutekeleza vikwazo juu ya kutawanya magari siku ya kupiga kura na kupata vibali kwa ajili yao ambavyo inapaswa kuonyeshwabayana.
(d) kujiepusha na kuwahudumia au kusambaza pombe siku ya kupiga kura na wakati wa masaa ishirini na nne kabla yake;
(e) kutoruhusu makutano yasiyo ya lazima kwa kukusanywa, karibu na makambi ya kuanzisha na vyama vya siasa na wagombea karibu vibanda vya kupigia kura ili; kuepuka mapambano na mvutano kati ya wafanyakazi na wafuasi wa vyama na mgombea; na
(f) kuhakikisha kwamba kambi za mgombea itakuwa rahisi. Hawataonyesha mabango yoyote, bendera, au alama nyingine yoyote nyenzo propaganda. Vyakula havitasambazwa kwa makundi ya watu katika

makambi.

Vituo na Vibanda vya kupigia kura
22. Maafisa wa Polisi wana wajibu katika vituo vya kupigia kura wanapaswa kuhakikisha usalama katika eneo hilo na kwamba hakuna mtu mwingine zaidi ataruhusiwa katika kituo cha kupigia kura: -
(a) Afisa mkuu;
(b) Afisa wa kura Msaidizi;
(c) Wakala;
(d) mpiga kura;
(e) Mtu wa kusaidia mpiga kura asiejiweza kwa mujibu wa kifungu 61;
(f) waangalizi wa kimataifa au wa ndani walioidhinishwa kwa maandishi na Tume ya Uchaguzi;
(g) mgombea;
(h) maafisa wa Tume ya Uchaguzi;
iI) Afisa wa uchaguzi au Msaidizi wa Afisa wa Uchaguzi;
(j) mtu mwingine yeyote alieidhinishwa kwa maandishi na Tume ya Uchaguzi kuwa katika kituo cha kupigia kura.
23. Maafisa wa polisi katika vituo vya kupigia wanapaswa kuhakikisha kuwa, hakuna mtu mwingine ataingia vibanda vya kupigia kura isipokuwa mpiga au mtu mwenye kibali halali toka tume ya uchaguzi.

NAMNA YA KUIFADHI MAGARI YALIYOZUILIWA KATIKA KITUO CHA POLISI KWA MUJIBU WA SHERIA:

1. Madhumuni ya amri hii ni kuonyesha utaratibu wa kisheria unaohusianan na uchukuaji wa magari pale inapolazimika kutoka barabarani katika matukio ya ajali au katika mazingira yoyote yanayosababisha msafara wa magari mengine barabarani.

2. Askari polisi wanalazimika kuondoa gari hilo kwa mijibu wa Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 (RE 2002) katika mazingira yafuatayo; -

    a) Gari liko barabarani, haliwezi kwenda na linazuia magari mengine kutumia barabara.

b) Dereva au mwenye gari amekufa au amejeruhiwa katika hali ambayo hawezi kuliendesha gari hilo.

c) Katika mazingira ambayo gari haliwezikuendesheka, hatari kwa usalama barabarani na dereva anaweza kufanya maamuzi, uondoshaji wa gari hilo lazima livutwe kwa gharama binafsi za mmiliki wa gari hilo.

Kumbukumbu za Magari:

3. Kila gari liletwalo au livutwalo mpaka kituo cha polisikuhusiana na mashauri ya usalama barabarani lazima yawekwe kwenye kumbukumbu za kimaandishi.

4. Gari lolote linalobaki kituoni bila kuchukuliwa na mumiliki wake ndani ya mwaka mmoja litachukuliwa kama mali ya kuokota. Au mali ambayo haina mwenyewe, na taratibu zitafanyika kwa mujibu wa PGO 304. Baada ya juhudi kufanyika za kumtafuta mhusika bila mafanikio.

PGO -358

USIMAMIZI YA WAHALIFU WAZOEFU

KWA AMRI YA MAHAKAMA
Sheria
1. Sheria inayohusiana na usimamizi wa polisi ipo chini ya vifungu 341, 342 na 343 cha Sheria ya Makosa ya Jinai, Sura ya. 20, R.E. 2002, na utaratibu wa Jinai (Taratibu za Usimamizi wa Polisi), 1952.

2. Lengo kuu la Amri ya Usimamizi ni kuwezesha polisi kwa njia ya

kisheria ya kutekeleza usimamizi juu ya wahalifu wazoefu na, hasa, wezi nawavunjaji nyumba ili wapate kuzuiwa kuendelea na kazi ya uhalifu.

Ufafanuzi wa wahalifu wazoefu

3. Kwa madhumuni ya Mpango huu, makosa ya jinai itakuwa ni pamoja na wezi wavunjaji, wapokeaji, wakabaji na matapeli ambao wamepatikana na hatia mara tatu au zaidi kwa makosa makubwa ya kuwania mali.

Wakati wa kuomba amri ya usimamizi

4. Ambapo "Mhalifu mzoefu" mgeni asiye na makaazi ametiwa hatiani na Mahakama ya chini kwa uhalifu mkubwa, hasa wizi, kuvunja nyumba, ghala au kuvunja duka, mwendesha mashitaka wa polisi atafanya maombi Mahakamani kwa utaratibu wa usimamizi wa polisi dhidi ya mfungwa.

Njia ya Maombi

5. (a) Mwendesha Mashtaka wa Polisi atafanya maombi yake kwa ajili ya amri ya Usimamizi *mbele ya Mahakama ya chini iliyotoa hukumu ya mfungwa*.

(b) Mahakama ikikubaliana na maombi, mwendesha mashitaka aombe Mahakama kuamuru kwamba mwangaliwa lazima kuishi katika eneo ambapo ajira inapatikana au ambapo jamaa zake wanajulikana kwa kuishi (isipokuwa kama kuna utawala imara au sababu tofauti za kipolisi).
(c) Pale mahakama kwa hiari yake yenyewe itakapotoa amri ya kuelekeza usimamizi kwamba mtu aliyetiwa hatiani atakuwa chini ya usimamizi wa polisi baada ya kumalizika muda wa adhabu yake ya awali, Waendesha Polisi lazima muwe tayari kufanya mapendekezo kama ambapo mwangaliwa anapaswa kuishi.

Majukumu ya mahakama wakati wa kutoa amri ya usimamizi
6. Wakati wa kutoa amri ni wajibu wa mahakama, chini ya kifungu 342 (1), kutaja masharti ya usimamizi na kumjulisha mfungwa ipasavyo. Waendesha mashitaka lazima kumkumbusha Hakimu juu ya wajibu huu kama imesahaulika. Hii ni muhimu kama kushindwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha kuachiwa baadae mwangaliwa aliyeshtakiwa kwa kushindwa kutii masharti ya amri yake ya usimamizi.

Majukumu ya mwendesha mashtaka wakati amri ya usimamizi imetolewa
7. Wakati amri imetolewa, mwendesha anatakiwa mara moja kuomba karani wa mahakama nakala mbili zilizothibitishwa za Amri ya Mahakama (Fomu ya

Mahakama CF 28 (a)) na kuzituma Kitengo cha uchunguzi.

Kifungo cha waangaliwa

8. Mipango imefanywa kati ya Inspekta Jenerali wa Polisi na Kamishna Mkuu wa Magereza (wafanyakazi gerezani wakiruhusu) kwa ajili ya wote walio hatiani chini ya usimamizi na kuhamishiwa Gereza daraja la 1 karibu na wilaya ambayo mwangaliwa atatakiwa kupelekwa.
Mamlaka ya gereza itatekeleza uhamisho huo angalau wiki sita kabla ya kumaliza kifungo.

Utaratibu wa nyaraka za waangaliwa

9. Miezi miwili kabla ya kutolewa kutoka gerezani waangaliwa, Afisa i / c magereza atapeleka kumbukumbu ya hatia za awali Kabla Kushitakiwa (PF. 18C) kwa Mkuu wa kitengo cha uchunguzi.

10. Mkuu wa kitengo cha uchunguzi, baada ya kupokea fomu PF. 18C atachukua hatua zifuatazo: -
(a) Kuandaa na kupeleka kwa Afisa i / c gerezani kwa ajili ya ulinzi wa wangaliwa: -

(i) Kadi ya Utambulisho wa mwangaliwa (PF. 155), ikiwa na nambari ya TCRO;
(ii) Fomu ya Kupokea (F.B. 5) katika nakala tatu; na
(iii) Fomu ya Taarifa (F.B. 3).

(b) Kuwasilisha kwa RCO katika Mkoa ambao mwangaliwa ataishi na ripoti: -

(i) nakala ya Amri ya Mahakama (Jud. 28A);
(ii) nakala ya Fomu ya Taarifa (F.B. 3), na
(iii) Fomu ya kumbukumbu za jinai (PF. 18B).

11. Afisa upelelezi Mkoa, ndani ya masaa 48 ya kupokea karatasi zilizotajwa chini ya aya ya 10 (b) hapo juu, atafanya yafuatayo: -

(a) kuwashauri Afisa i / c magereza kwa barua juu ya tarehe na mahali mwangaliwa anatakiwa kuripoti;
(b) kuandaa Karatasi ya Usimamizi wa Polisi (PF21) katika nakala mbili (nakala moja ambayo itakuwa katika jalada Makao Makuu ya mikoa);
(c) kupeleka faili la mwangaliwa lenye nakala moja ya Karatasi ya Usimamizi wa Polisi (PF. 21) na nakala ya Amri ya Mahakama kwa

Mkuu wa upelelezi Wilaya au OCD katika eneo hilo ambalo mwangaliwa ataishi;
(d) kurudisha Fomu ya kumbukumbu za Jinai (PF. 18B) na O / C. Forensic Bureau.
(e) Kuandika kwa Afisa Upelelezi wa Mkoa ambao Mkoa mwangaliwa amehukumiwa kwenda na kumtaka kupanga kwa ajili ya kumchukuwa picha, hii itafanyika kwa njia zifuatazo: -

(i) Kitengo cha matukio ya Uhalifu (kama kipo) kuandaa picha nne, kutuma mbili kwa RCO na kuomba Afisa huyo kutuma nyingine mbili negative kwa O / C. FB kwa ajili ya kufungua jalada, na
(ii) kama hakuna kitengo cha matukio ya uhalifu, negative itapelekwa O / C. FB pamoja na maelekezo ya kutuma picha mbili kwa RCO anayezihitaji.

(f) Baada ya kupokea picha ya mwangaliwa tuma moja kwa OC - C.I.D. na nakala moja Makao Makuu ya Mkoa.

12. barua katika aya ya 11 (c) hapo juu itaunda ripoti mwangaliwa na itafanywa na kudumishwa na O / C - C.I.D.au ambapo hakuna Kitengo cha C.I.D., na OCD.Afisa upelelezi Mkoa pia atakuwa na nakala ya ripoti ya kila mwangaliwa. Ripoti itapewa nambari ya kumbukumbu (prefixed na abbreviation Station) kama ilivyoelekezwa katika PGO No 359 na kufuatiwa na barua SHS (Supervisee History sheet), supervisee's TCRO number na C.I.D.Serial number, kwa mfano MOS/SHS/241/59/3, kuonyesha kwamba ripoti ilifanywa mjini Moshi kwa mwangaliwa mwenye kadi ya utambulisho na 241/59 na kutunzwa kama Makala No 3 katika Rekodi ya Ofisi ya CID.

13. index ya mwangaliwa itaoneshwa na index ya majina yaliyo kwa maafisa CID Wilaya na Mikoa.

14.mawasiliano yote yanayohusiana na waangaliwa yataoana na namba za T.C.R.O zao na nakala zote za mawasiliano hayo yatumwe kwa Maafisa upelelezi Mkoa na O / C. Forensic Bureau.

Ubao wa waangaliwa

15. (a) ubao wa waangaliwa ukionyesha "katika mtazamo" msimamo wa mwangaliwa utasimamiwa na Maafisa wa CID Wilaya na Mikoa katika fomu inavyoonekana katika Kiambatisho "B". Kila mwangaliwa atakuwa chini ya disc, upande mmoja wa ambayo itaonyesha jina, namba ya kumbukumbu ya T.C.R.O na ripoti ya tarehe ya kumalizika kwa muda wa usimamizi. picha ya mwangaliwa itakuwa imewekwa nyuma mwa disc.

(b) kumbukumbu za mwangaliwa zitawekwa kwenye sehemu ya "IN VIEW" katika ubao, kuonyesha maelezo binafsi. "OUT VIEW" zimeonyeshwa kwa upande wa nyuma ya disc kuonyesha picha kwa wapelelezi wote kuona.
(c) waangaliwa walitiwa hatiani tena wataonyeshwa kwenye sehemu ya "IN PRISON" kwenye ubao na maelezo ya ziada ya tarehe ya kutolewa kutoka gerezani.

Uangalizi - Utekelezaji wa

16. Baada ya kutolewa kwa mwangaliwa, itakuwa wajibu wa Afisa CID wa Mkoa kuhakikisha kwamba anawasiliana mara moja na mwangaliwa na kufahamu masharti ya usimamizi wake.

17. Wakati mwangaliwa ripoti mara ya kwanza kwenye kituo cha Polisi ambacho yeye akuwa anasimamiwa, Mkuu wa Kituo atapanga kwa ajili ya kuangaliwa na kila askari wa GD na CID.

18. Itakuwa basi ni wajibu wa Mkuu wa upelelezi Wilaya, au ambapo hakuna Kitengo cha C.I.D., ni wa OCD kuwapangia askari wa upelelezi kuwajibika kwa usimamizi wa mwangaliwa ili mpelelezi huyo aweza kuwafahamu mwenyewe kwa kina kabisa juu ya tabia, sifa, na washirika wa mwangaliwa.

19.utatakiwa kuwasiliana na mwangaliwa angalau mara moja kila wiki nyumbani kwake au sehemu ya ajira wakati wote kwa usiku na mchana, pamoja na taarifa ya hiari katika kituo cha polisi au mamlaka za asili. Itakuwa pia wajibu wa O / C- C.I.D. kuhakikisha kwamba waangaliwa wanaoishi umbali mrefu kutoka Vituo vya Polisi na walioruhusiwa kutoa taarifa kwa Serikali za Mitaa wanatembelewa na mamlaka ya asili katika vipindi sawa na kwa wafanyakazi wa CID. Rekodi ya ziara ya kuonyesha hali dhahiri na njia ya kuondoka na nyingine yoyote ya taarifa muhimu juu ya mwangaliwa itafanyika katika daftari la kumbukumbu za afisa wa polisi na juu ya kurudi kwake kituoni, taarifa hii kunakiliwa katika ripoti ya mwangaliwa.
KUMBUKA: Usimamizi wa Mamlaka za Wenyeji uwekwe kwa kiwango cha chini na inaweza tu ikaruhusiwa katika kesi ya ugumu wa maisha halisi isipokuwa kwa aelekezo ya Mahakama iliyotoa amri.
20. mpelelezi kwa ajili ya mwangaliwa atajulisha maelezo ya kuwasiliana na mwangaliwa kila wiki kwa Mkuu wa Kituo au Kitengo cha C.I.D. ambaye atakuwa anatunza maelezo ya mawasiliano kwenye karatasi ya taarifa ya mwangaliwa (PF. 21).

Malipo ya Kudumu ya Makazi

21. (a) mwangaliwa anaweza kuhamisha nafasi yake ya makazi kutoka

Wilaya moja hadi nyingine bila ridhaa ya maandishi ya Afisa Tawala au OCD ambayo kwa sasa anaishi na Afisa Tawala au OCD wa Wilaya ambayo anatarajia kuishi. (kifungu cha 342 (1) (b) na (c)).
(b) maombi kwa ajili ya malipo ya makazi itakuwa kupita kwa Afisa CID wa Mkoa ambaye kwa sasa ni mkoa wa makazi ya mwangaliwa. Afisa huyu atakuwa rejea maombi ya CID wa Mkoa Afisa karibu na mahali pa yaliyokusudiwa mpya ya makazi au kama nafasi mpya ya makazi ni katika mkoa huo, kwa Wilaya husika CID Afisa pamoja na nakala ya karatasi ya historia supervisee na sababu za mabadiliko ya taka ya makazi.
(c) Baada ya kupokea maelezo iliyotajwa katika aya ndogo ya (b) hapo juu, Wilaya ya Mkoa / CID Afisa ambaye eneo supervisee anatamani kuishi itakuwa kutambua uhalali na / au kuhitajika kwa hoja ya supervisee katika eneo lake na atakushauri CID wa Mkoa Afisa msimamizi wa eneo supervisee ya sasa ya makazi, kwa maandishi, ya kukubali kwake au vinginevyo.
(d) Wakati mabadiliko ya makazi yamethibitishwa kwa maandishi na maafisa wote, Afisa wa CID Mkoa ambao kwa sasa ni eneo analoishi mwangaliwa, atahakikisha kwamba taarifa inatangulia mapema ya namna ya kusafiri na tarehe na muda wa kuondoka na kuwasili kwa afisa anayempokea na atatakiwa, kama ni muhimu, kutoa msindikizaji.
(e) taarifa za mwangaliwa za Mkoa / Wilaya zitatumwa kwa afisa mpokeaji na endapo makazi mapya ni katika mkoa mwingine, Afisa wa CID Mkoa atafuata utaratibu uliowekwa katika aya ya 11 (c) hapo juu. CO Ofisi ya kiuchunguzi atashauriwa na afisa mpokeaji juu ya mabadiliko ya makazi kwa barua.

Mabadiliko ya makazi ya muda

22. Endapo mwangaliwa anaruhusiwa mwenyewe kuondoka wilayani kwake kwa zaidi ya siku 30, kadi yake, pamoja na barua katika fomu iliyo katika Kiambatisho "A" itapelekwa katika wilaya ambayo anatarajia kuishi kwa muda. Mabadiliko haya yatatambuliwa kama uhamisho wa muda.

Uvunjaji wa sheria ya uangalizi

23. Uvunjaji wowote wa Amri ya Uangalizi atakuwa ilivyoripotiwa kwa taarifa za haraka kwa CO Forensic Bureau na baada ya hapo mwangaliwa atahesabiwa kama mtu anaye tafutwa chini ya sheria ya PGO No.37 na jalada la uchunguzi litafunguliwa bila kuchelewa. Afisa C.I.D. Mkoa atatakiwa, katika mazingira haya, kurudisha Fomu 28A kwa CO Forensic Bureau.

24. Mwangaliwa atahesabiwa kuwa "haonekani (Out of View)" mwezi mmoja kuanzia tarehe yake yeye mara ya mwisho kuonekana, isipokuwa katika hali ya kuwa na ruhusa ya maandishi ya kukosekana.

Ukomaji wa Usimamizi

25. Baada ya kumalizika kwa kipindi cha usimamizi wa mwangaliwa, kadi

yake (PF. 155) itaondolewa na kupelekwa kwa Afisa CID wa Mkoa ambaye, baada ya kukamilisha rekodi yake, atarudisha kadi hiyo kwa CO Forensic Bureau kwa uteketezaji. Ripoti ya mwangaliwa itatakiwa kubakia kwa Vitengo vya CID wilaya na Mikoa na mwangaliwa kuchukuliwa kama mhalifu mzoefu kwa mujibu wa PGO NO. 359.

KIAMBATISHO "A" Kwa P.G.O. No 358

Kwa: Mkuu wa Polisi Wilaya ya ....
1. Mimi leo kwa ridhaa yangu nimekubali kwa maandishi kuwa mwangaliwa wa Polisi ambaye maelezo yake yametolewa hapa chini kuendelea na kuishi huko katika wilaya yako kwa kipindi cha siku .... kuanzia tarehe ya leo. Ningependa kukuomba kurudisha nakala mbili, zilizokamilika kihalali,za barua hii kwangu kwa hatua zaidi.

2. Tafadhali nipe taarifa, kwa telegram, kama mhusika hajawasili kwako ndani ya siku saba.
Afisa i / c polisi ..... Wilaya ya.....
Tarehe .....
Nakala kwa: CO Forensic Bureau.
C.R.O. No ....
Jina ....
Kabila ....
Umri ....
Maelezo ....

Sehemu ambayo mwangaliwa anatarajia kutembelea .....
Kwa: Afisa i / c Polisi .... Wilaya.
Mwangaliwa aliyetajwa hapo juu amejulisha kuwasili kwake katika wilaya hii tarehe.....
Yeye anaishi katika .... na
....
Wakati wa kukaa kwake katika wilaya hii na yeye alitoka kwako tarehe
..... baada ya maelekezo yako ya kuripoti ndani ya siku saba.
Afisa i / c Polisi ..... Wilaya ya
Tarehe .....
Nakala kwa: CO Forensic Bureau.

KIAMBATISHO "B" Kwa P.G.O. Na 358
WAANGALIWA KILIMANJARO SPECIMEN I

DISTRICT	IN VIEW	OUT OF VIEW	IN PRISON
Mwanga	OOOOOOOOO	OOOO	
Moshi	OOOOO	O	
Hai	OOOO	OO	
Same	OOO		
Rombo	OOOOO	OOO	

APENDIX "B"

To P.G.O. No. 358

SUPERVISEES

MOSHI DISTRICT

SPECIMEN II

STATION	IN VIEW	OUT OF VIEW	IN PRISON
Central	OOOO	OO	
Majengo	OOO	O	
Himo	OOOOO	OOO	

PGO 373.

UTARATIBU WA KUONGOZA MISAFARA YA MAGARI BARABARANI:

Amri ya ujumla

1. Madhumuni ya amri hii ni kuweka miongozo ya udhibiti na usimamizi wa misafara ya magari barabarani.
2. Mpango kazi wa udhibiti wa misafara ya magari barabarani inaweza kufanyika katika mazingira yafuatayo;-
    a) Matukio ya ajali barabarani.
    b) Wakati wa msongamano wa magari barabarani.
    c) Misafara ya viongozi wakuu wa serikali.
    d) Matukio maalum (wakati wa misafala ya watu au magari yanayopita taratibu kwa shughuli maalum, gwaride, mashindano ya baiskeli au magari au michezo mingine).
    e) Dharura yoyote
    f) Taa za kuongozea magari yanapharibika barabarani.

Mavazi yanayoonekana kwa urahisi.

3. Askali polisi waongozaji wa misafara lazima wavae jaketi au makoti ya mvua yanayoweza kuakisi mwanga na kuonekana kwa urahisi wakati wa kazi zinapofanyika usiku au wakati wa mvua na wakati mwingine wowote ambao mwonekano wa kitu unakuwa hafifu.

Kudhibiti wa Msafara wa magari panapotokea matukio ya moto.

4. Askari Polisi wanaoamriwa kudhibiti msafara wa magari wakati wa matukio ya moto wanakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba barabara katika eneo la tukio linapitika kwa magari yanayokuja katika tukio hilo. Askari polisi katika tukio la moto anaweza kufunga barabara kama itaonekana kunaulazima ili kuwezesha magari ya dharura kufika eneo la tukio. Askali ataendelea kudhibiti msafara wa magari mpaka tukio hilo limetatuliwa au amepokelewa kazi na askali mwingine.

PGO - 374

USALAMA BARABARANI

KUENDESHA GARI KATIKA HALI YA ULEVI:

1. Wakati mtu anakamatwa kwa kuendesha au kujaribu kuendesha gari au mkokoteni unaovutwa na mnyama katika barabara au sehemu yoyote ya jumuiya akiwa katika hali ya ulevi inayomwondolea uwezo wake wa kuendesha. Askari anayeshughulikia shauri hilo atapanga utaratibu wa kumpima kiwango cha ulevi kilichopo katika damu yake.

2. Kama udhibitisho kwamba kiwango cha ulevi kilichomo katika damu yake kinazidi kiwango cha kawaida, dereva huyo atashitakiwa. Pia ikidhibitika kwamba kiwango cha ulevi kilicho kwenye damu yake hakizidi kiwango cha kawaida, dereva huyo ni vema akaachiwa mara moja, isipokuwa anashikiliwa kwa sababu zingine za kisheria.

PGO - 375

USALAMA BARABARANI

UPELELEZI WA AJARI ZA BARABARANI:

1. Kwa mujibu wa sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 (RE 2002), dereva wa gari lililohusika kwenye ajali ataitajika kutoa taarifa polisi katika mazingira yafuatayo;-

a) Kama dereva huyo amehusika katika ajali ya gari ambayo imesababisha majeruhi kwa mtu mwingine (hataitajika kutoa taarifa ya ajali iwapo derva peke yake ndiye aliyepata majeraha)

b) Kama amehusika kwenye ajali iliyosababisha gari linguine kuharibika au kama mnyama yeyote afugwae ambaye hakuchukuliwa kwenye gari lake na hakusimama na hakutoa jina lake na anuani yake na hakutoa jina na anuani ya mwenye gari na alama ya utambulisho wa gari kwa mtu yeyote ambaye ana sababu za msingi za kutaka kufahamu mambo yaliyotajwa hapo juu aliyekuwepo katika eneo la ajali (haitajiki kutoa taarifa kama gari lililoumia ni mali yake au mnyama aliyejeruhiwa alipakiwa kwenye gari la dereva huyo na hakuitajiki kutoa taarifa ya ajali hiyo kama baada ya ajali iliyosababisha kuumia kwa gari linguine au kujeruhiwa kwa mnyama afugwaye ambaye hakupakiwa kwenye gari lake kama dereva huyo ametoa taarifa zinazohusiana na jina lake, anuani yake au jina la mwenye gari na anuani yake. Au alama za utambulisho wa gari lake kwa mtu ambaye ameitaji taarifa hiyo kwenye eneo la ajali.

c) Kama dereva huyo amehusika kwenye ajali iliyosababisha kuharibika kwa mali amabyo sio yak wake na hakusimama na kutoa jina na anuani yake na hakutoa jina na anuani ya mwenye gari na hakutoa alama za utambulisho wa gari kwa mtu yeyote aliyekuwa na sababu za msingi za kuhitaji taarifa hizo katika eneo la ajali.

2. Katika kupokea taarifa ya ajali ya usalama barabarani kutokea askari polisi mwenye jukumu la kupeleleza jalada la kesi hiyo lazima aende kwenye eneo la tukio mara moja. Fomu inayohusiana na taarifa usalama barabarani, vifaa vya huduma ya kwanza, kipimo cha kiwango cha kilevi, kipimo cha urefu na upana, chaki au unga mweupe kwa ajili ya kuweka alama barabarani na katika ajali kubwa, kamera na alama za tahadhari na taa zichukuliwe iwapo itaoneka kuna ulazima.

3. Katika kufika kwenye eneo la tukio la ajali, hatua zifuatazo lazima zichukuliwe;-

a) Kusimamia utoaji wa huduma ya kwanza kwa amjeruhi na kufanya utaratibu wa kuwapeleka hospitali kwa matibabu. Uharaka ni muhimu katika kushughulikia majeruhi. Majina na anuani za majeruhi ni muhimu zifahamike na majina ya mtu wa karibu pale unapotokea ulazima. Hatua za muhimu zichukuliwe kuwezesha kufahamu utambuzi wa majeruhi waliopoteza fahamu.

b) Iwapo barabara imezuiwa, hakikisha msafara wa magari unapita

njia nyingine kukwepa eneo la ajali au ondoa magari yaliyohusika kwenye ajali kwa upande mwingine wa barabara baada ya kuweka alama za magurudumu katika barabara.

c) Pata majina na anuani za mashahidi walioshuhudia ajali hiyo na zuia watembea kwa miguu kuepusha msongamano.

d) Wakati wa uchukuaji wa taarifa muhimu katika fomu namba 3 ya Polisi ni vema kukamilisha kitu kimoja kwa wakatikadri iwezekanavyo, kwa mfano kama magari mawili au zaidi yamehusika kwenye ajali, pata taarifa zote zinazohitajika kuhusiana na gari moja kabla ya kushughulikia gari nyingine. Ruhusu magari kuondoka haraka iwezekanavyo ili kupunguza uzuiaji wa barabara baada ya kuchukua taarifa kama kuna uharibifu na kagua hali ya breki, usukani, honi, n.k. kama kunamatatizo ya kiufundi yaliyotiliwa mashaka ukaguzi lazima ufanyike na mkaguzi wa magari. Na ukaguzi huo pia utahusiana na ajali zilizosababisha vifo. Madereva na magari hayo lazima wasaidiwe kama ni muhimu, pia katika majina na anuani zao na taarifa zinazohusiana na makampuni ya bima.

e) Kama kuna sababu za kuamini kwamba uwezo wa madereva ulidhoofika kutokana na ulevi chukua hatua kwa mujibu wa amri namba 374.

f) Chukua vipimo vya barabarani na tayarisha ramani ya tukio kuonyesha vipimo vya barabara, sehemu za mseleleko wa magurudumu baada ya kufunga breki na eneo linaloonyesha magurudumu kusota kwenye barabara, maeneo yaliyo na miili ya marehemu, magari, vioo vilivyovunjika, aina ya udongo uliopo kwenye vifaa vya kuzuia tope kwenye magurudumu na ushahidi mwingine unahusiana. Vipimo vichukuliwe kwa usahihi na penye ulazima picha zipigwe.

4. Majeruhi lazima wahojiwe baada ya kupata ruksa ya mganga na maelezo yao lazima yachukuliwe kuangalia kama fomu namba 3 ya Polisi imejazwa kikamilifu na mganga kwa kila majeruhi. Mtu wa karibu na majeruhi ni lazima ajulishwe kama ajali imesababisha kifo au majeraha ya hatari.

5. Maelezo ya madereva waliohusika katika ajali yachukuliwe na maelezo ya abiria pamoja na mashahidi. Leseni ya kuendeshea gari,cheti cha bima ya gari na leseni ya gari vitakaguliwa kuangalia kama havijaisha muda wake wa matumizi.

Ajali za kugonga na kukimbia.

6. (a) katika ajali za upelelezi wa ajali za kugonga na kukimbia, kitu muhimu kinachoitajika na uharaka wa kuzuia uharibifu wa ushahidi unaothibitisha kosa. Mara hatua muhimu kama ilivyoelezwa katika aya ya 3 ya amri hii kuchukuliwa, mpelelezi ajulishe gereji bubu na gereji zinazotambuliwa kisheria kutoa taarifa kamilifu za magari yaliyohusika katika ajali ili kuondoa uwezekano wa kufanyia matengenezo gari yoyote ilihusika katika ajali na kukimbia.

   (b) uhangalifu lazima uchukuliwe ili kukusanya vioo vilivyovunjika, vyuma, rangi za fedha na ushahidi mwingine wowote utakaogundulika katika eneo la tukio la ajali lazima uhifadhiwe kwa ajili ya ulinganifu mara gari husika litakapopatikana.

   (c) askari wa usalama barabarani na askari wa kawaida lazima wataadhalishwe kutafuta gari lolote linaloonekana kuwa na uharibifu mpya au kufanyiwa matengenezo ya karibuni lichukuliwe kama gari linalotafutwa. Wamiliki wa gereji pia wajulishwe.

   (d) wakati gari husika likiwa limepatikana, mpangilio lazima ufanyike kuweza kukaguliwa kabla halijaondolewa sehemu zote za bodi ya gari zilizotengenezwa kwa ajili ya kutafuta damu, nywele, vitu vingine, mikwaruzo, sehemu zilizobonyea n.k. Vitu vingine vyovyote lazima viondolewe na kuhifadhiwa kwa ajili ya uchunguzi wa kisayansi.

7. wakati kifo kimetokea kwa ajili ya ajali barabarani, mtafiti wa kifo atajulishwa kwa kuwasilisha fomu “B” na mwili utatambuliwa na jamaa au marafiki mbele ya mganga anayefanya uchunguzi katika mwili mbele ya shahi aliyeshuhudia katika eneo la ajali kwa ajili ya utambuzi na atalazimika kufika mbele ya mahakama kwa ajili ya kutoa ushahidi. Taarifa uchunguzi wa kifo atakayofanya mganga itapatikana katika fomu “D” (M.F.L 6) kutoka kwa mganga ikiwa imesahiniwa.

8. Kuhusiana na kupokea taarifa ya gari, taarifa itaingizwa katika kitabu cha matukio cha kituo (fomu ya polisi namba 162). Pamoja na taarifa ya awali (sehemu ya nyuma ya fomu ya polisi namba 162). Jukumu la Mkuu wa Chumba cha Mashitaka ni kumjulisha mara moja Mkuu wa Kituo au Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani na kumwomba atoe idadi ya kutosha ya wapelelezi katika mashauri yote ya ajali za barabarani zilizosababisha vifo au majeruha ya hatari au uharibifu mkubwa, Mkuu wa Kituo au Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani atakwenda kwenye eneo la tukio na kusimamia upelelezi. Ujumbe wa onyo la kwanza (kama ilivyoelekezwa katika PGO 314) itapelekwa kama inaitajika na katika matukio ya ajali za barabarani

zilizosababisha vifo, taarifa kamili zitapelekwa kwa ofisa wa kazi wa eneo husika Jalada la Usalama barabarani (Polisi fomu 89) (nene au jembamba) kwa mujibu wa PGO 371 hitatumika.

9. Baada ya kukamilisha upelelezi unaohusisha ajali za barabarani za vifo au ajali kubwa, ulevi, makosa makubwa ya uendeshaji gari au ambayo maofisa muhimu wa serikali au ofisa wa polisi wamehusika, jalada la usalama barabarani litapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya au mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani na mapendekezo kwa ajili ya kusitakiwa au hatua zaidi.

10. Tahadhali ichukuliwe katika taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika mashauri ambayo magari ya polisi yamehusishwa katika ajali, kama ilivyoelekezwa katika PGO 196 “Ajali za magari ya polisi”.

11. Kadi ya takwimu ya ajali za barabarani (Polisi fomu namba 212) zitakamilishwa kwa kuzingatia taarifa zote zilizotolewa za majeruhi kutokana na ajali za barabarani.

12. Pitia PGO 371 “fomu za usalama barabarani zinatumika kwa” au aina mbalimbali za fomu za usalama barabarani ambazo zinahitajika kukamilishwa.

Utunzaji na mwisho wa majalada ya mashauri ya usalama barabarani.

12. (a) Mashauri yalioendeshwa mbele ya mahakama lazima yapelekwe Makao Makuu ya Wilaya na kuzuiliwa kwa mwaka moja na Mkuu wa Polisi wa Wilaya kama ilivyoelekezwa na PGO 286.

PGO - 401

HAKI, MARUPURUPU NA MIKUTANO YA VYAMA VYA SIASA.

1. (a) Shughuli, haki na marupurupu ya vyama vya Siasa Tanzania vinaratibiwa na Katiba ya ya Jamuhuri ya Muungano ya mwaka 1977, Sura ya 2 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na Sheria ya vyama vya siasa Sura ya 258 (RE 2002), Sheria ya Uchaguzi ya Taifa Sura ya 343 (RE 2002), Sheria ya Serikali za Mitaa (Uchaguzi) Sura ya 293 (RE 2002) NA Sheria ya Polisi na Wasaidizi wa Polisi, Sura ya 322 (RE2002) kati ya sheria nyinginezo.

(b) Kwa upekee, ofisa kiongozi wa eneo ambalo vyama vya siasa vinaendesha shughuli zake vinatakiwa kuhakikisha kwamba sheria za nchi na kanuni zake vinazingatiwa kwanza bila kuathiri shughuli za kisheria zinazoendeshwa na vyama hivyo.

(c) Ili kuhakikisha kwamba shughuli za vyama vya siasa zinafanyika vilivyo katika mikoa na wilaya, Makamanda wa Polisi wa mikoa na Wakuu wa Polisi wa wilaya wanawajibu wa kuona kwamba mikutanona maandamano katika maeneo yao yanaendeshwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258, (RE 2002). Hii ni kutokana na ukweli kwamba kila chama kilichopata usajili wa muda na wa kudumu vinawajibu ufuatao:-

I. Kuitisha na kuhutubia mikutano kwenye maeneo yote ya Jamuhuri ya Muungano baada ya kutoa taarifa kwa kiongozi wa Polisi wa eneo husika kwa madhumuni ya kujitangaza na kushawishi kupata wanachama.

II. Kulinda na kusaidia uwepo wa mawakala wa usalama kwa madhumuni ya kuhakikisha amani na utulivu vinatawala kwenye mikutano.

2. (a) Endapo maandamano ya vyama vya siasa yamepangwa kuendeshwa nje ya wilaya moja katika mkoa, suala kwamba maandamano hayo yatavuka nje ya wilaya moja au nyingine litaamuliwa na Wakuu wa Polisi wa wilaya zote husika kwa kupata ushauri toka kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa. Vinginevyo Mkuu wa Polisi wa eneo husika ana mamlaka ya kukubali au kukataa kufanyika kwa maandamo hayo kwa kuzingatia vifungu vya sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 (RE 2002)

(b) Mkuu wa Polisi wa Wilaya haruhusiwi kuruhusu chama cha siasa chenye usajili wa muda kuendesha kampeni ya kumunadi mgombea yeyote katika uchaguzi wa Ubunge au Uraisi au kwenye Uchaguzi wa serikali za Mitaa wakati chama cha namna hiyo kimekatazwa kufanya hivyo.

3. Bila ya kuathiri sheria yeyote iliyopo kinyume na vifungu vya 43, 44, 45 na 46 vya Sheria ya Jeshi la Polisi na Wasaidizi wake, Sura ya 322 (RE 2002) (rejea kiambatanisho A cha kanuni hii) vinatumika na vitaathiri mikutano yote itakayofanyika kwenye Jamuhuri ya Muungano kwa Chama chochote cha siasa chenye usajili wa muda au kudumu.

4. Mkuu wa Polisi wa wilaya lazima ahakikishe kwamba chama cha siasa hakifanyi mikutano au maandamano kwenye eneo lolte la umma lililo

wazi labda taarifa ya maandishi iwe imetolewa sio chini ya muda wa masaa 48 kabla ya mkutano huo kufanyika.

5. Mkuu wa Polisi wa Wilaya atahakikisha kwamba taarifa ya maandishi iliyotajwa kwenye aya ya 4 juu itaeleza japo kwa ufupi mambo yafuatayo:-

    a) Jina la chama kilichotoa taarifa.

    b) Eneo na muda ambao mkutano unatarajiwa kufanyika;

    c) Mada au dhumuni la jumla la mkutano huo.

6. Mkuu wa Polisi wa Wilaya lazima awe makini kwamba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (zamani waziri wa Usalama wa Raia), anaweza mara kwa mara kutoa tangazokatiga Gazeti la serikali taarifa nyinginezo zinazoweza kutakiwa kutolewa kwenye taarifa hiyo ya maandishi. Taarifa hizo zikitolewa ni lazima zizingatiwe na vyama husika vya siasa.

7. Endapo chama cha siasa kitawakilisha taarifa kwa mujibu wa aya ya 4 juu kinaweza kuendelea kuendesha mkutano husika kama ilivyopangwa hadi kitakapopokea amri kutoka kwa kiongozi wa Polisi wa eneo husika akieleza kwamba mkutano huo usifanyike kama ilivyotolewa taarifa.

8. Mkuu wa Polisi wilaya ambaye amepelekewa taarifa kwa kuzingatia aya ya 4 hataweza kutoa amri ya zuio kwa kuzingatia aya ya 7 kwa kuhusisha taarifa hiyo labda awe amejiridhisha kwamba;-

    a) Taarifa ilishawahi kutolewa na chama kingine cha siasa au watu wengine kufanya mkutano au shughuli nyingine au maandamano katika eneo hili hilo na muda huo huo kama ilivyokusudiwa na mwombaji.

    b) Mkutano au maandamano yanayokusudiwa kufanyika ni kinyume na sheria za nchi.

    c) Mkutano endapo utafanyika kuna taarifa za kutokea uvunjifu wa amani.

    d) Chama cha siasa au kundi la watu lilitoa taarifa sio chama cha siasa kilichosajiliwa.

    e) Kuwepo au kuendelea kuwepo kwa mkutanoau maandamano katika eneo la wazi ni kinyume na taarifa zilizotolewa na waombaji au kumezuiliwa na waziri.

9. (a) Amri ya zuio iliyotolewa kwenye aya ya 8 lazima iwe kwenye maandishi na katika fomu hiyo kufafanuliwe sababu za kuzuia na endapo chama hicho cha siasa kinaweza kuendesha mkutano eneohilo kwa muda mwingine au tarehe itakayokuwa na nafasi.

   (b) Amri ya zuio itatolewa kama hatua ya mwisho na kwamba Mkuu wa Polisi wa Wilaya hatakiwi kuofia shughuli za kisiasa za chama cha siasa labda kuwepo na sababu za msingi na za kisheria za kufanya hivyo.

PGO - 403

MIKUTANO MINGINE YA HADHARA MAANDAMANO

1 (a) Mtu yeyote mwenye nia ya kuitisha, kukusanya, kuandaa mkutano au maandamano katika eneo la wazi, atatoa kwa polisi si chini ya masaa arobaini na nane kabla ya wakati mkutano au maandamano umepangwa kufanyika, kuwasilisha taarifa ya maandishi ya mkutano wake au maandamano kwa afisa wa polisi katika eneo hilo ili kubainisha: -
(i) mahali na wakati ambapo mkutano utafanyika;
(ii) Madhumuni ya mkutano kwa ujumla, na
(iii) maelezo mengine kama Waziri atakavyobainisha mara kwa mara, katika tangazokatika Gazeti la Serikali,.
(b) Iwapo mtu atatoa taarifa kwa mujibu wa aya iliyotangulia, anaweza kuendelea na kuitisha, kukusanya, kuunda au kuandaa mkutano au maandamano kama ilivyopangwa, mpaka atakapopata amri ya kumzuia kutoka kwa Afisa Polisiwa eneo hilo kuelekeza kwamba mkutano au maandamano hayo hayatafanyika.
(c) Ofisa wa Polisi aliejulishwa kwa mujibu wa aya (1) (a), hatazuia mkutano/ maandamano hayo isipokuwa kama ataridhika kwamba mkutano au maandamano hayo ni uwezekano wa kusababisha uvunjaji wa amani au usalama wa umma au ya yatatumika kwa madhumuni yoyote kinyume cha sheria.
(d) Ofisa msimamizi wa Polisi anaweza kusitisha au kuzuia kufanya au kuendelea kwa mkutano au maandamano yaliyoitishwa, au kupangwa kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kutoa au kutoa amri kama hizo kama anaweza kufikiria muhimu au afadhali, ikiwa ni pamoja na maagizo kwa ajili ya usambazaji wa mkutano yoyote vile au maandamano kama ilivyotajwa.
(e) Katika muktadha huu "mahali pa umma" ina maana yoyote ya barabara, Hifadhi ya umma, kawaida au bustani yoyote pwani ya bahari, ziwa au pwani, na yeyote daraja ya umma, barabara, mitaani, mstari, njia za miguu, mraba, mahakama, kama faragha au la, na ni pamoja na sehemu yoyote, kama jengo au la, na ambayo kwa wakati huo umma wanaruhusiwa kutumia, iwe kwa ya

malipo au vinginevyo.
2. Ikumbukwe kwamba Vibali haviwatakiwi kwa ajili ya mikutano/ maandamano yafuatayo;
(a) Mikutano ambayo wasemaji ni Mawaziri wa Serikali akizungumza katika nafasi zao za utumishi.
(b) ya kidini, kijamii, kielimu, burudani au michezo mikutano (GN 169/58).
(c) Mkutano ulioitishwa na Serikali za Mitaa ndani ya eneo la mamlaka yao kwa madhumuni yanayohusiana na majukumu yao rasmi (GN No. 98/60)

PGO ZILIZOTAFSIRIWA

PGO NAMBA:

I - 20, 23, 32 -40, 43 – 48, 53 – 61, 81 – 88, 90,

101 – 111, 169 – 174, 191, 193 – 198, 211, 221 – 223,

225, 227, 229 – 233, 236 - 238, 272 – 275, 277, 278, 280,

284 – 288, 292 – 295, 297 – 312, 314 – 320, 351- 358,

373 -375, 401 NA 403

PGO AMBAZO HAZIJATAFSIRIWA

PGO NAMBA:

21, 22, 31, 41, 42, 49, 50, 51, 52, 89. 121, 122, 123, 124, 125,

126, 127, 128, 129, 130 , 131, 132, 133, 134, 135, 141, 142,

143, 151, 152, 153, 154, 155, 156, 157, 158, 159, 160,161,

162,

163. 164.165, 166, 167, 168, 199, 212, 213, 228, 239, 240, 271,

276, 279, 281, 282,283,289, 290, 291, 296, 313, 359, 371,

372, 402, 411,412, 413, 414,415, 416, 417, 418.

PGO ZILIZOFUTWA KWA MAREJEO YA MWAKA 2006

PGO NAMBA

24 – 30, 62 – 80, 91 – 100, 111 – 120, 136 – 140, 144 – 150,

174 – 190, 200 – 210, 214 – 220, 241 – 270, 360 – 370,

376 – 400, 404 – 410 NA 419 - 420